**21 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Thelathini – Tarehe 21 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Monni.

Na. 391

### Hitaji la wataalam wa *X-Ray* na *Ultra Sound* Hospitali ya Wilaya Chemba

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini wataalam wa *X-Ray* na *Ultra Sound* watapelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Dodoma una jumla ya wateknolojia mionzi *(radiographer)* 14. Halmashauri ya Wilaya ya Chemba imepelekewa mtaalamu wa mionzi Oktoba, 2023 ambaye anatoa huduma ya *Ultra Sound* na *X-Ray* katika Hospitali ya Wilaya ya Chemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuboresha huduma za uchunguzi za radiolojia na *Ultrasound* kwa kuwezesha kusimika mashine za *X-Ray* na *Ultrasound* katika vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi nchini ikiwa ni pamoja na kuajiri wataalam wenye ujuzi wa kutumia mashine hizo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, hospitali hiyo hiyo ya wilaya haina mtaalam wa maabara. Je, ni lini Serikali italeta mtaalam huyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kituo cha Afya Farkwa kimekamilika lakini hakina wataalam ili kianze kufanya kazi. Je, ni lini Serikali italeta wataalam ili kianze kufanya kazi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Monni, kwani amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na upatikanaji wa watumishi katika vituo vyake na Hospitali ya Halmashauri. Naomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba na Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma kuhakikisha wanafanya *internal reallocation* ya mtaalam wa maabara angalau mmoja ili apelekwe haraka iwezekanavyo katika hospitali hii ya Halmashauri ambayo Mheshimiwa Mbunge anasema haina mtaalam wa maabara ili aanze kutoa huduma wakati tunasubiri vibali vya ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusiana na wataalam kukosekana katika kituo hicho cha Farkwa, naomba nimhakikishie kwamba tunaendelea kuajiri wataalam. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa kibali. Kwa hiyo, itakapofika hatua ya kuajiri tutahakikisha kuwa tunapeleka watumishi kwenye kituo hicho ili kianze huduma kwa wananchi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Nollo uliza swali lako.

Na. 390

**Kukamilika kwa Zoezi la Kuhamia Dodoma**

**MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini zoezi la kuhamia Dodoma litakamilika na Taasisi ngapi zimeshahamia Dodoma?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma lilianza rasmi mnamo mwaka 2016. Hadi sasa jumla ya watumishi 25,039 kutoka Serikali Kuu, Bunge, Mahakama, vyombo vya ulinzi na usalama, pamoja na taasisi 65 wameshahamia Dodoma na wanaendelea kutekeleza majukumu yao wakiwa Makao Makuu ya Nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatarajia kukamilisha mpango wake wa kuhamia Makao Makuu ya Nchi, Dodoma kwa kuzingatia mpango kazi maalum na ujenzi wa awamu ya pili wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi utakaohitimishwa ifikapo mwaka 2025.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini vile vile nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kusimamia vyema zoezi hili la Serikali kuhamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, pamoja na kwamba taasisi 65 zimeshahamia hapa Dodoma, lakini mwisho kabisa wa taasisi zote kuhamia Dodoma ni lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; Makao Makuu ya Nchi ambako viongozi wengi wa Serikali wanafanya kazi ni lazima kuwe na makazi yao rasmi. Je, ujenzi wa makazi rasmi ya viongozi wa Serikali utaanza lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU (MHE. UMMY H. NDERIANANGA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea pongezi hizo za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utekelezaji mzuri wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini mwisho wa taasisi za Serikali kuhamia Dodoma, kama nilivyojibu katika swali la msingi la Mheshimiwa Kenneth Nollo kwamba tunaendelea na uchambuzi. Taarifa itakapokamilika, tutawaambia ni taasisi ngapi zimeshahamia na ngapi zimebaki. Tunatarajia mwaka 2025 taasisi zote ziwe zimeshahamia Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikijibu swali lake la pili, kwanza naendelea kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri. Nimhakikishie kwamba Serikali ilianza ujenzi wa nyumba za viongozi kuanzia mwaka 2021/2022. Kupitia Wakala wa Majengo *(TBA)* tulijenga nyumba 20 na Septemba, 2023 nyumba 150 za watumishi zilizinduliwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tuko kwenye zoezi la kupanga eneo ambalo tumelitwaa kwa ajili ya kujenga nyumba za viongozi wa Serikali na watumishi. Sasa hivi tuko kwenye hatua ya kujipanga kwa kupitia hao wenzetu wa *TBA* watuainishie vizuri, na tutakuwa na ekari 4,654. Tumetwaa eneo kati ya Mji wa Serikali Mtumba na Ikulu hapo kwa ajili ya kujenga nyumba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwahakikishie Watanzania kuwa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tunaendelea vizuri na uendelezaji wa Mji wa Serikali Mtumba na kila jambo linaendelea vizuri. Kwa hiyo, niwatoe mashaka na niwakaribishe sekta binafsi, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Mbunge ameshakukuelewa. Tunaendelea, Mheshimiwa Luhanga Nelson Mpina kwa niaba Mheshimiwa Flatey, uliza swali.

Na. 392

**Kujenga Zahanati kila Kijiji Nchini**

**MHE. FLATEY G. MASSAY K.n.y. MHE. LUHAGA J. MPINA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga zahanati katika kila kijiji nchini ili kusogeza huduma za afya kwa Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi, Serikali inaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi, ambapo katika kipindi cha mwaka 2020/2021 hadi 2022/2023, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 89.9 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 1,798 ya zahanati kote nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni 18.8 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 376 ya zahanati kote nchini. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya shilingi bilioni 18.76 zimeshatolewa. Mpango wa Serikali wa ujenzi wa zahanati katika vijiji ni endelevu. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Flatey.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika Jimbo la Kisesa zipo zahanati na nguvu za wananchi zimetumika, je, lini mnamalizia zahanati zilizobaki katika Jimbo la Kisesa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Jimbo la Mbulu Vijijini pia kuna zahanati 13 wananchi wameshajenga na ziko kwenye hatua mbalimbali. Je, ni lini mnapeleka fedha ili Jimbo la Mbulu Vijijini tukapate huduma hiyo ya afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tumeshafanya *mapping* ya zahanati zote ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi katika halmashauri zote 184. Serikali imeendelea kutenga fedha na kupeleka fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma. Ndiyo maana katika mwaka huu wa fedha 2023/2024 mpaka Machi, tayari fedha zote 100%, shilingi bilioni 18.8 zimeshapelekwa na zahanati zinaendelea kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba hizo zahanati za Jimbo la Kisesa na zahanati za Jimbo la Mbulu Vijijini ni sehemu ya kipaumbele na tutaendelea kupeleka fedha ili ziweze kukamilishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Galapo Jimbo la Babati Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa bahati njema nilishafanya ziara katika Kituo cha Afya cha Galapo na tulifanya mkutano wa hadhara tukiwa pamoja na Mbunge wa Jimbo, na tayari kituo kile kimeingizwa kwenye mpango wa Benki ya Dunia kwa ajili ya kujengwa. Wakati wowote tunatarajia fedha ikitoka tutakwenda kuanza ujenzi Galapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilave.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 tuliambiwa Wabunge wengi hapa tuandike vipaumbele vya zahanati mbili mbili kila jimbo na sisi tuliweza kuandika zahanati hizo. Je, ni lini Serikali itaweza kujenga zahanati hizi katika majimbo yetu, hasa Jimbo la Temeke Kata 14 na Sandali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tulishaleta hapa fomu za kujaza kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya; kimoja kila jimbo, lakini tulishaainisha pia zahanati ambazo zinahitaji kukamilishwa katika kila jimbo. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kazi hii inaendelea na kila mwaka wa fedha tutaendelea kutenga fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka ya fedha yote mitatu au minne iliyopita Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 89.9 na zahanati zaidi 1,798 zimekamilishwa. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba zoezi hili linaendelea na tutahakikisha tunaendelea kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango gani wa kupandisha hadhi zahanati ambazo zimekidhi vigezo kuwa vituo vya afya katika Jimbo la Mbagala?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, zahanati ambazo zimekidhi vigezo vya kuwa vituo vya afya tumeshaelekeza halmashauri, kwa maana ya Mganga Mkuu wa Halmashauri, Mkurugenzi kupitia kwa Katibu Tawala wa Mkoa kuleta maombi maalum Ofisi ya Rais, TAMISEMI ili na sisi tuweze kuwasiliana na Wizara ya Afya na kusajili na kupandisha hadhi ikiwa vinakidhi kwa miundombinu na *population*. Kwa hiyo,

naomba nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke kufuata utaratibu huo mapema iwezekanavyo ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Jacqueline Kainja, uliza swali lako.

Na. 393

**Kujenga Uzio Shule za Bweni za Wasichana Urambo**

**MHE. JACQUELINE K. ANDREW** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kujenga uzio kwenye Shule zote za Bweni za Wasichana Wilayani Urambo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uzio kwenye shule za bweni za wasichana nchini kwa ajili ya usalama wa mali na wanafunzi zikiwemo shule za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo. Aidha, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni ujenzi wa miundombinu ya msingi inayowezesha wanafunzi wote kupata fursa ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Serikali itapeleka shilingi bilioni 2.4 katika Jimbo la Urambo kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali yakiwemo madarasa 16, mabweni nane na matundu ya vyoo 20 katika shule mbili za sekondari mpya za kata katika Kata ya Nsenda Kijiji cha Mtakuja na Kata ya Ukandamoyo Kijiji cha Tumaini. Aidha, kwa mwaka 2024/2025 zimetengwa jumla ya shilingi milioni 110 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya walimu *(two in one)* ambayo itajengwa katika Kata ya Uyogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, itaendelea kutenga na kupeleka fedha kwa ajili ya

ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari kulingana na vipaumbele vyake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jacqueline.

**MHE. JACQUELINE K. ANDREA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nimeuliza maswali kuhusu uzio wa shule za mabweni za wasichana. Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa pamoja kwa ajili ya ujenzi wa majengo, madarasa pamoja na mabweni ili ziende sambamba na uzio wa shule hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; mwaka 2023 Shule ya Sekondari ya Uyungu, Kidato cha Sita walivamiwa na vibaka. Je, hawaoni sababu ya kuweka uzio katika shule hizo ambazo ni Shule ya Margaret Simwanza Sitta pamoja na Shule ya Sekondari ya Urambo Day?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge, amekuwa ni mtetezi mkubwa sana wa mazingira ya wanafunzi kwa kuhakikisha wanasoma katika mazingira yaliyo mazuri, bora na yenye usalama zaidi. Naomba nijibu maswali yake yote mawili kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa miundombinu ikiwemo hiyo ya uzio. Kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi, kwamba Serikali imeweka kipaumbele zaidi katika ujenzi wa miundombinu ya msingi ambayo inawawezesha wanafunzi wote kupata fursa ya elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa uzio katika shule zetu hizi, naomba nimkumbushe Mkurugenzi wa Halmashauri afanye tathmini na kuweka katika mipango ya kibajeti katika halmashauri inayotokana na mapato ya ndani ili

kuona kwa kadiri fedha zitakapokuwa zinapatikana waweze kujenga uzio huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Je, ni lini Serikali itajenga uzio kwenye Sekondari ya Mlongwema, Ubiri pamoja na Shambalai?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nirejee majibu yangu ya awali kwamba, miradi ya Serikali Kuu ni miradi ambayo ni *complimentary,* lakini halmashauri zenyewe zina wajibu wa kuhakikisha kwamba na zenyewe zinakuwa ni sehemu ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza miundombinu hii muhimu. Kwa hiyo, nitumie nafasi hii kumkumbusha Mkurugenzi aweze kufanya tathmini na kuweka katika mipango ya kibajeti ili fedha kadiri zitakapokuwa zinapatikana waweze kujenga uzio katika shule aliyoitaja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo, Mheshimiwa Yustina Rahhi.

Na. 394

**Idadi ya Mbwa Nchini**

**MHE. YUSTINA A. RAHHI** aliuliza: -

Je, kuna mbwa wangapi nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya sampuli ya Sensa ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu *(NBS)* mwaka 2020, nchi yetu ilikadiriwa kuwa na mbwa

2,776,918. Aidha, kupitia taarifa hiyo mikoa iliyoongoza kwa mbwa wengi ni Geita 302,879, Mwanza 287,270 na Tabora 243,768.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu katika kuhakikisha takwimu sahihi za mifugo ikiwemo mbwa zinapatikana kwa wakati ili kuwezesha mipango ya Serikali ya kuendeleza Sekta ya Mifugo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rahhi, swali la nyongeza.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na pia naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la kwanza; ugonjwa wa kichaa cha mbwa ni changamoto kubwa hasa kwa jamii ya wafugaji walioko vijijini na matibabu yake ni shida kwa sababu katika zahanati na vituo vya afya, matibabu hayo hayapatikani. Kwa hiyo, takribani Watanzania 1,500 hupoteza maisha kila mwaka. Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti kabisa kichaa cha mbwa katika nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; namna pekee ambayo Serikali inadhibiti mbwa wazururaji ni kuwapiga risasi na kukiuka haki za wanyama. Kutokana na idadi hii kubwa ya mbwa, hivi nchi yetu haijafikiria kufanya uchumi wa mbwa ikiwa ni pamoja na kuwafundisha na kuuza ndani na nje ya nchi hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hili la kwanza kwamba anataka kujua mkakati wa Serikali kwenye kudhibiti kichaa cha mbwa, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni kwamba Serikali imesharuhusu wadau mbalimbali kutoa chanjo kupitia sekta binafsi na dawa ya kwanza ya kichaa cha mbwa ni kumchanja mbwa mwenyewe. Tusisubiri mpaka mbwa augue kichaa cha mbwa ndiyo achanjwe kwa sababu mbwa akishakuwa ameugua, matibabu yake huwa ni magumu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nitoe rai kwa wadau wote kuendelea kuchanja mifugo yetu aina ya mbwa ili kudhibiti kichaa cha mbwa kwa sababu hakuna mbadala mwingine tofauti na hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba mbwa wote walioko ndani ya Taifa letu wanaendelea kuchanjwa kwa wakati kama ambavyo tumekuwa tukifanya huko nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hili la pili, anataka kujua ni mkakati gani wa kudhibiti mbwa wanaozagaa mtaani? Mbwa anapokuwa ameshaumwa kichaa kudhibiti kwake ni pamoja na kuchukua hatua ngumu kidogo, hatua zenyewe ni pamoja na kumwondoa hapa duniani. Kwa hiyo, hatuna mbadala mwingine wa kuendelea kuishi na mbwa ambaye ameshachanganyikiwa. Katika hali hiyo, Serikali hutoa vibali vya kumwondoa mbwa hapa duniani, lakini tupo tayari kuendelea kuzungumza na Mheshimiwa Mbunge atupe *alternative* pengine ya mawazo yake jinsi ambavyo Serikali inaweza ikashirikiana naye na nimhakikishie kwamba tuko tayari kushirikiana naye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante, ameshakuelewa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Mheshimiwa Manyanya hayupo, kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Ntara.

Na. 395

**Serikali Kuipatia Gari Ruwasa Wilaya ya Nyasa**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA K.n.y. MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka gari RUWASA Wilaya ya Nyasa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Jimbo la Nyasa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* inaendelea kutatua changamoto za uhaba wa vitendea kazi ikiwemo magari katika mikoa 25 na Wilaya 128 Tanzania Bara zinazohudumiwa na Taasisi hiyo. Katika kutekeleza azma hiyo, RUWASA katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeshalipia ununuzi wa magari mapya 35 na yanatarajiwa kupokelewa hivi karibuni kwa ajili ya kusambazwa kwenye mikoa na wilaya zenye uhitaji nchini ikiwemo Wilaya ya Nyasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Nyasa ni miongoni mwa Wilaya ambazo zina changamoto kubwa sana kutokana na ukubwa wa jiografia yake lakini pia hata maumbile yake, milima, mabonde na barabara nyingine ni mbaya za vumbi. Kwa hiyo, unakuta miradi mingi ya maji haikaguliwi vizuri kutokana na kutokuwa na gari. Je, Mheshimiwa Waziri haya majibu yako ya leo yatakuwa ni ya ukweli? Kwa sababu hata mwaka juzi ulinijibu hivyo hivyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kutokana na changamoto hizo na ucheleweshaji mkubwa wa kuagiza magari, ni namna gani mtafanya huduma ya haraka hasa katika maeneo hayo ambayo yanachangamoto kubwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu haya ya Serikali ni majibu ya kweli, lakini ni kweli kabisa kwamba vitendea kazi vimechelewa na kwa sababu ya utaratibu wa mchakato wa manunuzi sisi kama

Wizara, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa kiasi cha shilingi bilioni 6.14 kwa ajili ya ununuzi wa hayo magari 35 lakini yakiwa yanazingatia mahitaji ya maeneo mbalimbali na jiografia ya maeneo mbalimbali na ndiyo maana tuna magari aina ya *Hardtop,* tuna *Double Cabin*, na pia tuna *Nissan* ambayo yanaenda kugawanywa kulingana na hali halisi ya maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile, majibu ya swali la pili, Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan ina azma ya kuhakikisha kwamba ina harakisha upatikanaji wa miundombinu safi ili kuweza kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Hivyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, na ni kweli kabisa amekuwa akiongelea changamoto hii. Sisi kama Serikali tunaendelea kuipokea lakini pia Serikali ina mkakati wa kuhakikisha kwamba miradi ambayo imechelewa kukamilika tunaenda kuikamilisha ili wananchi wapate huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Kilumbe Shabani uliza swali lako.

Na. 396

**Ukarabati wa Reli ya Kati**

**MHE. KILUMBE S. NG`ENDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ukarabati wa Reli ya Kati kwa kuwa miundombinu yake ni chakavu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia *TRC* inaendelea na ukarabati wa miundombinu ya njia ya reli iliyopo ambapo hadi sasa imekamilisha ukarabati wa njia ya reli kipande cha Dar es Salaam – Isaka ya Kilometa 970 kupitia mradi wa Tanzania *Intermodal Rail Project (TIRP)*. Halikadhalika, *TRC* imesaini mkataba

wa ukarabati wa njia ya reli ya kati kwa kipande cha Tabora – Kigoma yenye urefu ya kilometa 411 tarehe 23 Juni, 2023 na Kaliua – Mpanda ya kilometa 210 tarehe 26 Novemba, 2022. Kazi ya ukarabati inaendelea, na kwa upande wa Tabora – Kigoma ya kilometa 411 inatarajia kukamilika baada ya miezi 54 na Kaliua – Mpanda inatarajia kukamilika mwezi Mei, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo *TRC* imesaini mkataba wa ununuzi wa malighafi za ukarabati wa reli (mataruma na vifungio) kwa ajili ya ukarabati wa njia ya reli ya Kaskazini ikijumuisha kipande cha *Ruvu – Mruazi Junction.*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Moja ni kwamba, tangu mkataba wa ukarabati umefanywa mwaka 2023 mpaka leo kipande cha Tabora - Kigoma chenye urefu wa kilometa 411 hakuna kazi yoyote mpaka sasa inayoendelea. Haijafanyika kazi yoyote na bajeti ya mwaka 2023 na mwaka 2022 mmekuwa mkitenga fedha kwa ajili ya ukarabati na hakuna kazi inayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kwamba, mliongeza mabehewa katika reli hiyo ili kuongeza safari za *train* kutoka tatu kwa wiki mpaka nne kwa wiki, na mpaka leo bado safari ni tatu na mabehewa yaliyoongezeka yapo na ya ukarabati yapo lakini hakuna kinachoendelea. Nini mpango wa Serikali kwenye jambo hili?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda kwa kukubali majibu ya Serikali ambayo tumeyatoa na kimsingi katika swali lake la kwanza la nyongeza anaweka mkazo kwamba dhamira hii ya Serikali ambayo imeonekana inafaa mpaka tumefika hatua ya kupitisha na hatimaye kusaini mkataba pengine angependa kuona ianze mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri huu na tunaendelea kujipanga kuhakikisha katika muda ambao tumeusema, basi ukarabati huu tunauanza mara moja kwa ajili ya kusaidia wanakigoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inakwenda sambamba na kwenda kutazama hii habari ya *route* ambayo amezungumza pamoja na kuongeza mabehewa, lakini bado hatujaanza *route,* tumelipokea, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kanyasu.

Na. 397

**Ukomo wa Kuweka Alama za Upana wa Barabara**

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, upi ukomo wa kuweka alama za upana wa Barabara Vijijini na kuwataka Wananchi kubomoa nyumba kutumia Sheria ya Mwaka 1932 na 2007?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sheria ya Barabara Na. 40 ya Mwaka 1932, hifadhi ya barabara zinazosimamiwa na *TANROADS* ilikuwa mita 22.5 kutoka katikati ya barabara kila upande isipokuwa kwa barabara ya Morogoro ambao hifadhi yake ilikuwa kati ya mita 22.5 hadi 121.9 kuanzia *Dar es Salaam City Hall* hadi Daraja la Ruvu. *TANROADS* imeweka alama ya 'X' ya rangi nyekundu kwa mali za wananchi zilizopo ndani ya mita 22.5 na kuwataka wananchi waondoe mali hizo kwa gharama zao wenyewe kwa kuwa wamevamia eneo la hifadhi ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007 iliongeza hifadhi ya barabara zinazosimamiwa na

*TANROADS* kutoka mita 22.5 kuwa mita 30 kutoka katikati ya barabara kila upande. Katika kutekeleza Sheria hii, *TANROADS* imeweka alama ya 'X' za rangi ya kijani kuonesha eneo la mita 7.5 liliongezeka kila upande ambapo wananchi waliopo katika eneo hili hawapaswi kuondoa mali zao mpaka watakapolipwa fidia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru pia Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, zimekuwepo barabara ambazo vikao vya Mikoa *RCC* pamoja na halmashauri tunaomba wenyewe kuzipandisha hadhi kutoka kwenye barabara za *TARURA* kwenda kwenye barabara za *TANROAD,* lakini awali barabara hizo zilikuwa za vijijini. Kwa nini sheria ile ile ambayo inatumika kwenye barabara za *TANROAD* hiyo ya mwaka 32 na hii nyingine inaendelea kutumika kwenye maeneo mapya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; natambua uwepo wa hizi sheria na kwamba *TANROAD* wamekuwa wakiweka alama kwenye nyumba za wananchi, lakini wanaweka alama leo kabla hawaja-*plan* kujenga barabara na matokeo yake nyumba za wananchi zinaharibika na hawawezi kuziendeleza. Ni upi ukomo wa Wizara kuweka alama hizi ili kuruhusu wananchi kutumia haki yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema tunatumia sheria zilizowekwa za *TANROADS* kwa maana ya barabara ambazo zinapandishwa hadhi. Hata hivyo, maeneo mengi kama barabara imepandishwa hadhi, tunajiridhisha upana wake ili wananchi ambao walikuwa katika maeneo ya barabara ambao walikuwa nje ya barabara, basi wanakuwa wanastahili kulipwa

kwa sababu walikuwa kwenye barabara ambazo zilikuwa zinahudumiwa kulingana na sheria ambayo ilikuwa inaelekeza barabara ya upana ambao uko *TARURA*. Labda kama kuna changamoto *specific,* naomba Mheshimiwa Mbunge aweze kuonana nami ili tuweze kujua changamoto iko wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, tunaweka alama baada ya barabara hiyo hasa kuwa imefanyiwa usanifu ili wananchi wasiendelee kufanya maendelezo kwenye maeneo ambayo tayari ni hifadhi ili kuachana na ile kuja kubomoa tena mali ambazo tayari watakuwa wanajua ni hifadhi ya Barabara, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kuna ujenzi wa barabara ya lami kwenye Mji wetu wa Kalumwa, na tayari kuna vigingi upande wa kushoto na kulia mita 30, na lami hii ina upana takribani mita nane, wananchi hawa wanashindwa kubomoa au kuendeleza kujenga zile nyumba zao. Serikali ina mpango gani wa kupunguza vigingi hivyo ili mji ule uendelee kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara zote ambazo ni za *TANROADS* zinalindwa na Sheria ya Mwaka 2007 ambayo upana wake ni mita 30 na hata kama itatumika mita saba lakini maana yake ni kwamba ile hifadhi ya barabara itaendelea kulindwa na itakuja kutumika pale itakapohitajika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE.ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sheria hii ya mwaka 1932 ndiyo iliyotumika kuvunja makazi kwa ajili ya upanuzi wa barabara njia nane kuanzia Kimara mpaka Kibaha, na wananchi bado wanaendelea na sintofahamu juu ya

uhalali huo wa kuvunjiwa: Je, Serikali iko tayari kutoa maelekezo kwa Mamlaka za Wilaya na Mkoa kutoa majibu rasmi kwa wananchi ili wasiendelee kufuatilia kwenye Ofisi za Mbunge? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba hii Sheria ya Mwaka 1932 na hasa kwa barabara ya kuanzia Dar es Salaam hadi Ruvu kulikuwa na maeneo ambayo ni mita 22.5 lakini kuna maeneo ambayo ilikuwa ni mpaka mita 121. Kwa hiyo, niseme tu ni sheria iliyotumika na wananchi wa maeneo husika hasa katika Kijimbo la Kibamba wanatakiwa waelewe kwamba Serikali ilitumia sheria hiyo ya mwaka 1932.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Ng'wasi, uliza swali lako.

Na. 398

**Ujenzi wa Barabara za *Flyover* Mwanza**

**MHE. NG'WASI D. KAMANI** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia hatua gani katika ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya barabara katika Jiji la Mwanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Mwanza, Serikali tayari imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya juu katika makutano ya Buzuruga yaliyoko katika barabara ya Mwanza Mjini hadi Nyanguge yenye urefu wa kilomita 35. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ng'wasi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru sana Serikali kwa majibu yake mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa Mkoa wa Mwanza umethibitika kuwa ndiyo mkoa ambao ni wa pili kwa idadi kubwa ya watu katika nchi yetu kwa sasa, na kwa kuwa tayari barabara hizi zimeshakuwa na *jam* kubwa inayozuia shughuli za maendeleo kufanyika kwa wakati: Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati wa kutenga fedha katika bajeti hii ya mwaka unafuata ili kutengeneza barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; ni nini mpango wa Serikali wa kujenga barabara nne katika Barabara ya Usagara – Buhongwa - Mkolani kuja katika Jiji la Mwanza na katika zile barabara za makutano ya pale Kenyatta ili pia kupunguza msongamano katika barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyojibu katika jibu la msingi, ni kweli Mji wa Mwanza sasa hivi una msongamano mkubwa wa magari na ndiyo maana Serikali tayari tumeshakamilisha usanifu kwa ajili ya kuweka *flyover* katika eneo la Buzuruga. Kwa hiyo, Serikali inatafuta fedha kuhakikisha kwamba inajenga *flyover*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kupunguza msongamano katika Jiji la Mwanza, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pia tumeshakamilisha usanifu kutoka katikati ya Jiji la Mwanza kwenda Usagara na vile vile kutoka katikati ya Jiji kwenda Nyanguge ili ziwe njia nne ikiwa ni lengo la kupunguza foleni katika Jiji la Mwanza, na tayari tumeshakamilisha usanifu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Wilayani Chunya kuna barabara ya muhimu

sana inayotoka Makongorosi kwenda Rungwa. Je, ni lini Serikali itaanza kuijenga barabara hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli barabara hii ni muhimu ambayo inaunganisha mikoa ya nyanda za juu na kaskazini. Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba barabara hii ijengwe yote ya kuanzia Makongorosi - Rungwa hadi Itigi, na pia Makongorosi – Rungwa na kwenda Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi tuko kwenye maandalizi ya kutafuta fedha na tusubiri pia bajeti itakayokuja. Nini tutakuwa tumefanya? Tumetenga kuanza ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Stella Fiyao.

Na. 399

**Ujenzi wa Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, hadi sasa ni kilometa ngapi zimejengwa kwa kiwango cha lami Barabara ya Mbalizi - Mkwajuni?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara ya Mbalizi – Mkwajuni yenye urefu wa kilometa 92 ni sehemu ya barabara ya Mbalizi – Chang’ombe – Mkwajuni, Mkwajuni hadi Makongolosi yenye urefu wa kilometa115 inayounganisha Mkoa wa Mbeya na

Songwe. Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hii unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa 10.4 zimejengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, taratibu za manunuzi ya Mkandarasi kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa kilometa tano katika Mji wa Mkwajuni Mkoani Songwe na kilometa 3.5 kwa upande wa Mkoa wa Mbeya zinaendelea, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kutokana na umuhimu wa barabara hii hasa ukizingatia kwamba ina mchango mkubwa sana katika pato la Mkoa wa Songwe, Mbeya na nchi kwa ujumla, nataka kujua ni lini kilometa zote 115 zitakamilika?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; nataka kujua mpango na hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa barabara inayotoka Mlowo – Isansa – Magamba mpaka Mkwajuni ili kurahisisha huduma kwa wananchi wa Wilaya ya Songwe hasa wanapohitaji huduma mkoani? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Swali alilouliza Mheshimiwa Mbunge linafanana sana na alilouliza Mheshimiwa Fyandomo, ni barabara ambayo inaunganisha. Ukifika Makongolosi unaenda Mkwajuni, kisha unaenda Mbalizi na tayari tumeshaanza hiyo barabara. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nimesema, tumeshaanza kwa hatua, ingawa lengo ni kuijenga barabara yote. Kwa hiyo, kadiri tunavyopata fedha, tutahakikisha tunaikamilisha barabara yote kwa kuunganisha hiyo mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali lake la pili, tayari tunaendelea kufanya usanifu kwenye hii barabara ya pili aliyoitaja, lakini kuna maeneo ambayo ni ya *TARURA* na

tunashirikiana nao ili kuunganisha Mkoa wa Songwe na Wilaya ya Songwe yenyewe bila kupita Mkoa wa Mbeya. Kwa hiyo, ni moja ya wazo kubwa na mapendekezo ya Mkoa wa Songwe kuhakikisha kuwa tunauunga Mkoa wa Songwe na Wilaya yake ya Songwe, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Oran, halafu Mheshimiwa Prof. Ndakidemi jiandae.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi kwa kiwango cha lami Barabara ya Mbalizi – Shigamba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ya Mbalizi – Shigamba ambayo inaunganisha Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya, kwa maana ya Wilaya ya Mbeya na Wilaya ya Ileje, iko kwenye hatua za manunuzi. Tutaijenga kwa awamu, lakini lengo ni kuunganisha Mbalizi – Shigamba na Itumba – Ileje. Kwa hiyo, tayari tuko kwenye hatua za manunuzi, kwa maana ya hatua za kwanza za barabara kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Barabara ya Uru - Mamboleo na Materuni hupeleka watalii *Materuni Water Falls*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuikamilisha barabara hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii *TANROADS* Mkoa wa Kilimanjaro wanaihudumia, lakini fedha tunapata kutoka kwa wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hata hivyo, kwa sababu ya umuhimu wake Serikali iliamua *TANROADS* wawe wanaijenga. Kwa hiyo, tunawasiliana na wenzetu wa *TARURA,* ili waweze kutupatia fedha

tuijenge. Pia, sasa hivi ipo kwenye mpango wa kuiendeleza, ili kuikamilisha yote kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justine.

**MHE. JUSTINE L NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa barabara ya kutoka Ipogolo hadi Kilolo inajengwa. Je, Serikali haioni umuhimu wa kuiunganisha barabara hiyo pale Kilolo kwenda Kibaoni – Kitowo ili iweze kutoka kwenye Wilaya ya Iringa Vijijini kwa sababu ya umuhimu wake, kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tunajenga kwa kiwango cha lami kilometa 33 ambazo tayari Mkandarasi yuko *site*. Lengo ni kuhakikisha kwamba, tunaendelea kwa kadiri fedha zinavyopatikana kuweza kuiunganisha Kilolo na Iringa Vijijini. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge avute subira, kadiri fedha inavyopatikana barabara hiyo tutaijenga kwa kiwango cha lami.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani. Mheshimiwa Kabati.

Na. 400

**Hitaji la Ofisi ya Polisi – Wilaya ya Kilolo**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Polisi ya Wilaya ya Kilolo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilolo na uko kwenye hatua ya umaliziaji.

Mnamo tarehe 7 Februari, 2024 Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 400, kwa ajili ya kumalizia ujenzi huo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa Ofisi hiyo kwa sababu, zaidi ya miaka 12 tumekuwa tukifuatilia ujenzi wa Ofisi ya Polisi, Kilolo. Nina maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, askari karibu wote wa Wilaya ya Kilolo wamekuwa wakiishi uraiani kwa bei tofauti tofauti za pango: Je, ni lini sasa Serikali itakuwa na Mpango wa kuwajengea makazi askari hao, ili kuondoa changamoto hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Kwa kuwa, Vituo vya Polisi vya Mtitu, Ruaha Mbuyuni, Nyalumbu na Boma la Ng'ombe ni vituo vinavyohitaji ukarabati mkubwa: Je, ni lini Serikali itatenga Bajeti ili viweze kukarabatiwa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tunatambua uhaba wa Nyumba za Makazi ya Askari katika maeneo mbalimbali, ikiwepo Wilaya ya Kilolo. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutatenga fedha kwa jinsi ya upataikanaji wake, kwa ajili ya kujenga Nyumba za Askari wetu wa Wilaya ya Kilolo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali la pili la ukarabati wa Vituo vya Polisi alivyovitaja, namhakikishia kwamba vitaingia kwenye mpango. Hata hivyo, naagiza Jeshi la Polisi kufanya tathmini ili kujua kiasi cha fedha kinachotakiwa ili tuweze kufanya ukarabati wa vituo hivyo. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Butondo.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali. Ofisi ya *OCD* Wilaya ya Kishapu imejengwa kwa nguvu za wananchi pamoja na wadau wa maendeleo, ukiwepo Mgodi wa Mwadui, mpaka kufikia katika hatua ya upauaji. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri alifika na kuahidi kwamba, watahakikisha wanatoa shilingi milioni 271, kwa ajili ya kukamilisha mradi huo...

**NAIBU SPIKA:** Uliza swali.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** ...Mradi huo wa Kituo cha Polisi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Butondo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawapongeza wananchi wa jimbo lake kwa kazi kubwa walioifanya ya kujenga Kituo cha Polisi hadi hatua ya *linter*. Pia, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itatenga fedha kama alivyoahidi Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ajili ya kumalizia kituo hicho kilichojengwa kwa nguvu za wananchi, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Kilindi ilipatikana mwaka 2002, lakini toka mwaka 2015 nimeingia hapa Bungeni, nimekuwa nikiomba Kituo cha Polisi cha Wilaya. Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi cha Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua Wilaya ya Kilindi ni Wilaya kubwa na ni kweli haina kituo cha Polisi cha Wilaya. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatenga fedha kwa mwaka wa fedha unaokuja 2025/2026, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kilindi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** *Advocate*.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Wananchi wa Lengatei, Magungu na Chekanao wameshaanzisha Vituo vya Polisi. Lini Serikali itawasaidia kumalizia vituo hivyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Lekaita, Mbunge wa Kiteto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kuwa wananchi wameshaanza kazi nzuri ya ujenzi wa Vituo vya Polisi kwenye maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Serikali yetu kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa inamalizia Vituo vya Polisi ambavyo ni maboma 77 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na ujenzi wa vituo vipya 12. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa vituo vyako pia viko kwenye mpango kwa ajili ya kumaliziwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Vituo vingi vya Polisi nchini vimechakaa na vingine havitamaniki kabisa. Ningependa kufahamu, nini mkakati wa Serikali wa pamoja kuhakikisha vituo hivyo vinakarabatiwa, kwa maana ya nchi nzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lambert, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kwamba, kuna Vituo vingi vya Polisi ambavyo ni chakavu na ni vya muda mrefu. Hata hivyo, katika hali ya kawaida huwezi kujenga vyote kwa pamoja. Kwa hiyo, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kila awamu tutatenga fedha kwenye bajeti ili kuhakikisha tunavikarabati awamu kwa awamu na mwisho wa siku tutavimaliza vyote.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tunaendelea na Wizara ya Elimu, Mheshimiwa Michael Mwakamo uliza swali lako.

Na. 401

**Hitaji la Ujenzi wa Vyuo vya Ufundi kwenye Halmashauri zote Nchini**

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO** aliuliza:-

Je, Serikali haioni haja ya kuanzisha vyuo vya mafunzo katika fani za kilimo, mifugo na ufundi ili kuwawezesha vijana kupata elimu ya ufundi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ili kutoa mafunzo kwa wananchi kwa lengo la kuwapatia ujuzi utakaowawezesha kutekeleza shughuli zao mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, mifugo pamoja na shughuli nyingine kulingana na fursa zinazopatikana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza azma hiyo, Serikali kwa sasa inaendelea kutekeleza Mpango wa Kujenga Chuo cha Ufundi Stadi katika kila Mkoa na Wilaya ambazo zilikuwa

hazijajengewa Vyuo vya Ufundi Stadi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilitenga kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya kujenga Vyuo vya Ufundi Stadi katika Wilaya 64, pamoja na Chuo cha *VETA* cha Mkoa wa Songwe. Ujenzi wa vyuo hivi unaendelea kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo yatakayokuwa yanatolewa na vyuo hivi yamezingatia shughuli za kiuchumi katika maeneo husika ikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji wa madini, utalii pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakamo.

**MHE. MICHAEL C. MWAKAMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Nafahamu kwamba kwenye Sera ya Elimu ya *VETA*, chuo kinajengwa kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Kwa kuwa Jimbo la Kibaha Vijijini ni moja ya jimbo lililopo kwenye Wilaya yenye majimbo mawili, nataka nijue: Je, Serikali haioni sasa ni muda sahihi wa kutujengea Shule ya Sekondari ya Elimu Amali, ili kuendana na mbadala wa Chuo cha *VETA*?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa, nimeshaandika barua na nimefanya mawasiliano na Wizara ya Elimu mara nyingi na katika Bajeti ya Serikali ya 2023/2024, Waziri ametangaza uwepo wa shule 26 za elimu ya amali. Je, Waziri haoni sasa ni muda sahihi wa kumwagiza Mkurugenzi ili aandae eneo kwa ajili ya kunipatia shule moja kati ya hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakamo, Mbunge wa Kibaha Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli katika Sera yetu mpya iliyoboreshwa, Toleo la 23, ile Sera ya 2014, upo Mchepuo wa Amali. Pia ili kutekeleza azma hii au mtaala huu Serikali imeazimia

kujenga shule 100 katika majimbo ambayo yalikuwa hayana Vyuo vya *VETA*. Kwa hiyo, namwondoa wasiwasi Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli alifika ofisini mara kadhaa na kuonana na Katibu Mkuu na pia, ni kweli kabisa aliandika hiyo barua. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, miongoni mwa utekelezaji wa shule hizi 100, Shule 26 zinaanza katika mwaka huu wa fedha 2023/2024. Kwa hiyo, namwondoa wasiwasi, yupo katika mpango wa zile shule 26 na tutaanza kutekeleza hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili. Ni kwa vile tayari yumo katika mpango wa zile shule 26 zinazoanza, basi naomba sasa nichukue fursa hii niweze kumwagiza Mkurugenzi, kwa kushirikiana na Mheshimiwa Mbunge waweze kutenga eneo ili tuweze kwenda kulifanyia ukaguzi na ujenzi huu uweze kuanza mara moja pale Kibaha Vijijini. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga Shule Maalumu ya Ufundi niliyoiomba katika Kata ya Kisawasawa, Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nijibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Asenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu kwenye maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mwakamo, Serikali ina mpango wa kujenga zile shule 100 kwenye majimbo yote ambayo yalikuwa hayana Vyuo vya *VETA*. Miongoni mwa majimbo hayo ni Jimbo la Mheshimiwa Asenga kule Ifakara. Namwondoa wasiwasi, yeye shule yake iko katika mpango ule wa pili wa mwaka 2024/2025. Kwa hiyo, tutaanza kutekeleza kunako Julai, Mosi, 2024. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Mkenge.

Na. 402

**Mkakati wa Kufufua Zao la Nazi – Bagamoyo**

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kufufua zao la nazi katika Ukanda wa Pwani hususan Bagamoyo ili kuleta tija kwa wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mikakati iliyopo sasa katika kufufua zao la nazi ni Wizara kupitia Kituo cha Utafiti cha *TARI* Mikocheni, imeanza kutekeleza mpango wa awamu ya kwanza wa kuzalisha miche bora ya nazi, ambapo hadi sasa miche 140,000 imezalishwa na itasambazwa kwa wakulima kabla ya Desemba, 2024. Aidha, utekelezaji wa mpango huo unahusisha wadau wenye teknolojia za kisasa za uzalishaji wa nazi, ikiwemo Kampuni ya *Deejay Coconut Farm* ya Nchini India ambayo imeonesha nia ya kuingia makubaliano ya ushirikiano na *TARI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia Msimu wa 2024/2025 Wizara kwa kushirikiana na wabia wa maendeleo itaendelea na programu ya uzalishaji wa miche bora kutoa mafunzo ya kilimo bora cha nazi kwa Maafisa Ugani na Wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa nazi, ikiwemo Bagamoyo, sambamba na kuwaunganisha wakulima na masoko. Vilevile Wizara ipo katika jitihada za kutafuta wawekezaji, kwa ajili ya kuongeza mnyororo wa thamani wa zao la nazi ambao watakuwa tayari kujenga viwanda nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mkenge.

**MHE. MUHARAMI S. MKENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kituo cha *TARI* kilichopo Chambezi, Bagamoyo, ni wazalishaji wakubwa sana wa miche ya minazi. Je, Serikali ina mpango gani kwa hii miche inayozalishwa

angalau kuwagawia Wanabagamoyo miche 10 kila kaya ili kuweza kufufua zao la minazi Bagamoyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Je, Wizara sasa haioni umefika wakati wa kuanza kufundisha makundi mbalimbali kuotesha miche ya minazi, kama wanavyofanya kwenye korosho, ili kuleta wingi na uharaka wa uzalishaji wa miche hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ombi la Mheshimiwa Mbunge la kugawa miche kwa kila Kaya, hilo linazungumzika na linawezekana kutekelezeka kulingana na idadi ya miche. Kwa hiyo, tutaanza kutekeleza hilo kwa kaya na kwa awamu. Kwa hiyo, nakuahidi tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakuja katika Halmashauri yako ya Bagamoyo na tutalitekeleza hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuwafundisha wakulima namna ya kupanda miche ya minazi, kwa maana ya kuzalisha miche. Tutaiagiza *TARI,* Chambezi iliyoko pale Bagamoyo ianze kufanya zoezi hilo ili kupunguza hii adha ya Serikali muda wote kupeleka nguvu kwa wananchi. Kwa hiyo, hilo tutalitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, zao la karanga na soya lilimwa kwa wingi miaka ya zamani kwenye Jimbo langu la Nachingwea. Kwa kuzingatia mahitaji ya sasa ya mazao haya kwenye soko la dunia, ni nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha inafufua zao hili kwenye Jimbo la Nachingwea na maeneo mengine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha tunafufua mazao yote ambayo yamekuwa na tija kubwa kwa wananchi, ikiwemo soya ambayo sasa hivi inapelekwa sana nchini China ambao wamekuwa ni waagizaji wakubwa wa zao hili. Kwa hiyo, jambo hili lipo katika

mpango na tumeshazielekeza taasisi zetu za kitafiti ziongeze utafiti na uzalishaji wa mbegu ili tuwafikishie wananchi. Kwa hiyo, wananchi wa Nachingwea wakae tayari kwa jambo hilo kwa sababu liko katika mipango yetu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Mheshimiwa Pondeza hayupo, kwa niaba yake atauliza Mheshimiwa Ramadhani Ramadhani.

Na. 403

**Uwekezaji Kwenye Michezo Mbalimbali Nchini**

**MHE. RAMADHANI SULEIMAN RAMADHANI K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaamua kuwekeza kwa nguvu katika Viwanja, Walimu na Mawakala wa michezo inayoonekana kuleta tija kwa Taifa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, ambalo limeulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mbunge wa Chakechake, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza ujenzi wa viwanja vya mpira wa miguu vya Arusha, Dodoma, Fumba-Zanzibar, Ilemela Jijini Mwanza pamoja na Akademia na Hosteli katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya. Vilevile, Serikali inaendelea na ukarabati wa Viwanja vya Benjamin Mkapa na Uhuru – Dar es Salaam, Amani na Gombani vya Zanzibar kwa ajili ya maandalizi ya *CHAN* 2023 na *AFCON* 2024. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa ukarabati wa miundombinu ya shule 56 za michezo pamoja na viwanja vitano vya mpira wa miguu vya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa kuna walimu wa kutosha wa michezo, Serikali imekuwa ikiongeza udahili katika vyuo vinavyotoa mafunzo ya walimu wa michezo, hususan Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hadi kufikia mwaka 2023/2024 jumla ya wanafunzi 812 wamehitimu katika Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Baraza la Michezo la Taifa imeendelea kusajili Mawakala wa Michezo mbalimbali, ambapo jumla ya mawakala 233 walisajiliwa kuanzia mwaka 2018 hadi mwezi Desemba, 2023, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ramadhan.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa Serikali imetoa majibu mazuri sana, naomba niulize swali moja la nyongeza. Ni lini sasa viwanja vipya ambavyo Serikali ina mpango wa kuvijenga kwa ajili ya matayarisho ya *AFCON* vitakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kwa mujibu wa ratiba na mahitaji, viwanja hivi vinatakiwa kukamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka ujao 2025 tayari kwa ajili ya ukaguzi wa kikanuni wa *CAF* ambao utafanyika ili kuhakikisha tuko tayari kuandaa michezo ya *AFCON*.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mara nyingi michezo huendana na mazoezi na wakati mwingine mazoezi husababisha *injury*. Katika kupambana, wanamichezo wengi hupata majeraha ambayo mengine ni ya muda mrefu. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha watu wote wanaojihusisha na *elite sports (professionals)* wanapata Bima ya Afya ili waweze kuendelea kufanya vizuri katika michezo, tofauti na ilivyo sasa? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anatropia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa ikitilia mkazo mashindano yote ya ki-*professional* ambayo yanahusisha timu ziweke bima kwa ajili ya wachezaji wao na hata mahali ambapo wachezaji wanatumika kwa ajili ya Timu za Taifa, Serikali imekuwa ikihakikisha wachezaji hao wanakuwa wana bima ili kuhakikisha hawapati madhara ya kudumu na hata kama wakipata madhara ya kudumu Serikali inaweza kuwatibia kwa kutumia bima hizo.

**NAIBU SPIKA:** Wachezaji wote wa Simba wana bima. Vilabu vingine viige Simba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Naibu Waziri kwa sababu sasa hivi Mwanza imekuwa ikisahaulika sana kwenye michezo kwa kutokuwa na timu ambayo imeingia kwenye *Premier League* na sasa hivi *Pamba FC* Wanatipilindanda wako katika *Premier League*. Ni lini uwanja wa CCM Kirumba utakarabatiwa ikiwa ni pamoja na ule wa mazoezi ya *AFCON* wa Ilemela utakuwa tayari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu kwenye jibu la msingi, kwa sasa mpango uliopo ni kuanza kujenga kiwanja kipya cha Ilemela lakini hata Uwanja wa CCM Kirumba uko katika viwanja vitano ambavyo tunaanza navyo kuvikarabati ambavyo viko chini ya Chama cha Mapinduzi kama ambavyo nilishasema. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, asiwe na wasiwasi Wanatipilindanda watakuwa na sehemu ya kuchezea michezo yao ya Ligi Kuu kuanzia msimu ujao ambapo kitakuwa kimekarabatiwa na kitakuwa katika kiwango cha kupendeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Mheshimiwa Giga.

Na. 404

**Tamaduni za Kigeni kwenye Sanaa za Kitanzania**

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA** aliuliza: -

Je, kwa nini Tamaduni za kigeni zimetawala sanaa zetu kuliko utamaduni wetu wakati BASATA ipo kuhimiza na kukuza utamaduni wetu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kuu zinazosababisha tamaduni za kigeni kutawala kwenye sanaa zetu ni utandawazi pamoja na ukuaji wa teknolojia. Sababu hizi zimesababisha dunia kuwa kijiji hali inayotoa fursa kwa wasanii kupitia majukwaa ya kidigitali kuona mambo mbalimbali yanayofanyika duniani na kuyaiga na hivyo, kuathiri sanaa ya kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) linafanya kazi ya kufufua, kukuza na kuendeleza sanaa zenye asili ya Kitanzania kupitia *program* mbalimbali mfano: Sanaa Mtaa kwa Mtaa na BASATA *Vibes* ili kutoa elimu kwa wasanii kuhusu umuhimu wa kuzienzi tamaduni zetu kupitia kazi za sanaa, kushirikiana na wadau wa sanaa kuandaa matamasha mbalimbali yanayolenga kutangaza utamaduni wetu. Hata hivyo, BASATA inaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wadau wa sanaa wanaokiuka kanuni za maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, BASATA kwa kushirikiana na Kamati Maalum imetengeneza Kivunge cha Mtozi *(Producers Kit)* chenye vionjo zaidi ya 400 vya midundo ya makabila ya Kitanzania kitakachowezesha wasanii wa muziki kutumia midundo na vionjo vyenye asili ya Tanzania.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Giga.

**MHE. NAJMA MURTAZA GIGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana; pamoja na jitihada nzuri zinazofanywa na Serikali katika kulinda tamaduni za Kitanzania nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kwamba kuna baadhi ya filamu watoto wa kiume wana-*act* au wanaigiza kama watoto wa kike: Je, BASATA na Serikali hawaoni kwamba hili linaweza kuchochea watoto wetu wa kiume waone kwamba kuwa watoto wa kike ni jambo la kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kuhusu maudhui na miziki au filamu na mziki zilizomo ndani ya mabasi yaendayo mikoani. Mavazi yanayovaliwa na vijana wetu mle ndani hasa watoto wa kike ni nusu ya utupu. Je, Serikali au BASATA haioni kwamba hii ni kinyume cha sheria na kwamba ni tabia mbaya ambayo inaporomosha maadili ya nchi yetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwenye swali la kwanza lina mtego kidogo kwa sababu kazi ya wasanii pamoja na mambo mengine ni kuburudisha. Sasa wasanii wanaweza wakavaa uhusika wa aina yoyote. Wasanii mara nyingi wameimba nyimbo wakiigiza kuwa madaktari, wakiigiza kuwa waganga wa kienyeji, wakiigiza kuwa walevi, walioathirika na kadhalika. Kwa hiyo, kuvaa uhusika ni jambo moja ambalo limekaa kimtego na namna ya Serikali kulishughulikia ni kuangalia tu namna ambavyo kama litakuwa limezidi na linaakisi kupelekea kwenye kuisukuma jamii kufanya vitendo visivyofaa hapo ni lazima tutachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tunaendelea kufuatilia kwa karibu kupitia Baraza la Sanaa la Taifa kuhakikisha kwamba maudhui yaliyopo katika filamu na nyimbo zetu hayakiuki misingi ya maadili ya

Mtanzania na tunachukua hatua kila wakati inapofaa kufanya hivyo. Hata hivyo, tunaendelea kuwaelimisha wasanii kwa namna moja ama nyingine kuhusiana na jambo hili na kuhakikisha kama na wao wanabaki kwenye misingi na Maadili ya Kitanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jibu hili pia linakwenda kwenye swali lake la pili kuhusiana na mavazi ambayo yanakuwa ni nusu uchi kwenye nyimbo zilizorekodiwa ama filamu ambazo zinaoneshwa kwenye mabasi. Tunachoendelea kukifanya ni kuhakikisha maudhui yote yaliyoko katika nyimbo ikiwemo *video* zake na filamu za Kitanzania hayakiuki maadili ya Kitanzania ili kuepusha tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge amelisema, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuanzisha kampeni maalum kuondoa kasumba ambayo imejengeka kwetu sisi Watanzania kwamba tunapotumia mambo ya kimagharibi sana ni tafsiri ya kuonesha kwamba tumestaarabika? Kwa mfano, mtu unapoonekana unaweza kuongea Kiswahili peke yake na huwezi kuongea Kiingereza wewe hujasoma, wakati Wachina na Wafaransa hawajui Kiingereza na bado wanaheshimika; au kuonekana ukiwa unatumia mvinyo ambao unatoka nchi za magharibi wewe umestaarabika na ni msomi, lakini ukitumia mivinyo yetu ya ndani ya nchi wewe ni mshamba…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sichalwe uliza swali lako. Mheshimiwa Waziri.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama nimemwelewa vizuri ni kuhusu umagharibi kuingia kwenye tamaduni zetu na maisha yetu ya kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, dunia imekuwa kama Kijiji, kwa hivyo ni suala la ridhaa ya mtu na namna ambavyo anataka kuendesha maisha yake, lakini sisi ambacho tunakifanya ni kuhakikisha tunaendelea kuelimisha. Pamoja na mambo mengine kwa sasa tunafanya filamu ambazo zina maudhui ambayo yanaonesha umuhimu wa kuweka mbele utamaduni wetu kuliko kuiga tamaduni za kimagharibi. Tunaendelea na suala hili kupitia Baraza la Sanaa la Taifa, Baraza la Kiswahili la Taifa na Bodi ya Filamu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge, hili jambo sisi tunaendelea kulifanya japo ni ridhaa ya mtu mwenyewe anaamua anavyotaka maisha yake yafanyike, lakini tutaiweka katika namna ambayo itaonesha kufuata utamaduni wa kimagharibi siyo ujanja wowote na unaweza kuendelea kufuata utamaduni wa Kitanzania na ukaonekana una *class* unayotaka ionekane unayo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Michezo.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini niongezee kwenye hoja kwamba ili kuhakikisha wasanii wetu wanazingatia Maadili ya Kitanzania, tumeenda kubadilisha kanuni pale BASATA, tumeingiza wadau wengine ambao wanahusika kwenye *production* ya hizo *video* na nyimbo, kwa sababu mwanzoni tulikuwa tunamwadhibu msanii wakati *producer* ndio anatengeneza ile *content* na ndio anamwambia msanii avae vipi na a-*behave* vipi? Sasa hata *producer* na wadau wengine wa kwenye p*roduction* tumewaingiza katika mfumo wa kanuni na wanaadhibiwa ili kuhakikisha tunakomesha vitendo hivyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tunapambana sana na maadili ya watoto, Wizara haioni sasa ni wakati wa kuzuia ule uhusika ambao unapelekea kuchochea watoto kuingia kule kwenye tabia zile mbaya hasa

wale wanaume ku-*act* kama wanawake na baadaye kupelekea watoto kuona tabia za kishoga ni za kawaida?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu wakati najibu moja ya maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Giga, jambo ni lile lile ambalo Wizara inalitilia mkazo na inalifanya kwa nguvu nyingi, kuhakikisha tunatoa elimu kwa wasanii wetu. Halikadhalika tunachukua hatua pale inapostahili kufanya hivyo kama ambavyo tunaona kwamba wanakiuka maadili ya kitanzania. Kwa hiyo, hili ni jambo ambalo tunaendelea kulifanya kwa nguvu nyingi na tunahitaji ushirikiano wa kila Mtanzania kuhakikisha tunakemea jambo hili, ahsante.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya Jambo la Dharura.

**NAIBU SPIKA:** Kaa chini. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza wageni waliokaa Jukwaa la Spika ambao ni wageni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Viwanda na Biashara na hawa ni Mheshimiwa Omar Saidi Shaaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda - Zanzibar; Dkt. Hashil Twaib Abdallah, Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara; Mhandisi Bashir Juma Mrindoko, Mwenyekiti wa Bodi ya *TIRDO*; Mhandisi Musa Nyamsigwa, Mwenyekiti wa Bodi ya *SIDO*; Prof. Neema Mori, Mwenyekiti wa Bodi *BRELA*; Prof. Othman C. Othman, Mwenyekiti wa Bodi *TBS;* Mhandisi Prof. Valerian Silayo, Mwenyekiti wa Bodi *CAMARTEC;* Prof. Wineaster Anderson, Mwenyekiti wa Bodi ya *CBE;* Ndugu Frank Nyabundege, Kaimu Mwenyekiti wa Bodi *WRRB;* na Prof. Eliza Mwakasungula, Mwenyekiti wa Bodi *(WMA)*. *(Makofi)*

Pia tunaye Profesa Mkumbukwa Mtambo, Mkurugenzi Mkuu *TIRDO;* Profesa Edda Tandi Lwoga, Mkuu wa Chuo cha *CBE;* Bi. Latifa Khamis, Mkurugenzi Mkuu *TANTRADE*; Bi. Lorence Ansermet, *Officer in Charge UNIDO*; Ndugu Vedastus Tomothy, *Programme*

*Specialist UNIDO*; na Bwana William Erio, Mkurugenzi Mkuu *FCC*. *(Makofi)*

Tunaye Dkt. Muhajir Kachwamba, mume wa Mheshimiwa Waziri. Ahsanteni, naona na mhusika mwenyewe anatabasamu humu ndani. *(Makofi/Kicheko)*

Tunaye Bwana Abubakar Muhajir, mtoto wa Mheshimiwa Waziri na Bi. Blandina William, mdogo wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Pia tunaye Bi. Rehema Henry Mponzi, mke wa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni 30 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati ambao ni watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe kutoka Mkoa wa Geita. Hongera Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, maana wengine hapa wanaleta Kamati ya Siasa tu. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, mpiga kura wake kutoka Babati Vijijini, Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Hassan Mtenga, Mwandishi wa Habari na Mtangazaji kutoka Idhaa ya Kiswahili ya *BBC*. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ramadhani Ramadhan, rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Amandus Chinguile, mpiga kura wake kutoka Nachingwea. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Isack Kamwele, Daktari na Wauguzi kutoka *DCMC* Ntyuka, Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 14 wa Mheshimiwa Florent Kyombo, ndugu zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, wageni wanne kutoka Wilaya ya Uvinza, Mkoa wa Kigoma. *(Makofi)*

Wapo wageni watano kutoka *Binti Salha Foundation* ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wanafunzi 10 kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini Iringa, karibuni. *(Makofi)*

Wanafunzi 105 na walimu sita kutoka Shule ya Sekondari Canossa ya Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 na walimu 10 wa Shule ya Awali na Msingi Chemchemi ya Jijini Dodoma na wanafunzi 50 na walimu wawili Shule ya Msingi Kaloleni ya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

## HOJA YA DHARURA

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 54 kuahirisha Shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikieleza humu ndani changamoto ambayo imekuwa ikiwapata Wakulima wa Wilaya ya Kyerwa hususan Kata za Mpakani Murongo, Bugomora, Kibale na maeneo mengine. Msimu wa kahawa kumekuwa na utaratibu kwamba watu hawawezi kuvuna mpaka wapewe vibali hata kama pale ambapo kahawa zimeiva na wakati mwingine huchelewa kupatiwa vibali mpaka kahawa kuharibika wakati wanaokota.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, wakati mwingine kutoka shamba moja kwenda lingine wanalazimika kupewa kibali cha kwenda kuvuna kahawa na kutoa sehemu moja kwenda nyingine. Sasa ambacho kinasikitisha zaidi, kuna wananchi ambao nitawataja kwa majina hapa akiwepo Livingstone Leopold, Wilbard na mwingine wamepatiwa kibali cha kuhamisha kahawa, kuvuna kutoka kwenye shamba moja kwenda shamba lingine. Wamevuna wanapeleka kwao wakakamatwa na vyombo vya ulinzi, wakapigwa na haya

yamekuwa yanafanyika kutoka nyumba moja kwenda nyumba nyingine. Wanaambiwa kwamba wanataka kuvusha kahawa. Vyombo vya Dola vinawakuta vinaanza kuwapiga, kuwavunja miguu na kuwavunja mikono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninataka Wabunge wajadili na kueleza ni kwa nini tumefikia hapo na utaratibu gani ambao tunapaswa kuutumika ili kuhakikisha wananchi wanalima na kuvuna kahawa zao na kufaidika kwa mazao yao bila kuumizwa kama ilivyo sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ukiona inafaa, Wabunge wajadili ili ziweze kupata mustakabali.

**NAIBU SPIKA:** Subiri kwanza. Mheshimiwa Anatropia nashukuru kwa hoja yako. Naelekeza sasa Waziri wa Kilimo akutane na wewe, mlijadili na mlimalize hilo suala muda huu huu asubuhi. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaanza sasa kusikiliza Taarifa ya Bajeti ya Wizara, Mheshimiwa Waziri karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 23 Machi, 2024, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya

Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema kwa kutujalia baraka na afya njema na kumudu kuyatekeleza yale tuliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Watanzania wote kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama tunaomba mtoke nje au mwingie ndani kwa utaratibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba Mwenyezi Mungu kwa rehema yake atukopeshe tena uhai na afya njema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili tuyatekeleze malengo haya ambayo tunajiwekea leo kwenye sekta hii ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu tangu ashike madaraka na kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema, hekima na busara ili matamanio ya Watanzania yaweze kufikiwa chini ya uongozi wake hasa ya kukuza uchumi wa Taifa letu kupitia uwekezaji kwenye sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama takwimu zinavyotueleza kwamba kati ya miradi 526 iliyosajiliwa na Kituo cha Uwekezaji Tanzania mwaka 2023 kwenye sekta za uzalishaji hapa nchini, miradi 237 sawa na 45% ya miradi yote ipo kwenye sekta ya uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa dhati ya moyo wangu kwa kuendelea kuniamini kuongoza Sekta hizi muhimu za Viwanda na Biashara kwani ndiyo sekta mama kwenye ukuaji wa uchumi wa Taifa lolote lile duniani. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, viongozi, watumishi wa Wizara na taasisi zake tutaendelea kutekeleza maono yake kwenye sekta hii ya

viwanda na biashara kwa nguvu, weledi, uadilifu na umakini mkubwa ili mchango wake kwenye pato la Taifa na maisha ya wananchi wetu uweze kuongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa miongozo yao yenye kutia chachu na hamasa katika kuimarisha sekta ya viwanda na biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ya bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 3 Aprili, 2024. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa mwaka 2024/2025 ambayo Wizara ya Viwanda na Biashara itaizingatia katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Watanzania wote kwa ujumla, kwa kuondokewa na Hayati Alhaj Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile natoa pole kwa kuondokewa na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matukio hayo yasiyozoelekeza yalifululiza na kutuacha na majonzi makubwa, tunaendelea kumwomba Mwenyezi Mungu awarehemu viongozi wetu hao wapendwa, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024 Bunge letu liliondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Mtenga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Naomba nitoe pole kwako, Mheshimiwa Naibu Spika,

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na jamaa wa marehemu, tunaomba mwenyezi Mungu aendelee kuwa mfariji mkuu katika kadhia hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa wananchi waliokumbwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa hayo, Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa ahueni waathirika wote ili warejee katika hali njema na hivyo kuendelea kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Othman Masoud Othman Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuendelea kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu na kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza masuala ya sekta ya viwanda na biashara. Katika kudumisha ushirikiano huo, leo amesafiri kutoka Zanzibar na amekuja kuniunga mkono hapa Bungeni ninapowasilisha mafanikio ya sekta yetu ya viwanda na biashara. Hakika nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mashaka Biteko Mbunge kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Vilevile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi mbalimbali za uongozi ndani ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Spika wetu Dkt. Tulia Ackson kwa kuchaguliwa na

Baraza la Umoja wa Wabunge Duniani kwa kura nyingi kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani akiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika kushika wadhifa huo kwenye chombo hiki muhimu cha maamuzi ya Wabunge Duniani. Imani hii aliyopewa inathibitisha umahiri na umakini wake katika kuliendesha Bunge letu Tukufu kwa weledi wa hali ya juu. Tunampa hongera sana na kumtakia heri anapoendelea kuliheshimisha Taifa letu katika siasa za Kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nakupongeza sana pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri wenu wa kuliongoza na kulisimamia Bunge letu, Mwenyezi Mungu awalinde na kuwasimamia katika kuliendesha Bunge letu kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika na Mwenyekiti wa Kamati yetu kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi, hususan Baraza la Taifa la Biashara, Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania, Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania, Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania, na Baraza la Kilimo Tanzania kwa michango yao ya hali na mali katika kuendeleza sekta ya viwanda biashara na masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia wamiliki na waandishi wa vyombo vya habari kwa michango yao mikubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji

wa Wizara na Taasisi zake na kuhimiza uzalishaji viwandani. Naomba tuendeleze ari hiyo ili tuweze kukuza uelewa kwa umma na hatimaye ushiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi kwenye mafanikio tuliyoyapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kondoa kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Kitaifa na ya Kijimbo ambayo najua leo wanawakilishwa na Wenyeviti wote na Wenezi wote wa Kata zote 21 ndani ya Jimbo la Kondoa. Nawapongeza kwa namna wanavyojibidiisha katika kujiletea maendeleo kwa kushiriki shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, nawaahidi kwamba nitaendelea kuwa mtetezi wa maslahi yao hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo chanya kwa mtu mmoja mmoja na hatimaye kuongeza mchango wetu kwa Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe - Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dkt. Hashil Twaibu Abdallah, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara, napenda kuwapongeza sana. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani usingekuwa rahisi bila maombi na dua njema kutoka kwa watu wangu wa karibu. Nawashukuru sana wazazi wangu wapendwa Baba Alhaj Abdallah Kijaji na Mama yangu Hajat Aziza Selemani. Aidha, namshukuru mume wangu mpenzi, Dkt. Muhajir Kachwamba na watoto wangu Samirah na Aboubakar, ahsanteni sana kwa upendo wenu, uvumilivu na utayari wenu unaonipatia ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na ueledi wangu wote. Vilevile, viongozi wangu wa dini, ndugu,

jamaa na marafiki wote, nawashukuru sana kwa kuendelea kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niendelee kulitumikia Taifa letu. Napenda kuwaahidi nyote na Watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na malengo ya mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya viwanda na biashara kwa kiasi kikubwa inategemea shughuli za sekta binafsi ambayo ndiyo inayowekeza mitaji yao viwandani na kwenye miamala ya kibiashara ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma nchini unakuwepo wakati wote. Hivyo, jukumu kubwa la Wizara ni kusimamia masuala ya utafiti, ushauri, uratibu na kutoa mwelekeo kwenye tasnia hii ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, Wizara imeendelea na jitihada za kuhamasisha ujenzi, uanzishwaji na upanuzi wa viwanda vikiwemo viwanda vya kuongeza thamani malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wake, kutengeneza ajira na kukuza mauzo nje ya nchi. Katika jitihada hizo za uhamasishaji, viwanda vipya vimeendelea kujengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi kwa uchache wake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni viwanda vya kuunganisha magari. Tanzania ina jumla ya viwanda 13 vya magari, kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili vinaunganisha magari ambavyo ni *GF Trucks and Equipment Ltd* kilichopo Kibaha Pwani na *Saturn Corporation Limited* kilichopo Kigamboni Dar es Salaam. Viwanda 11 vinavyosalia vinatengeneza matrela. Kiwanda cha *GF Truck* kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha magari 200 kwa mwezi na kimewekeza kiasi cha shilingi bilioni 10.752 na kimetoa ajira 300 kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha *Saturn Corporation Limited* kimewekeza mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 64.3 na kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha vichwa vya magari 900 na tipa 270 kwa mwezi na kimeajiri Watanzania 250. Viwanda vyote hivi vinauza bidhaa zao kwenye soko la ndani ya nchi na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili ni viwanda vya kutengeneza vioo. Tanzania ina jumla ya viwanda vitatu vya kuzalisha bidhaa za vioo. Viwanda hivyo ni Kioo *Ltd* na Salehbhai *Glass Industries Ltd* ambavyo vipo katika Mkoa wa Dar es Salaam na *Sapphire Float Glass* (Tanzania) *Company Limited* ambacho kipo Mkuranga Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha Kioo *Limited* huzalisha chupa za vinywaji na viwanda vilivyosalia huzalisha vioo vya ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Sapphire* kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 700 kwa siku sawa na tani 189,000 kwa mwaka. Hata hivyo, kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha vioo tani 450 kwa siku sawa na tani 121,500 kwa mwaka. Asilimia 60 ya vioo vinavyozalishwa na kiwanda hiki huuzwa nje ya nchi kwenye nchi zote za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika pamoja na nchi za Arabuni. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 1,012 wa ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 3,857 wa ajira zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda kimewekeza mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 800.1 na kilianza uzalishaji mwezi Septemba 2023 baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Kiwanda cha Kioo *Limited* kwa mwaka 2023 kilizalisha bidhaa za chupa zenye uzito wa tani 131,105 na kuuza nje ya nchi yetu tani 67,393 za vioo yakiwemo masoko ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Malawi, Zimbabwe, Uganda, Rwanda, Kenya na nchi za Bara la Ulaya. Aidha, kiwanda hicho kimewekeza kiasi cha shilingi bilioni 4.4 na kutoa ajira za moja kwa moja 613 na wanaendelea kufanya upanuzi ili kuongeza uzalishaji na kufikia uhitaji ulioko sokoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, 80% ya malighafi zinazotumika na viwanda hivi vya vioo zinapatikana ndani ya nchi yetu, hivyo, Taifa letu lina nafasi kubwa ya kunufaika na masoko ya kikanda kama Afrika Mashariki, *SADC* na *CFTA* ambayo tayari tumeanza kunufaika nayo kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya saruji. Tanzania ina jumla ya viwanda vya saruji 14 ambapo viwanda vikubwa ni saba na vilivyosalia saba ni viwanda vidogo. Kwa mwaka 2023 viwanda vya saruji nchini vilizalisha tani 9,107,973 za saruji, ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni takribani tani 8,000,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 1,107,973 ambayo huuzwa nje ya nchi yetu katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*. Sekta hiyo imeajiri wafanyakazi 17,885 ambapo kati yao, wafanyakazi 4,176 ni ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 13,709 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za kuimarisha uzalishaji kwenye sekta ya saruji, Wizara ilitoa kibali kwa kampuni ya *Amsons Industries (Tanzania) Ltd* inayozalisha saruji aina ya Camel kuinunua Kampuni ya Mbeya *Cement Company Limited*. Muungano huo unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa yafuatayo:-

(i) Kuongeza uzalishaji wa kiwanda hicho ambapo uzalishaji wa clinker utaongezeka mara nne na kufikia tani 1,220,000 kutoka tani 305,000 kwa mwaka;

(ii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji kwa asilimia 60 hadi kufikia tani 1,680,000 kutoka tani 1,050,000 kwa mwaka;

(iii) Kuwezesha umiliki wa viwanda vikubwa kuwa mikononi mwa watanzania;

(iv) Kuongeza ajira; na

(v) Kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara ilifanikiwa kutoa uamuzi wa mwisho wa kuiruhusu kampuni ya Tanzania *Portland*

*Cement (Twiga Cement)* na Tanga *Cement PLC* kuungana kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuboresha ufanisi wa kiwanda cha Tanga *Cement* ambacho kilikuwa na historia ya kujiendesha kwa hasara kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa kiwanda cha Tanzania *Portland Cement PLC* kinajitosheleza kwa malighafi ya *clinker,* hakihitaji tena kuagiza *clinker* kutoka nje ya nchi kwa kuwa kinatumia malighafi hiyo kutoka kiwanda cha Tanga *Cement*. Kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita kiwanda hicho kiliagiza clinker wastani wa tani 321,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kufuatia muungano huo, hadi kufikia Machi, 2024, uzalishaji wa saruji kwa kampuni ya Tanga *Cement PLC* umeongezeka kutoka tani 980,000 hadi kufikia tani 1,200,000. Hivyo basi, kuongezeka huku kwa uzalishaji kunamaanisha ajira zote zilizokuwa hatarini kupotea sasa ziko salama ndani ya muungano wa kampuni hizi mbili na kodi ambazo hazikulipwa kwa miaka mitano mfululizo sasa zitalipika ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwenye sekta ya saruji kwa kutoza kodi ya 35% kwenye saruji inayoingia nchini kwa lengo la kuvilinda viwanda vyetu vya ndani. Aidha, Serikali inaendelea kuwahamasisha wazalishaji wa saruji kuongeza uzalishaji ili kupata tija na kuwa shindani katika masoko ya nje likiwemo soko la eneo Huru la Biashara Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda vya saruji nchini vinazalisha *clinker* ambayo ni malighafi muhimu sana kwa ajili ya kutengeneza bidhaa ya saruji. Viwanda hivi vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha malighafi ya *clinker* tani 7,564,564 kwa mwaka ambapo mahitaji ya soko la saruji nchini ni sawa na tani 6,000,000 za malighafi ya *clinker*. Hivyo, kuna ziada ya *clinker* ipatayo tani 1,564,564 kwa mwaka. Kwa mwaka 2023, uzalishaji halisi wa *clinker*, ulikuwa na ziada ya tani 652,921 ambapo ziada hiyo iliuzwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na nchi za *SADC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya mafuta ya kula. Tanzania ina jumla ya viwanda 789 vya kusindika mafuta ya kula. Kati ya hivyo, 17 ni viwanda vikubwa na vya kati na 772 ni vidogo na vidogo sana. Viwanda vidogo na vidogo sana vinatumia asilimia 20 ya uwezo wake kwa kusindika mbegu, wakati viwanda vikubwa na vya kati vinatumia asilimia kati ya 25 na 40 ya uwezo uliosimikwa. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 205,000 za mafuta ambapo tani 180,000 ni mafuta ya alizeti na tani 25,000 ni mafuta ya mawese na pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni zaidi ya tani 600,000 kwa mwaka hivyo, tani 395,000 huagizwa nje ili kutosheleza mahitaji ya ndani. Viwanda hivyo vinazalisha chini ya uwezo wake kutokana na kukosekana kwa malighafi ya mbegu bora na za kutosha za mafuta. Sekta hii imetoa ajira 5,136 za moja kwa moja na ajira 15,860 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa uwekezaji na hii imepelekea kuongezeka kwa mikoa inayolima mbegu za mafuta ya kula nchini kutoka mikoa 15 hadi mikoa 19. Hali hii inatokana na uhamasishaji wa programu ya kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini ambapo mikoa yenye uwezo wa kulima mbegu za mafuta imehamasishwa na kuanza kilimo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali iliondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani katika mafuta yaliyosafishwa yanayozalishwa na viwanda vyetu vya ndani kwa lengo la kupunguza bei ya mafuta ya kula ili yaweze kushindana na mafuta yanayotoka nje ya nchi. Vilevile, katika mwaka 2022 Serikali ilifanya mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha na kupunguza ushuru wa uagizaji wa mafuta ghafi ya chikichi kutoka asilimia 25 hadi 0. Lengo la mapendekezo hayo lilikuwa ni kusaidia viwanda vya ndani vinavyochakata mafuta ya chikichi vipate malighafi na kusaidia upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika moja ya bidhaa ambayo bei yake haikupanda kwa mwaka huu ni bidhaa hii ya mafuta ya kula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda vya chuma na bidhaa za chuma; Tanzania ina jumla ya viwanda 28 vya kuzalisha chuma na bidhaa zake. Viwanda hivyo vipo katika makundi mbalimbali yanayojumuisha nondo, mabati, mabomba, misumari na seng'enge na vimeajiri jumla ya Watanzania 25,358. Kati ya hao, wafanyakazi 4,169 ni ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 21,189 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya viwanda hivyo, viwanda 19 vinazalisha nondo na vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,299,240 kwa mwaka. Hadi kufikia Machi, 2024 viwanda hivyo vilizalisha nondo tani 900,000 ikilinganishwa na mahitaji ya nondo tani 605,369.6. Hivyo uzalishaji huo ulitosheleza mahitaji yote ya ndani na ziada kiasi cha tani 294,630.4 kiliuzwa katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inaondokana na utegemezi wa kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mbolea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024, Tanzania ina jumla ya viwanda 24**.** Kati ya viwanda hivyo, viwili ambavyo ni Minjingu na *Itracom Fertilizer Limited*; ni vikubwa. Kimoja ni cha kati na 21vilivyosalia ni viwanda vidogo ambavyo hufanya kazi ya kuchanganya mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda cha mbolea cha *Itracom Fertilizer Limited* kilichopo eneo la Nala jijini Dodoma kimesimika mitambo miwili iliyo na uwezo wa kuzalisha tani 400,000 za mbolea kwa mwaka. Vilevile, kiwanda kina mitambo mitatu ambayo ipo katika hatua ya kufungwa na itakamilika mwezi Juni, 2024. Hadi Machi 2024, *Itracom* wamezalisha tani 54,395 za mbolea na wameuza tani 3,819 katika soko la ndani na tani zilizobaki zimeuzwa katika soko la nje ikiwemo Burundi na Kenya. Kiwanda kimetoa ajira 1,002 katika ujenzi na uzalishaji kwa pamoja. Ajira za moja kwa moja ni 688 na zisizo za moja kwa moja ni 314.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Mbolea cha Minjingu kipo katika eneo la Minjingu katika Mkoa wa Manyara. Kiwanda kimewekeza mtaji kiasi cha shilingi bilioni 50 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 100,000 za mbolea aina ya

*Phosphate* kwa mwaka. Hadi Machi 2024, Kiwanda kimezalisha tani 51,914 zilizouzwa kwenye soko la ndani pamoja soko la nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwanda hiki kimetoa ajira za moja kwa moja kwa Watanzania 175 na ajira zisizo za moja kwa moja 560. Aidha, kwa sasa kiwanda kipo kwenye hatua nzuri za mwisho za kuongeza upanuzi na usimikaji wa mitambo zaidi ya kuzalisha mbolea aina ya *NPK* yenye uwezo wa kuzalisha tani 150,000 na kufanya jumla ya uwezo wa uzalishaji kufikia tani 250,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kujengwa kwa viwanda hivi vichache vipya nilivyovitaja pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani ni ushuhuda tosha kwamba imani ya wawekezaji kwenye Sekta ya Uzalishaji viwandani imeongezeka sana. Hivi ni baadhi ya viwanda vingi vilivyopo na vinavyoendelea kujengwa ndani ya Taifa letu. Viwanda hivyo vinazalisha bidhaa zinazotosheleza mahitaji ya ndani na kuuza bidhaa zinazobaki kwenye masoko ya nje na hatimaye kulileteea Taifa letu fedha za kigeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni majibu ya jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika kazi ya Mheshimiwa Rais wetu ni njema sana na anastahili pongezi na tuzo ya heshima. Hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwa hapa tulipofika tunahitaji kuvilinda viwanda hivi kwa wivu mkubwa sana ili viendelee kutengeneza ajira kwa vijana wetu wa kike na wa kiume. Naomba kuwahakikishia wenye viwanda wote kwamba Serikali yenu chini ya Jemedari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo tayari kuwalinda. Endeleeni kuleta mitaji zaidi ndani ya Taifa letu kwa usalama wa mama Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa biashara, Tanzania ina fursa mbalimbali za masoko ya kuuza mazao na bidhaa zinazozalishwa. Katika kutumia fursa hizo, Wizara imeendelea kushiriki majadiliano ya biashara baina ya nchi na

nchi, kikanda na kimataifa lengo likiwa ni kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu ya bidhaa na huduma na kuvutia biashara nchini. Katika mwaka 2023/2024 mwenendo wa biashara ulikuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika Soko la Ulaya iliongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 3.836 kutoka shilingi trilioni 2.446 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 56.8. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kilimo na viwandani kwenda katika nchi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya ulipungua kwa asilimia 8.1 hadi shilingi trilioni 4.045 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.404 kwa mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani na mitaji kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo ndani ya nchi ambapo bidhaa hizo zilikuwa zinaagizwa kutoka Soko la Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023, Tanzania iliendelea kuboresha mahusiano ya kibiashara na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko hilo ilikuwa shilingi trilioni 3.022 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.415 mwaka 2022 ikiwa ni upungufu wa asilimia 16.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hiyo imechangiwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za kilimo hususan kahawa, chai, mahindi, ngano, mchele, mbogamboga na bidhaa za viwandani zikiwemo vigae, na saruji. Kupungua kwa mauzo, mfano kahawa kumesababishwa na Tanzania kuuza bidhaa husika moja kwa moja kwenye masoko ya nje tofauti na ilivyokuwa awali ambapo bidhaa hiyo iliuzwa kupitia nchi ya Kenya. Vilevile, kuongezeka kwa mahitaji ya ndani kwa bidhaa za ujenzi ikiwemo vigae, saruji, chuma na bidhaa za chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023, bidhaa zenye thamani ya shilingi trilioni 1.34 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya shilingi trilioni

1.48 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia tisa. Upungufu huo umechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini na kusababisha kupungua manunuzi ya bidhaa za viwandani kutoka nchi za jirani ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia mpango wa *AGOA* yalikuwa shilingi bilioni 205.824 ikilinganishwa na shilingi bilioni 192.26 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.06. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za nguo na mavazi zinazouzwa kwenye soko hilo. Katika jitihada za kutumia zaidi fursa ya soko la *AGOA*, Tanzania imeomba kuongezewa miaka 10 baada ya ukomo wa mpango huu ambao unaisha mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya kampuni 11 za Tanzania zimeweza kuuza bidhaa katika nchi mbalimbali za Afrika kwa kutumia cheti cha uasili wa bidhaa cha Eneo Huru la Biashara Afrika ambapo, jumla ya vyeti 24 vimeweza kutolewa kwa kampuni hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, bidhaa ambazo zimeuzwa kwa wingi kupitia vyeti hivyo ni nyuzi za katani tani 426 kwenda nchi za Nigeria, Ghana, Morocco na Misri, kahawa tani 273.3 kwenda nchini Algeria na tumbaku tani 21.1 kwenda Nigeria. Faida zilizopatikana kwa wafanyabiashara hao ni kuweza kuuza bidhaa zao kwa kutozwa ushuru pungufu ikilinganishwa na ilivyokuwa awali. Wizara inaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kutumia fursa ya soko hilo kubwa kuweza kuuza bidhaa zao na kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wafanyabiashara wenzangu, milango na madirisha yote vimefunguka kwa ajili yetu ili tufanye biashara kwa masoko ya ndani na nje ya mipaka ya Taifa letu. Hivyo basi, ni wajibu wetu kuyalinda masoko haya kwa wivu mkubwa. Uadilifu na ukweli wetu tunapoamiliana na wateja wetu na washirika wetu ndiyo njia pekee ya kurejesha shukrani kwa mwanadiplomasia namba moja Mheshimiwa Rais wetu, Dkt.

Samia Suluhu Hassan, ambaye anapambana kututafutia fursa za masoko kwa ajili ya bidhaa zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa Sekta ya Viwanda ulikuwa 4.3% mwaka 2023 ikilinganishwa na 4.2% mwaka 2022. Aidha, mchango wa Sekta ya Viwanda katika pato la Taifa kwa mwaka 2023 ulikuwa asilimia saba ikilinganishwa na 7.1% kwa mwaka 2022.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wa Sekta ya Biashara katika pato la Taifa letu kwa mwaka 2023 ulikuwa 8.3% ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2022. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa 4.3% kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na 3.9% mwaka 2022. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza miradi ya kielelezo ya Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Chuma cha Liganga, Magadi Soda – Engaruka, kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools, kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa na kuboresha mazingira ya biashara. Maeneo mengine ya kipaumbele ni kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania, kuendeleza mitaa ya viwanda, kukuza na kuboresha hali ya ushindani sokoni, ubunifu, urasimishaji wa biashara, uhawilishaji na ukuzaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 92,348,837,623. Kati ya fedha hizo, shilingi 66,698,567,623 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizo zinajumuisha shilingi 9,254,956,938 za matumizi mengineyo na shilingi 57,443,610,685 za mishahara. Aidha, shilingi 25,650,270,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha zilizopokelewa. Hadi kufikia mwezi Machi, 2023, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 50,376,084,589.17, sawa na asilimia 76.03 ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,069,975,635.15 ni kwa ajili ya matumizi

mengineyo sawa na asilimia 79.09 na shilingi 43,306,108,954.02 ni kwa ajili ya mishahara, sawa na asilimia 75.56 ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu fedha za maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 9,770,269,727.63 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na 38.09% ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa mipango na shughuli za maendeleo kwa mwaka 2023/2024 umeelezwa kwenye Kitabu cha Hotuba kuanzia ukurasa wa 24 hadi 67. Kwa sababu ya muda niruhusu niwasilishe mbele yako na Bunge lako Tukufu miradi michache.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara chini ya uratibu wa Shirika la Taifa la Maendeleo *(NDC)* imeendelea na ukamilishaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Linganga. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 15,414,000,000 zimelipwa kati ya shilingi bilioni 15.424 kwa wafidiwa 1,129 kati ya 1,142. Idadi ya wafidiwa waliolipwa ni sawa na 99%. Kiasi ambacho hakijalipwa kwa wafidiwa 13 ni shilingi milioni 10.227.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi hao 13 ambao hawajalipwa kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo baadhi yao kutojitokeza na wengine kutokukamilisha nyaraka na taratibu za mirathi. Juhudi za kuwapata wafidiwa hao au warithi wao zinaendelea kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ili zoezi lihitimishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuhitimisha zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi katika eneo la mradi wa Liganga na Mchuchuma, Serikali inakamilisha taratibu za utoaji wa ardhi kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya kuendeleza mradi huo. Vilevile, Serikali inaendelea na majadiliano na mwekezaji kwa nia ya kuhitimishwa na kuanza utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali kubwa ya makaa ya mawe yaliyopo Mkoa wa

Njombe, Wizara ilisaini mikataba na wachimbaji wadogo wa makaa ya mawe kwenye eneo la Vitalu Kumi lilipoto nje ya mkataba wa Mradi wa Mchuchuma na Linganga mnapo mwezi Septemba, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, maandalizi ya awali ya utafiti na uchimbaji kwenye leseni ndogo yameanza ambapo kampuni mbili zimekamilisha taarifa ya kijiolojia na kampuni nyingine zinaendelea na utafiti wa kijiolojia. Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha kwamba miradi hiyo inaanza uzalishaji mapema.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inapunguza utegemezi wa uagizaji wa vifaatiba nchini, Wizara kupitia *TEMDO* imefanya utafiti na kutengeneza vifaa tiba na kuviuza katika hospitali mbalimbali hapa nchini. Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imeuza jumla ya vifaatiba 1,210 vya aina mbalimbali vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8. Kati ya vifaatiba hivyo, vifaatiba 842 vilipelekwa Jeshi la Wananchi wa Tanzania – Ngome, vifaatiba 160 vilipelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa na vifaatiba 208 vimepelekwa katika Hospitali za Bugando, *Mount Meru* na Levolosi.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa ya mradi huo ni pamoja na kujenga uwezo wa ndani wa kutengeneza vifaatiba na hivyo kuondokana na utegemezi wa kuagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi, kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa kupunguza uagizaji vifaatiba kutoka nje ya nchi na kukuza ujuzi na kutengeneza ajira nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea na utafiti wa utengenezaji wa mtambo wa kutengeneza sukari kwa kiwango cha mjasiriamali wa kati. Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 200 za miwa ghafi na kutoa tani 20 za sukari kwa siku moja. Mradi unatarajiwa kukamilika na kufanyiwa majaribio ya awali ifikapo mwezi Juni, 2024. Aidha, gharama za mradi huo ni shilingi bilioni 1.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2024 mradi umekamilika kwa asilimia 80. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa

na uwezo wa kutoa ajira za moja kwa moja 300 na ajira zisizo za moja kwa moja 1,800. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchakata miwa ya wakulima kwenye eneo la ukubwa wa ekari 400 na kutoa ajira kwa wahudumu wa shamba wasiopungua 5,600.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imekamilisha utafiti na kutengeneza teknolojia kwa ajili ya kuchakata mbegu za alizeti na kutengeneza mafuta ya kula. Usanifu na utengenezaji wa mtambo wa kuchakata alizeti ili kupata mafuta bora ya kupikia kwa kiwango cha kukidhi soko la ndani na nje ya nchi umekamilika. Mtambo huo una uwezo wa kusafisha mafuta lita 1,000 kwa siku, kutoa ajira za moja kwa moja 15 na ajira zisizo za moja kwa moja 60 na kuweza kuhudumia mashamba yenye ukubwa wa ekari 400 kwa msimu mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtambo uliokamilika umefungwa kwa mteja wa *Usa River* Jijini Arusha. Aidha, sehemu iliyofungwa mtambo huo inatumika kwa ajili ya mafunzo kwa wajasiriamali wengine wanaojihusisha na uongezaji wa thamani kwenye mafuta yatokanayo na alizeti. Mtambo huo una thamani ya shilingi milioni 96.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imefanikiwa kufanya ziara kwenye mikoa 10 na kufanya mikutano na wafanyabiashara na wenye viwanda katika mikoa hiyo. Lengo la ziara na mikutano ilikuwa ni kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Kupitia mikutano hiyo zaidi ya changamoto 20 zilitatuliwa papo kwa hapo. Wizara pia imefanya mikutano mitatu na uongozi wa soko la Kariakoo ambao nashukuru leo wapo pamoja nasi hapa, ambapo jumla ya changamoto 16 kati ya zilizowasilishwa mwaka 2023 kutoka kwa wafanyabiashara wa Kariakoo zimetatuliwa. Changamoto tano zilizobakia zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Nawashukuru sana uongozi wa Kariakoo pamoja na wafanyabiashara Kariakoo kwa kuendelea na ushirikiano huu na kuweza kukaa mezani kutatua changamoto zote hizi kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Wizara iliandaa mkutano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi uliofanyika Jijini Mbeya

kwa lengo la kuendelea kuimarisha mashirikiano baina ya sekta hizi mbili. Naomba nitumie fursa hii kuwahakikishia sekta binafsi kwamba Wizara hii ni ya kwao na itaendelea kufanya kazi kwa karibu nao kwani bila wao kufanya shughuli zao kikamilifu uchumi wa nchi yetu hauwezi kukua katika viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara imefanikisha upatikanaji wa masoko ya bidhaa za viwandani, kilimo na mifugo kwenye nchi za Saudi Arabia, Katar, Umoja wa Falme za Kiarabu, India, Misri, Nigeria, Afrika ya Kusini, Malawi, Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uholanzi, Oman, Vietnam, Ubelgiji, Rwanda, Zambia, Uganda na Sudani ya Kusini. Bidhaa zilizouzwa kwenye nchi hizi na thamani zao zimeoneshwa kwenye Aya ya 170 – 174 kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia imeanzisha mafunzo ya atamizi za biashara, ukuzaji teknolojia pamoja na mawazo bunifu, ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya vijana wapatao 205 wapo katika mafunzo hayo. Kati ya vijana hao 185 wameatamiwa na Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* na 20 wameatamiwa na *TIRDO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafunzo ya atamizi ya biashara yamegawanyika katika makundi matatu, yaani hatua ya kuandaliwa *(Pre-Incubation)*, hatua ya kulelewa *(Incubation stage)*, na hatua ya mwisho *(post incubation)*. Mafunzo hayo yanaanzia ngazi ya kubuni wazo la biashara mpaka kusajili majina ya biashara na hatimaye kusaidiwa kuanzisha biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia inaendelea kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati 24 kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za uongezaji thamani mazao kupitia kiatamizi cha teknolojia chini ya *TEMDO*, na baadaye kuwaunganisha na *SIDO* ili waweze kupata mikopo ya kununua mitambo na mashine mbalimbali kutoka *TEMDO*. Kwa upande mwingine, wabunifu wapatao 35 wanaendeleza bidhaa na huduma zao katika vituo vya teknolojia vya *SIDO* katika mikoa ya Arusha, Iringa, Morogoro, Rukwa, Singida, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kutengeneza na kuhawilisha teknolojia/mashine na vipuri kwa kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia vya *SIDO*. Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya mashine 576 na vipuri 1,204 vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na misitu vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali wetu. Teknolojia hizo zilizotengenezwa zimeweza kuingia sokoni na kuwezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 262 na kutoa ajira za moja kwa moja 1,021.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2024, Serikali kupitia Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 108.4 ili kuwezesha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda 37 vya uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mifugo nchini, kama vilivyooneshwa kwenye Aya ya 82 – 88 kwenye kitabu kikubwa cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hadi kufikia Machi, 2024 Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo imefanikisha ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuchakata nyama ya kuku kinachotumia teknolojia ya kisasa kabisa, kuanzia kwenye hatua ya utotoleshaji wa vifaranga na kuwafungasha kuku kwa ajili ya kwenda sokoni. Kiwanda hicho kina uwezo wa kutunza kuku 100,000 kwa kila mzunguko na kufanya shunguli za kuchinja na kupaki kuku 3,000 kwa saa moja. Kiwanda hicho ni moja ya viwanda vya kuku vikubwa katika eneo la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo, *SIDO* pamoja na Benki yetu ya Maendeleo ya Kilimo wataendelea kuchagiza uwekezaji wa sekta binafsi kwa kutoa mikopo kwa wadau wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia mahitaji na fursa katika mnyororo mzima wa thamani ikiwemo mikopo kwa waongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, vipaumbele vikuu vya Wizara ni sita. Aidha, vipaumbele hivyo vitatekelezwa na shughuli mbalimbali ndani ya Wizara na taasisi zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, vipaumbele vikuu vya Wizara ni: -

(a) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati;

(b) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuimarisha miundombinu na mazingira wezeshi;

(c) Kuboresha mazingira ya uwekezaji viwandani na ufanyaji biashara;

(d) Kuchochea maendeleo ya watu kwa kuboresha miradi na programu katika sekta za kiuchumi na kijamii inayohusisha elimu na mafunzo ya ujuzi;

(e) Kufanya intelijensia ya masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya kimkakati na ya kimataifa; na

(f) Kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 110,899,722,000 kwa fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,115,206,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 29,789,516,000 ni matumizi ya maendeleo. Kati ya shilingi 81,115,206,000 za matumizi ya kawaida, zinajumuisha shilingi 68,352,946,000 fedha za mishahara na shilingi 12,762,260,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuhitimisha kwa kuchukua fursa hii kuwashukuru tena Watanzania wote kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza sekta ya viwanda na biashara. Tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni rai yetu kwamba kila Mtanzania popote alipo anahitajika kutimiza wajibu wake, kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na kuendeleza uwekezaji katika viwanda na biashara. Inawezekana, tutimize wajibu wetu na kuunga mkono kwa vitendo jitihada kubwa za Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama alivyotuambia wakati ni sasa wa kutajirika kwa Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara pia. Baada ya kusema haya, naomba kuwakaribisha kuanzia wewe na Waheshimiwa Wabunge wote, muweze kupita kwenye mabada ya maonesho muone baadhi ya viwanda tulivyoviwasilisha hapa na vingine ambavyo hatukupata muda wa kuviwasilisha, kazi nzuri wanayoifanya ndani ya Taifa letu. Kwa pamoja tuwaunge mkono na tujisikie fahari kununua vitu vyetu vinavyotengenezwa ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maneno haya, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. ASHATU K. KIJAJI (MB.), WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 23 Machi, 2024, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2024/2025.

**2.** ***Mheshimiwa Spika;*** Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutujalia baraka na afya njema

na kumudu kuyatekeleza yale tuliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa niaba ya Watanzania wote kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na Tunamuomba Mwenyezi Mungu kwa Rehma zake atukopeshe tena uhai na afya njema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ili tuyatekeleze malengo haya ambayo tunajiwekea leo kwenye Sekta hii ya Viwanda na Biashara.

**3.** ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutimiza miaka mitatu (3) tangu ashike madaraka na kuendelea kuliongoza Taifa letu kwa ujasiri na uzalendo wa hali ya juu. Mwenyezi Mungu azidi kumpa afya njema, hekima na busara ili matamanio ya Watanzania yaweze kufikiwa chini ya uongozi wake. Aidha, namshukuru kwa dhati ya moyo wangu kwa kuendelea kuniamini kuongoza Wizara ya Viwanda na Biashara. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais ya kuwa kwa kushirikiana na Naibu Waziri wangu, Viongozi, Watumishi wa Wizara na Taasisi zake nitaendelea kuyatekeleza majukumu aliyonikabidhi na kufuata miongozo anayonipatia kwa uadilifu na umakini mkubwa.

**4.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miongozo yao yenye kutia chachu na hamasa katika kuimarisha Sekta ya Viwanda na Biashara nchini. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hotuba yake ya Bajeti iliyowasilishwa kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 3 Aprili, 2024. Hotuba hiyo imetoa mwelekeo na dira ya Serikali ya Awamu ya Sita kwa Mwaka 2024/2025 ambayo Wizara ya Viwanda na Biashara itaizingatia katika utekelezaji wake.

**5.** ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba nitumie nafasi hii kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na Hayati Alhaj

Ali Hassan Mwinyi, aliyekuwa Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, natoa pole kwa kuondokewa na Hayati Edward Ngoyai Lowassa, aliyewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Matukio hayo yasiyozoelekeza yalifululiza na kutuacha na majonzi makubwa. Tunaendelea kumuomba Mwenyezi Mungu awarehemu viongozi wetu hao wapendwa, Amina.

**6.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2023/2024 Bunge letu liliondokewa na wapendwa wetu Mheshimiwa Francis Mtenga, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbarali na Mheshimiwa Ahmed Yahya Abdulwakil, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kwahani. Naomba nitoe pole kwako Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote, familia, ndugu na jamaa wa marehemu. Tunaomba mwenyezi Mungu aendelee kuwa mfariji mkuu katika kadhia hizo.

**7.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ninapenda kuungana na viongozi wenzangu kutoa pole kwa wananchi waliokumbwa na maafa mbalimbali yaliyosababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa mali na mazingira. Nitumie fursa hii kuwapa pole wananchi wote waliopoteza ndugu, jamaa na mali zao kutokana na maafa hayo. Mwenyezi Mungu awatie nguvu na kuwapa ahueni waathirika wote ili warejee katika hali njema na hivyo kuendelea kulijenga Taifa letu.

**8.** ***Mheshimiwa Spika;*** Napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi; Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar; na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdullah, Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar kwa kuendelea kusimamia masuala yanayoimarisha Muungano wetu na kuwaletea Watanzania maendeleo. Aidha, namshukuru Mheshimiwa Omar Said Shaban, Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda (SMZ) kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Viwanda na Biashara.

**9.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kipekee, nampongeza

Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb) kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati. Vile, vile, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu walioaminiwa na kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kushika nafasi mbalimbali za Uongozi akiwemo Mheshimiwa Degratius John Ndejembi, Mbunge wa Chamwino na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu); Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi; Mheshimiwa Zainab Athumani Katimba, Mbunge wa Viti Maalum na Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI; na Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile, Mbunge wa Mufindi Kusini na Naibu Waziri wa Wizara ya Uchukuzi.

**10.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuchaguliwa na Baraza la Umoja wa Wabunge Duniani kwa kura nyingi kuwa Rais wa 31 wa Umoja wa Mabunge Duniani (Inter – Parliamentary Union - IPU) ukiwa ni mwanamke wa kwanza kutoka Barani Afrika kushika wadhifa huo kwenye chombo hiki muhimu cha maamuzi ya wabunge duniani kote. Imani hii uliyopewa inathibitisha umahiri na umakini wako katika kuliendesha Bunge letu tukufu kwa weledi wa hali ya juu. Hongera sana na tunakutakia kheri unapoendelea kuliheshimisha Taifa letu katika Siasa za Kimataifa. Vile vile, nawapongeza Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa umakini na umahiri wenu katika kuliongoza na kulisimamia Bunge letu. Mwenyezi Mungu awalinde na kuwasimamia katika kuliendesha Bunge hili kwa umahiri mkubwa na kuweza kusimamia na kuishauri Serikali ipasavyo.

**11.** ***Mheshimiwa Spika;*** Napenda pia kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Njombe Mjini, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, Mbunge wa Viti Maalum na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati kwa ushauri na umakini wao wakati wa kujadili Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Ushauri na maelekezo yao yamekuwa msingi muhimu katika kuandaa Hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Vile vile, nampongeza

Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb) na Mwenyekiti wa Kamati yetu kwa kuaminiwa na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**12.** ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutumia fursa hii kuwashukuru viongozi na watendaji wote wa sekta binafsi; hususan Baraza la Taifa la Biashara; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania; Chama cha Wafanyabiashara, Viwanda na Kilimo Tanzania; na Baraza la Kilimo Tanzania. Vile vile, nazishukuru Benki mbalimbali kwa michango yao katika kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko, Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo.

**13.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inafanya kazi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Hivyo, ninapenda kutumia nafasi hii kuwashukuru wadau wote wakiwemo Washirika wetu wa Maendeleo na wadau wa ndani na nje ya Taifa letu.

**14.** ***Mheshimiwa Spika;*** Nawashukuru pia wamiliki na waandishi wa vyombo vya habari kwa mchango wao mkubwa katika kuelimisha umma wa Watanzania kuhusiana na utendaji wa Wizara na taasisi zake na kuhimiza uzalishaji viwandani. Nawaomba tuendeleze ari hiyo ili tuweze kukuza uelewa kwa umma na hatimaye ushiriki kikamilifu katika kutekeleza masuala ya kuendeleza sekta hii na kutia chachu zaidi kwenye mafanikio tuliyoyapata.

**15.** ***Mheshimiwa Spika;*** Nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Kondoa kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kitaifa na ya Jimbo. Nawapongeza kwa namna wanavyojibidiisha katika kujiletea maendeleo kwa kushiriki shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii. Aidha, ninawaahidi kwamba nitaendelea kutetea maslahi yenu hapa Bungeni na hata nje ya Bunge ili kuhakikisha Jimbo linaendelea kushamiri na kuleta matokeo chanya kwa mtu mmoja mmoja na hatimaye kuongeza mchango wake kwa Taifa letu kwa ujumla.

**16.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii ya Bajeti ninayoiwasilisha leo ni matokeo ya uratibu na ushirikiano mzuri wa viongozi wenzangu katika Wizara, akiwemo Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe - Mbunge wa Mufindi Kaskazini na Naibu Waziri wa Wizara ya Viwanda na Biashara; Dkt. Hashil Twaibu Abdallah, Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara; Wakurugenzi; Wakuu wa Vitengo na Taasisi na Wafanyakazi wote wa Wizara. Napenda kuwapongeza sana. Aidha, namshukuru Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na Wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho mbalimbali ya Wizara kwa wakati.

**17.** ***Mheshimiwa Spika;*** Utekelezaji wa majukumu yangu ambayo muda mwingi nipo nje ya nyumbani usingekuwa rahisi bila Maombi na Dua njema kutoka kwa watu wangu wa karibu. Nawashukuru sana Wazazi wangu wapendwa Baba Alhaj Abdallah Kijaji na Mama yangu Hajat Aziza Selemani. Aidha, namshukuru Mume wangu Kipenzi Dkt. Muhajir Kachwamba na watoto wangu Samirah na Aboubakar; ahsanteni sana kwa upendo, uvumilivu na utayari wenu unaonipatia ari ya kuendelea kuwahudumia Watanzania kwa moyo, uzalendo na ueledi wangu wote. Vile vile, viongozi wangu wa Dini, ndugu, jamaa na marafiki wote; nawashukuru sana kwa kuendelea kuniombea kwa Mwenyezi Mungu ili niendelee kulitumikia Taifa letu. Napenda kuwaahidi nyote na Watanzania kwa ujumla kwamba nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa kutanguliza mbele maslahi ya Taifa.

**18.** ***Mheshimiwa Spika;*** Baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2023/2024 na vipaumbele vya mwaka 2024/2025.

## 2. HALI NA MWENENDO WA SEKTA YA VIWANDA NA BIASHARA NCHINI

### 2.1. Viwanda

**19.** ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya Viwanda na Biashara kwa kiasi kikubwa inategemea shughuli za sekta binafsi ambayo ndiyo inayowekeza mitaji yao viwandani na kwenye miamala ya

kibiashara ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma nchini unakuwepo wakati wote. Hivyo, jukumu kubwa la Wizara ni kusimamia masuala ya utafiti, ushauri, uratibu na kutoa mwelekeo kwenye Tasnia hii ya Viwanda na Biashara.

**20. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kuhamasisha ujenzi na uanzishwaji wa viwanda vikiwemo viwanda vya kuongeza thamani malighafi zinazopatikana nchini hususan mazao ya kilimo, na viwanda vinavyozalisha bidhaa zinazohitajika kwa wingi nchini kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wake, kuzalisha ajira na kukuza mauzo nje ya nchi. Katika jitihada hizo za uhamasishaji, viwanda vipya vimeendelea kujengwa na vingine vimefanyiwa upanuzi kama ifuatavyo:-

***A. Viwanda vya Kuunganisha Magari***

**21. *Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 13 vya magari, kati ya viwanda hivyo, viwanda viwili (2) vinaunganisha magari ambavyo ni *GF Trucks and Equipment Ltd* kilichopo Kibaha, Pwani na *Saturn Corporation Limited* kilichopo Kigamboni, Dar es Salaam. Viwanda 11 vilivyosalia vinatengeneza matrela. Kiwanda cha GF Truck kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha magari 200 kwa mwezi na kimewekeza kiasi cha shilingi bilioni 10.752 na kimetoa ajira 300. Mradi wa Kiwanda cha *Saturn Corporation Limited* umegharimu mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 64.3 na kina uwezo uliosimikwa wa kuunganisha vichwa vya magari 900 na tipa 270 kwa mwezi na umeajiri wafanyakazi 250. Kiwanda kinauza bidhaa zake ndani ya nchi na nje ya nchi pia. Aidha, kiwanda cha TATA ambacho ujenzi wake unaendelea kimewekeza jumla ya shilingi bilioni 19 na kinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kiwanda hicho kitakapokamilika kinatarajia kuunganisha vichwa vya magari, tipa pamoja na pikipiki.

***B. Viwanda vya kutengeneza Vioo***

**22. *Mheshimiwa Spika*;** Tanzania ina jumla ya viwanda vya vioo vitatu (3) vya kuzalisha bidhaa za vioo nchini. Viwanda hivyo ni *Kioo Ltd na Salehbhai Glass Industries Ltd* ambavyo vipo katika Mkoa wa Dar es Salaam na *Sapphire Float Glass (Tanzania)*

*Company Limited* ambacho kipo Mkuranga Mkoa wa Pwani. Kiwanda cha *Kioo Limited* huzalisha chupa za vinywaji na viwanda vilivyosalia huzalisha vioo vya majumbani (Ujenzi). Kiwanda cha *sapphire* kinatumia malighafi zaidi ya asilimia 80 zinazopatikana nchini kuzalisha vioo. Malighafi hizo ni pamoja na madini aina ya *dolomite, silica sand, limestone* na *feldspar*. Kiwanda kimewekeza mtaji wa kiasi cha shilingi bilioni 800.1. Kiwanda hicho kilianza uzalishaji mwezi Septemba, 2023 baada ya kuzinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Kampuni ya KEDA Ceramic Limited inajenga Kiwanda kingine kikubwa cha kutengeneza vioo katika eneo la Mkuranga Mkoa wa Pwani ambacho ujenzi wake umegharimu shilingi bilioni 795 na ujenzi wake umefikia asilimia 80 na kinatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2024. Kiwanda cha KEDA kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kuzalisha tani 600 za vioo kwa siku.

**23.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Sapphire kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 700 kwa siku sawa na tani 189,000 kwa mwaka. Hata hivyo, kwa sasa kiwanda hicho kinazalisha vioo tani 450 kwa siku sawa na tani 121,500 kwa mwaka. Asilimia 60 ya vioo vinavyozalishwa na kiwanda huuzwa nje ya nchi. Nchi hizo ni pamoja na Madagascar, Burundi, Zambia, Rwanda, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na Afrika Kusini. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 1,012 wa ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 3,857 wa ajira zisizo za moja kwa moja. Aidha, kiwanda hicho kitakapofikia uwezo wake wa uzalishaji uliosimikwa kitatoa ajira za moja kwa moja 1,650 na ajira zisizo za moja kwa moja 6,000.

**24.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa kiwanda cha *Kioo Limited* kwa mwaka 2023 kilizalisha bidhaa za chupa zenye uzito wa tani 131,105 na kuuza nje ya nchi yetu tani 67,393 za vioo katika nchi mbalimbali zikiwemo DRC, Malawi, Zimbabwe, Uganda, Rwanda, Kenya na nchi za Bara la Ulaya. Aidha, kiwanda hicho kimewekeza kiasi cha shilingi bilioni 4.4 na kutoa ajira za moja kwa moja 613. Asilimia 80 ya malighafi zinazotumika na kiwanda hicho zinatoka ndani ya Tanzania. Hivyo, Taifa letu lina nafasi kubwa ya kunufaika na masoko ya kikanda kama EAC, SADC na AfCFTA ambayo tumeanza kunufaika kwa kiwango kikubwa na masoko haya.

**C. Viwanda vya Marumaru**

**25.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina viwanda viwili (2) vya marumaru ambavyo ni kiwanda cha *Goodwill (Tanzania) Ceramic Company Ltd* na *KEDA (Tanzania) Ceramics Company Ltd.* Viwanda hivyo vina jumla ya uwezo uliosimikwa wa kuzalisha marumaru mita za mraba 149,000 kwa siku sawa na mita za mraba 40,230,000 kwa mwaka (wastani wa siku 270 kwa mwaka/ siku za kazi). Hata hivyo, viwanda hivyo kwa sasa vinazalisha jumla ya mita za mraba 125,000 kwa siku sawa na mita za mraba 33,750,000 kwa mwaka. Uzalishaji huo unakidhi mahitaji ya marumaru nchini ambayo ni kiasi cha mita za mraba 80,000 kwa siku. Hivyo, viwanda hivi vina ziada ya marumaru mita za mraba 45,000 ambapo kati ya hizo, marumaru zenye mita za mraba 25,000 huuzwa nje ya nchi kwa siku. Aidha, viwanda hivyo vinaendelea na juhudi za kutafuta masoko nje ya nchi.

**26.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Goodwill (T) Ceramic Company Ltd* kipo katika Wilaya ya Mkuranga, Mkoa wa Pwani na kinazalisha bidhaa za aina mbalimbali za marumaru. Kiwanda kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha mita za mraba 100,000 za marumaru kwa siku sawa na mita za mraba 27,000,000 kwa mwaka. Hata hivyo, kiwanda hicho kinazalisha mita za mraba 78,000 kwa siku sawa na mita za mraba 21,060,000 kwa mwaka. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 1,269 wa ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 6,500 ambao ni ajira zisizo za moja kwa moja.

**27.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha KEDA (Tanzania) *Ceramics Company Limited (Twyford)* kilichopo katika Wilaya ya Chalinze, Mkoa wa Pwani, kinazalisha bidhaa za aina mbalimbali za marumaru. Kiwanda kina uwezo uliosomikwa wa kuzalisha mita za mraba 49,000 za marumaru kwa siku sawa na mita za mraba 13,230,000 kwa mwaka. Hata hivyo, kiwanda hiki kwa sasa kinazalisha mita za mraba 47,000 kwa siku sawa na mita za mraba 12,690,000 kwa mwaka. Kiwanda hicho kimeajiri wafanyakazi 1,000 wa ajira za moja kwa moja na ajira 6,000 zisizo za moja kwa moja. Kiwanda cha KEDA kinategemea kufanya upanuzi utakao husisha ujenzi wa majengo na ununuzi wa mitambo yenye thamani ya shilingi bilioni 25.7 kwa ajili ya kuzalisha marumaru.

**D. Viwanda vya Saruji**

**28.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda vya saruji 14 ambapo viwanda vikubwa (intergrated plant) ni saba (7) na vilivyosalia saba (7) ni viwanda vidogo. Kutokana na takwimu za uzalishaji wa saruji kwa mwaka 2023 ambazo zinaakisi hitaji la soko hasa matumizi ya saruji katika miradi mikubwa inaonesha kuwa, viwanda vya saruji nchini vilizalisha tani 9,107,973 za saruji kwa mwaka ambapo mahitaji ya ndani ya nchi ni takriban tani 8,000,000 kwa mwaka. Hivyo, kuna ziada ya tani 1,107,973 ambayo huuzwa nje ya nchi. Viwanda vinavyozalisha saruji na kuuza nje ya nchi ni pamoja na *Dangote Industries Ltd, Tanzania Portland Cement PLC, Lake Cement Co. Ltd, Mbeya Cement Co. Ltd, na Tanga Cement PLC*. Viwanda hivyo huuza saruji katika nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo (DRC) na Zambia. Sekta hiyo imeajiri wafanyakazi 17,885 ambapo kati ya hao, wafanyakazi 4,176 ni ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 13,709 ni ajira zisizo za moja kwa moja.

**29.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika jitihada za kuimarisha uzalishaji kwenye sekta ya saruji, Wizara ilitoa kibali kwa kampuni ya *Amsons Industries (T) Ltd* inayozalisha saruji aina ya *Camel* kuinunua Kampuni ya Mbeya *Cement Company Limited*. Mpango huo unatarajiwa kuwa na manufaa yafuatayo: -

(i) Kuongeza uzalishaji wa kiwanda hicho baada ya wawekezaji wa mwanzo (LafargeHolcim) kuamua kujiondoa Tanzania ambapo uzalishaji wa *Clinker* utaongezeka mara nne (4) na kufikia tani 1,220,000 kutoka tani 305,000 kwa mwaka;

(ii) Kuongezeka kwa uzalishaji wa saruji kwa asilimia 60 hadi kufikia tani 1,680,000 kutoka tani 1,050,000 kwa mwaka;

(iii) Kuwezesha umiliki wa viwanda vikubwa kuwa mikononi mwa watanzania; Kuongeza ajira; na

(iv) Kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi. Kuimarika kwa uzalishaji baada ya muungano huo kutaleta ushindani madhubuti kwa viwanda vikubwa vya saruji ambavyo

vimelitawala soko kwa muda mrefu na kupatikana kwa unafuu wa bei ya saruji.

**30.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara ilifanikiwa kutoa uamuzi wa mwisho wa kuiruhusu kampuni ya *Tanzania Portland Cement Plc* (Twiga Cement) na *Tanga Cement Plc* kuungana kwa lengo la kuongeza uzalishaji na kuboresha ufanisi wa kiwanda cha *Tanga Cement Plc* ambacho kilikuwa na historia ya kujiendesha kwa hasara kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo (2015-2021). Kwa sasa, kiwanda cha *Tanzania Portland Cement PLC* kinajitosheleza kwa malighafi ya *clinker*, hakihitaji kuagiza kutoka nje ya nchi kwa kuwa kinatumia malighafi hiyo kutoka kiwanda cha *Tanga Cement PLC*. Kwa miaka mitatu (3) iliyopita kiwanda hicho kiliagiza *clinker* wastani wa tani 321,000 kwa mwaka. Kufuatia muunganiko huo, hadi kufikia Machi, 2024, uzalishaji wa saruji kwa kampuni ya *Tanga Cement PLC* umeongezeka kutoka tani 980,000 mwaka 2021 hadi kufikia tani 1,200,000. Kuongezeka kwa uzalishaji kunapelekea kuimarika kwa ajira na makusanyo ya kodi yanayotokana na kukua kwa uzalishaji wa viwanda hivyo.

**31.** ***Mheshimiwa Spika;*** Sambamba na hilo**,** Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwenye sekta ya saruji kwa kutoza kodi ya asilimia 35 kwenye saruji inayoingia nchini kwa lengo la kuvilinda viwanda vya ndani. Aidha, Serikali inaendelea kuwahamasisha wazalishaji wa saruji kuongeza uzalishaji ili kupata tija na kuwa shindani katika masoko ya nje likiwemo Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika (AfCFTA).

**32.** ***Mheshimiwa Spika;*** Viwanda vya saruji nchini vinazalisha Clinker ambayo ni malighafi muhimu sana kwa ajili ya kutengeneza bidhaa ya saruji. Viwanda hivi vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha malighafi ya *clinker* tani 7,564,564 kwa mwaka ambapo mahitaji ya soko la saruji nchini, ni sawa na tani 6,000,000 za malighafi ya *clinker*. Hivyo, kuna ziada ya *clinker* ipatayo tani 1,564,564 kwa mwaka. Kwa mwaka 2023, uzalishaji halisi wa *clinker*, ulikuwa na ziada ya tani 652,929 ambapo ziada hiyo iliuzwa katika nchi za DRC, Rwanda, Uganda, Malawi, Zambia na Msumbiji.

***E. Viwanda vya Nguo na Mavazi***

**33.** ***Mheshimiwa Spika;*** Sekta ya nguo na mavazi ina jumla ya viwanda nane (8) vinavyofanya kazi. Viwanda hivyo na mahali vilipo ni: *21 Century Textile Mills Ltd* (Morogoro), *Sunflag Textiles Ltd* (Arusha), Mwatex (2001) Ltd (Mwanza), Namera Textiles Mills (DSM), *NIDA Textiles Mills Ltd* (DSM), *A to Z Textile Mills Ltd* (Arusha), *Manzava Fabrics & Production Ltd* (Morogoro) na *Tanzania Touku Garments* (DSM). Bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo ni pamoja na khanga, vitenge, fulana, vyandarua, blanketi, vitambaa vya pamba (linen), nyuzi, shuka, mavazi, suruali za *jeans* (men's jeans) na nguo za michezo.

**34.** ***Mheshimiwa Spika;*** Viwanda vya nguo vina uwezo uliosimikwa wastani wa kusokota nyuzi (spinning) tani 66,552 kwa mwaka; kuseketa vitambaa (weaving) mita milioni 145 kwa mwaka; kufuma vitambaa (knitting) tani 7,920 kwa mwaka na uwezo wa kutengeneza nguo tofauti tofauti milioni 43 kwa mwaka. Kwa mwaka 2023/2024, viwanda hivyo vimezalisha nyuzi tani 46,586.4 (70%), vimeseketa vitambaa mita milioni 79.75 (55%), vimefuma vitambaa tani 7,128 (90%) na kutengeneza nguo tofauti milioni 98. Ongezeko la kutengeneza nguo limetokana na utumiaji wa vitambaa vya pamba vilivyotengenezwa na viwanda vyetu pamoja na kutumia vitambaa vya polista (polyester fabric) kutoka nje. Bidhaa zinazozalishwa na viwanda hivyo zinauzwa nchini, kwenye nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Afrika Kusini, Ulaya, Canada na Marekani kupitia Sheria ya Fursa ya Ukuaji wa Biashara Afrika (Afica Growth and Opportunity Act - AGOA). Viwanda hivyo vimetoa ajira za moja kwa moja 15,300 na ajira zisizo za moja kwa moja 45,000.

**35.** ***Mheshimiwa Spika;*** Viwanda vya nguo na mavazi vimekuwa vikikabiliana na changamoto mbalimbali zikiwepo; gharama kubwa za kununua pamba kwa wakati mmoja kutokana na upatikanaji wake wa msimu, udanganyifu unaofanywa na wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu, bei kubwa ya nishati ya umeme na uchakavu wa mitambo. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali inaendelea kusaidia sekta binafsi kwa kutekeleza sera zinazolenga kushughulikia vikwazo mbalimbali vya kuendeleza sekta hiyo. Vile vile, Serikali imeondoa Ushuru wa

Forodha katika maeneo mbalimbali kwenye malighafi, vipuri na mashine zinazotumika katika kutengeneza nguo na viatu vya ngozi; na imefuta Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT).

***F. Viwanda vya Mafuta ya Kula***

**36.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda vya kusindika mafuta ya kula 789. Kati ya hivyo, 17 ni viwanda vikubwa na vya kati; na 772 ni vidogo na vidogo sana. Viwanda vidogo na vidogo sana vinatumia asilimia 20 ya uwezo wake wa kusindika mbegu, wakati viwanda vikubwa na vya kati vinatumia asilimia kati ya 25 na 40 ya uwezo uliosimikwa. Aidha, viwanda hivyo vinazalisha tani 205,000 za mafuta ambapo tani 180,000 ni mafuta ya alizeti na tani 25,000 ni mafuta ya mawese na pamba. Mahitaji ya mafuta ya kula nchini ni zaidi ya tani 600,000 kwa mwaka na tani 395,000 huagizwa ili kutosheleza mahitaji ya ndani. Viwanda hivyo vinazalisha chini ya uwezo wake kutokana na kukosekana kwa malighafi ya mbegu bora za mafuta. Sekta hiyo imetoa ajira 5,136 za moja kwa moja na ajira 15,860 zisizo za moja kwa moja.

**37.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuweka mazingira mazuri kwa uwekezaji na hii imepelekea kuongezeka kwa Mikoa inayolima mbegu za mafuta ya kula nchini kutoka mikoa 15 hadi mikoa 19. Mikoa iliyoongezeka ni Tanga, Kilimanjaro, Arusha na Njombe. Hali hii inatokana na uhamasishaji wa programu ya kujitosheleza kwa mafuta ya kula nchini ambapo mikoa yenye uwezo wa kulima mbegu za mafuta imehamasishwa na kuanza kilimo hicho. Aidha, Serikali imeondoa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) katika mafuta yaliyosafishwa yanayozalishwa na viwanda vya ndani kwa lengo la kupunguza bei ya mafuta ya kula ili yaweze kushindana na mafuta yanayotoka nje ya nchi. Vile vile, katika mwaka 2022 Serikali ilifanya Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha na kupunguza ushuru wa uagizaji wa mafuta ghafi ya chikichi (Crude Palm Oil) kutoka asilimia 25 hadi 0. Lengo la mapendekezo hayo lilikuwa ni kusaidia viwanda vya ndani vinavyochakata mafuta ya chikichi (Crude Palm Oil) vipate malighafi na kusaidia upatikanaji wa bidhaa hiyo kwa bei nafuu.

***G. Viwanda vya Chuma na Bidhaa za Chuma***

**38.** ***Mheshimiwa Spika;*** Tanzania ina jumla ya viwanda 28 vya kuzalisha chuma na bidhaa za chuma. Viwanda hivyo vipo katika makundi mbalimbali yanayojumuisha nondo, mabati, mabomba, misumari, senyenge na kadhalika. Kati ya viwanda hivyo, viwanda 19 vinazalisha nondo na vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 1,299,240 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 900,000 kwa mwaka sawa na asilimia 82.8 ya uwezo uliosimikwa. Viwanda tisa (9) vilivyosalia vinazalisha bidhaa nyingine za chuma. Aidha, viwanda hivyo vimeajiri jumla ya wafanyakazi 25,358, kati ya hao wafanyakazi 4,169 ni ajira za moja kwa moja na wafanyakazi 21,189 wa ajira zisizo za moja kwa moja. Kwa ujumla katika kipindi cha mwaka 2022 hadi mwaka 2023, matumizi ya bidhaa za chuma nchini yameongezeka kutoka tani 1,000,000 hadi kufikia tani 1,200,000 kwa mwaka, ikiwa ni ongezeko la asilimia 20. Kwa upande wa viwanda vya nondo, hadi kufikia Machi, 2024, mahitaji ya nondo nchini kwa mwaka ni tani 605,369.6. Hivyo, uzalishaji huo hutosheleza mahitaji yote ya ndani na ziada kiasi cha tani 294,630.4 huuzwa katika nchi za DRC, Burundi na Rwanda.

***H. Viwanda vya Mabati***

**39.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa mabati, Tanzania ina viwanda vikubwa viwili (2) vinavyozalisha bidhaa hiyo kuanzia hatua ya awali (intergrated). Viwanda hivyo ni ALAF na MMI Steel vilivyoko mkoa wa Dar es Salaam vyenye uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jumla ya tani 158,000 kwa mwaka na uzalishaji halisi ni tani 58,189 kwa mwaka sawa na asilimia 37 ya uwezo uliosimikwa. Sambamba na viwanda hivyo vikubwa, Tanzania ina viwanda vidogo zaidi ya 50 ambavyo hufanya kazi ya kuweka migongo na kukata mabati katika vipimo vya urefu unaotakiwa.

**40.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha MMI kimefanya upanuzi ambao umewezesha kuzalisha mabati ya rangi (color roofing) kuanzia ngazi ya awali. Upanuzi huo ulihusisha ujenzi wa jengo na kusimika mitambo mipya ambayo ina uwezo wa kuzalisha mabati tani 50,000 kwa mwaka. Vile vile, viwanda vya Lodhia na ALAF vipo katika hatua ya upanuzi utakaowezesha pia kuzalisha

mabati ya rangi. Kiwanda cha Lodhia kinatarajia kukamilisha upanuzi mwezi Julai, 2024 na pindi kitakapokamilika kitazalisha mabati tani 75,000 kwa mwaka. Aidha, kwa upande wa kiwanda cha ALAF, upanuzi utakamilika mwezi Desemba, 2024 na kuzalisha tani 70,000 za mabati ya rangi. Kwa ujumla upanuzi wa viwanda hivyo unategemea kutoa ajira zaidi ya 10,000.

**I. Viwanda vya Mbolea**

**41.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha kuwa nchi yetu inaondokana na utegemezi wa kuagiza mbolea kutoka nje ya nchi, Wizara imeendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya mbolea ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2024, Tanzania ina jumla ya viwanda 24 **(Jedwali Na. 1).** Kati ya viwanda hivyo, viwili (2) ni vikubwa ambavyo ni Minjingu na *Intracom Fertilizer Limited*; kimoja (1) ni cha kati; na vilivyosalia (21) ni viwanda vidogo ambavyo hufanya kazi ya kuchanganya mbolea (Blending)

**42.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha mbolea cha *Itracom Fertilizer Limited* kilichopo eneo la Nala jijini Dodoma kimesimika mitambo miwili (2) iliyo na uwezo wa kuzalisha tani 400,000 za mbolea kwa mwaka. Vile vile, kiwanda kina mitambo mitatu (3) ambayo ipo katika hatua ya kufungwa na itakamilika mwezi Juni, 2024. Kiwanda kimetoa ajira 1,000 katika ujenzi na uzalishaji kwa pamoja. Ajira za moja kwa moja ni 393 na zisizo za moja kwa moja ni 607. Usimikaji mitambo yote ukikamilika kiwanda kitatoa ajira za moja kwa moja 3,000 na ajira zisizo za moja kwa moja 8,000. Kiwanda hicho kinategemea kuwekeza kiasi cha shilingi bilioni 463.1 na kitakuwa na uwezo wa kuzalisha mbolea tani 1,000,000 na chokaa tani 300,000 kwa mwaka.

**43.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha mbolea cha Minjingu kipo katika eneo la Minjingu katika Mkoa wa Manyara. Kiwanda kimewekeza mtaji kiasi cha shilingi bilioni 50 na kina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha tani 100,000 za mbolea aina ya *Phosphate* kwa mwaka. Hata hivyo, kwa sasa kiwanda kinazalisha tani 50,000 na kimetoa ajira 175 za moja kwa moja na ajira 560 zisizo za moja kwa moja. Aidha, kwa sasa kiwanda kipo kwenye hatua za mwisho za kuongeza upanuzi na usimikaji wa mitambo zaidi ya kuzalisha mbolea aina ya NPK yenye uwezo wa

kuzalisha tani 150,000 na kufanya jumla ya uwezo wa uzalishaji kufikia tani 250,000 kwa mwaka 2025.

**44.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa sasa mahitaji ya mbolea ni tani 1,000,000 ambapo zaidi ya asilimia 60 ni mbolea ya chumvi chumvi ambayo huagizwa kutoka nje ya nchi. Kwa ujumla uzalishaji wa mbolea nchini unaendelea kuimarika ambapo hadi kufikia mwaka 2025 uzalishaji unatarajiwa kuwa tani zaidi ya 1,000,000 kwa mwaka. Malighafi zinazotumika kuzalisha mbolea katika viwanda vyetu hupatikana hapa nchini na nyingine huagizwa kutoka nje ya nchi hususan mbolea ya chumvi chumvi. Aidha, ili kupunguza uagizaji wa mbolea nje ya nchi, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta mwekezaji mahiri atakayeweza kutumia gesi asilia kuzalisha mbolea ya chumvi chumvi.

**45.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kujengwa kwa viwanda vipya pamoja na upanuzi wa viwanda vya zamani ni ushuhuda tosha kwamba imani ya wawekezaji kwenye eneo la viwanda imeongezeka. Na haya ni majibu ya jitihada za kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Jemedari wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hakika kazi yake ni njema sana na anastahili pongezi na tuzo ya heshima. Hongera sana Mheshimiwa Rais wetu.

### 2.2. Biashara

**46.** ***Mheshimiwa Spika***; Tanzania ina fursa mbalimbali za masoko ya kuuza mazao na bidhaa zinazozalishwa. Katika kutumia fursa hizo, Wizara imeendelea kushiriki majadiliano ya biashara baina ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (*Regional*) na Kimataifa (*Multilateral*) lengo likiwa ni kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu ya bidhaa na huduma na kuvutia biashara nchini. Katika mwaka 2023/2024 mwenendo wa biashara ulikuwa kama ifuatavyo: -

***A. Soko la Ulaya***

**47.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika Soko la Ulaya iliongezeka hadi kufikia shilingi trilioni 3.836 kutoka shilingi trilioni 2.446 mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 56.8 **(Jedwali Na. 2).** Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa za kilimo na viwandani kwenda katika nchi hizo. Aidha, uagizaji wa bidhaa kutoka Jumuiya ya Ulaya ulipungua kwa asilimia 8.1 hadi shilingi trilioni 4.045 mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.404 kwa mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa za viwandani na mitaji kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa zilizokuwa zinaagizwa kutoka Soko la Ulaya ikiwemo vilainishi vya magari**.**

***B. Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)***

**48.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2023, Tanzania iliendelea kuboresha mahusiano ya kibiashara na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Katika kipindi hicho, thamani ya bidhaa zilizouzwa kwenye soko hilo ilikuwa shilingi trilioni 3.022 ikilinganishwa na shilingi trilioni 3.415 mwaka 2022 ikiwa ni upungufu wa asilimia 16.6 **(Jedwali Na. 3).** Hali hiyo imechangiwa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa za kilimo, hususan kahawa, chai, mahindi, ngano, mchele, mbogamboga na bidhaa za viwandani zikiwemo vigae, na saruji. Kupungua kwa mauzo, mfano kahawa kumesababishwa na Tanzania kuuza bidhaa husika moja kwa moja kwenye masoko ya nje tofauti na ilivyokuwa awali ambapo bidhaa hiyo iliuzwa kupitia nchi ya Kenya. Vile vile, kuongezeka kwa mahitaji ya ndani kwa bidhaa za ujenzi ikiwemo vigae, saruji, chuma na bidhaa za chuma.

**49.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2023, bidhaa zenye thamani ya shilingi trilioni 1.34 ziliagizwa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ikilinganishwa na bidhaa zenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 9. Upungufu huo umechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani nchini na kusababisha kupunguza manunuzi ya bidhaa za viwandani kutoka nchi za jirani ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

## C. Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)

**50.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2023, thamani ya bidhaa zilizouzwa katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) ilikuwa ni shilingi trilioni 4.422 ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.614 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 4.1 **(Jedwali Na. 4).** Upungufu huo umetokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la ndani kwa bidhaa zilizokuwa zikiuzwa katika soko hilo ikiwemo chuma na bidhaa za chuma, pamba, vigae na saruji. Vile vile, bidhaa zilizouzwa kwa wingi katika soko hilo ni pamoja na madini, chai, parachichi, vioo vya kujengea, kahawa, vyandarua, sabuni na mafuta ya kupaka. Aidha, kwa mwaka 2023, bidhaa zilizoagizwa kutoka SADC zilikuwa na thamani ya shilingi trilioni 2.01 ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.411 mwaka 2022.

## D. Bara la Asia

**51.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2023, thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia hususan kwa nchi za China, India, Japan na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ilikuwa shilingi trilioni 7.486 ikilinganishwa na shilingi trilioni 10.948 mwaka 2022 sawa na upungufu wa asilimia 31.6. Vile vile, katika kipindi husika, uagizaji wa bidhaa kutoka nchi za Bara la Asia ulikuwa na thamani ya shilingi trilioni 21.528 ikilinganishwa na shilingi trilioni 23.324 mwaka 2022, sawa na upungufu wa asilimia 7.7. Upungufu huo ulitokana na kupungua kwa bidhaa za mitaji na bidhaa za kawaida zilizokuwa zikiagizwa kutoka Bara la Asia.

## *E. Soko la Marekani Kupitia Mpango wa AGOA*

**52.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwaka 2023, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia mpango wa AGOA yalikuwa jumla ya shilingi bilioni 205.824 ikilinganishwa na shilingi bilioni 192.256 kwa mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 7.06 **(Jedwali Na. 5).** Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za nguo na mavazi zinazouzwa kwenye soko hilo. Katika jitihada za kutumia zaidi fursa ya soko la AGOA, Tanzania imeomba kuongezewa miaka 10 baada ya ukomo wa mpango wa AGOA ambao unaisha mwaka 2025.

### *F. Soko la Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA)*

**53.** ***Mheshimiwa Spika;*** Biashara ya ndani ya Afrika imeendelea kukua siku hadi siku kutokana na kuanza kwa utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA) mwezi Januari, 2021. Kupitia mkataba huo, nchi zimeanza kuondoleana vikwazo vya kibiashara vya kiushuru na visivyokuwa vya kiushuru. Aidha, katika kujipanga kukuza biashara ndani ya Bara la Afrika, Wizara imekamilisha Mkakati wa Kitaifa kwa ajili ya kutekeleza mkataba huo. Kupitia mkakati huo, Wizara imeunda kamati ya kitaifa ya utekelezaji wa mkataba wa AfCFTA. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na vyama vya wafanyabiashara na wadau mbalimbali wa maendeleo, imeendelea kutoa mafunzo, warsha na semina kwa wafanyabishara na wajasiriamali kuhusu fursa za soko hilo.

**54.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia fursa hiyo, jumla ya makampuni 11 ya Tanzania yameweza kuuza bidhaa zake katika nchi mbalimbali za Afrika kupitia mkataba huo kwa kutumia cheti cha uasili wa bidhaa cha AfCFTA ambapo, jumla ya vyeti 24 vimeweza kutolewa kwa Kampuni hizo. Bidhaa ambazo zimeuzwa kwa wingi kupitia vyeti hivyo ni nyuzi za katani tani 426.4 kwenda nchi za Nigeria, Ghana, Morocco na Misri, kahawa tani 273.3 kwenda nchini Algeria na tumbaku tani 21.1 kwenda Nigeria. Faida zilizopatikana kwa wafanyabiashara hao ni kuweza kuuza bidhaa zao kwa kutozwa ushuru pungufu ikilinganishwa na ilivyokuwa awali. Wizara inaendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kutumia fursa ya soko hilo kubwa kuweza kuuza bidhaa zao na kuongeza uzalishaji.

### 2.3. Mwenendo na Bei za Bidhaa Muhimu za Viwandani

**55.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kukusanya na kuchambua taarifa za mwenendo wa bei za bidhaa za viwandani, hususan bidhaa za mabati, nondo na saruji na kutoa taarifa kwa umma kuhusu mwenendo wa bei za bidhaa hizo tarehe 15 ya kila mwezi. Taarifa hizo hutangazwa katika vyombo vya habari vikiwemo redio, magazeti na pia husambazwa kupitia tovuti ya Wizara. Lengo ni kuwawezesha wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na watumiaji wa bidhaa hizo kupata taarifa za bei za

bidhaa zitakazowasaidia kufanya ulinganifu wanapotaka kununua bidhaa hizo na hatimaye kufanya maamuzi sahihi.

**56.** ***Mheshimiwa Spika;*** Bei ya wastani ya saruji nchini kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 unaonesha kuwa bei ya saruji aina ya 32.5N ilikuwa ni shilingi 18,996 kwa mfuko wa kilo 50. Vile vile, bei ya wastani ya saruji aina ya 42.5N katika kipindi hicho ilikuwa ni shilingi 20,232 kwa mfuko wa kilo 50.

**57.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa bidhaa za nondo, hususan nondo za mm 10 na mm 12 ambazo ndizo zinatumiwa na wananchi wengi nchini, bei ya wastani ya nondo ya mm 10 nchini kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikuwa ni shilingi 19,542 kwa nondo, wakati bei ya wastani ya nondo mm 12 kwa kipindi hicho ilikuwa ni shilingi 24,800.

**58.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa upande wa bati nyeupe geji 30 na geji 28, bei ya wastani ya bati hizo kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2023 hadi Machi, 2024 ilikuwa ni shilingi 24,021 na shilingi 34,095 kwa bati mtawalia.

### 2.4. Mchango wa Sekta ya Viwanda na Biashara Nchini

**59.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa kwa mwaka 2023 ulikuwa asilimia 7.0 ikilinganishwa na asilimia 7.1 mwaka 2022**.** Aidha, ukuaji wa Sekta ya Viwanda ulikuwa asilimia 4.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.2 mwaka 2022.

**60.** ***Mheshimiwa Spika; Mchango*** wa Sekta ya Biashara katika Pato la Taifa kwa mwaka 2023 ulikuwa asilimia 8.3 ikilinganishwa na asilimia 8.2 mwaka 2022. Aidha, kasi ya ukuaji wa Sekta ya Biashara ilikuwa asilimia 4.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.9 mwaka 2022. Ukuaji huo umechangiwa na uboreshaji wa mazingira ya ufanyaji biashara.

## 3. MIKAKATI INAYOSIMAMIWA NA WIZARA

**61.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara inasimamia mikakati mbalimbali ambayo inaiwezesha kufikia malengo yake. Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

***i. Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika wa Mwaka 2023***

**62.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara Afrika wa mwaka 2023. Zoezi linaloendelea kwa sasa ni ukamilishaji wa Hadidu za Rejea za Kamati ya Kitaifa itakayosimamia utekelezaji wa Mkakati huo ambazo zinatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwezi Juni, 2024. Lengo la Mkakati ni kuweka mazingira mazuri ya biashara nchini ili kuhakikisha wafanyabiashara na wawekezaji wa kitanzania wanatumia ipasavyo fursa za biashara zilizopo katika soko la Eneo Huru la Biashara Afrika pamoja na kuendelea kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu fursa mbalimbali za soko hilo.

***ii. Mkakati wa Taifa wa Biashara Mtandao wa Mwaka 2024/2025 – 2029/2030 (National E-Commerce Strategy)***

**63.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha tunaenda sambamba na maendeleo na mabadiliko yanayotokea duniani katika nyanja ya biashara, Wizara inaendelea na ukamilishwaji wa Mkakati wa Taifa wa Biashara Mtandao *(National E-Commerce Strategy)*. Lengo la mkakati huo ni kuwezesha zaidi Watanzania kufanya biashara kwa njia ya mtandao pamoja na kuweka mazingira rafiki na salama ya kufanya biashara kwa njia ya mtandao. Faida za kuwa na Mkakati huo ni pamoja na: Kuwa na mfumo wa Biashara Mtandao ulio salama na wenye kuaminika kwa Watanzania na wadau wengine; Kuongezeka kwa mchango wa biashara mtandao katika Pato la Taifa; Kuongezeka kwa teknolojia wezeshi za mawasiliano na biashara kwa njia ya mtandao; na Kuongezeka kwa jamii yenye maarifa katika masuala ya biashara kwa njia ya mtandao na hivyo kukuza fursa ya ajira ndani na nje ya nchi. Mkakati huo utahusisha maeneo makuu matano (5) ambayo ni:- Miundombinu ya TEHAMA na Huduma za Mawasiliano ya Simu; Mfumo wa Malipo ya

Kimtandao; Usafirishaji na Uchukuzi; Maendeleo katika Ujuzi na Maarifa; na Masuala ya Kisera na Kisheria. Rasimu ya Mkakati huo imekamilika na hatua iliyopo ni kupata maoni ya wadau.

## 4. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2023/2024

**64.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2023/2024, Wizara imeendelea kutekeleza maeneo ya kipaumbele ikiwemo kuendeleza miradi ya Kielelezo ya Makaa ya Mawe – Mchuchuma na Chuma cha Liganga; Magadi Soda Engaruka; Kuendeleza Kiwanda cha Kilimanjaro Machine Tools -KMTC; Kuratibu majadiliano baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa; na Kuboresha mazingira ya biashara. Maeneo mengine ya kipaumbele ni: Kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania; Kuendeleza mitaa ya viwanda; Kukuza na kuboresha hali ya ushindani sokoni, ubunifu, urasimishaji wa biashara, uhawilishaji na ukuzaji wa teknolojia.

### 4.1. Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka 2023/2024

#### 4.1.1. Fedha Zilizoidhinishwa

**65.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2023/2024 Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Fungu 44 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 92,348,837,623. Kati ya fedha hizo, shilingi 66,698,567,623 ziliidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida fedha hizo zinajumuisha shilingi 9,254,956,938 za Matumizi Mengineyo (OC) na shilingi 57,443,610,685 za Mishahara. Aidha, shilingi 25,650,270,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

#### 4.1.2. Fedha Zilizopokelewa

*a) **Fedha za Matumizi ya Kawaida***

***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia mwezi Machi, 2024, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya shilingi 50,376,084,589.17, sawa na asilimia 76.03 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 7,069,975,635.15 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC), sawa na asilimia 79.09 na shilingi 43,306,108,954.02 kwa ajili ya Mishahara sawa na asilimia 75.56 ya fedha zilizotengwa.

***b) Fedha za Maendeleo***

**66.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia mwezi Machi, 2024 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 9,770,269,727.63 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 38.09 ya fedha zilizotengwa.

**4.2. Utekelezaji wa Mipango**
**4.2.1. Maendeleo ya Viwanda**

**A. Tathmini ya Sekta Ndogo ya Mkonge**

**67.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanya utafiti katika sekta ndogo ya mkonge kwa lengo la kupima ufanisi wa viwanda vilivyoko katika sekta ndogo hiyo. Matokeo ya utafiti huo yamebaini uwepo wa viwanda 56 vinavyosindika mkonge kupata nyuzi (singa); kuongezeka kwa uzalishaji wa singa kutoka tani 36,379.08 mwaka 2019 hadi tani 56,732.70 mwaka 2023; na uwepo wa viwanda sita (6) vinavyozalisha bidhaa za mkonge (magunia, mazulia na kamba). Viwanda hivyo ni TPM 1998, *Sisalana Tanzania Company Ltd (cordage), Ubena Spinning Mill, Amboni Spinning Mill, Winafr company Ltd,* na *Tanga Sisal Spinning Mills.* Vile vile, tathmini imebaini viwanda hivyo sita (6) vina uwezo uliosimikwa wa kuzalisha jumla ya tani 48,760 za bidhaa za mkonge. Aidha, katika miaka mitano (5) iliyopita viwanda hivyo vilizalisha jumla ya tani 24,792 ya bidhaa za mkonge.

**68.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mwenendo wa mauzo ya nyuzi (singa) unaonesha kuwa, nyuzi huuzwa zaidi nje ya nchi ikilinganishwa na biashara ya ndani. Biashara ya ndani ni wastani wa tani 12,947.86 kwa mwaka ikilinganishwa na tani 26,737.60 za mauzo ya nje ambapo wastani wa mapato ya biashara ya ndani kwa mwaka ni shilingi bilioni 39.76 ikilinganishwa na shilingi bilioni 105.41 kwa mauzo nje ya nchi. Sekta ya mkonge kwa ujumla wake imechangia kutoa ajira 1,904,293.

***B. Kuwezesha Uanzishwaji wa Viwanda Vipya na Kongani za Viwanda***

**69.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika jitihada za kuendelea kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani, Wizara inaratibu uanzishwaji wa Kongani za Viwanda na Maeneo Maalum ya Kiuchumi kama ifuatavyo:-

**i. Kongani ya Viwanda ya Kwala-Pwani**

**70.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imewezesha uratibu wa ujenzi wa kongani iliyopo katika eneo la Kwala Mkoa wa Pwani ambapo kunatarajiwa kuwa na viwanda 202 pindi ujenzi utakapokamilika. Katika hatua ya awali ya ujenzi ambayo inahusisha ekari 500 kati ya 2,500, ujenzi uliokamilika ni pamoja na barabara kuu ya ndani, jengo la utawala ambalo litakuwa na Taasisi za Serikali (*one stop centre*), jengo la zimamoto, jengo la hosteli, majengo mawili ya viwanda na jengo la kufundishia mafundi. Ujenzi unaoendelea kwa sasa ni pamoja na majengo mawili (2) ya viwanda ambayo yamekamilika kwa asilimia zaidi ya 50. Aidha, ujenzi wa umeme mkubwa (50 MW) umefikia asilimia 60 ambapo nguzo tayari zimesimikwa na kwasasa uvutaji wa nyaya za umeme unaendelea.

**71.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika Kongani hiyo, tayari viwanda viwili (2) vimeanza uzalishaji ambavyo ni kiwanda cha nguo cha *House of Garments* kilichoajiri wafanyakazi 50. Kiwanda cha pili ni cha vipodozi *KVS Chemicals* ambacho kina jumla ya wafanyakazi 25. Mwekezaji ambaye ni *Sino Tan* anatarajia kukamilisha ujenzi wote wa kongani ifikapo mwaka 2027.

**ii. Kongani ya Kisasa ya Viwanda (Modern Industrial Park) – Pwani**

**72.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa Kongani ya Kisasa ya Viwanda ulianza kujengwa mwezi Julai, 2023 katika eneo la ekari 1,077 huko Disunyara/Kikongo, Wilaya ya Chalinze. Pindi ujenzi utakapokamilika unatarajiwa kugharimu jumla ya shilingi trilioni 3.5. Eneo hilo limegawanywa katika viwanja 210, ambapo viwanja 202 ni kwa ajili ya viwanda, viwanja viwili (2) ni kwa ajili ya vituo vya umeme, viwanja viwili (2) ni vya maeneo ya biashara,

viwanja vitatu (3) ni kwa ajili ya huduma za jamii na kiwanja kimoja (1) ni kwa ajili ya bandari kavu na eneo lililobaki ni kwa ajili ya miundombinu ya barabara. Hadi kufikia Machi, 2024 viwanja vilivyouzwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda ni 10 na viwanja vilivyoshikiliwa vikisubiri kusainiwa kwa mikataba ni 24. Aidha, wawekezaji watatu (3) wamekamilisha hatua za awali za ujenzi ambazo ni Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA) na michoro.

***iii. Kuendelea na Ujenzi wa Miundombinu ya Msingi katika Kongani ya Viwanda – TAMCO***

**73.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kufanya uboreshaji wa miundombinu katika Kongani ya TAMCO – Kibaha linalosimamiwa na NDC yenye ukubwa wa ekari 182.893 sawa na mita za mraba 741,143 ambapo ekari 115 sawa na asilimia 63 ya eneo lote zimekodishwa kwa wawekezaji saba (7). Eneo hilo lina viwanda vinne (4) vinavyoendelea na uzalishaji ambavyo ni: - Kiwanda cha *Tanzania Biotech Company Limited* kinachozalisha bidhaa za kibiolojia; Kiwanda cha *Hester Bioscience Limited* kinachozalisha Chanjo za Wanyama; Kiwanda cha *Global Packing Limited* kinachozalisha Vifungashio; na Kiwanda cha *GF Vehicle Assemblers Limited* kinachounganisha magari. Viwanda hivyo, vimezalisha ajira za moja kwa moja 329 na zisizo za moja kwa moja 658.

**74.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imekamilisha ujenzi wa barabara yenye urefu wa mita 230 kwa kiwango cha lami. Barabara zilizoboreshwa zimefikia urefu wa kilomita 1.53 kati ya kilomita 4.5 ndani ya eneo la TAMCO. Maboresho hayo yamesaidia kupunguza adha ya uharibifu wa barabara hasa katika kipindi cha mvua. Aidha, kutokana na uboreshaji wa miundombinu, wawekezaji wapya watatu (3) ambao ni Kampuni ya TATA wameanza kujenga Kiwanda kikubwa cha Kuunganisha Magari na Mitambo; na Kampuni za *New Force na Fortes Energies* ambazo zimeanza ujenzi wa miundombinu ya huduma wezeshi zikiwemo Kituo cha mafuta kwa ajili ya viwanda na magari makubwa na kituo cha biashara ambacho kitakuwa na huduma mbalimbali zikiwemo za kibenki.

*4.2.2. Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo*

***A. Kutunisha Mtaji wa Mfuko wa Wajasiriamali Wananchi (NEDF)***

**75.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara kupitia Mfuko wa Wajasiriamali Wananchi (NEDF) imeweza kutoa jumla ya mikopo 956 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.3 kwa riba ya asilimia 9. Asilimia 51 ya mikopo hiyo ilitolewa kwa wanawake na asilimia 28 ilitolewa kwa miradi ya vijijini. Vile vile, Wizara iliweza kuwaunganisha wajasiriamali wawili (2) kupitia Mfuko wa Dhamana wa Serikali (CGS) na kupata mikopo minne (4) yenye thamani ya shilingi milioni 120 na kutengeneza ajira 12 kupitia Benki ya CRDB. Aidha, kupitia programu ya SANVN, SIDO, Azania Bank, NSSF, VETA na NEEC waliingia Hati ya Makubaliano mwaka 2020. Kupitia makubaliano hayo, wanufaika wa SIDO katika sekta ya viwanda wanaohitaji mikopo wanaunganishwa na Benki ya Azania na kupata mkopo kuanzia shilingi milioni 8 hadi milioni 500. Hivyo, mikopo 11 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.3 ilitolewa kupitia Azania Benki na kutengeneza ajira 103 katika mwaka 2023/2024.

**B. Wajasiriamali Walioelelewa na Kukua Kupitia SIDO**

**76.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea na jitihada za kuwalea na kuwakuza wajasiriamali kupitia SIDO. Hadi kufikia Machi, 2024 kulikuwa na jumla ya wajasiriamali watano (5) waliolelewa na kukua kupitia SIDO. Wajasiriamali hao ni wamiliki wa Kiwanda cha *Akross Ltd* – Mtwara; Kiwanda cha Kigoma *Tansoap Enterprises* – Kigoma; Kiwanda cha *Choice Coffee* – Kilimanjaro; Kiwanda cha *BAKEL Company Ltd- Dodoma na Kiwanda cha Double Natural Products* - *Mbeya*. Maelezo ya kila kiwanda ni kama ifuatavyo: -

**i. Kiwanda cha Akross Ltd - Mtwara**

**77.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Akross Ltd kilichopo Manispaa ya Mtwara Mikindani Wilaya ya Mtwara kinachojihusisha na ubanguaji Korosho kilianza uzalishaji mwaka 2018 kwa mtaji wa shilingi milioni 20 na kuajiri wafanyakazi 50 ambapo mauzo yake yalikuwa kiasi cha shilingi milioni 100 kwa mwaka. Aidha, kiwanda kimeendelea kulelewa na SIDO kwa

kupewa jengo la kuzalishia bidhaa lenye ukubwa wa mita za mraba 300 na kuweza kukua. Kwa sasa, kiwanda kimeongezewa majengo kufikia ukubwa wa mita za mraba 1,150 pamoja na eneo la wazi kwa shughuli za ubanguaji wa korosho. Hadi kufikia Machi, 2024, Kiwanda hicho kilikuwa na mtaji wa shilingi milioni 400. Kiwanda kimeajiri wafanyakazi 350 (Wanaume 12 na wanawake 338) na kinazalisha tani 145 za korosho kwa mwaka. Kati ya tani zinazozalishwa, tani tano (5) huuzwa katika soko la ndani na tani 140 huuzwa soko la nje katika nchi za Misri, Kuwait, Dubai, Bahrain, Canada na Afrika ya Kusini. Mauzo ya kiwanda hicho kwa mwaka ni shilingi bilioni 1.5 kwa sasa.

**ii. Kiwanda cha Kigoma Tansoap Enterprises - Kigoma**

**78. *Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha Kigoma *Tansoap Enterprises* kilichopo katika Mkoa wa Kigoma kinachojishughulisha na utengenezaji wa sabuni aina mbalimbali zikiwemo sabuni za mche na maji kilianzishwa mwaka 2006 kwa mtaji wa shilingi milioni nne (4) na kutoa  ajira za moja kwa moja (3) na ajira 12 zisizo za moja kwa moja ambapo mauzo yalikuwa shilingi milioni 35.16 kwa mwaka. Kiwanda kimesajiliwa na kupata nembo ya ubora kutoka Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na hivyo kutanua wigo wake wa soko. Kutokana na jitihada hizo, hadi kufikia Machi, 2024 mauzo yameongezeka na kufikia kiasi cha shilingi milioni 114 kwa mwaka na kuongeza ajira kufikia wafanyakazi 11 wa kudumu na wa muda 37. Vile vile, bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho huuzwa nchi ya Kenya na hivyo kupelekea kuchangia pato la nchi.

**iii. Kiwanda cha Choice Coffee - Kilimanjaro**

**79. *Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Choice Coffee* kilichopo Wilaya ya Moshi, Mkoa wa Kilimanjaro kinachojishughulisha na utengenezaji wa Kahawa, kilianzishwa mwaka 2004 kwa mtaji wa shilingi laki 3 na kuajiri watu watatu (3) ambapo mauzo yalikuwa shilingi milioni mbili (2) kwa mwaka. Aidha, Kiwanda hicho kimeendelea kulelewa na SIDO na kuweza kukua ambapo hadi kufikia Machi, 2024, kiwanda kina mtaji wa shilingi milioni 70 na kuajiri wafanyakazi 20. Kiwanda kinazalisha tani mbili (2) kwa mwezi na kina mauzo ya shilingi milioni 384 kwa mwaka. Kati ya

tani zinazozalishwa, tani 1.5 huuzwa soko la ndani na tani 0.5 huuzwa soko la nje katika nchi za Ulaya.

**iv. Kiwanda cha BAKEL Company Ltd- Dodoma**

**80.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *BAKEL Company Ltd* cha kutengeneza Mvinyo wa Zabibu kilichopo Wilaya ya Dodoma Mjini, kilianza mwaka 2019 kwa mtaji wa shilingi 500,000 na ajira za watu watatu (3) ambapo mauzo yake yalikuwa shilingi 600,000 kwa mwaka. Aidha, Kiwanda hicho kimeendelea kulelewa na SIDO na kuweza kukua na kufikisha mtaji wa shilingi milioni 340 na kuajiri wafanyakazi 63 kati ya hao, 31 ni wa ajira za moja kwa moja na 32 ni ajira zisizo za moja kwa moja. Vile vile, kiwanda hicho kinazalisha lita 60,000 kwa mwaka na kufanya mauzo ya shilingi milioni 385.2 ambapo lita 50,000 huuzwa soko la ndani na lita 10,000 soko la nje katika nchi ya Kenya.

**v. Kiwanda cha Double Natural Products - Mbeya**

**81.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kiwanda cha *Double Natural Products* kilichopo Mkoa wa Mbeya kinachojihusha na usindikaji wa unga wa mbegu za parachichi, vipodozi, mafuta ya nywele, mafuta ya kupaka na sabuni za kufulia kilianzishwa mwaka 2017 kwa mtaji wa shilingi 150,000 na kutoa ajira kwa wafanyakazi watatu (3) ambapo mauzo yake yalikuwa shilingi milioni 2 kwa mwaka. Aidha, kiwanda kimeendelea kulelewa na SIDO na kukua ambapo kwa sasa kiwanda kina mtaji wa shilingi milioni 50 na kuajiri wafanyakazi 25.

**vi. Utoaji wa Mikopo Kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania kwa ajili ya Uongezaji Thamani Mazao ya Kilimo na Mifugo**

**82.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Serikali kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ilitoa mikopo ya shilingi bilioni 108.43 ili kuwezesha uanzishaji na uendelezaji wa viwanda vya uongezaji thamani wa mazao ya kilimo na mifugo nchini. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 38.003 zilitolewa kwa ajili ya uwekezaji na shilingi bilioni 70.427 zilitolewa kwa ajili ya uendeshaji. Aidha,

uwekezaji huo umeendelea kuwahakikishia masoko ya uhakika wakulima, wafugaji na wavuvi nchini.

**83.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya viwanda 37 vilikopeshwa na TADB. Mikopo iliyotolewa kwa njia ya moja kwa moja ilielekezwa kwenye maeneo yafuatayo;

i. Viwanda vya kukamua mafuta ya kula (oil seeds) ambapo mikopo ya shilingi bilioni 19.0 ilitolewa kwa viwanda vitatu (3) vilivyopo katika Mkoa wa Pwani na Singida;

ii. Viwanda vya mahindi na mpunga ambapo mikopo ya shilingi bilioni 22.7 ilitolewa kwenye viwanda 12 vilivyopo katika Mikoa ya Shinyanga, Katavi, Tabora, Kigoma, Ruvuma, Pwani, Mbeya na Iringa; iii. Viwanda vya nyama, maziwa na vyakula vya mifugo ambapo mikopo ya shilingi bilioni 7.0 ilitolewa kwenye viwanda sita (6) vilivyopo katika Mikoa ya Kilimanjaro, Pwani, Kagera na Dar es Salaam;

iii. Viwanda vya awali vya kuchambua zao la pamba (primary processing) ambapo mikopo ya shilingi bilioni 31.3 ilitolewa kwenye viwanda vitano (5) vilivyopo katika Mikoa ya Geita, Shinyanga, Mwanza na Simiyu; na

iv. Viwanda vya awali vya kuchakata zao la kahawa (primary processing) ambapo mikopo ya shilingi bilioni 26.9 ilitolewa kwenye viwanda sita (6) vilivyopo katika Mikoa ya Kagera na Songwe.

**84.** ***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, jumla ya shilingi bilioni 1.5 zilitolewa kwa njia ya moja kwa moja kusaidia viwanda vidogo vidogo vya uchakataji wa mazao ya zabibu, parachichi, korosho pamoja na uzalishaji wa viuatilifu vilivyopo katika maeneo mbalimbali nchini.

**85.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia mfuko wa dhamana kwa wakulima wadogo (SCGS), TADB ilitoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 34.299. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 21.17 kilielekezwa kwenye miradi ya uchakataji wa mazao ya kilimo, shilingi bilioni 8.086 zilitumika kufadhili miradi ya

kutengeneza pembejeo za kilimo na shilingi bilioni 5.043 zilitolewa kuwezesha kiwanda cha kutengeneza vifungashio vya bidhaa za kilimo (packaging materials).

**86.** ***Mheshimiwa Spika;*** Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kiwanda kikubwa na cha kisasa cha uzalishaji wa mafuta ya soya, alizeti, pamba na chikichi kinachojengwa Mkoa wa Pwani kupitia mkopo wa TADB kitaanza uzalishaji hivi karibuni. Kiwanda hicho chenye uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita 70,000 za mafuta kwa siku kinatarajiwa kupunguza pengo la uzalishaji wa mafuta ya kula na utegemezi wa uagizaji mafuta ya kula kutoka nje ya nchi.

**87.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, hadi kufikia Machi, 2024, TADB imefanikisha ujenzi wa kiwanda kikubwa cha kuku kinachotumia teknolojia ya kisasa (full automated) kuanzia kwenye hatua ya ututoleshaji wa vifaranga na kuwafungasha kuku kwa ajili ya kwenda sokoni. Kiwanda hicho kina uwezo wa kutunza kuku 100,000 kwa kila mzunguko na kufanya shunguli za kuchinja na kupaki kuku 3,000 kwa saa moja. Kiwanda hicho ni moja ya viwanda vya kuku vikubwa katika eneo la Afrika Mashariki.

**88.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ili kujenga uchumi shindani wa viwanda na kuiletea nchi yetu maendeleo, TADB itaendelea kuchagiza uwekezaji wa sekta binafsi kwa kutoa mikopo kwa wadau wa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuzingatia mahitaji na fursa katika mnyororo mzima wa thamani ikiwemo mikopo kwa waongezaji wa thamani wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi.

***4.2.3. Mtangamano wa Biashara***

***Kuendeleza Majadiliano ya Kibiashara Kati ya Nchi na Nchi (Bilateral), Kikanda (Regional) na Kimataifa (Multilateral)***

**A. Nchi na Nchi (Bilateral)**

**89.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imeendelea kushiriki kwenye mikutano mbalimbali ya uwili ambapo katika mwaka 2023/2024 Wizara ilishiriki katika mikutano ifuatayo:- Mkutano wa Pili wa Tume ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kati ya Tanzania na Angola

uliofanyika mwezi Februari, 2024 Zanzibar kwa lengo la kuendeleza na kuimarisha biashara na nchi mbalimbali rafiki; Mkutano wa majadiliano na vyama vya wasafirishaji, wamiliki wa vyombo vya usafirishaji na madereva wanaotoa huduma za usafirishaji wa mazao na bidhaa katika mpaka wa Tunduma/Nakonde kwa lengo la kutatua changamoto zinazokwamisha ufanyaji wa biashara katika mpaka wa Tanzania na Zambia.

**90.** ***Mheshimiwa Spika;*** Lengo kuu la vikao hivyo lilikuwa ni kubainisha na kukusanya changamoto za wadau hao na kuziwasilisha katika Mkutano wa Uwili kati ya Tanzania na Zambia uliofanyika mwezi Oktoba, 2023 katika mpaka wa Nakonde; na iliandaa Mkutano wa Mawaziri wa biashara wa Tanzania na Zambia uliofanyika mwezi Novemba, 2023 Tunduma, Mkoa wa Songwe kwa lengo la kuendeleza biashara na kutatua changamoto za kibiashara zilizopo.

**91.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, kupitia Mkutano wa Mawaziri kati ya Tanzania na Zambia, jumla ya vikwazo saba (7) vilitatuliwa na vikwazo vitatu (3) vinaendelea kufanyiwa kazi. Kutokana na umuhimu wa nchi ya Zambia kwenye mizigo inayopita kupitia Kituo cha Pamoja cha Forodha cha Tunduma, Wizara itaendelea kufuatilia na kuhakikisha vikwazo hivyo vinaondolewa ili kuongeza kasi ya ufanyaji biashara baina ya Tanzania na Zambia.

**92.** ***Mheshimiwa Spika***; Sambamba na hilo, Wizara ilisaini Hati ya makubaliano baina ya Tanzania na Marekani mwezi Oktoba, 2023 Jijini Dar es Salaam, kwa lengo la kuanzisha mazungumzo ya biashara, kuimarisha uhusiano na kukuza biashara kati ya nchi hizo. Baada ya Hati hiyo kusainiwa, Wizara imefanya vikao na Ubalozi wa Marekani hapa nchini vya kujipanga na kuweka mikakati ya namna ya utekelezaji wa Hati hiyo. Kwa sasa Mpango Kazi wa utekelezaji wa Hati hiyo umekamilika ikiwa ni pamoja na uanzishwaji wa vikundi kazi katika maeneo ya kimkakati ambayo mijadala ya kibiashara itakuwa inafanyika. Maeneo hayo ni uchumi wa kidigitali, mazingira ya biashara, ufikiwaji wa soko na jumbe za biashara. Utekelezaji wa Hati hiyo utasaidia kuibua na kuja na mikakati ya kuhakikisha tunatumia soko la Marekani kikamilifu kupitia Mpango wa AGOA.

**B. Kikanda (Regional)**

**93.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika Kusimamia na Kuratibu Utekelezaji wa Mkataba wa Eneo Huru la Biashara la Afrika (African Continental Free Trade Area – AfCFTA), Wizara imeendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kutumia vema fursa za soko la AfCFTA kupitia mpango wa majaribio unaojulikana kama *Guided Trade Initiative* (GTI). Tanzania ilichaguliwa kuwa miongoni mwa nchi nane (8) zilizokuwa zimekamilisha taratibu za kuanza biashara chini ya AfCFTA ili kuwa katika mpango wa majaribio wa kuuza na kununua bidhaa kupitia mkataba wa AfCFTA. Nchi nyingine ni Tunisia, Kenya, Rwanda, Mauritius, Cameroon, Ghana na Misri.

**94.** ***Mheshimiwa Spika***; Kutokana na Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Mikutano ya AfCFTA, Wizara ilishiriki na kuongoza Mkutano wa 12 na wa 13 wa Baraza la Mawaziri wa Eneo Huru la Biashara la Afrika uliofanyika mwezi Desemba, 2023 Dar es Salaam na mwezi Januari, 2024 Durban, Afrika Kusini mtawalia. Matokeo ya mikutano hiyo ilikuwa ni pamoja na kupitishwa kwa Itifaki ya AfCFTA ya Wanawake na Vijana katika biashara *(AfCFTA Protocol on Women and Youth in Trade);* Itifaki ya AfCFTA ya Biashara Mtandao *(AfCFTA Protocol on Digital Trade);* na kupitishwa kwa mwongozo wa malipo kwa wajumbe wa Bodi ya Rufaa ya Utatuzi wa Migogoro ya Biashara ya AfCFTA.

### *4.2.4. Maendeleo ya Biashara*

### *A. Utayarishaji wa Viwango 640 vya KitaifaKatika Sekta/Nyanja Mbalimbali*

**95.** ***Mheshimiwa Spika*;** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imekamilisha viwango muhimu katika kilimo, chakula, uhandisi na aina nyingine mbalimbali za viwango. Kati ya viwango 268 vilivyokamilika, viwango 41 ni katika nyanja ya kemikali, viwango sita (6) katika nyanja ya ujenzi, viwango 81 katika nyanja ya kilimo na chakula, viwango 49 katika nyanja ya nguo na ngozi, viwango 40 katika sekta mtambuka, viwango 10 katika nyanja ya mazingira, viwango 36 katika nyanja ya uhandisi umeme, na viwango vitano (5) katika nyanja ya uhandisi mitambo. Aidha,

viwango 423 sawa na asilimia 66.1 ya lengo la kuandaa viwango 640 kwa mwaka vipo katika hatua mbalimbali za uchakataji ambapo uchakataji huo hutumia muda wa hadi mwaka mmoja (1).

**B. Usajili wa Majengo ya Maeneo ya Uzalishaji, Uuzaji na Usambazaji wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi**

**96. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imesajili majengo, maeneo ya uzalishaji, uuzaji na usambazaji wa bidhaa za chakula na vipodozi 6,134. Usajili huo ni sawa na asilimia 61.3 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 10,000 kwa mwaka. Usajili wa majengo unafanyika ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazalishwa kwa kuzingatia matakwa ya kiwango husika. Aidha, uhifadhi na usambazaji wake unafanyika pasipo kusababisha uharibifu au kupunguza ubora na usalama wa bidhaa.

**C. Usajili wa Bidhaa za Chakula na Vipodozi**

**97. *Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara ilisajili bidhaa za chakula na vipodozi 1,021 ambavyo ni sawa na asilimia 46.4 ya lengo la kusajili na kutoa vibali 2,200 kwa mwaka. Usajili wa bidhaa hizo hufanyika kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. Lengo ni kuhakikisha kuwa bidhaa hizo zinakidhi matakwa ya viwango husika, ikiwa ni pamoja na kuhakiki ubora na usalama wake na kuwezesha ushindani wa soko huru la kibiashara na kulinda afya ya watumiaji.

***D. Ukaguzi na Utoaji wa Vibali kwa Bidhaa za Ndani na* Zitokazo Nje ya Nchi**

**98. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya vyeti vya ubora 81,541 vimetolewa kwa shehena za bidhaa zitokazo nje ya nchi; hii ni sawa na asilimia 68.5 ya matarajio ya kutoa jumla ya vyeti vya ubora wa bidhaa 120,000 kwa mwaka. Kati ya vibali hivyo, vibali 28,183 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nje ya nchi (PVoC) na vibali 53,358 ni kwa bidhaa zilizokaguliwa nchini (Destination Inspection). Ukaguzi wa bidhaa kutoka nje ya nchi husaidia kulinda usalama na afya ya walaji pamoja na mazingira; kuondoa ushindani usio sawa unaosababishwa na bidhaa duni

kutoka nje dhidi ya bidhaa zinazozalishwa nchini na hivyo kulinda viwanda vya ndani pamoja na kuzuia Tanzania kuwa jalala la bidhaa duni.

**99.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara kupitia TBS ilikagua jumla ya shehena 63,378 kabla hazijaingizwa nchini sawa na asilimia 96 ya lengo la kukagua shehena 66,000. Aidha, jumla ya shehena 124,395 zilikaguliwa kutoka nje ya nchi baada ya kufika nchini sawa na asilimia 92.8 ya lengo la kukagua shehena 134,000. Aidha, kufuatia ukaguzi huo, jumla ya shehena zenye uzito wa tani 4,397.78 zenye thamani ya shilingi bilioni 11.3 zilizuiliwa kutumika zikiwa ni bidhaa mbalimbali zikiwemo; bidhaa za chakula zenye uzito wa tani 2,724.33 na thamani ya shilingi bilioni 4.2; bidhaa za vipodozi zenye uzito wa tani 97.86 na thamani ya shilingi milioni 865.1; mitumba (undergarments) yenye uzito wa tani 16.2 na thamani ya shilingi milioni 115.8; bidhaa za ujenzi (mabati na saruji) zenye uzito wa tani 1,503.87 na thamani ya shilingi bilioni 5.6; bidhaa za mifuko mbadala zenye uzito wa kilogramu 34 na thamani ya shilingi milioni 1.1, bidhaa za mafuta ya breki za magari na malighafi za kuzalisha sigara zenye uzito wa tani 40.19 na thamani ya shilingi milioni 468.9; na bidhaa za umeme zenye uzito wa tani 15.3 na thamani ya shilingi milioni 8.4.

**100.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, jumla ya bidhaa zenye uzito wa tani 3,124.22 na thamani ya shilingi bilioni 9 ziliteketezwa. Bidhaa hizo ni pamoja na bidhaa za chakula zenye uzito wa tani 1,909.63 na thamani ya shilingi bilioni 4.7; bidhaa za vipodozi zenye uzito wa tani 112.95 na thamani ya shilingi bilioni 1.6; mitumba (undergarments) yenye uzito wa Kilogramu 600 na thamani ya shilingi milioni 30.4; bidhaa za ujenzi (mabati na saruji) zenye uzito wa tani 1,060.91 na thamani ya shilingi bilioni 2.3; na bidhaa za kemikali zenye uzito wa tani 40.14 na thamani ya shilingi milioni 468.2.

***E. Kufanya Ukaguzi wa Ubora na Kutoa Leseni za Ukaguzi wa Magari Yaliyotumika***

**101.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya magari 35,924 yaliyotumika nje ya nchi yalikaguliwa, hii ni sawa na asilimia 78.1 ya lengo la kukagua magari 46,000 kwa mwaka.

Kupitia ukaguzi huo wa magari nje ya nchi, umesaidia kuhakikisha watanzania wanapata magari yaliyokidhi viwango na kuepusha athari za kiafya, kimazingira na gharama za matengenezo kwa mteja. Vile vile, mfumo huo umesaidia kuharakisha uondoshaji wa magari bandarini na kuondoa gharama za uhifadhi.

**F. Kuthibitisha Kampuni Chini ya Mifumo ya Ubora ya Uendeshaji**

**102. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya kampuni 12 zilithibitishwa sawa na asilimia 80 ya lengo la kuthibitisha kampuni 15 kwa mwaka. Kampuni zilizopata ithibati hufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kuwa utendaji wao unazingatia mipango iliyopo na hivyo husaidia kuongeza tija na ufanisi, kupunguza gharama za uendeshaji na kuzuia kurudia kazi, kusaidia kuboresha uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma, na kuwezesha kampuni kuzalisha bidhaa kwa ubora ule ule wakati wote na kuongeza imani kwa wateja.

**G. Kufanya Ugezi kwa Vifaa/Mashine Mbalimbali**

**103. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya vifaa 7,465 vilifanyiwa ugezi. Hii ni sawa na asilimia 68.9 ya lengo la kufanyia ugezi vifaa 11,000 kwa mwaka. Ugezi wa vifaa husaidia kutoa ulinganifu unaoleta usahihi *(traceability)* wa vipimo vinavyolingana na taratibu zinazokubalika kimataifa *(international best practice)*.

***H. Kuweka Kinasaba Katika Mafuta ya Petroli, Dizeli na* Mafuta ya Taa**

**104. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024 jumla ya lita 3,224,617,859 za mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa ziliwekewa kinasaba, hii ni sawa na asilimia 80.6 ya lengo la kuweka kinasaba katika lita 4,000,000,000 za mafuta kwa kipindi cha mwaka mzima. Uwekaji vinasaba kwenye mafuta husaidia kudhibiti uchakachuaji wa mafuta pamoja na kuzuia mafuta yanayouzwa nchini kinyemela.

**I. Kusajili Kampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma, Hataza na vyeti vya Viwanda**

**105. *Mheshimiwa Spika***; Kupitia maboresho ya mifumo ya usajili wa kimtandao yanayoendelea kufanyika hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imefanikiwa kusajili jumla ya Makampuni 10,651 kati ya 15,000 yaliyokusudiwa sawa na asilimia 71, kusajili Majina ya Biashara 19,040 kati ya 28,000 yaliyopangwa, sawa na asilimia 68, kusajili Alama za Biashara na Huduma 1,998 kati ya 4,200 zilizokuwa zimepangwa, sawa na asilimia 48 na kupokea na kuchakata maombi ya Hataza 45 kati ya maombi 40 yaliyokuwa yamepangwa sawa na asilimia 125 ya lengo lililowekwa. Hatua hizo zimetokana na juhudi kubwa za kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kurasimisha biashara kupitia matamasha, warsha, maadhimisho na makongamano mbalimbali nchini.

**J. Kutoa Leseni na Kufanya Kaguzi Elimishi za Leseni za Biashara kundi 'A' na za Viwanda**

**106. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imefanikiwa kutoa Leseni za Viwanda 159 kati ya leseni 210 zilizokuwa zimepangwa sawa na asilimia 73. Vile vile, Wizara imetoa Leseni za Biashara kundi "A'' 12,501 kati ya leseni 14,000 zilizopangwa sawa na asilimia 89. Matokeo hayo yanatokana na jitihada za Serikali katika kusimamia na kudhibiti taratibu za ufanyaji wa biashara unaozingatia sheria.

**107. *Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imefanya jumla ya kaguzi elimishi nne (4) za Viwanda na Leseni za Biashara katika Mikoa ya Manyara, Iringa, Simiyu na Kigoma ambapo elimu kuhusu Sheria ya Leseni na Usajili wa Viwanda vya Taifa, Sura ya 46 na Sheria ya Leseni za Biashara Na. 25 ya Mwaka 1972 imetolewa. Jumla ya biashara 728 zilikaguliwa ambapo kati ya hizo, biashara 471 zilikuwa na leseni halali za biashara, biashara 177 hazikuwa na leseni ya biashara, biashara 48 zilikuwa na leseni za biashara zilizoisha muda na biashara 32 zilikuwa na leseni za biashara kundi 'B' badala ya kundi 'A'.

**108. *Mheshimiwa Spika***; Vile vile, kwa upande wa Leseni za Viwanda jumla ya viwanda 333 vilikaguliwa ambapo kati ya

hivyo, viwanda 46 vilikuwa na leseni, viwanda 279 havikuwa na leseni na viwanda 8 havifanyi kazi. Hatua zilizochukuliwa kwa viwanda ambavyo havina leseni za viwanda ni pamoja na:- Kuwaelekeza wafanyabiashara na wamiliki wa viwanda waliokuwa hawana leseni kuomba leseni kwenye Mamlaka husika, kuhuisha leseni zilizoisha muda wake, na kuwaelekeza kuomba leseni papo kwa papo.

**109.** ***Mheshimiwa Spika***; Hatua nyingine ni pamoja na: - Kutoa elimu kwa wafanyabiashara kuhusu umuhimu wa kufanya biashara kwa kufuata Sheria za Nchi; Kuzikumbusha Halmashauri kuhusu uzingatiaji wa Jedwali la Aina za Biashara na Ada katika utoaji wa Leseni za Biashara ili kutoingilia kundi la Mamlaka nyingine; Kuwakumbusha wamiliki wa viwanda kuwasilisha taarifa za maendeleo ya viwanda kwa kuwa taarifa hizo ni hitaji la kisheria. Vile vile, elimu kuhusu mifumo ya kielektroniki inayotumika katika kutoa leseni za viwanda na leseni za biashara kundi "A" kwa njia ya mtandao ilitolewa kwa jumla ya wafanyabiashara 1,061 katika maeneo mbalimbali ya nchi.

**110.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha taratibu za kisheria kwa ajili ya kutoa msamaha wa ada ya kuwasilisha nyaraka za kampuni nje ya muda kwa kampuni zilizosajiliwa kabla ya mwaka 2018 ambazo taarifa zake hazijajumuishwa kwenye Mfumo wa Usajili wa Kampuni kwa njia ya Mtandao. Lengo la uamuzi huo ni kutoa unafuu wa ada kwa kiwango cha 50% ili kuwezesha kampuni hizo kuhuisha taarifa zao kwenye Mfumo wa Usajili kwa njia ya Mtandao.

**K. Kusimamia, Kuhakiki na Kukagua Vipimo vyote Vitumikavyo na Viingiavyo Nchini**

**111.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imekagua na kuhakiki vipimo 612,404 sawa na asilimia 101 ya lengo la kukagua vipimo 604,641. Kati ya vipimo vilivyokaguliwa na kuhakikiwa, vipimo 19,671 sawa na asilimia 3 vilirekebishwa na vipimo 571 sawa na asilimia 0.1 vilikataliwa. Aidha, Wizara imeendelea kufanya kaguzi za kawaida na kaguzi za kushtukiza ambapo jumla ya kaguzi 2,516 kati ya kaguzi 2,083 zimefanyika sawa na asilimia 121 ya kaguzi zilizopangwa kufanyika ambapo

vipimo mbalimbali vitumikavyo kwenye biashara, afya na mazingira vilikaguliwa.

**112.** ***Mheshimiwa Spika*****;** Vipimo vilivyokaguliwa kwa wingi ni pampu za kuuzia mafuta ya nishati (Fuel Dispensing pumps), *Flow meters* zitumikazo kupimia mafuta kwenye bohari na maghala ya kuhifadhia Mafuta, tenki za kusafirishia mafuta (Fuel Vehicle Tankers) na tenki za kuhifadhia mafuta (Fixed and Bulk Storage Tanks), mita za maji, mizani inayotumika kupimia bidhaa mbalimbali, vipimo vya urefu (Dip tape, Meter rulers na Tape Measures) na malori yabebayo kokoto, mchanga na vifusi. Ukaguzi wa vipimo hivyo husaidia kupata usahihi wa kipimo ili mteja asidhulumiwe kulingana na kiasi cha fedha alicholipa na muuzaji auze kulingana na kiasi alicholipwa.

**L. Kuboresha Hali ya Ushindani katika Soko**

**113.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imeendelea na jukumu la kuboresha hali ya ushindani katika soko ambapo hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imetekeleza majukumu yafuatayo:-

**i.Kuchunguza na Kukamilisha Mashauri Yanayohusu Mienendo Inayoashiria Ukiritimba katika Soko**

**114.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara ilipanga kuendelea na uchunguzi wa mashauri 12 yanayohusu mienendo inayosababisha ukiritimba katika soko. Kati ya mashauri hayo, mashauri 10 yanahusu miungano ambayo haikuidhinishwa na Tume ya Ushindani (Unnotified Mergers) na mashauri mawili (2) yakihusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara ilikamilisha uchunguzi wa mashauri tisa (9) ya miungano ya kampuni ambazo hazikuidhinishwa ambapo mashauri manne (4) kutoka sekta ya madawa yalifungwa kwa kuwa hawakuwa na kesi ya kujibu na mashauri matano (5) kutoka sekta za usafirishaji, ujenzi, madawa yalitolewa Uamuzi wa Awali (*Provisional Findings*) na shauri moja (1) bado lipo katika hatua za uchunguzi. Wizara inaendelea na uchunguzi kwenye mashauri mawili (2)

yanayohusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko kwenye masoko ya vinywaji vikali na kuku wa nyama (broiler).

**116.** ***Mheshimiwa Spika***; Vile vile, Wizara ilipanga kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu mashauri 15 ya miungano ya kampuni ambayo haikuidhinishwa na Wizara kupitia FCC na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu matumizi mabaya ya nguvu ya soko kwa mashauri sita (6). Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imetoa maamuzi ya mwisho kwa mashauri tisa (9) kuhusu miungano ya makampuni ambayo hayajaidhinishwa na FCC. Aidha, mashauri sita (6) yapo katika hatua mbalimbali za maamuzi. Kwa upande wa matumizi mabaya ya nguvu ya soko, mashauri mawili (2) yametolewa maamuzi na mashauri manne (4) yapo katika hatua za mwisho za kufanyiwa maamuzi. Vile vile, FCC kwa kushirikiana na Mamlaka za udhibiti na BRELA ilibaini uwepo wa kampuni 65 zilizoungana bila kuitaarifu FCC. Tume inaendelea kufanya uchunguzi kama miungano hiyo ilifanyika kinyume na Sheria ya Ushindani.

### ii. Kuchunguza na Kukamilisha Mashauri Yanayohusu Mienendo ya Upangaji Njama Kila Mwaka

**117.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara ilipanga kuendelea na uchunguzi kuhusu mashauri mawili (2) na kutoa uamuzi wa mwisho kuhusu mienendo ya kula njama. Wizara inaendelea kukamilisha uchunguzi kuhusu shauri moja (1) linalohusiana na kula njama katika soko la kununua na kuuza Korosho. Aidha, Wizara inakamilisha uchambuzi wa majibu ya hoja yaliyowasilishwa na wadaawa 18 katika shauri linalohusu kula njama kwenye soko la uzalishaji na usambazaji wa nondo, na kupanga kuendelea na majadiliano na wadaawa saba (7) kati ya 20 waliowasilisha maombi ya suluhu.

### iii. Kusajili Mikataba ya Watumiaji (Consumers)

**118.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imeshughulikia mikataba 309 ya watumiaji iliyoandaliwa upande mmoja (Standard Form Consumer Contracts) kutoka katika Sekta za Fedha na Bima. Kati ya mikataba hiyo, mikataba 21 ilisajiliwa na kupewa hati. Aidha, mikataba 239 ilijumuishwa na mikataba

ya watoa huduma 1,176 wanaondesha shughuli zao pasipo kutimiza takwa la kisheria la kusajili mikataba kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani No. 8 ya mwaka 2003 na Kanuni za Mikataba ya Mlaji za mwaka 2014.

**iv. Kushughulikia/kushauri Kuhusu Malalamiko ya Watumiaji (Consumers)**

**119.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imeshughulikia malalamiko 50 ya walaji wa bidhaa na huduma. Kati ya mashauri hayo, mashauri 27 yalitolewa maamuzi, mashauri manne (4) yalipelekwa kwenye mamlaka zingine zikiwemo EWURA, Polisi na Mahakama na mashauri 19 yako katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**M. Mapambano Dhidi ya Bidhaa Bandia katika Soko**

**120.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara imefanya kaguzi katika Bandari ya Dar es Salaam na Bandari Kavu (ICDs) ambapo jumla ya makasha (containers) 5,086 yalikaguliwa. Kati ya hayo, makasha 232 yalikutwa na bidhaa zilizokiuka Sheria ya Alama za Bidhaa ya Mwaka 1963 yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 7.52. Vile vile, Wizara imefanya kaguzi 20 za kushtukiza (raids) katika maduka na stoo katika Mikoa ya Mwanza, Dodoma na Dar es Salaam ambapo bidhaa bandia zenye thamani ya shilingi milioni 227.3 zilikamatwa.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***; Udhibiti wa bidhaa bandia umesaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha usalama wa watumiaji wa bidhaa na uchaguzi wa bidhaa wanazozipenda bila kudanganywa kwa kuuziwa bidhaa bandia. Vile vile, udhibiti wa bidhaa bandia unasaidia kulinda biashara na uwekezaji kwa kulinda nembo au alama za bidhaa dhidi ya watu wanaotumia nembo/alama hizo bila idhini ya wamiliki.

***N. Kupokea, Kusikiliza na Kutoa Maamuzi ya Mashauri ya Rufaa Yanayowasilishwa katika Baraza***

**122.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imepokea jumla ya kesi 37 zinazoendelea kusikilizwa na

kuamuliwa. Kati ya kesi hizo, 13 ni kesi mpya na 24 ni kesi zilizokuwa hazijaamuliwa katika kipindi cha mwaka 2022/2023. Wizara imeweza kusikiliza na kuzitolea maamuzi kesi 22 na kesi 15 zinaendelea kusikilizwa katika hatua mbalimbali.

**123.** ***Mheshimiwa Spika;*** Utatuzi wa mashauri hayo umeweza kupunguza migogoro ya wafanyabiashara, wawekezaji na walaji inayohusu ushindani wa kibiashara na udhibiti wa soko. Matokeo ya mashauri yaliyoamuliwa, yameongeza uwajibikaji na kuimarisha ushindani wa kweli katika sekta ya biashara na udhibiti wa soko. Hatua hiyo imeongeza ufanisi na uzalishaji, usambazaji wa huduma na bidhaa, kukuza ubunifu, kuwezesha matumizi ya rasilimali yenye ufanisi na kumlinda mlaji.

**O. Elimu na Mafunzo Mbalimbali**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika mwaka 2023/2024, Wizara imetoa elimu na mafunzo kwa wadau wakiwemo wajasiriamali kuhusu fursa za masoko, umuhimu wa kufanya sajili za kibiashara na namna ya kuimarisha uwezo wa kutumia mifumo na kufanya biashara katika soko lenye ushindani kama ifuatavyo:-

i. **Mafunzo Kuhusu Fursa za Masoko ya Kimataifa, Kikanda na Baina ya Nchi na Nchi**

**125.** ***Mheshimiwa Spika*;** Wizara imeendelea kutoa elimu na kujenga uwezo wa wadau kuhusu fursa nafuu za masoko na uwekezaji ambazo zimepatikana kupitia majadiliano mbalimbali ya biashara ya kimataifa, kikanda na baina ya nchi na nchi na taratibu za kuyafikia masoko hayo ili fursa hizo ziweze kutumika kikamilifu na nchi kunufaika ipasavyo. Mafunzo hayo yamefanyika kwa awamu mbili (2) ambapo awamu ya kwanza ilifanyika katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe, Mtwara, Ruvuma, Katavi, Kigoma na Geita mwezi Julai, 2023. Aidha, awamu ya pili ya mafunzo hayo ilifanyika katika ya Mikoa ya Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera, Mara, Simiyu na Shinyanga) na Kanda ya Kati (Dodoma, Singida, Rukwa na Tabora) mwezi Februari, 2024. Jumla ya washiriki 201 kutoka Sekta ya Umma na Binafsi walipatiwa mafunzo hayo. Wizara inaendelea na utoaji wa

elimu hiyo katika maeneo mengine ya nchi ikilenga kufikia wazalishaji na wafanyabiashara wadogo zaidi.

**ii. Utoaji wa Elimu kwa Wafanyabiashara Kuhusu fursa za AfCFTA**

**126.** ***Mheshimiwa Spika***; Wizara kwa kushirikiana na Chemba ya Wanawake Tanzania (TWCC), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulika na Wanawake (UN Women) na Shirika la *Trade Mark Afrika* (TMA) ilitoa mafunzo kwa wanawake na vijana wajasiriamali kuhusu fursa za soko la AfCFTA mwezi Novemba, 2023 na mwezi Januari, 2024. Mafunzo hayo yalifanyika katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Songwe, Ruvuma na Zanzibar. Kupitia mafunzo hayo, wanawake na vijana wajasiriamali 595 walijengewa uwezo kuhusu namna ya kufikia soko la AfCFTA; na kuwajengea uwezo wafanyabiashara wadogo kuhusu masuala muhimu ya kuzingatia katika uzalishaji wa bidhaa na uuzaji wa bidhaa ndani ya soko la AfCFTA. Sambamba na hilo, wajasiriamali hao walipewa mafunzo kuhusu nyenzo zitakazowasaidia katika kutumia fursa za soko la AfCFTA. Nyenzo hizo ni pamoja na mifumo ya uondoaji wa ushuru wa forodha katika bidhaa (the online tariff negotiation portal) na mfumo wa kuripoti vikwazo vya biashara kwa njia ya mtandao.

**127.** ***Mheshimiwa Spika*;** Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na *The Chartered Institute of Logistics and Transport* iliandaa warsha ya kuwajengea uwezo wadau wa lojistiki na usafirishaji mwezi Machi, 2024, Jijini Dar es Salaam. Kupitia warsha hiyo, wadau hao walijengewa uwezo kuhusu fursa mbalimbali za AfCFTA, ufunguaji wa Sekta ya Biashara ya Huduma pamoja na umuhimu wa Sekta ya Uchukuzi katika kuwezesha biashara ndani ya Bara la Afrika.

**P. Uratibu na Ushiriki wa Maonesho Mbalimbali**

**128.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2023/2024 Wizara imeratibu na kushiriki maonesho mbalimbali yakiwemo Maonesho ya SIDO, Nane Nane, CTI na Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambapo kupitia maonesho ya SIDO yaliyofanyika mwezi Oktoba, 2023 Njombe, Wizara imehamasisha umma wa watanzania kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini zinazotokana na viwanda vidogo na vya kati. Katika maonesho

hayo, jumla ya wajasiriamali 1,302 wamepata fursa ya kutangaza na kushawishi wananchi kutumia bidhaa zinazotengenezwa nchini.

**129.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara imeweza kutangaza huduma zake na bidhaa za wajasiriamali kupitia mitandao ya kijamii ya SIDO na kuwafikia wajasiriamali 59,600, kati yao wajasiriamali 3,000 ni wapya. Aidha, wajasiriamali 1,302 wameweza kushiriki maonesho kama ifuatavyo:- Sabasaba (188); Nanenane (312); CTI (70); Mtandao wa mazingira na maendeleo (112); na Maonesho ya SIDO kitaifa Njombe (620). Kupitia maonesho hayo, jumla ya mauzo ya shilingi milioni 923.6 yalifanyika na wajasiriamali 646 wameunganishwa na kupata vifungashio kwa wasambazaji wa vifungashio 25.

**130.** ***Mheshimiwa Spika****;* Pia, Wizara imeratibu Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (47$^{th}$ DITF) yaliyofanyika mwezi Juni hadi Julai, 2023 kwa lengo la kutangaza bidhaa na huduma, kukutanisha wazalishaji na wanunuzi, kufanikisha mikakati ya wafanyabiashara katika masoko ya ndani na nje ya nchi ambapo mafanikio yafuatayo yalifikiwa: - Kuwezesha ushiriki wa kampuni 3,500 zikiwemo kampuni za ndani 3,233 na kampuni 267 kutoka nchi 23 kuonesha na kunadi bidhaa na huduma kwa sekta na tasnia mbalimbali; Kufanikisha mauzo ya papo kwa papo ya jumla ya shilingi bilioni 3.94 yakichangiwa zaidi na wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa; Kufanikisha maulizo (*enquiry*) ya bidhaa za ndani na nje ya nchi zenye thamani ya shilingi bilioni 21.74; Kuingia mikataba ya makubaliano yenye thamani ya shilingi bilioni 16.98 kutokana na Mkutano wa Biashara kwa Biashara (B2B) uliofanyika baina ya Tanzania na jimbo la Haryanna India; na Kupatikana kwa ajira 11,869 za muda mfupi wakati wa maonesho hayo katika kutoa usaidizi wa huduma mbalimbali ikiwemo usafirishaji, migahawa, mapambo, ufundi na ujenzi.

### 4.3. Mafanikio ya Wizara ya Viwanda na Biashara katika Serikali ya Awamu ya Sita

**131.** ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara imepata mafanikio makubwa katika maeneo mbalimbali yakiwemo; uendelezaji wa miradi ya

kimkakati na kielelezo, ubunifu wa mitambo na upatikanaji wa teknolojia mbalimbali, utafutaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania, na kuendeleza mitaa ya viwanda. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:-

**A. Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Liganga**

**132.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara chini ya uratibu wa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imeendelea na ukamilishaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi Unganishi wa Mchuchuma na Linganga. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya shilingi bilioni 15.414 zimelipwa kati ya shilingi bilioni 15.424 kwa wafidiwa 1,129 kati ya 1,142. Idadi ya wafidiwa waliolipwa ni sawa na asilimia 99. Kiasi ambacho hakijalipwa kwa Wafidiwa 13 ni milioni 10.227. Wananchi hao 13 ambao hawajalipwa ni kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo baadhi yao kutojitokeza, na wengine kutokukamilika kwa nyaraka na taratibu za mirathi. Juhudi za kuwapata wafidiwa hao au warithi wao zinaendelea kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa ili zoezi lihitimishwe.

**133.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha nchi inanufaika na rasilimali kubwa ya makaa ya mawe yaliyopo Mkoa wa Njombe, Wizara ilisaini mikataba na wachimbaji wadogo (Primary Mining Licences) wa Makaa ya Mawe kwenye eneo la vitalu 10 lililopo nje ya mkataba wa mradi wa Mchuchuma na Liganga mnamo mwezi Septemba, 2023. Aidha, maandalizi ya awali ya utafiti na uchimbaji kwenye leseni ndogo yameanza ambapo kampuni mbili (2) zimekamilisha taarifa ya kijiolojia na kampuni nyingine zinaendelea na utafiti wa kijiolojia. Wizara itaendelea kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha miradi hiyo inaanza uzalishaji mapema.

***B. Kuendeleza mradi wa kimkakati wa Magadi Soda Engaruka***

**134.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imekamilisha maandalizi yote ya kuanza utekelezaji wa mradi wa Magadi Soda Engaruka ikiwa ni pamoja na kukamilisha upembuzi yakinifu, kupata cheti cha mazingira, utafiti wa kina wa kiwango cha rasilimali madini, uainishwaji wa miundombinu wezeshi, stadi ya masoko ya ndani na nje ya nchi,

na uthamini wa mali za wananchi watakaopisha mradi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi, na Halmashauri ya Monduli imekamilisha uhakiki wa fidia ambapo kiasi cha shilingi bilioni 14.5 kinatarajiwa kulipwa kwa wananchi 599 kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari 60,884. Aidha, Wizara imekamilisha zoezi la kugawanya eneo la mradi katika maeneo matatu (3) ambayo yatatangazwa kwa ajili ya kupata wawekezaji. Lengo kuu la kugawa eneo hilo ni kuwezesha kupata wawekezaji tofauti kwa kila eneo wenye uwezo wa kifedha, uzoefu na masoko. Hadi sasa jumla ya wawekezaji 22 wameonesha nia ya kuwekeza kwenye eneo hilo.

**135. *Mheshimiwa Spika;*** Mradi wa magadi soda unatarajiwa kuchochea ukuaji wa viwanda vya kemikali nchini vinavyotumia magadi kama malighafi kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo nguo, vioo, sabuni, vinywaji, madawa na rangi. Mradi huo unatarajiwa kuokoa fedha za kigeni zaidi ya shilingi trilioni 320.65 kwa mwaka zinazotumika kuagiza malighafi ya magadi pamoja na bidhaa zinazotokana na magadi kutoka nje ya nchi. Kulingana na taarifa ya upembuzi yakinifu, mradi unatarajiwa kutoa ajira 223 za moja kwa moja na ajira 2,453 zisizo za moja kwa moja.

**C. Kuendelea na Ukarabati wa Kiwanda cha KMTC Katika Mkoa wa Kilimanjaro**

**136. *Mheshimiwa Spika;*** Serikali ya Awamu ya Sita imefufua kiwanda mama cha Kilimanjaro Machines Tools (KMTC) ambacho kilisimama kufanya kazi kwa zaidi ya miaka 30. Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara kupitia Shirika la Maendeleo (NDC) imekamilisha ujenzi wa mtambo mdogo wa kuweka utando wa kuzuia kutu (small galvanizing kettle) ambao utekelezaji wake umekamilika kwa asilimia 100; kukamilika kwa ukarabati wa majengo awamu ya kwanza; na kujenga na kukamilika kwa mafunzo ya kutumia kinu cha kuyeyushia chuma kwa wataalam wa kiwanda. Aidha, majaribio ya awali yameanza ya kuweka utandu wa zink kwenye chuma kuzuia kutu kwa kutumia mtambo mdogo.

**137. *Mheshimiwa Spika;*** Kufuatia maboresho yaliyofanyika, kiwanda cha KMTC kimefanikiwa kuzalisha mashine 10 na vipuri

mbalimbali 35 zenye thamani ya shilingi milioni 117.4 vilivyohitajika katika viwanda vitatu (3) na Taasisi moja (1). Viwanda hivyo ni Kiwanda cha Sukari cha TPC kilichopo Moshi, Kiwanda cha Ngozi 'Kilimanjaro Leather Industry co. Ltd' na Kiwanda cha Vifungashio 'Harsho Packaging Co. Ltd' na Taasisi ya Wakala wa Misitu (TFS). Vile vile, kiwanda kimezalisha vipuri vyenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya mitambo inayotumika katika migodi mbalimbali hapa nchini na hatimaye kupunguza uagizaji wa vipuri hivyo kutoka nje ya nchi.

**D. Kiwanda cha Bidhaa za Kibailojia (TBPL)**

**138.** ***Mheshimiwa Spika****;* Hadi kufikia Machi, 2024, kiwanda cha *Tanzania Biotech Products Limited (TBPL)* kinachomilikiwa na Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) kimezalisha lita 90,733 za viuwatilifu kwa ajili ya kuua viluwiluwi vya mbu. Kati ya kiasi kilichozalishwa, jumla ya lita 44,613 zenye thamani ya shilingi milioni 588.9 zimeuzwa katika masoko mbalimbali ndani ya nchi. Mchanganuo wa mauzo yaliyofanyika unajumuisha lita 19,880 zenye thamani ya shilingi milioni 262.4 ambazo zimenunuliwa na Mradi wa Shirika la Misaada la Uswis (Swiss TPH TEMT Project) kwa ajili ya kupambana na malaria kwenye kambi za wakimbizi; Lita 8,617.42 zenye thamani ya shilingi milioni 113.8 zimenunuliwa na Shirika la Madaktari Wasio na Mipaka (MSFCH -TANZANIA MISSION); Lita 5,680 zenye thamani ya shilingi milioni 75 zimenunuliwa na Wizara ya Afya Zanzibar; na Lita 10,435.43 zenye thamani ya shilingi milioni 137.8 zimenunuliwa na Hoteli, Zahanati na wateja binafsi.

**139.** ***Mheshimiwa Spika****;* Katika kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na kuhakikisha dawa hizo zinafika katika soko la SADC na Afrika Mashariki, Wizara imefanya vikao na balozi zetu zilizopo kwenye Ukanda wa SADC mwezi Oktoba, 2023 na Ubalozi wa Uganda mwezi Aprili, 2024. Kwa upande wa ubalozi wa Uganda pamoja na mambo mengine pande zote mbili zilikubaliana kuhusu utaratibu wa kusafirisha dawa za viuadudu zilizotolewa na Serikali ya Tanzania kama msaada kwa nchi ya Uganda.

**140.** ***Mheshimiwa Spika;*** Ili kuhakikisha kiwanda kinajiendesha kibiashara na kusaidia kupunguza matumizi ya fedha za kigeni na kuboresha Afya za watanzania, Kiwanda kimeanza kuzalisha viuatilifu hai (Biopesticides) ambavyo vina uwezo mkubwa wa kupambana na wadudu waharibifu aina ya viwavi (chewing pests) kwenye mazao ya pamba, mahindi na mbogamboga. Dawa hizo tayari zimefanyiwa majaribio na kupata Ithibati ya Ubora na kusajiliwa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA).

**141.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya lita 19,445 za viuatilifu hai zilizalishwa kibiashara kwa kutumia mitambo ya kiwanda ambapo kati ya kiasi hicho, jumla ya lita 421 zenye thamani ya shilingi milioni 4.2 zimeuzwa. Mauzo ya viuatilifu yanatarajiwa kuongezeka zaidi wakati wa msimu wa kilimo cha mazao yaliyokusudiwa (mahindi, pamba, maua na mboga mboga) pamoja na kipindi cha hali ya hewa ambapo hakuna mvua nyingi.

**142.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo inaendelea na utekelezaji wa mkakati wa kuhakikisha dawa hizo zinawafikia wakulima wengi nchini. Vile vile, kiwanda kinatekeleza mkakati wa masoko kwa kushirikisha Sekta Binafsi ambapo mazungumzo na wasambazaji pamoja na mawakala wa dawa za mimea na wanyama (agrovets) tayari yamefanyika. Kupitia mazungumzo hayo, kampuni mbili (2) zimesaini Mkataba wa Uwakala wa usambazaji wa Viuatilifu hai katika maeneo mbalimbali nchini.

**E. Kusanifu na Kuendeleza Utengenezaji wa Vifaa Tiba**

**143.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuhakikisha kuwa nchi inapunguza utegemezi wa uagizaji wa vifaa tiba nchini, Wizara kupitia TEMDO imefanya utafiti na kutengeneza vifaa tiba na kuvisambaza katika hospitali mbalimbali hapa nchini. Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imesambaza jumla ya vifaa tiba 1,210 vya aina mbalimbali vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8. Kati ya vifaa tiba hivyo, vifaa tiba 842 vilipelekwa JWTZ-Ngome; vifaa tiba 160 vilipelekwa Halmashauri ya Wilaya ya Maswa; na vifaa tiba

208 vimepelekwa katika Hospitali za *Mount Meru* na Levolosi (Arusha), na Bugando (Mwanza).

**144.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha utafiti na utengenezaji wa jokofu la kuhifadhia maiti la miili sita (*six body mortuary cabinet*) ambapo jokofu hilo limefungwa na linatumika katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tabora. Vile vile, Wizara imekamilisha usanifu wa *stretchers, theatre trolleys, Autoclave na Laundry machines*. Kwa sasa maandalizi ya michoro ya kiufundi ya vifaa tiba vilivyosanifiwa yanaendelea.

**145.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara imefanikiwa kutafiti na kutengeneza vichomea taka 50 vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.5 na kuvisambaza katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kwenye hospitali, vituo vya afya, viwanja vya ndege, vyuo vikuu na Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Aidha, kupitia mradi wa utengenezaji vifaa tiba, Wizara imefanikiwa kutoa mafunzo kwa vitendo kwa vijana wa vyuo vya ufundi, vya kati na vya elimu ya juu wapatao 50. Manufaa ya mradi huo ni pamoja na kujenga uwezo wa ndani wa kutengeneza vifaa tiba na hivyo kuondokana na utegemezi wa kuagiza vifaa hivyo kutoka nje ya nchi; Kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kwa kupunguza uagizwaji vifaa tiba kutoka nje ya nchi; na Kukuza ujuzi na kutengeneza ajira nchini.

**146.** ***Mheshimiwa Spika****;* Wizara kupitia SIDO imetengeneza vifaa tiba (Vipimo vya urefu) ili kutambua hali ya udumavu na kuweza kusaidia vituo vya afya kuhamasisha uboreshaji wa hali ya lishe kwa watoto chini ya miaka mitano (5). Hadi kufikia Machi, 2024 Wizara imetengeneza vifaa hivyo vyenye thamani ya shilingi milioni 356.7 na kuvisambaza kwenye vituo 1,551 vyenye upungufu wa vifaa vikiwemo vituo vya afya 980, zahanati 204 na hospitali za Wilaya 45, Mashirika yasiyo ya kiserikali 314 na watoa huduma wa sekta binafsi wanne (4). Aidha, jumla ya Halmashauri 88 za Mikoa 21 ya Tanzania Bara zimefikiwa. Uwezeshaji huo umechangia upatikanaji wa taarifa ambazo zimesaidia kuhamasisha suala la lishe bora kwa watoto chini ya miaka mitano (5) kwenye Halmashauri husika.

***F. Utengenezaji wa Kiwanda Kidogo cha Kuchakata Sukari***
**(Sugar mill mini-processing plant - Capacity 200 TCD)**

**147. *Mheshimiwa Spika;*** *Wizara* imeendelea na utafiti na utengenezaji wa mtambo wa kutengeneza sukari kwa kiwango cha mjasiriamali wa kati (sugar mill mini-plant, Capacity 200 TCD). Mtambo huo utakuwa na uwezo wa kuchakata tani 200 za miwa ghafi na kutoa tani 20 za sukari (*brown sugar*) kwa siku moja. Mradi unatarajiwa kukamilika na kufanyiwa majaribio ya awali ifikapo mwezi Juni, 2024. Aidha, gharama za mradi huo ni shilingi bilioni 1.6. Hadi kufikia Machi, 2024 mradi umekamilika kwa asilimia 80. Kiwanda kitakapokamilika kitakuwa na uwezo wa kutoa ajira za moja kwa moja 300 na ajira zisizo za moja kwa moja 1,800. Kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kuchakata miwa ya wakulima kwa eneo la ukubwa wa ekari 400 na kutoa ajira kwa wahudumu wa shamba wasiopungua 5,600 kwa msimu.

**148. *Mheshimiwa Spika;*** Kukamilika kwa mtambo huo kutakuwa na manufaa yafuatayo:- Kupunguza au kutatua ukubwa wa tatizo la kutojitosheleza kwa sukari nchini (sugar gap) kwa kuchangia tani 3,000 za sukari kwa mwaka kwa kila kiwanda kimoja; Kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza sukari nje ya nchi; Kusaidia wakulima wanaozunguka viwanda (*outgrowers*) miwa yao isiharibike pale viwanda vikubwa vinaposhindwa kununua miwa yote ya wakulima kwa kuwa viwanda pia vina mashamba yake; na Kutengeneza ajira 2,100 kwa watanzania kwa kila kiwanda kimoja, na hivyo kuinua kipato chao.

***G. Teknolojia za Kuchakata na Kusafisha Mafuta ya Kula***
**(Alizeti na Chikichi)**

**149. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha utafiti na kutengeneza teknolojia kwa ajili ya kuchakata alizeti itakayosaidia kupunguza uhaba wa mafuta ya kula nchini na kuwaondolea wajasiriamali usumbufu wa kuzifuata teknolojia hizi nje ya nchi. Usanifu na utengenezaji wa mtambo wa kuchakata alizeti ili kupata mafuta bora ya kupikia kwa kiwango cha kukidhi soko la ndani na nje ya nchi umekamilika. Mtambo huo umekamilika kwa kiwango bora kinachohitajika kwa soko la ndani

na nje ya nchi na una uwezo wa kusafisha mafuta lita 1,000 kwa siku, kutoa ajira za moja kwa moja 15 na ajira zisizo za moja kwa moja 60 na kuweza kuhudumia mashamba yenye ukubwa wa ekari 400 kwa msimu mmoja. Mtambo uliokamilika umefungwa kwa mteja wa *Usa River* Jijini Arusha. Aidha, sehemu iliyofungwa mtambo huo inatumika kwa ajili ya mafunzo kwa wajasiriamali wengine wanaojihusisha na uongezaji wa thamani kwenye mafuta yatokanayo na alizeti. Mtambo huo una thamani ya shilingi milioni 96.

**150.** ***Mheshimiwa Spika;*** Aidha, Wizara imekamilisha usanifu wa mtambo wa kusafisha mafuta yatokanayo na zao la chikichi. Mtambo huo mkubwa utakapokamilika utakuwa na thamani ya shilingi bilioni 2 na utaongeza thamani ya zao la chikichi na kutoa mafuta yatakayokuwa na ubora wa kuuzwa katika soko la ndani na nje.

**H. Kubuni, Kuhaulisha na Kukuza Teknolojia**

**151.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara, imeanzisha Kiwanda Darasa cha kubangua Korosho katika Wilaya ya Manyoni Mkoa wa Singida chenye jumla ya mashine na vifaa 129. Kiwanda hicho kina uwezo wa kubangua zaidi ya tani tatu (3) za korosho ghafi kwa siku na kutoa ajira kwa wanawake na vijana zaidi ya 100 kwa mwaka. Thamani ya kiwanda hicho ni shilingi milioni 600.

**152.** ***Mheshimiwa Spika;*** Pamoja na kiwanda darasa hicho, Wizara inaendelea na ujenzi wa ghala la kuhifadhia korosho; na uchimbaji wa kisima kirefu cha maji kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa maji yatakayotumika katika Kiwanda hicho. Kazi itakayofuata ni ujenzi wa Hosteli kwa ajili ya wananchi watakaojifunza kuhusu ubanguaji wa korosho, ukarabati na utunzaji wa mashine.

***I. Kufanya Upembuzi Yakinifu wa Ujenzi wa Mitambo ya Bayogesi, Utafiti na Tathmini ya Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia***

**153.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, Wizara imefanya Upembuzi Yakinifu ili kuangalia uwezekano wa kujenga

mitambo ya bayogesi kwenye Magereza 50. Hadi kufikia Machi, 2024, hatua iliyofikiwa ni kuandaliwa kwa makubaliano ya awali ya ujenzi wa mitambo ya bayogesi katika Magereza 18 kwa mwaka 2023/2024; Kufanya utafiti na tathmini juu ya matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia katika Taasisi za Umma 100 katika mikoa yote ya Tanzania na Kambi 24 za Jeshi la Wananchi Tanzania; Kufanikiwa kutengeneza sampuli kifani za aina nne (4) zenye jumla ya vifaa 62 vya kuwashia na kuzimia moto kwenye mbuga za wanyama kwa ajili ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ambapo vifaa hivyo ni viwashia moto (drip fuel torches) vitano (5) vinavyotumia matone ya mchanganyiko wa dizeli na petrol; virusha maji vya kuzimia moto (Knapsack Sprayer pumps) 15; vipigia moto (fire beaters) 22; na reki ngumu 20 kwa ajili ya maandalizi ya mipaka ya moto.

**154.** ***Mheshimiwa Spika;*** Vile vile, Wizara imeweza kutoa utaalamu uliofanikisha kupatikana kwa mikanda (aina ya C51) 80 kwa ajili ya kuendeshea mashine za kufyekea (mower) na utengenezaji wa majiko banifu ya mkaa na kuni manne (4) yenye ujazo wa lita 200 na majiko mawili (2) ya Bayogesi yenye ujazo wa lita 200.

**J. Utoaji wa Leseni za Uendeshaji Ghala**

**155.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imefanikiwa kutoa jumla ya leseni 95; kati ya hizo 66 zikiwa za Waendesha Ghala na 29 zikiwa za Meneja Dhamana. Leseni hizo zilitolewa katika Mikoa ya Dar es Salaam, Iringa, Kagera, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mtwara, Pwani, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga na Songwe. Vile vile, Wizara imeratibu jumla ya kaguzi 188 kwenye ghala 95, katika mikoa 16 yenye jumla ya wilaya 41. Kaguzi hizo zilihusu ukaguzi kabla ya utoaji leseni na wakati msimu ukiendelea.

***K. Kusimamia Utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala***

**156.** ***Mheshimiwa Spika***; Katika kusimamia utekelezaji wa mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa Waendesha Ghala na Meneja Dhamana wa mazao mbalimbali, Wizara iliratibu utoaji wa mwongozo wa pamoja wa zao la korosho "Mwongozo Namba

Moja wa Usimamizi wa Masoko na Mauzo ya Korosho Ghafi wa Mwaka 2023/2024 Toleo la Kwanza" na "Mwongozo wa Biashara kwa Kutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala uliotolewa Chini ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kwa zao la vitunguu saumu Toleo la Mwaka 2023". Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imeratibu ukusanyaji wa mazao kilogramu milioni 371 yenye thamani ya shilingi bilioni 905. Mazao hayo ni Mbaazi kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Manyara ambayo yaliingiza shilingi bilioni 1.6 kwa Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato kwa mkulima shilingi bilioni 94.6; Kakao kwa Mikoa ya Morogoro na Mbeya ambayo yalizipatia mapato ya shilingi bilioni 1.4 Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato ya shilingi bilioni 102.9 kwa wakulima; Korosho kwa Mikoa ya Mtwara, Ruvuma, Pwani na Lindi ambayo ilizipatia shilingi bilioni 7 Halmashauri za Mikoa hiyo na mapato kwa wakulima shilingi bilioni 407.9; Choroko Mkoa wa Mwanza ambayo iliipatia shilingi milioni 1 kwa Halmashauri na mapato kwa wakulima shilingi milioni 58.6; na mazao yaliyouzwa kupitia Meneja Dhamana (mchele, mpunga na mihogo) ambayo yaliwapatia mapato ya shilingi bilioni 299.7 wakulima **(Jedwali Na. 6).**

**157. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanya mapitio ya namna bora ya kusimamia uendeshaji ghala na kuwawajibisha Waendesha Ghala wenye mwenendo usioridhisha. Aidha, imefanya vikao na wanunuzi wakubwa wa mazao yaliyo katika mfumo ili kufahamu maeneo yenye changamoto wanazokutana nazo katika ununuzi kwa kutumia mfumo huo na kuzitatua changamoto hizo. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na:- baadhi ya Waendesha Ghala kutoa taarifa hewa; upungufu wa bidhaa ghalani na kutokuwa na kiwango madhubuti kinachotoa maelekezo juu ya usimamizi wa changamoto hizo. Kupitia vikao hivyo, jumla ya changamoto nane (8) zilitolewa na wanunuzi, ambazo zinahusisha wadau wa mfumo, ikiwa ni pamoja na Ushirika, Waendesha ghala, na mazingira ya biashara kwa ujumla. Kati ya changamoto hizo, changamoto sita (6) zimefanyiwa kazi. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala itaendelea kusimamia uendeshaji wa ghala katika maeneo ya kimkakati na kuondoa waendesha ghala wenye utendaji usioridhisha.

**158.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia mfumo huo, Wizara imefanikiwa kuongeza orodha ya bidhaa mpya kwenye mfumo ambapo mazao mapya manne (4) yameingia katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na kupata bei nzuri iliyotokana na ushindani sokoni. Mazao hayo ni ufuta kwa Mikoa ya Morogoro na Songwe, ambapo kwa mikoa hiyo ufuta umewapatia wakulima shilingi bilioni 31 na mapato ya shilingi milioni 260 kwa Halmashauri; Mbaazi kwa Mikoa ya Mtwara, Lindi, Manyara, na Morogoro, iliwapatia wakulima shilingi bilioni 96 na mapato ya shilingi bilioni 1.4 kwa Halmashauri; Zao la kakao kwa Mkoa wa Morogoro, liliwapatia wakulima shilingi bilioni 8.8 na mapato ya Halmashauri ya shilingi milioni 32; Mkoa wa Mbeya, kakao iliingiza wastani wa shilingi bilioni 84.5 na mapato ya Halmashauri yakiwa wastani wa shilingi milioni 277.5; na Choroko kwa Mikoa ya Ruvuma na Kanda ya Ziwa, iliwapatia wakulima shilingi milioni 228.8 na mapato ya shilingi milioni 6.5 kwa Halmashauri.

**159.** ***Mheshimiwa Spika;*** Mauzo ya mazao hayo kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yamesaidia upatikanaji wa bei nzuri ya soko kutokana na ushindani wa wanunuzi na hivyo kuwanufaisha wakulima wa maeneo husika ambapo bei ya kakao kabla ya mfumo ilikuwa shilingi 2,500 na baada ya mfumo bei ilikuwa shilingi 32,000 kwa kilogramu; Ufuta bei kabla ya mfumo ilikuwa shilingi 500 hadi shilingi 800 baada ya mfumo bei iliongezeka na kuwa shilingi 2,800 hadi shilingi 4,500 kwa kilogramu. Jumla ya wakulima 2,925,680 wamenufaika na bei nzuri ya mazao hayo

**160.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Mamlaka ya Usimamizi wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Soko la Bidhaa, na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, Bodi imeongeza usimamizi kutoka ngazi ya uzalishaji hadi kufikia soko na hivyo kuondoa changamoto zilizobainishwa. Kupitia jitihada hizo, imani ya kuendelea kutumia mfumo katika ununuzi wa bidhaa zinazotumia mfumo huo imeongezeka.

***L. Utoaji wa Leseni za Nembo ya Ubora na Mafunzo kwa* Wazalishaji na Wajasiriamali**

**161.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya leseni 382 za nembo ya ubora ya TBS zilitolewa sawa na asilimia 47.8 ya

lengo la kutoa leseni 800 kwa mwaka 2023/2024. Kiwango hicho cha utekelezaji kimechangiwa na baadhi ya wajasiriamali kutokamilisha mchakato wa upatikanaji wa leseni ya nembo ya ubora pamoja na mwitikio mdogo wa ukaguzi wa awali kwa ajili ya kupatiwa leseni. Miongoni mwa leseni hizo, leseni 168 zilitolewa kwa wajasiriamali wadogo wanaozalisha bidhaa mbalimbali kama vile unga, siagi ya karanga, viungo, achari za embe, mbilimbi na sabuni. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia na kutekeleza viwango vya bidhaa ambazo zimetengenezewa virutubisho kama vilivyopendekezwa na watalaam wa lishe. Bidhaa hizo ni pamoja na unga wa mahindi, mafuta ya kula na chumvi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika kupitia kitengo chake cha kutathmini madhara yatokanayo na chakula (Food risk Assessment section) limeendelea kufuatilila mwenendo wa hali ya usalama wa chakula nchini ikiwa ni pamoja na kufanya uchunguzi wa matumizi ya virutubisho na viambata katika vyakula husika hivyo kuweka msingi wa udhibiti wa usalama wa chakula nchini.

**162.** ***Mheshimiwa Spika;*** Shirika limeendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wadau mbalimbali wakiwemo wazalishaji wa bidhaa za viwandani, wasindikaji na umma kuhusu dhana nzima za kuzingatia mifumo ya ubora ili kuzalisha bidhaa zenye ubora. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya wadau 959 wa sekta nne (4) ndogo za uokaji, asali, nafaka na mimea jamii ya kunde, pamoja na bidhaa za matunda na mbogamboga walipewa mafunzo juu ya masuala ya viwango. Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Manyara, Arusha, Mbeya, Tanga, Njombe, Kilimanjaro, Lindi, Kigoma, Rukwa, Katavi na Iringa. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu katika mikoa mingine iliyosalia.

**M. Kuboresha Mazingira ya Biashara**

**163.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika kuboresha mazingira ya biashara na kusogeza huduma za sajili na leseni karibu na wananchi, Wizara imetoa mafunzo kwa Maafisa Biashara 490 kutoka mikoa 26 na Halmashauri 185 za Tanzania Bara kuhusu Sheria ya Leseni za Biashara Sura, 208 na Sheria ya Taifa ya Usajili na Utoaji wa Leseni za Viwanda Sura, 46. Mafunzo hayo yamesaidia kuwajengea uwezo Maafisa Biashara kuhusiana na urasimishaji

na utekelezaji wa sheria zinazosimamia biashara nchini na kutoa usaidizi wa karibu kwa wananchi.

**164.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kufanya ziara kwenye mikoa 10 na kufanya mikutano na Wafanyabiashara na wenye viwanda katika mikoa hiyo. Lengo la ziara na mikutano ilikuwa ni kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na sekta binafsi. Kupitia mikutano hiyo, zaidi ya changamoto 20 zilitatuliwa papo kwa hapo. Wizara pia imefanya mikutano mitatu (3) na uongozi wa soko la Kariakoo ambapo jumla ya changamoto 16 kati ya 21 zimetatuliwa. Changamoto tano (5) zilizobakia zipo katika hatua mbalimbali za utatuzi. Vile vile, Wizara iliandaa mkutano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi uliofanyika jijini Mbeya kwa lengo la kuendelea kuimarisha mashirikiano baina ya sekta hizi mbili. Naomba nitumie fursa hii, kuwahakikishia sekta binafsi kwamba Wizara itaendelea kufanya kazi kwa karibu nanyi kwani bila ninyi kufanya shughuli zenu kikamilifu uchumi wa nchi yetu hauwezi kukua.

**N. Miungano ya Makampuni (Mergers)**

**165.** ***Mheshimiwa Spika***; Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imefanya uchambuzi wa maombi 41 ya miungano ya kampuni kati ya maombi 45 kutoka katika Sekta za Kilimo, Fedha, Afya, Utalii, Uzalishaji, Madini, Mawasiliano, Mafuta, Gesi na Nishati. Kati ya maombi hayo, maombi 31 yalitolewa maamuzi ambapo kati ya hayo, maombi 28 yalipitishwa bila masharti, maombi mawili (2) yalipitishwa kwa masharti na ombi moja (1) liliamuliwa kutokuamuliwa "Not to be Determined". Maombi 10 yaliyobaki yapo katika hatua mbalimbali za uchunguzi. Lengo ni kuhakikisha miungano hiyo haiathiri hali ya ushindani wa masoko katika sekta zinazohusika. Matokeo ya miungano hiyo imewezesha kampuni kukuza mitaji, ajira, ufanisi na uzalishaji.

**166.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara iliridhia kununuliwa kwa kampuni 14 katika Sekta ya Kilimo. Kampuni hizo ni pamoja na *Mtanga Foods Limited*; Kampuni ya uzalishaji wa parachichi ya *Rungwe Avocado Company Ltd;* Kampuni ya uchenjuaji mpunga ya *MW Rice Millers Ltd* na *Mring'a Estates Ltd*. Vile vile, Wizara iliidhinisha miungano ya makampuni ya AMY

*Holdings Ltd* kununua kampuni mbili (2) za Tanzania *Tobacco Processors Ltd (TTPL)* na *Tanzania Leaf Tobacco Company Ltd (TLTC)* zilizokuwa zimefungwa kwa zaidi ya miaka minne (4). Kupitia miungano hiyo, zaidi ya ajira 3,000 zilipatikana. Aidha, tayari viwanda hivyo vimefufuliwa na vimeanza uzalishaji.

**167. *Mheshimiwa Spika;*** Katika Sekta ya Mawasiliano, Wizara iliridhia ombi la *Vodacom Tanzania Plc* kuinunua Kampuni ya *Smile Communications Tanzania Limited* iliyokua inatoa huduma za data kwa kasi ya *4G Long Term Evolution (LTE)* na huduma za sauti katika mikoa tisa (9) ya Tanzania Bara. Kutokana na Kampuni ya *Smile* kuwa na changamoto ya kifedha, kampuni hiyo haikuweza kuwafikia walaji wote nchi nzima. Hivyo, hatua hiyo itaiwezesha *Vodacom Tanzania Plc* kutumia miundombinu ya *Smile Communications Tanzania Limited* kuongeza wigo wa utoaji huduma za kimawasiliano na kuharakisha matumizi ya teknolojia za kidijitali nchini hususan maeneo ya vijijini ambapo huduma za mawasiliano hazijafika.

**168. *Mheshimiwa Spika*;** Kwa upande wa sekta ya gesi, Wizara ilitoa ruhusa ya masharti kwa kampuni ya *Etablissements Maurel & Prom S.A* yenye usajili wake nchini Ufaransa kuinunua kampuni ya *Wentworth Resources Plc.* Aidha, ununuzi huo ulifanyika kwa sharti la kampuni hiyo kuiuzia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) nyongeza ya asilimia 20 ya haki ya umiliki (*participating interest*) katika kitalu cha uchimbaji gesi cha Mnazi Bay hivyo kufanya TPDC kuwa na jumla ya asilimia 40 za umiliki katika kitalu cha gesi cha Mnazi Bay.

**169. *Mheshimiwa Spika;*** Ongezeko la umiliki wa kitalu cha gesi kwa TPDC unafaida nyingi kwa nchi ikiwa ni pamoja na kuwa sehemu ya maamuzi katika uendeshaji wa biashara ya uchimbaji na usambazaji gesi katika kitalu cha Mnazi Bay; kuongezeka kwa mapato ya kodi na yasiyo ya kikodi kupitia ongezeko la gawio; kujenga uwezo wa kampuni za ndani kushindana na kampuni kubwa ya gesi; na kupata teknolojia mpya (technology transfer) kupitia mashirikiano na kampuni hizo.

**O. Kutafuta Masoko ya Bidhaa za Tanzania**

**170.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara imefanikisha upatikanaji wa masoko kama ifuatavyo:-

**i. Soko la Nyama**

**171.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kupata soko la nyama nchini Saudi Arabia, Qatar na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) ambapo Kampuni za *Tanchoice na Eliya Food Industries* zimekidhi vigezo vya kuuza nyama katika masoko hayo. Kupitia masoko hayo, nyama tani 986.6 zenye thamani ya shilingi bilioni 12.5 ziliuzwa katika soko la Saudi Arabia; tani 1,262.7 zenye thamani ya shilingi bilioni 13.98 zimeuzwa katika soko la Qatar; na tani 2,248.4 zenye thamani ya shilingi bilioni 30.3 zimeuzwa katika soko la UAE.

**i. Soko la Mazao na Bidhaa**

**172.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imefanikiwa kuratibu ushiriki wa wadau 18 wa biashara katika majukwaa ya Kimataifa ya Kibiashara ikiwemo Maonesho ya Biashara ya Kimataifa Cairo Misri, Maonesho ya *Made in Africa* (Afrika Kusini), Maonesho ya Biashara ya Bidhaa ya China (CIIE), na Maonesho ya Uingizaji Bidhaa ya YIWU, China (China Import Commodities Trade Fair). Majukwaa hayo yalilenga kutangaza fursa na kuimarisha mauzo katika masoko ya Kimataifa hususan China.

**173.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia majukwaa hayo, Kampuni ya *Evrmax Co. Ltd* kutoka Tanzania imefanikiwa kuiuzia Kampuni ya *Sedra Industries Ltd* ya Misri, kontena mbili (2) za nyuzi za katani zenye thamani ya shilingi milioni 208.4. Vile vile, Kampuni ya *Afritea and Coffee Bleanders Ltd* ilifanya mauzo yenye thamani ya shilingi milioni 143.1. Aidha, kampuni hiyo ilifanikiwa kufanya mazungumzo ya awali na kampuni ya *Weihai Huwatan Supply Chain Management* ya China ya kuwa na mauzo ya kahawa na chai.

**P. Kuratibu Ziara za Wafanyabiashara na Mauzo ya Bidhaa**

**174.** ***Mheshimiwa Spika;*** Kupitia ziara za wafanyabiashara katika nchi mbalimbali ikiwemo Malawi, Afrika Kusini, UAE, Oman, Qatar, Kenya, China, India na Saudi Arabia imewezesha Tanzania kupata fursa ya masoko ya bidhaa za kilimo ambapo Tanzania imefanikiwa kuuza korosho tani 37 zenye thamani ya shilingi milioni 521.5 nchini Afrika Kusini; kuuza kahawa tani 11,470 yenye thamani ya shilingi bilioni 3.4 katika nchi za Marekani, Japani na Uswisi; kuuza korosho tani 192,296.4 yenye thamani ya shilingi bilioni 771 katika nchi za Vietnam, China na India; kuuza chai tani 1,149.8 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.6 katika nchi za Kenya, Misri na Falme za Kiarabu (UAE); kuuza parachichi tani 4,195.8 yenye thamani ya shilingi bilioni 16.7 katika nchi za Afrika Kusini, China, India, Uholanzi, Saudi Arabia na Uswisi; kuuza nafaka tani 2,886 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.9 katika nchi za Sudani Kusini, Afrika Kusini, Kenya, Malawi, na DRC; na kuuza pembejeo zenye thamani ya shilingi milioni 257.3 nchini Malawi.

**Q. Kuendeleza Mitaa ya Viwanda**

**175.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imekamilisha makadirio ya gharama za ujenzi na michoro ya kihandisi ya majengo saba (7) ya viwanda katika mikoa ya Dodoma, Kigoma na Simiyu ambapo taratibu za kupata mzabuni kwa ajili ya kuendelea na ujenzi zinaendelea. Aidha, Wizara imeendelea na ukamilishaji wa majengo mapya matano (5) ya viwanda ambapo majengo matatu (3) ya viwanda katika Mikoa ya Geita, Singida na Tanga yamekamilika na majengo mawili (2) ya viwanda katika Mkoa wa Shinyanga yapo katika hatua ya upauaji. Utekelezaji wa kazi hiyo umefikia asilimia 65.

**176.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imewezesha kuanzishwa kwa kiwanda cha vifungashio katika mtaa wa Viwanda wa SIDO Mkoa wa Mbeya. Kiwanda hicho cha vifungashio kina uwezo wa kuzalisha chupa milioni 36 kwa mwaka na hivyo kupunguza changamoto ya upatikanaji wa vifungashio vya chupa kwa wajasiriamali wa Mkoa huo na Mikoa ya jirani. Vile vile, Wizara imeanzisha kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi ya chikichi katika

Mkoa wa Kigoma. Kiwanda hicho kina uwezo wa kusafisha tani 624 za mafuta kwa mwaka.

**R. Kuhawilisha Teknolojia kwa Kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCS)**

**177.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeendelea kutengeneza na kuhawilisha teknolojia/mashine na vipuri kwa Kuimarisha Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) vya SIDO. Hadi kufikia Machi, 2024, jumla ya mashine 576 na vipuri 1,204 vya kuchakata mazao ya kilimo, mifugo na misitu vilitengenezwa na kuuzwa kwa wajasiriamali. Aidha, Vituo vya Uendelezaji Teknolojia (TDCs) vya Lindi, Mbeya na Kilimanjaro viliweza kubuni teknolojia tatu (3) za kusaga mwani, kubangua mbegu za makadamia na kukamua mafuta ya parachichi ili kuongeza ufanisi katika uchakataji. Teknolojia hizo zilizotengenezwa zimeweza kuingia sokoni na kuwezesha kuanzishwa kwa jumla ya viwanda vipya 262 na kutoa ajira za moja kwa moja 1,021.

**S. Mafunzo ya Atamizi za Biashara, Ukuzaji wa Teknolojia na Kuendeleza Mawazo ya Wabunifu**

**178.** ***Mheshimiwa Spika;*** Wizara imeanzisha mafunzo ya atamizi za biashara, ukuzaji teknolojia pamoja na mawazo bunifu ambapo hadi Machi, 2024 jumla ya vijana wapatao 205 wapo katika mafunzo hayo. Kati ya vijana hao, 185 wameatamiwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) na 20 wameatamiwa na TIRDO. Mafunzo ya atamizi ya biashara yamegawanyika katika makundi matatu (3) yaani hatua ya kuandaliwa (Pre-Incubation), hatua ya kulelewa (Incubation stage), na hatua ya mwisho (post incubation). Mafunzo hayo yanaanzia ngazi ya kubuni wazo la biashara mpaka kusajili majina ya biashara na hatimaye kusaidiwa kuanzisha biashara.

**179.** ***Mheshimiwa Spika*;** Kupitia mafunzo hayo tayari vijana 18 wamefikia hatua ya mwisho na kwa sasa wanaendesha biashara zao katika Mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Mbeya. Biashara za vijana hao zimejikita katika maeneo ya biashara mtandao, utengenezaji wa sabuni na viatu, uzoaji taka kwa njia ya mtandao, ushonaji, usindikaji wa asali na alizeti,

kutengeneza mvinyo pamoja na kutengeneza matofali ya plastiki. Vile vile, wataamizi 20 ambao wapo kwenye bunifu za teknolojia, kati yao, wabunifu watano (5) wameweza kusajili kampuni chini ya uangalizi wa atamizi. Mbunifu mmoja (1) amefanikiwa kuzalisha bushi za bajaji, magari aina ya IST na *canter* kwa kutumia malighafi inayotokana na urejeshaji wa taka za plastiki kwa mtambo uliosimikwa na TIRDO na tayari kwa sasa ameanza kuzalisha kibiashara.

**180. *Mheshimiwa Spika;*** Wizara pia inaendelea kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati 24, kwa kuwapatia mafunzo ya teknolojia za uongezaji thamani mazao kupitia kiatamizi cha teknolojia chini ya TEMDO, na baadaye kuwaunganisha na SIDO ili waweze kupata mikopo ya kununua mitambo na mashine mbalimbali kutoka TEMDO. Kwa upande mwingine, wabunifu wapatao 35 wanaendeleza bidhaa/huduma zao katika vituo vya teknolojia vya SIDO katika mikoa ya Arusha, Iringa, Morogoro, Rukwa, Singida, Dodoma, Mwanza na Dar es Salaam. Hadi kufikia Machi, 2024, Wizara kupitia SIDO imewezesha wajasiriamali wabunifu wanne (4) katika vituo vya:- Morogoro (utengenezaji wa samani na mapambo kwa kutumia taka ngumu); Mwanza (3D printing); na Njombe (utengenezaji wa alamu ya kufukuza ndege kwenye mashamba).

## 5. VIPAUMBELE VYA BAJETI YA MWAKA 2024/2025

**181. *Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024/2025, vipaumbele vikuu vya Wizara ni sita (6). Aidha, vipaumbele hivyo vitatekelezwa na shughuli mbalimbali za Wizara.

**182. *Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024/2025, vipaumbele vikuu vya Wizara ni kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati;

ii. Kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma kwa kuimarisha miundombinu na mazingira wezeshi;

iii. Kuboresha mazingira ya biashara;

iv. Kuchochea maendeleo ya watu kwa kuboresha miradi na programu katika sekta ya jamii inayohusisha elimu na mafunzo ya ujuzi;

v. Kuendelea na utafutaji wa masoko kwa bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini; na

vi. Kuchochea ukuaji wa Sekta binafsi nchini.

**183.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024/2025 shughuli zitakazotekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vikuu vya Wizara ni pamoja na: -

i. Kuendeleza miradi ya kimkakati ya Magadi Soda Engaruka na Makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma cha Liganga;

ii. Kuendeleza miradi ya kiwanda cha viuadudu (TBPL) na kiwanda cha KMTC;

iii. Kuendelea kukiwezesha Kiwanda cha TBPL kuzalisha mbolea hai (Biofertilizer) kwa kutumia mitambo iliyopo;

iv. Kusanifu na kuendeleza utengenezaji wa vifaa tiba vya hospitali awamu ya tatu;

v. Utengenezaji wa kibiashara wa viwanda vidogo vya kuchakata sukari (sugar mill mini-processing plant - Capacity 200 TCD);

vi. Kutengeneza Mitambo ya nishati mbadala na teknolojia za wachimbaji wadogo wa madini (ASM) ili ziweze kusaidia katika utunzaji wa mazingira;

vii. Kuanzisha mitaa ya viwanda kwa ajili ya kongano za viwanda na biashara katika Wilaya moja kila Mkoa ili kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi;

viii. Kuendelea kupambana na uingizaji wa bidhaa bandia ili kulinda nembo au alama za bidhaa dhidi ya watu wanaotumia nembo/alama hizo bila idhini ya wamiliki;

ix. Kufanya mafunzo kwa maafisa biashara kwa lengo la kuwafikia na kurahisisha shughuli za sajili na leseni kwa wafanyabiashara;

x. Kuwarasimisha wafanyabiashara na wenye viwanda waliopo kwenye sekta isiyo rasmi kwa kuendesha kliniki za biashara kwenye kila Halmashauri nchini.

xi. Kujenga uwezo na kutoa elimu kwa wadau kuhusu fursa zitokanazo na mashirikiano ya uwili, kikanda na kimataifa na kuwaunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na wawekezaji;

xii. Kufanya intelijensia ya masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini kwenye masoko ya kimkakati;

xiii. Kuingiza orodha ya bidhaa mpya kwenye mfumo na kutanua mfumo ulioboreshwa kwenye maeneo ya mifugo, uvuvi, madini yasiyo vito na bidhaa za mbogamboga;

xiv. Kukamilisha Mfumo wa Taarifa za Viwanda (National Industrial Information Management System – NIIMS) na tathmini ya viwanda na kuainisha fursa za uwekezaji (Industrial Mapping) katika kanda ya Ziwa;

xv. Kuimarisha usimamizi wa ubora na usalama wa bidhaa nchini zikiwemo bidhaa za chakula na vipodozi;

xvi. Kukamilisha uandaaji wa kuzalisha Kinasaba cha Mafuta *(Fuel Marker)* nchini; na

xvii. Kuimarisha uwajibikaji wa Wasimamizi wa Ghala kwa kushirikiana na kampuni za uhakiki wa bidhaa katika ghala.

## 6. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2024/2025

**184.** ***Mheshimiwa Spika;*** Katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Viwanda na Biashara inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 110,899,722,000 kwa Fungu 44. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,115,206,000 ni matumizi ya kawaida, na shilingi 29,784,516,000

ni matumizi ya Maendeleo. Kati ya shilingi 81,115,206,000 za matumizi ya kawaida, zinajumuisha shilingi 68,352,946,000 fedha za Mishahara na shilingi 12,762,260,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**7. HITIMISHO**

**185.** ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba nichukue fursa hii kuwashukuru tena watanzania wote kwa kuendelea kutuunga mkono katika jitihada zetu za kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara. Tutaendeleza jitihada za kujenga na kuimarisha misingi thabiti ya uchumi kwa kuvutia wawekezaji na ujenzi wa viwanda kama ilivyobainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 - 2025. Ni rai yetu kwamba kila Mtanzania popote alipo anahitajika kutimiza wajibu wake, kujituma, kubadilisha mtizamo na kuwa mstari wa mbele kulinda na kutetea jitihada na kuendeleza uwekezaji katika viwanda na biashara. Inawezekana, tutimize wajibu wetu na kuunga mkono kwa vitendo jitihada kubwa za Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**186.** ***Mheshimiwa Spika;*** Hotuba hii pia inapatikana katika Tovuti ya Wizara **www.mit.go.tz.**

**187.** ***Mheshimiwa Spika;*** Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa maneno yako haya. Mnaelekea kuzuri sana, na mtabadilisha suala la viwanda nchini mwetu. Hongera sana na hasa kukutana na wadau wa Kariakoo wakati wana shida, mnakaa nao na mnayamaliza. Sasa Kocha wa Simba Mgunda anasema *ball* linatembea, na wewe tukuombe *walk the talk*. Ahsante.

Sasa, namwita Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. FRANCIS I. MTINGA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika, naomba sasa kutoa taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/2024, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fungu 44 kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu ya muda, naomba Taarifa hii iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maelezo ya jumla na utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (fungu 44) kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi wa Kamati. Msingi wa uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6 (1)(a) ikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio ya matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 23 Machi, 2024 Kamati ilichambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu

utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Taarifa hii inatokana na uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mawanda ya uchambuzi wa taarifa, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo: -

(a) Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/2024;

(b) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufikia mwezi Februari, 2024;

(c) Uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2023/2024; na

(d) Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, muundo wa taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kuhusu muundo wa taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo: -

(a) Sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi wa muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya pili inazungumzia uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2024/2025; na

(c) Sehemu ya tatu inahusu maoni, ushauri wa Kamati, na hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala yaliyobainishwa hapo juu yanajitokeza katika Taarifa hii. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri uliotolewa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya pili, inahusu msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2023/2024 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Baada ya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na:-

(i) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(iv) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa shilingi 25,650,272,000 fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya

Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea asilimia 37 tu ya fedha zilizotengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo haukuwa wa kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea asilimia 37 tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hali hiyo inaonesha kuwa, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi hicho ulikuwa nyuma kwa asilimia 63. Upatikanaji huu wa fedha wa kusuasua unachangia baadhi ya miradi kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa katika Mpango wa Bajeti ya Wizara ya mwaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kuliomba Bunge, kuhimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuwezesha kukamilika utekelezaji wa miradi iliyopangwa kabla mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam kuanzia tarehe 12 hadi 18 Machi, 2024. Lengo la ziara hii ilikuwa kukagua miradi iliyotengewa fedha katika Wizara hii, miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CARMATEC)* - (Mradi Na. 6260) ulioko Arusha;

(ii) Mradi wa Kiwanda cha Kutengeneza Mashine na Vipuri *(Kilimanjaro Machine Tools – KMTC*) – (Mradi Na. 6260) uliopo Kilimanjaro; na

(iii) Mradi wa Jengo la Utawala la *TIRDO* ulioko Dar es Salaam. *TIRDO* imekusudia kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa Teknolojia na Viatamizi – (Mradi Na. 6260).

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi. Uchambuzi wa Kamati katika Miradi mitatu iliyotembelewa ulibaini uwepo wa mafanikio na changamoto, ambapo ulitoa ushauri wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *CAMARTEC* katika mwaka wa fedha 2023/2024 ulitengewa shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 taasisi hii ilikuwa imepokea pesa yote, shilingi 1,500,000,000 iliyoidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kupatiwa fedha zote ilizotengewa, bado kiasi hicho hakitoshelezi mahitaji ambayo ni shilingi bilioni 7.4 kwa mwaka. Kamati inaishauri kuwa, Serikali itengee fedha za kutosha Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali yetu inawekeza fedha nyingi kwenye Sekta ya Kilimo. Upatikanaji wa zana za kilimo na teknolojia mpya kupitia *CAMARTEC* ni wa muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Kilimanjaro *Machine Tools (KMTC)* kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ulitengewa shilingi 1,600,000,000 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo hadi Kamati inatembelea Wizara ilikuwa imepokea shilingi 626,725,000 tu sawa na asilimia 45.4 ya fedha zilizotengwa. Kamati hairidhishwi na upatikanaji huu wa fedha kwa kuwa unasababisha shughuli za Kiwanda kutotekelezeka kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kukifufua Kiwanda hiki kilichokaa zaidi ya miaka 25 bila kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri kuwa Serikali iipatie *KMTC* shilingi bilioni 3.46 inazohitaji kama mtaji ili iweze kujiendesha na kufikia lengo ililojiwekea. Kiasi hiki cha fedha

kitaisaidia *KMTC* kuzalisha shilingi bilioni 10.2 kwa kipindi cha miaka mitano ijayo zitakazochangia mapato ya Serikali. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kukipatia kiwanda hiki fedha zilizotengwa na Bunge kwa wakati ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitendo cha kuchelewesha kuipatia *KMTC* fedha za kutosha kinakwamisha kazi nzuri na yenye tija ya kuzalisha mashine zaidi ya 300, vipuri mbalimbali na kutoa ajira takribani 207 za moja kwa moja na 1,200 zisizo za moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *TIRDO* katika mwaka wa fedha 2023/2024 ulitengewa shilingi 1,500,000,000. Hadi Machi, 2024 Kamati ilipoitembelea *TIRDO*, ilikuwa imepokea shilingi 665,766,558.86, sawa na 44.38% ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kamati inashauri kuwa Serikali iipatie *TIRDO* kiasi cha fedha kilichobaki ili iweze kutekeleza kikamilifu shughuli ilizojipangia kabla ya mwaka wa fedha wa 2023/2024 kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati imebaini uwepo wa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali. Ucheleweshaji huu unasababisha miradi kuchelewa kukamilika na gharama kupanda. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe fedha kwa wakati ili Wakandarasi wakamilishe kazi zao kwa wakati kama zilivyopangwa. Kuongezeka kwa gharama za miradi kunachangia ongezeko la ulipaji wa kodi nchini mwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa watumishi. Utendaji wa ufanisi wa taasisi yoyote ile unategemea pamoja na mambo mengine, uwepo wa rasilimali watu ya kutosha kwa kufanya kazi hizo. Kamati imebaini uwepo wa upungufu mkubwa wa watumishi wa kudumu katika taasisi ilizozitembelea. Vilevile, lipo tatizo la baadhi ya maafisa kukaimu kwa zaidi ya miaka mitano bila kuthibitishwa kwenye nafasi hizo. Ili kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iajiri watumishi wa kutosha katika nafasi husika za taasisi hizi. Aidha, Kamati inashauri Maafisa wenye sifa wanaokaimu, wathibitishwe katika nyadhifa zao;

(ii) Serikali ifanyie mabadiliko kwenye sheria zinazohusiana na ajira za vijana hapa nchini ambazo zinataka sifa za kuajiriwa kuwa Kidato cha Nne na kuendelea, badala yake iruhusu wahitimu wa darasa la saba waliopitia mafunzo ya ufundi waweze kuajiriwa. Mathalani, zipo fani kama mafundi mchundo na sanifu ambazo zina watu wengi wenye sifa na weledi ambao wamehitimu elimu ya msingi lakini hawaajiriki kwa kuwa hawana elimu ya Kidato cha Nne; na

(b) Bidhaa zinazozalishwa katika Viwanda vya nchini mwetu kununuliwa na Taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi za Serikali zinapaswa kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na viwanda vya nchini mwetu. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya Taasisi zinaagiza bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zingeweza kununuliwa hapa nchini mwetu tena kwa wakati na kwa gharama nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iviwezeshe viwanda vyetu ili vizalishe kwa wingi bidhaa zenye ubora wa kuvutia watumiaji wa ndani zikiwemo Taasisi zetu za Umma. Kwa mfano, vifaa kama vitanda vya hospitali, majokofu ya kuhifadhia maiti, makabati, matrekta, mashine za kupandia mbegu na kuvuna mazao ya aina mbalimbali na kadhalika, vinapaswa kuzalishwa kwa wingi na ubora wa hali ya juu kutoka kwenye viwanda vya ndani vya *CAMARTEC, TEMDO, SIDO* na *Kilimanjaro Machine Tools*. Kufanya hivi kutaokoa fedha za kigeni zinazotumika kufanya manunuzi nje ya nchi na kuongeza ufanisi wa viwanda vya ndani na kuongeza ajira na vipaji kwa Watanzania.

(c) Uhaba/uchakavu wa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, viwanda vilivyotembelewa vinakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi na vilivyopo vingi vimechakaa. Kamati inashauri kuwa Serikali ivipatie viwanda hivi vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kufanya utafiti na kuzalisha bidhaa zitakazowafikia wakulima na wafugaji wengi kwa gharama nafuu.

(d) Kutangaza bidhaa zinazozalishwa na *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kwamba, wakulima na wafugaji wengi walioko mijini na vijijini hawafahamu uwepo wa bidhaa zinazozalishwa na kituo hiki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wakulima na wafugaji kote nchini wanapata uelewa kuhusu bidhaa zinazozalishwa na kituo hiki. Wananchi wengi wanatumia njia za zamani ambazo zinawachukulia muda mrefu na hazileti tija inayokusudiwa kwa kuwa hawafahamu shughuli zinazotekelezwa na *CAMARTEC*. Aidha, wengi huagiza vifaa kama matrekta kutoka nje ya nchi wakati yanazalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali ianzishe vituo kwenye maeneo mengine vitakavyokuwa na jukumu la kuuza matrekta yanayozalishwa na *CAMARTEC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu 44 iliidhinishiwa shilingi 66,256,618,827 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ulivuka lengo ambapo Wizara ilikuwa imepokea asilimia 68.01 mwezi Februari, 2024 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa Wizara itafikia malengo iliyojiwekea endapo asilimia 31.99 ya fedha zilizobaki zitaendelea kutoka kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 yaliyotolewa wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Kamati iliishauri Wizara mambo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Taarifa ya mtoa hoja ilionesha kuwa, Serikali

imetekeleza maagizo ya Kamati. Aidha, baadhi ya maagizo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa agizo mojawapo lililotekelezwa ni suala la ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma, ambapo mwezi Februari, 2024, Serikali ililipa wahusika shilingi bilioni 15.38 kati ya shilingi bilioni 15.42, sawa na asilimia 98.86.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika kuona ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Serikali iipatie Wizara hii fedha ilizoidhinishiwa na Bunge ili iweze kukamilisha utekelezaji wa maagizo iliyopewa na kuwa maagizo mengine yanakwama kutekelezwa kutokana na kukosekana kwa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Lengo la uchambuzi huo pamoja na mambo mengine, lilikuwa ni kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu 44 inaomba kutengewa jumla ya shilingi 110,899,722,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 81,115,206,000 sawa na asilimia 73.14 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 29,784,516,000 sawa na asilimia 26.86 ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Makadirio ya Bajeti yameongezeka kwa asilimia 21 ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Mishahara imeongezeka kwa asilimia 19. Ongezeko hili linatokana na kupandisha watumishi madaraja na uwepo wa ikama ya ajira mpya; *(Makofi)*

(iii) Fedha za Maendeleo za Ndani zimeongezeka kwa asilimia 16 kulinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha. Uchambuzi unaonesha kwamba ongezeko hili linaashiria kuleta msukumo chanya kwenye utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo endapo Serikali itatoa fedha hizi kwa wakati kama zilivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea Bajeti Wizara hii kwani kwa kufanya hivi kutawezesha utafiti wa viwanda na masoko kufanyika. Nchi zilizoendelea zimepata mafanikio hayo kwa sababu ya kuwekeza kwenye viwanda vya ndani. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu ni maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2023, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuataao kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(a) Upatikanaji wa fedha na utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na Serikali kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, bado Kamati inaona kuwa, kiasi hiki ni kidogo kuweza kufikia Mapinduzi ya Viwanda yanayokusudiwa. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali iendelee kuongeza Bajeti ya Wizara hii kila mwaka ili kufanikisha Mapinduzi ya Viwanda; na

(ii) Serikali ihakikishe kuwa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kila mwaka inatolewa yote na kwa wakati.

(b) Mazingira ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yetu bado inahitaji uwekezaji zaidi wa ndani na nje. Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Iboreshe mazingira ya uwekezaji ili Sekta Binafsi iendelee kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza ajira, uongezaji wa thamani na mapato ya fedha za kigeni;

(ii) Iendelee kulinda viwanda vilivyopo nchini hasa vile ambavyo uzalishaji wake una mchango mkubwa kwenye ajira na kuokoa fedha za kigeni kama viwanda vya sukari; na *(Makofi)*

(iii) Ni vema maamuzi yoyote ambayo yanaweza kuwa na madhara ya kudhoofisha uwekezaji kwenye viwanda, yafanyiwe tathmini ya kina kabla ya kufanywa.

(c) Mradi wa Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutolewa kwa shilingi bilioni 15.38 kwa waliopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma mnamo mwezi Februari, 2024 ni hatua inayofanikisha tija ya Mradi wa Liganga na Mchuchuma. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita, kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na hatua ya Mradi huu kuendelea kusuasua kwa muda mrefu. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikamilishe majadiliano na Mwekezaji ili kazi za uchimbaji wa chuma na makaa ianze haraka. *(Makofi)*

(d) Upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa zinazozalishwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, matangazo ni njia mojawapo inayohabarisha watu na kuongeza soko kwenye biashara. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini zinakosa soko kwa sababu ya kutotambuliwa na wananchi walio wengi kutokana na kutotangazwa; kwa mfano, bidhaa zinazozalishwa na *CAMARTEC, TEMDO, KMTC* na *SIDO* zinanunuliwa na wananchi/taasisi chache.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile vipo viwanda vya watu binafsi vinavyozalisha bidhaa ambazo taasisi mbalimbali

zingeweza kuzitumia badala ya kuagiza nje ya nchi. Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Ichukue hatua za makusudi kuhakikisha inatangaza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini ili wakulima na wafugaji wafahamu uwepo wa bidhaa hizo;

(ii) Serikali itafute namna ya kuziunganisha taasisi za umma ili zifahamu bidhaa zinazotengenezwa na wenzao; kwa mfano, *TEMDO* wanatengeneza bidhaa ambazo zinaweza kutumiwa na Wizara ya Afya. Aidha, uwepo mkakati wa kuzitaka taasisi mbalimbali kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini badala ya kuagiza ili kuokoa fedha za kigeni; na

(iii) Wizara ya Kilimo ione namna inavyoweza kununua zana zinazozalishwa *TEMDO* na *CAMARTEC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na juhudi za Serikali za kufufua baadhi ya viwanda vilivyokuwa vimesimamisha uzalishaji kwa muda mrefu, bado viwanda hivyo vinakabiliwa na upungufu wa mitaji, jambo linalosababisha kutochangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, Kiwanda cha Kutengeneza Mashine na Vipuri *(KMTC)* kina uwezo wa kuzalisha shilingi bilioni 10.2 kwa kipindi cha miaka mitano endapo Serikali itakipatia mtaji wa shilingi bilioni 3.46 zilizoombwa na kiwanda hiki. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikipatie kiwanda hiki mtaji huo, ili kufikia malengo. Aidha, viwanda vingine viwekewe mazingira wezeshi, ili kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wameendelea kutumia mfumo wa rumbesa kuuza na kununua bidhaa, hasa mazao ya wakulima, kwa lengo la kuwanyonya na kuikosesha Serikali mapato. Kamati inashauri kuwa:-

i. Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi sehemu mbalimbali kuhusu faida ya kuuza kwa kutumia vipimo sahihi (mizani) na athari inayopatikana kwa kutumia rumbesa.

ii. Serikali itoe mwongozo kuhusiana na suala la rumbesa ambalo ni suala mtambuka, ili Halmashauri zote ziweze kusimamia kwa uwiano ambao utaleta manufaa kwa wakulima. Aidha, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wengine wanaohusika wahakikishe wakulima hawadhulumiwi wanapouza mazao yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa Stakabadhi Ghalani umeanza kuonesha mafanikio kwa kufanya vizuri kwenye mazao ambayo yameshaingizwa. Ili kuendelea kuboresha mfumo huu, Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

i. Ipanue wigo kwa kuongeza mazao ambayo bado hayajaingizwa kwenye mfumo.

ii. Ihakikishe vyama vya msingi vinawalipa wakulima fedha zao kwa wakati mara taratibu za mauzo zinapokamilika. Hali hii itaondoa migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na Wananchi.

iii. Ihakikishe kuwa tozo za mazao ya wakulima zinapunguzwa kwa kuwa, baadhi zinasababisha kero. Marekebisho ya tozo yatawapa imani zaidi wakulima kwa Serikali yao na wengi watajitokeza kuuza bidhaa zao kwenye masoko halali badala ya kutumia mifumo isiyo rasmi ikiwemo kangomba.

iv. Serikali iendelee kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wadau wa mfumo wa stakabadhi za ghala kuhusu kutumia mfumo rasmi kuuza na kununua bidhaa mbalimbali. Matumizi sahihi ya mfumo huo ndiyo suluhisho la kero wanazopata wakulima kuhusiana na mifumo ya masoko yetu kwa ujumla wake.

v. Maghala yajengwe maeneo ambako mazao yanalimwa au uwekwe utaratibu mzuri wa kuyachukua kwa kusogeza vituo vya kuuza karibu na wakulima, ili kuwapunguzia gharama za kusafirisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu ni jambo muhimu katika uendeshaji wa

viwanda. Wamiliki wa viwanda wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa umeme wa kutosha na wa uhakika, hali inayosababisha kutumia fedha nyingi kununua nishati ya mafuta, kwa ajili ya kuendesha jenereta. Kamati inashauri kuwa, Serikali iweke miundombinu ya umeme wa uhakika na wa bei nafuu katika maeneo yote ya viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mandhari nzuri ya masoko ni kivutio cha biashara yoyote iwayo. Yapo baadhi ya masoko hapa nchini ambayo hayana mandhari nzuri kutokana na miundombinu yake kuwa ya muda mrefu na hivyo, yamechakaa na kuwa kero hasa kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali itenge fedha, kwa ajili ya ukarabati na utanuzi wa masoko, ili yawe katika hali nzuri. Kwa kufanya hivyo, mandhari itakuwa ya kuvutia, wateja wataongezeka, biashara itaimarika na mapato ya Serikali yataongezeka. Aidha, Wizara ya Viwanda ikishirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iandae mwongozo wa ujenzi na ukarabati wa masoko ndani ya Halmashauri, Manispaa na Majiji kwa mujibu wa mipango iliyowekwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na yawe katika maeneo rafiki na mwonekano mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Machinga ni kundi kubwa hapa nchini na ambalo bado linapata taabu ya kupata maeneo maalum, kwa ajili ya kufanya biashara zao. Wengi wao wanazunguka mitaani kutafuta wateja, hali inayochangia ukusanyaji wa kodi ya Serikali kuwa mgumu kwani baadhi yao hawalipi kodi kwa kuwa, hawana maeneo maalum.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuwatengea Machinga wote maeneo maalum ya kufanyia biashara ambayo ni rafiki, ikiwemo kuweka miundombinu itakayosaidia kukusanya kodi kwa kutumia mifumo rahisi na ya kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho. Naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa

hii kumshukuru Spika wetu ambaye pia, amekuwa akiliongoza Bunge kwa weledi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, napenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge, na Wenyeviti wa Bunge, kwa weledi na umahiri wao katika kusaidia kuongoza Vikao vya Bunge la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge, ambaye ni Waziri wa Viwanda na Biashara. Namshukuru Mheshimiwa Exaud Silaoneka Kigahe, Mbunge, Naibu Waziri, Dkt. Hashil Twaibu Abdallah, Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc*, kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi. Napenda pia kuwashukuru sana wananachi wa Mkalama kwa kuendelea kuniombea Mbunge wao kuwa na afya njema na kuendelea kuwawakilisha vizuri katika Bunge lao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Fungu – 44, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**21 MEI, 2024**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FUNGU – 44 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni kwa mujibu wa Masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Kanuni ya 6 (1)(a) ikisomwa pamoja na Kanuni ya 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inahusu uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yaliyotaka Taarifa za utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni.

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 23 Machi, 2024 Kamati ilichambua Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Taarifa hii inatokana na

uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii inahusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi iliyochambuliwa inahusu maeneo yafuatayo: -

(i) Mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Utekelezaji wa kazi zilizofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kufikia mwezi Februari, 2024;

(iii) Uzingatiaji wa Ushauri na Maoni ya Kamati uliotolewa Bungeni wakati wa kupitisha Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; na

(iv) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 1.4 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kuhusu Muundo wa Taarifa inayowasilishwa Bungeni. Taarifa hii imegawanyika katika sehemu tatu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya **Pili** inazungumzia Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025; na

(c) Sehemu ya **Tatu** inahusu Maoni, Ushauri wa Kamati, na Hitimisho.

**Mheshimiwa Spika**, masuala yaliyobainishwa hapo juu yanajitokeza katika Taarifa hii. Kwa muktadha huo, naliomba Bunge lako Tukufu lifuatilie kwa kina mtiririko wa Taarifa hii ili kupata msingi wa ushauri unaotolewa na Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO KAMILI KUHUSU UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, sehemu hii inahusu msingi wa ushauri wa Kamati uliotokana na Hoja ya Waziri wa Viwanda na Biashara. Masuala yanayochambuliwa ni Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### 2.2 Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na:-

(i) Hali ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(iii) Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina; na

(iv) Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa kazi zilizopangwa kufanyika kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

### 2.2.1 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa **Shilingi 25,650,270,000** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024, Wizara ilipokea **asilimia 37** tu ya Fedha zilizotengwa.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za ndani kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo haukuwa wa kuridhisha, kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Wizara ilipokea **asilimia 37** tu ya fedha zilizoidhinishwa. Hali hiyo inaonesha kuwa, utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi hicho ulikuwa nyuma kwa asilimia **63.** Upatikanaji huu wa fedha wa kusuasua unachangia baadhi ya Miradi kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara ya mwaka husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuliomba Bunge, kuihimiza Serikali kukamilisha upelekaji wa fedha kwa Wizara hii kama zilivyoidhinishwa na Bunge ili kuiwezesha kukamilisha utekelezaji wa Miradi iliyopangwa kabla mwaka wa fedha kumalizika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 inayoitaka Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kufanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha, Kamati ilifanya ziara katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam, kuanzia tarehe 12 hadi 18 Machi, 2024. Lengo la ziara hii ilikuwa kukagua Miradi iliyotengewa fedha katika Wizara hii. Miradi hiyo ni:-

(i) Mradi wa Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini *(CARMATEC)* – (Mradi Na. 6260) ulioko Arusha;

(ii) Mradi wa Kiwanda cha Kutengeneza Mashine na Vipuri (*Kilimanjaro Machine Tools – KMTC*) – (Mradi Na. 6260) uliopo Kilimanjaro; na

(iii) Mradi wa Jengo la Utawala la *TIRDO* ulioko Dar es Salaam. *TIRDO* imekusudia kuanzisha Kituo cha Taarifa za Viwanda na Ubashari wa Teknolojia na Viatamizi – (Mradi Na. 6260).

### 2.2.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika Miradi mitatu iliyotembelewa ulibaini uwepo wa mafanikio na changamoto, ambapo ilitoa ushauri wa hatua zinazopaswa kuchukuliwa kama ifuatavyo:-

(a) **Upatikanaji wa Fedha za Miradi ya Maendeleo**

(i) **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa *CAMARTEC* katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulitengewa **Shilingi 1,500,000,000,** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Februari, 2024 Taasisi hii ilikuwa imepokea pesa yote, **Shilingi 1,500,000,000** iliyoidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kupatiwa fedha zote ilizotengewa, bado kiasi hicho hakitoshelezi mahitaji ambayo ni **Shilingi bilioni 7.4** kwa mwaka. Kamati inaishauri kuwa, Serikali itengee fedha za kutosha Wizara hii iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo hasa katika kipindi hiki ambacho Serikali yetu inawekeza fedha nyingi kwenye Sekta ya Kilimo. Upatikanaji wa zana za kilimo na teknolojia mpya kupitia *CAMARTEC* ni wa muhimu sana.

(ii) **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kilimanjaro Machine Tools *(KMTC)* kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, ulitengewa **Shilingi 1,600,000,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo hadi Kamati inatembelea Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 726,725,000** tu sawa na **asilimia 45.4** ya fedha

zilizotengwa. Kamati hairidhishwi na upatikanaji huu wa fedha kwa kuwa unasababisha shughuli za Kiwanda kutotekelezeka kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kukifufua Kiwanda hiki kilichokaa zaidi ya miaka 25 bila kufanya kazi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri kuwa, Serikali iipatie *KMTC* **Shilingi bilioni 3.46** inazohitaji kama mtaji ili iweze kujiendesha (*Working Capital*) na kufikia lengo ililojiwekea. Kiasi hiki cha fedha kitaisaidia *KMTC* kuzalisha **Shilingi bilioni 10.2** kwa kipindi cha miaka mitano ijayo zitakazochangia mapato ya Serikali. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kukipatia Kiwanda hiki fedha zilizotengwa na Bunge kwa wakati ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kitendo cha kuchelewesha kuipatia KMTC fedha za kutosha kinakwamisha kazi nzuri na yenye tija ya kuzalisha mashine zaidi ya 300, vipuri mbalimbali na kutoa ajira takriban 207 za moja kwa moja na 1,200 zisizo za moja kwa moja.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa *TIRDO* katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 ulitengewa **shilingi 1,500,000,000.** Hadi Machi, 2024 Kamati ilipoitembelea *TIRDO*, ilikuwa imepokea **shilingi 665,766,558.86,** sawa na **asilimia 44.38** ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge. Kamati inashauri kuwa, Serikali iipatie *TIRDO* kiasi cha fedha kilichobaki ili iweze kutekeleza kikamilifu shughuli ilizojipangia kabla ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 kumalizika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati imebaini uwepo wa tatizo la ucheleweshaji wa malipo ya Wakandarasi wanaotekeleza miradi mbalimbali. Ucheleweshaji huu unasababisha miradi kuchelewa kukamilika na gharama kupanda. Kamati inashauri kuwa, Serikali itoe fedha kwa wakati ili Wakandarasi wakamilishe kazi zao kwa wakati kama

zilivyopangwa. Kuongezeka kwa gharama za miradi kunachangia ongezeko la ulipaji wa kodi nchini mwetu.

**(b) Upungufu wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika,** utendaji wa ufanisi wa taasisi yoyote ile unategemea pamoja na mambo mengine, uwepo wa rasilimali watu ya kutosha wa kufanya kazi hizo. Kamati imebaini uwepo wa upungufu mkubwa wa watumishi wa kudumu katika taasisi ilizozitembelea. Vilevile, lipo tatizo la baadhi ya maafisa kukaimu kwa zaidi ya miaka mitano bila kuthibitishwa kwenye nafasi hizo.

Ili kukabiliana na changamoto hizi, Kamati inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali iajiri watumishi wa kutosha katika nafasi husika za taasisi hizi. Aidha, Kamati inashauri Maafisa wenye sifa wanaokaimu, wathibitishwe katika nyadhifa zao.

(ii) Serikali ifanyie mabadiliko kwenye sheria zinazohusiana na ajira za vijana hapa nchini ambazo zinataka sifa za kuajiriwa kuwa Kidato cha Nne na kuendelea, badala yake iruhusu wahitimu wa darasa la saba waliopitia mafunzo ya ufundi waweze kuajiriwa. Mathalani, zipo fani kama mafundi mchundo na sanifu ambazo zina watu wengi wenye sifa na weledi ambao wamehitimu elimu ya msingi lakini hawaajiriki kwa kuwa hawana elimu ya Kidato cha Nne.

**(c) Bidhaa zinazozalishwa katika Viwanda vya nchini mwetu kununuliwa na Taasisi za Serikali**

**Mheshimiwa Spika,** Taasisi za Serikali zinapaswa kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na viwanda vya nchini mwetu. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya Taasisi zinaagiza bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo zingeweza kununuliwa hapa nchini mwetu tena kwa wakati na kwa gharama nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iviwezeshe viwanda vyetu ili vizalishe kwa wingi bidhaa zenye ubora wa kuvutia watumiaji wa ndani zikiwemo Taasisi zetu za Umma. Kwa mfano, vifaa kama

vitanda vya hospitali, majokofu ya kuhifadhia maiti, makabati, matrekta, mashine za kupanda mbegu na kuvuna mazao ya aina mbalimbali na kadhalika, vinapaswa kuzalishwa kwa wingi na ubora wa hali ya juu kutoka kwenye viwanda vya ndani vya *CAMARTEC, TEMDO, SIDO* na Kilimanjaro Machine Tools. Kufanya hivi kutaokoa fedha za kigeni zinazotumika kufanya manunuzi nje ya nchi na kuongeza ufanisi wa viwanda vya ndani na kuongeza ajira na vipaji kwa Watanzania.

**(d) Uhaba/uchakavu wa vifaa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, viwanda vilivyotembelewa vinakabiliwa na uhaba wa vifaa vya kufanyia kazi na vilivyopo vingi vimechakaa. Kamati inashauri kuwa, Serikali ivipatie viwanda hivi vifaa vya kisasa vitakavyosaidia kufanya utafiti na kuzalisha bidhaa zitakazowafikia wakulima na wafugaji wengi kwa gharama nafuu.

**(e) Kutangaza bidhaa zinazozalishwa na *CAMARTEC***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, wakulima na wafugaji wengi walioko mijini na vijijini hawafahamu uwepo wa bidhaa zinazozalishwa na Kituo hiki. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wakulima na wafugaji kote nchini wanapata uelewa kuhusu bidhaa zinazozalishwa na Kituo hiki. Wananchi wengi wanatumia njia za kizamani ambazo zinawachukulia muda mrefu na hazileti tija inayokusudiwa kwa kuwa hawafahamu shughuli zinazotekelezwa na *CAMARTEC*. Aidha, wengi huagiza vifaa kama matrekta kutoka nje ya nchi wakati yanazalishwa hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri kuwa, Serikali ianzishe vituo kwenye maeneo mengine vitakavyokuwa na jukumu la kuuza matrekta yanayozalishwa na *CAMARTEC*.

***2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida***

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Wizara ya Viwanda na Biashara – **Fungu 44** iliidhinishiwa **Shilingi 66,254,618,827.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea maelezo ya Waziri yaliyofafanua upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kama **Kielelelezo Na. 1** kinavyoonesha.

**Kielelezo Na. 1: Ulinganifu wa Bajeti iliyoidhinishwa 2023/2024 na kiasi cha fedha zilizopatikana kufikia Mwezi Februari, 2024 - Fungu 44**

| **Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka 2023/2024 - Fungu 44** | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Kilichoidhinishwa** | **Kilichopokelewa** | **Asilimia** |
| Mishahara | 57,315,546,827 | 38,463,019,372.63 | 67.11 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 8,939,072,000 | 6,596,815,929.75 | 74 |
| **JUMLA** | **66,254,618,827** | **45,059,835,302.38** | **68.01** |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara**

**Kielelezo Na. 2: Ufafanuzi kuhusu upatikanaji wa fedha kwa asilimia - Fungu 44**




Chanzo: Randama ya Wizara ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi umeonesha kuwa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2024 ulivuka lengo ambapo Wizara ilikuwa imepokea **asilimia 68.01** mwezi Februari, 2024 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mwenendo huu wa upatikanaji wa fedha unaonesha kuwa Wizara itafikia malengo iliyojiwekea endapo **asilimia 31.99** ya fedha zilizobaki zitaendelea kutoka kwa wakati.

### 2.2.5 Hali ya Uzingatiaji wa Ushauri Uliotolewa na Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya mapitio ya utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa Fungu 44 yaliyotolewa wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kamati iliishauri Wizara mambo mbalimbali yaliyolenga kuboresha utekelezaji wa majukumu yake. Taarifa ya Mtoa Hoja ilionesha kuwa, Serikali imetekeleza maagizo ya Kamati. Aidha, baadhi ya maagizo yapo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Agizo mojawapo lililotekelezwa ni suala la ulipaji fidia kwa wananchi wanaopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma, ambapo mwezi Februari, 2024, Serikali ililipa wahusika **Shilingi bilioni 15.38** kati ya **Shilingi bilioni 15.42,** sawa na **asilimia 98.86.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imeridhika kuona ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, Kamati inashauri kuwa, Serikali iipatie Wizara hii fedha ilizoidhinishiwa na Bunge ili iweze kukamilisha utekelezaji wa maagizo iliyopewa kwa kuwa maagizo mengine yanakwama kutekelezwa kutokana na kukosekana kwa fedha.

## 2.3 Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea na kuchambua Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara – Fungu 44 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Lengo la uchambuzi huo pamoja na mambo mengine, lilikuwa ni kujihakikishia iwapo Mpango na Makadirio haya umezingatia Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano, Mwongozo wa Mpango wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya Fedha pamoja na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 - 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Viwanda na Biashara - **Fungu 44** linaomba kutengewa jumla ya **Shilingi 110,899,722,000**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi 81,115,206,000** sawa na **asilimia 73.14** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 29,784,516,000** sawa na **asilimia 26.86** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. (**Kielelezo Namba 3).**

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Fedha zilizoombwa kwa Mwaka 2023/2024 na Fedha zinazoombwa 2024/2025**

| **Ulinganisho wa Bajeti Fungu 44 kwa Mwaka 2023/2024 na 2024/2025** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **2023/2024** | **2024/2025** | **Ongezeko/ Pungufu** | **Asilimia** |
| Mishahara | 57,315,546,82 7 | 68,352,946,000 | 11,037,399,173 | 19 |
| Matumizi Mengineyo (OC) | 8,939,072,000 | 12,762,260,000 | 3,823,188,000 | 43 |
| **Jumla Ndogo 1** | **66,254,618,82 7** | **81,115,206,000** | **14,860,587,173** | **22** |
| Maendeleo (Ndani) | 25,650,270,00 0 | 29,784,516,000 | 4,134,246,000 | 16 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Maendeleo (Nje) | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla Ndogo 2** | **25,650,270,00 0** | **29,784,516,000** | **4,134,246,000** | **16** |
| **Jumla ya ulinganifu** | **91,904,888,82 7** | **110,899,722,000** | **18,994,833,17 3** | **21** |

**CHANZO: Randama ya Wizara - Fungu 44**

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa:-

(i) Makadirio ya Bajeti yameongezeka kwa **asilimia 21** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024;

(ii) Mishahara imeongezeka kwa **asilimia 19.** Ongezeko hili linatokana na kupandisha watumishi madaraja na uwepo wa ikama ya ajira mpya;

(iii) Fedha za Maendeleo za Ndani zimeongezeka kwa **asilimia 16** kulinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha**.** Uchambuzi unaonesha kwamba, ongezeko hili linaashiria kuleta msukumo chanya kwenye utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo endapo Serikali itatoa fedha hizi kwa wakati kama zilivyopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuiongezea Bajeti Wizara hii kwani kwa kufanya hivi kutawezesha utafiti wa viwanda na masoko kufanyika. Nchi zilizoendelea zimepata mafanikio hayo kwa sababu ya kuwekeza kwenye viwanda vya ndani. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuiongezea fedha Wizara hii ili iweze kufikia Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu

44) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, pamoja na mapendekezo ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

**(a) Upatikanaji wa Fedha na Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara**

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na Serikali kuendelea kuongeza Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara, bado Kamati inaona kuwa, kiasi hiki ni kidogo kuweza kufikia Mapinduzi ya Viwanda yanayokusudiwa. Kamati inashauri kwamba:-

(i) Serikali iendelee kuongeza Bajeti ya Wizara hii kila mwaka ili kufanikisha Mapinduzi ya Viwanda; na

(ii) Serikali ihakikishe kuwa bajeti inayoidhinishwa na Bunge kila mwaka inatolewa yote na kwa wakati.

**(b) Mazingira ya Biashara**

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu bado inahitaji uwekezaji zaidi wa ndani na nje. Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Iboreshe mazingira ya uwekezaji ili Sekta Binafsi iendelee kuwekeza kwenye ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza ajira, uongezaji wa thamani na mapato ya fedha za kigeni;

(ii) Iendelee kulinda viwanda vilivyopo nchini hasa vile ambavyo uzalishaji wake una mchango mkubwa kwenye ajira na kuokoa fedha za kigeni kama viwanda vya sukari; na

(iii) Ni vema maamuzi yoyote ambayo yanaweza kuwa na madhara ya kudhoofisha uwekezaji kwenye viwanda, yafanyiwe tathmini ya kina kabla ya kufanywa.

**(c) Mradi wa Liganga na Mchuchuma**

**Mheshimiwa Spika**, kutolewa kwa **Shilingi bilioni 15.38** kwa waliopisha Mradi wa Liganga na Mchuchuma mnamo mwezi Februari, 2024 ni hatua inayofanikisha tija ya Mradi wa Liganga

na Mchuchuma. Kamati inampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita, kwa hatua hiyo. Hata hivyo, Kamati hairidhishwi na hatua ya Mradi huu kuendelea kusuasua kwa muda mrefu. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikamilishe majadiliano na Mwekezaji ili kazi za uchimbaji wa chuma na makaa ianze haraka.

**(d) Upatikanaji wa Masoko kwa Bidhaa Zinazozalishwa Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, matangazo ni njia mojawapo inayohabarisha watu na kuongeza soko kwenye biashara. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini zinakosa soko kwa sababu ya kutotambuliwa na wananchi walio wengi kutokana na kutotangazwa; kwa mfano, bidhaa zinazozalishwa na *CAMARTEC, TEMDO, KMTC* na *SIDO* zinanunuliwa na wananchi/taasisi chache. Vilevile vipo viwanda vya watu binafsi vinavyozalisha bidhaa ambazo taasisi mbalimbali zingeweza kuzitumia badala ya kuagiza nje ya nchi. Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Ichukue hatua za makusudi kuhakikisha inatangaza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya hapa nchini ili wakulima na wafugaji wafahamu uwepo wa bidhaa hizo;

(ii) Itafute namna ya kuziunganisha taasisi za umma ili zifahamu bidhaa zinazotengenezwa na wenzao; kwa mfano, *TEMDO* wanatengeneza bidhaa ambazo zinaweza kutumiwa na Wizara ya Afya. Aidha, uwepo mkakati wa kuzitaka taasisi mbalimbali kutumia bidhaa zinazozalishwa hapa nchini badala ya kuagiza ili kuokoa fedha za kigeni; na

(iii) Wizara ya Kilimo ione namna inavyoweza kununua zana zinazozalishwa *TEMDO* na *CAMARTEC*.

**(i) Upungufu wa Mitaji Katika Viwanda/Taasisi za Uzalishaji**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi za Serikali za kufufua baadhi ya viwanda vilivyokuwa vimesimamisha uzalishaji kwa muda mrefu, bado viwanda hivyo vinakabiliwa na upungufu wa

mitaji, jambo linalopelekea kutochangia kikamilifu kwenye Pato la Taifa. Mfano, Kiwanda cha Kutengeneza Mashine na Vipuri (KMTC) kina uwezo wa kuzalisha **Shilingi Bilioni 10.2** kwa kipindi cha miaka mitano endapo Serikali itaipatia mtaji wa **Shilingi bilioni 3.46** zilizoombwa na kiwanda hiki. Kamati inashauri kuwa, Serikali ikipatie Kiwanda hiki mtaji huo ili kufikia malengo. Aidha, viwanda vingine viwekewe mazingira wezeshi ili kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

**(j) Changamoto ya Rumbesa**

**Mheshimiwa Spika**, wapo baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wameendelea kutumia mfumo wa rumbesa kuuza/kununua bidhaa hasa mazao ya wakulima kwa lengo la kuwanyonya na kuikosesha Serikali mapato. Kamati inashauri kuwa:-

(i) Serikali iendelee kutoa elimu kwa wananchi sehemu mbalimbali kuhusu faida ya kuuza kwa kutumia vipimo sahihi (mizani) na athari inayopatikana kwa kutumia rumbesa; na

(ii) Serikali itoe Mwongozo kuhusiana na suala la rumbesa ambalo ni suala mtambuka ili Halmashauri zote ziweze kusimamia kwa uwiano ambao utaleta manufaa kwa wakulima. Aidha, Wakurugenzi wa Halmashauri na Watendaji wengine wanaohusika, wahakikishe wakulima hawadhulumiwi wanapouza mazao yao.

**(k) Mfumo wa Stakabadhi za Ghala**

**Mheshimiwa Spika**, mfumo umeanza kuonesha mafanikio kwa kufanya vizuri kwenye mazao ambayo yameshaingizwa. Ili kuendelea kuboresha mfumo huu, Kamati inashauri kuwa, Serikali ifanye yafuatayo:-

(i) Ipanue wigo kwa kuongeza mazao ambayo bado hayajaingizwa kwenye mfumo;

(ii) Ihakikishe Vyama vya Msingi vinawalipa Wakulima fedha zao kwa wakati mara taratibu za mauzo zinapokamilika.

Hali hii itaondoa migogoro isiyo ya lazima baina ya Serikali na Wananchi;

(iii) Ihakikishe kuwa tozo za mazao ya Wakulima zinapunguzwa kwa kuwa baadhi zinasababisha kero. Marekebisho ya tozo yatawapa imani zaidi wakulima kwa Serikali yao na wengi watajitokeza kuuza bidhaa zao kwenye masoko halali badala ya kutumia mifumo isiyo rasmi ikiwemo kangomba;

(iv) Iendelee kutoa elimu ya uhamasishaji kwa wadau wa mfumo wa stakabadhi za ghala kuhusu kutumia mfumo rasmi kuuza na kununua bidhaa mbalimbali. Matumizi sahihi ya mfumo huo ndiyo suluhisho la kero wanazopitia wakulima kuhusiana na mifumo ya masoko yetu kwa ujumla wake; na

(v) Maghala yajengwe maeneo ambako mazao yanalimwa au uwekwe utaratibu mzuri wa kuyachukua kwa kusogeza vituo vya kuuza karibu na wakulima ili kuwapunguzia gharama ya kusafirisha.

**(I) Upatikanaji wa Umeme wa Uhakika Viwandani**

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu ni jambo muhimu katika uendeshaji wa viwanda. Wamiliki wa viwanda wanakabiliwa na changamoto kubwa ya kukosekana kwa umeme wa kutosha na wa uhakika, hali inayopelekea kutumia fedha nyingi kununua nishati ya mafuta kwa ajili ya kuendeshea jenereta. Kamati inashauri kuwa, Serikali iweke miundombinu ya umeme wa uhakika na wa bei nafuu katika maeneo yote ya viwanda.

**(j) Ukarabati na utanuzi wa masoko**

**Mheshimiwa Spika,** mandhari nzuri ya masoko ni kivutio cha biashara yoyote iwayo. Yapo baadhi ya masoko hapa nchini ambayo hayana mandhari nzuri kutokana na miundombinu yake kuwa ya muda mrefu na hivyo yamechakaa na kuwa kero hasa kipindi cha mvua. Kamati inashauri kuwa, Serikali itenge fedha kwa ajili ya ukarabati na utanuzi wa masoko ili yawe

katika hali nzuri. Kwa kufanya hivi mandhari itakuwa ya kuvutia, wateja wataongezeka, biashara itaimarika na mapato ya Serikali yataongezeka. Aidha, Wizara ya Viwanda ikishirikiana na TAMISEMI, iandae Mwongozo wa ujenzi na ukarabati wa masoko ndani ya Halmashauri, Manispaa na Majiji kwa mujibu wa mipango iliyowekwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na yawe katika maeneo rafiki na mwonekano mzuri.

**(k) Maeneo maalum kwa ajili ya wafanyabiashara ndogondogo (Machinga)**

**Mheshimiwa Spika,** Machinga ni kundi kubwa hapa nchini na ambalo bado linapata tabu ya kupata maeneo maalum kwa ajili ya kufanyia biashara zao. Wengi wao wanazunguka mitaani kutafuta wateja, hali inayochangia ukusanyaji wa kodi ya Serikali kuwa mgumu kwani baadhi yao hawalipi kodi kwa kuwa hawana maeneo maalum. Kamati inashauri kuwa, Serikali iendelee kuwatengea Machinga wote maeneo maalum ya kufanyia biashara na ambayo ni rafiki, ikiwemo kuweka miundombinu itakayosaidia kukusanya kodi kwa kutumia mifumo rahisi na ya kisasa.

**4.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kukushukuru na kukupongeza kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa weledi mkubwa. Vilevile, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Naibu Spika - Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb) na Wenyeviti wa Bunge, kwa weledi na umahiri wao katika kukusaidia kuongoza Vikao vya Bunge hili la Kumi na Mbili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kushiriki kikamilifu wakati wa kupitia, kuchambua na hatimaye kuwasilisha maoni kuhusu Bajeti ya Wizara hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Orodha yao ni kama inavyoonekana hapa chini na kwa ruhusa yako, naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard);*

1. Mhe. Deodatus Mwanyika, Mb, – Mwenyekiti
2. Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb, – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb, – Mjumbe
4. Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb, – Mjumbe
5. Mhe. Prof. Sospeter M. Muhongo, Mb, – Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb, – Mjumbe
7. Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb, – Mjumbe
8. Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb, – Mjumbe
9. Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb, – Mjumbe
10. Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb, – Mjumbe
11. Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb, – Mjumbe
12. Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb, – Mjumbe
13. Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb, – Mjumbe
14. Mhe. Francis Isaack Mtinga, Mb, – Mjumbe
15. Mhe. Lucy John Sabu, Mb, – Mjumbe
16. Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb, – Mjumbe
17. Mhe. Prof. Patrick Aloisi Ndakidemi, Mb, – Mjumbe
18. Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood, Mb, – Mjumbe
19. Mhe. Atupele Alfred Mwakibete, Mb, – Mjumbe
20. Mhe. Janejelly James Ntate, Mb, – Mjumbe
21. Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb, – Mjumbe
22. Mhe. Salim Hassan Turky Toufiq, Mb, – Mjumbe
23. Mhe. Pauline Phillip Gekul, Mb, – Mjumbe
24. Mhe. Mohamed Said Issa, Mb, – Mjumbe

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mb - Waziri wa Viwanda na Biashara, Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe, Mb - Naibu Waziri, Dkt. Hashil Twaibu Abdallah - Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Nenelwa Joyce Mwihambi, *ndc,* kwa kuratibu shughuli zote za Kamati na kuhakikisha inatekeleza majukumu iliyopangiwa kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya

**Wizara ya Viwanda na Biashara - Fungu 44** kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Mwanyika, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**
21 Mei, 2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mwenyekiti kwa kusoma vizuri. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii, kwanza wapo wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wageni wa Mheshimiwa Ashatu Kijaji, Waziri wa Viwanda na Biashara; yupo Dkt. Yamungu Kayandabila, Mwenyekiti wa Bodi (*NDC)* na Dkt. Aggrey Mlimka, Mwenyekiti wa Bodi *(FCC)*. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Ashatu Kijaji, Waziri wa Viwanda na Biashara, ni Viongozi na Watumishi wa Wizara, Wakuu na Watumishi wa Taasisi za Wizara, Wakuu na Watumishi wa Taasisi za Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo. Pia, wapo Wakuu na Watumishi wa Taasisi Nyingine za Umma, Wageni wa Kifamilia, Wadau wa Viwanda na Biashara, Ofisi ya Mbunge, Jimbo la Kondoa, viongozi wa CCM, Wenyeviti, Wenezi wa Kata, Wilaya ya Kondoa pamoja na Viongozi wa Kamati ya Siasa ya UVCCM Wilaya ya Kondoa na Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Tunao Viongozi wa Soko la Kariakoo, karibuni sana. Mameneja wa *SIDO* wa Mikoa, karibuni na Umoja wa Wajasiriamali Tanzania. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Venant Daud, ambaye ni Dada yake kutoka Igalula Mkoa wa Tabora. Wageni watatu wa Mheshimiwa Costantine Kanyasu. Hawa ni Makada wa CCM kutoka Mkoa wa Arusha na wengine ni wageni 55 wa

Mheshimiwa Angelina Malembeka, Mbunge, kutoka Taasisi ya Tanzania *One* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Zainab Katimba, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana *(TYPC),* anaomba kuwatangazia kuwa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania unapenda kutoa Taarifa kwa Wabunge wote vijana chini ya umri wa miaka 40 kwamba, kutakuwa na tukio la Uzinduzi wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2024/2029 pamoja na Katiba ya Umoja huo, litakayofanyika hivi leo katika Ukumbi wa Hoteli ya Rafiki iliyopo hapa Jijini Dodoma.

Tukio hilo muhimu litafanyika kuanzia Saa Saba Mchana hadi Saa Tisa Alasiri, litahudhuriwa na Mgeni Rasmi ambaye ni Naibu Spika wa Bunge, Mheshimiwa Zungu. Hivyo, anapenda kuwakaribisha wanachama wote wa umoja huu kufika bila kukosa katika tukio hilo la kihistoria. *(Makofi)*

Waheshimiwa, sasa tunaanza mjadala. Tunaanza na Mheshimiwa Prof. Sospeter Muhongo, atafuata Mheshimiwa Kirumbe, Mheshimiwa Charles Kimei na ajiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. *(Makofi)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Hii bajeti ya Viwanda na Biashara, Waheshimiwa Wabunge, naomba tuipitishe japokuwa ni ndogo. Kwa kuwa, ndiyo tunaendelea kujenga viwanda tuipitishe, lakini ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa maombi kutoka Mkoa wa Mara. Kuanzia miaka ya 60 mpaka 90 Mkoa wa Mara tulikuwa na viwanda, lakini kwa sasa hatuna kiwanda hata kimoja. Kwa hiyo, ombi namba moja ni kama tuko kwenye mapinduzi ya viwanda mahali pa kuweka viwanda ni Mkoa wa Mara. Kwani ni wakulima bingwa wa pamba, tunaomba *ginneries* zetu tatu zifanye kazi. Tunaomba kiwanda kipya cha nguo, hakuna masuala ya kufufua *MUTEX*. *Machines* za *MUTEX* ni za zamani sana, hazina hata vipuri duniani hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi ni wavuvi mashuhuri. Kwa sasa hivi hatuna kiwanda hata kimoja cha samaki, kilichopo kinafanya kazi chini ya 15% kwa hiyo, tunaomba angalau viwanda vitatu vya samaki. Sisi ni wafugaji bingwa, tulikuwa na viwanda viwili vya maziwa, lakini sasa havipo. Kwa hiyo, Mkoa wa Mara tunaomba viwanda vipya vya maziwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarime tunalima Kahawa. Tunaomba vile viwanda vya Kahawa vipewe fursa ya kupanuka zaidi. Haya ninayaomba najua siyo ya Wizara ya Viwanda, lakini tunaomba Wizara ya Viwanda ishirikiane na Wizara nyingine, angalau Mkoa wa mara turudi kuwa na viwanda visivyopungua 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa baada ya hilo la jimboni na Mkoani kwangu, mimi leo naomba niongelee Liganga na Mchuchuma. Nadhani nipo kwenye nafasi nzuri kuliongelea hilo na unajua hiki kitu ni nyeti, kwa hiyo, nikifika mwisho huko uongeze muda tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwamba ile Liganga na Mchuchuma niwarejeshe nyuma; imekuwepo enzi ya utawala wa Mjerumani na Muingereza. Kazi muhimu zilizofanyika mwaka 1928 mpaka 1948 tukiwa na *Geological Survey Department* ya Muingereza ndio walienda huko Liganga wakafanya *mapping.* Ripoti zao zipo kwenye *archives* za *Geological Survey* ya Uingereza, Nottingham.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwaka 1952 Kampuni ya Canada ilifanya *airborne survey magnetic*. Mwaka 1956 mpaka 1957 kampuni kubwa za Australia, Reo Tinto na *BHP,* ambazo bado ndiyo kampuni kubwa kweli kweli duniani za kuchimba chuma, zilienda Liganga. Tunavyoongea sasa hivi ni lazima tuisaidie hii Wizara, huu mgodi una historia ndefu sana, msije mkawahukumu hawa labda hawahusiki, ni sisi wote, tuache ya nyuma tusonge mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunaanza 2011 wakati *NDC* ilipoingia ubia na kampuni ya Wachina. Sasa Liganga yenyewe na watakaoenda kufanya majadiliano na uwekezaji wa

Liganga. Liganga kitaalam ni kwamba, kuna madini zaidi ya hicho chuma, lakini kwa wepesi utakuwa unaongelea chuma cha Liganga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kitaalamu tunasema ni *polymetallic,* yaani una *metals* zaidi ya moja; kuna chuma, kuna *titanium,* kuna *vanadium*, kuna *chromium,* halafu madogo kama *aluminium* pia, yapo. Kwa hiyo, unavyoenda Liganga usijadili chuma tu, wakati inagundulika watu walikuwa hawapendi *vanadium* na *titanium,* ilikuwa haitumiki duniani. Kwa hiyo, watu walisema sisi tuna chuma Liganga, lakini tatizo kinachafuliwa na *titanium* na *vanadium.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi *titanium* na *vanadium* ndiyo madini ambayo ni muhimu zaidi kuliko hicho chuma. Kwa hiyo, *deposit* yetu sijui mashapo, Kiswahili ni nini? Watu wa Kiswahili, *deposit?*

Mheshimiwa Naibu Spika, *deposit* yetu ya Liganga mpaka sasa hivi inajulikana tuna tani milioni 129. Sasa, Mchuchuma kwenye makaa ya mawe *deposit* yetu ni tani milioni 422. Makaa ya Mchuchuma *(coal)* yanavuka viwango vyote vya kuzalisha umeme kwa sababu, ya kwetu ni ya katikati yanaitwa *bituminous coal.* Ni ya hapo katikati, haiko chini haipo juu sana, lakini vigezo vitatu vya *ash content, carbon content* na *calorific value,* vyote Mchumchuma anafaulu hapo, kwa hiyo, tunaweza kuzalisha umeme Mchuchuma. Sasa tukitaka kuongelea Liganga na Mchuchuma ni lazima tuangalie hali ya chuma duniani ipoje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *reserve* kubwa ya chuma duniani ipo Australia wana tani bilioni 51, Brazil ni ya pili ina tani bilioni 34 na huyu Mchina ambaye ndio *partner* wetu sasa hivi yeye ana *reserve* ya tani bilioni 20. Sisi ya Mchuchuma mpaka sasa hivi tuna tani milioni 129, huenda tukiendelea, labda tunayo nyingi. Sasa duniani *demand* ya chuma ni kiasi gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2023 biashara ya chuma ilikuwa kwenye *around 1.6 billion tones* na *market* yake ilikuwa ni dola bilioni 350. Wazalishaji wakubwa wa chuma, hawa ni lazima

tuwaangalie, ndiyo tunashindana na Liganga. Kuna wakubwa watano ambao wanazalisha 80% ya chuma chote duniani, hawa ni Australia, Brazil, China, India na Russia. Mtumiaji mkubwa ni huyu huyu *partner* wetu, China, ndiyo anatumia chuma kingi kuliko wote duniani. Mwaka 2023 ametumia chuma chenye thamani ya dola milioni 134.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimewaambia kuna madini zaidi ya chuma, kuna *titanium.* Watanzania tukienda kujadili na wenzetu wa China tusiongee tu chuma *(iron ore),* tuongee na *titanium. Titanium* ndio inatumika kwenye *engine* zote za ndege mnazoziona, ni kitu muhimu kweli kweli. Hata wale wanaocheza gofu vile vichuma vyote ni *titanium,* ina matumizi makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa duniani *titanium* inazalishwa, wakubwa ni wawili tu, Australia na *South Africa,* biashara hiyo ipo kwenye tani milioni sita. China, ambaye ni *partner* wetu, yeye ndio ana 30% ya *reserve* kubwa ya *titanium* duniani. Pia, msisahau kuwa tutaweza kupata *titanium,* Kenya wanasafirisha *titanium.* Kama unaenda Mombasa, pale *beach* ni sawa sawa na sisi tulivyotoa leseni kule Tanga, nadhani na wao watatoa *titanium.*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa *vanadium* yenyewe tunayo ambayo *demand* yake duniani. Kufikia mwaka 2030 itahitajika ya bilioni nne. Sasa nimalizie kwa *NDC* na China ambapo tunaanza kujadili *NDC* wana 20%. Kampuni ya China, *partner* wetu ina 80%, lakini kwenye migodi yote ya chuma duniani China kwenye *provinces* zake tano ana migodi 114.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu China na huyu mwenye kampuni ambaye wanashirikiana sasa hivi na *NDC* na kuna mwingine anayekuja anatoka *province* ya *Sichuan*. *Sichuan* ni moja katika *province* tano za China zenye migodi mikubwa. Mgodi mmoja wa *Sichuan* wa huyo ambapo tuna mbia wetu, anazalisha tani milioni 6.3. Kwa hiyo, *joint venture* yetu na hii ya *Sichuan* inasema itazalisha chuma tani milioni 2.9 ambayo wakii-*process* watatoa tani milioni moja kwa ajili ya *steel* na wanataka kuchimba makaa ya mawe tani milioni tatu kwa mwaka na kwa kuwa tuna tani milioni 428, hiyo chuma inatosha kwa zaidi ya miaka mia moja na kitu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pendekezo langu naishauri Serikali iongeze kasi na hii kampuni ambayo sasa hivi tunayo ubia lakini imetafuta mbia mwingine *Sichuan*. Huyu mbia mwingine ni wa Serikali ya *Province* ya *Sichuan*.

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, Wachina ni wakubwa sana kiuchumi. Hili jimbo peke yake tunaloshirikiana nalo, *GDP* yake ni ya bilioni 800, sasa ukichukua *GDP* ya *South Africa* ambayo ndiyo kubwa ya bilioni 380 inaingia zaidi ya mara tatu mara nne. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ili Tanzania tufanikiwe na naomba hili siyo la Waziri lakini la nchi, ni lazima tuwe na wataalamu. Sasa hivi wataalamu wa makaa ya mawe *(coal experts)* ni wachache mno hawavuki watatu wanne; halafu *metallurgist* (wanaoshughulika sasa na hizo *metals* tunazozisema) ninadhani nchini hawavuki wawili. Kama wapo, mimi siwafahamu lakini wengi walikuwa wanafunzi wangu ningewafahamu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Profesa kengele ya pili hiyo.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, haya namalizia. Ni kwamba ninaomba Serikali ya Tanzania ishawishi Serikali ya *China* iweze kushawishi hizo kampuni ambazo zina ubia na *NDC* waongeze kasi ya uwekezaji, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Profesa. Mimi nilifikiri unasema tuongeze na idadi ya *share* zetu! Namwita Mheshimiwa Kilumbe, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kimei na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia afya na uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kuanza mchango wangu kwa kuweka falsafa ambayo nafikiri inaweza ikatusaidia sana katika kuona ni nini mwelekeo wa kibiashara. Duniani nchi zote zinapimwa na kuwa na nguvu, kwanza kabisa kwa uchumi. Uchumi una mambo ambayo yanasababisha huo uchumi uwe katika nguvu na uhakika ambao unahitajika kwa mazingira ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha nchi ambazo zimejaliwa na Mungu kuwa na maliasili zinazowafanya wawe na nguvu za kiuchumi kama mafuta, gesi, dhahabu, almasi na nyingine, njia nyingine ambayo imezifanya nchi duniani kuwa na uchumi mzuri ni kuelimisha watu wake na kuwa na *technology*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukiangalia nchi kama Japani na nchi nyingine zote ambao ni ma-*giant* katika masuala ya viwanda, wanatengeneza magari, wanatengeneza ndege wanatengeneza nini, nao wamekuwa na hali nzuri sana kiuchumi kwa sababu wamewekeza katika elimu na maarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukikosa maeneo yote hayo mawili au ukiwa unapata kidogokidogo katika hayo maeneo mawili, eneo la maliasili una maliasili lakini ambazo siyo muhimu zinazohitajika sana duniani au kama unazo ni kwa kiwango kidogo, una elimu au *technology* kwa kiwango kidogo, eneo lingine linaloweza kukuokoa ni biashara. Biashara kwa maana ya kufika mahali kuchukua vitu kutoka kwa wazalishaji kupeleka kwa wahitaji na kutengeneza faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimeamua niseme haya kwa sababu Wizara hii ya Biashara bado bado ina kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba jambo hili la kuhakikisha Taifa letu linaziba mianya ambayo tunaikosa katika maliasili, tunaikosa katika elimu na maarifa, tuweze kupata kupitia biashara, bado hatujakaa vizuri sana. Ukishakosa hayo yote duniani, kinachofuata wewe ni kuwa nguvukazi tu, mpagazi wa wengine duniani, ukishakosa yote hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Mungu katujalia maliasili tunayo kiasi, elimu na maarifa tunayo ingawa siyo ya kujivunia sana

maana mpaka sasa hatujaweza hata kutengeneza *fork lifts* za kubeba mizigo yetu bandarini, ila tunaweza kutengeneza mashine za kufyatua tofali. Sasa, hatuwezi kujisifia katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa jambo pekee linaloweza kutusaidia kutuongezea hizi nguvu ni biashara. Kwa nini ninasema biashara? Kwa sababu biashara ina vigezo na mihimili yake. Ukishakuwa na bandari, ukishakuwa na barabara, ukishakuwa na reli, halafu huko vinakoelekea yaani majirani zako wana mahitaji ya vitu vinapita kwako, unaweza kufanya biashara vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa ukienda katika takwimu zilizotolewa, nilizitoa hapa na nitarudia kuzitoa; takwimu zilizotolea na Baraza la Biashara la Afrika Mashariki katika mwaka 2019 – 2021, nchi jirani yetu *(DRC Congo)* ambayo 80% - 85% ya mahitaji yake ya bidhaa mbalimbali wana-*import* kutoka nje, China ndiyo Taifa la kwanza linalofanya biashara kubwa na *Congo*. Linalofuata ni *South Africa*; nchi ya tatu inayofuata ni Zambia, ya nne Kenya, ya tano Rwanda, sisi Tanzania ambao tuna mpaka na *DRC Congo* ni wa saba. Hatujawa *serious*, tumeshindwa kufanya biashara pamoja na bandari tuliyonayo na miundombinu na ujirani tulionao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapofika mahali tukasema dada yangu Mheshimiwa Ashatu na Naibu wako mmekabidhiwa kazi ya kuleta msisimko wa kibiashara ili uchangie katika pato la Taifa, lazima mwende mbele zaidi kujiongeza kuangalia fursa zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii sasa imefika mahali sisi badala ya kuwapelekea *Congo*, sasa *Congo* wameanza kutuletea bidhaa. Kuna Wachina wameanzisha kiwanda cha saruji kinaitwa *Great Lakes Cement*, kule Kabimba *DRC* ambao sasa wameanza kuingiza *cement* pale Kigoma inaitwa *GLC*.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kumwongezea Mheshimiwa Kilumbe kwamba, pamoja na kuwa na bandari zaidi ya saba kwenye Ziwa Tanganyika lakini bado hatuwezi kuifikia *Congo* moja kwa moja. Wizara ya Uchukuzi pia wana jambo la kufanya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa kwa mikono miwili.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Taarifa. *(Makofi)*

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuingilia mchango mzuri anaotoa Mheshimiwa Mbunge ambaye ninakubaliana naye, ni kwamba lile neno alilosema kwamba hatuko *serious*, nataka nimhakikishie kwamba Serikali hii iko *serious*. Tunajenga reli tuifikie *Congo*, tunajenga bandari tuifikie *Congo*, tunajenga meli za kutosha tuifikie *Congo*. *(Makofi)*

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina hakika kama ile taarifa nilikuwa napewa mimi. Nafikiri taarifa alikuwa anapewa mtoa taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Ni wewe.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Alikuwa ananipa mimi?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Ah, basi tutajadiliana, nafikiri tuna jambo la kujadiliana. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe, endelea na mchango wako.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninachokusudia kusema ni kwamba tunatakiwa sisi kama Taifa tuangalie *opportunity* na kuzitumia kwa wakati. Sasa hivi inaelekea sasa kama tunaanza kuchelewa na hilo soko la Ukanda wa Ziwa Tanganyika kwa sababu mataifa makubwa yanakwenda kuwekeza huko. Hata pale ambapo sisi wenyewe tunaweka mipango kama aliyoisema sasa hivi Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye taarifa yake, suala ni kwamba tuna mipango mingi, utekelezaji na wakati ndiyo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano pale Kigoma kuna eneo sasa hivi lina zaidi ya miaka saba, linaitwa *Kigoma Special Economic Zone*. Yaani unaamua kuwa na *special economic zone*, unatenga ardhi unaacha ina miti, ina magugu, haina barabara, haina maji, haina umeme, unasema hili eneo la uwekezaji. Uwekezaji wa nini? Kufuga ng'ombe! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndiyo inaonekana kwamba hatuko *serious*. Unasema hili eneo ni la uwekezaji, basi eneo hilo la uwekezaji lazima uliwekee miundombinu. Ninyi mmekwenda mpaka Dubai huko kuona maeneo ya uwekezaji, ukifika pale kama ni kiwanda unaweka mitambo yako unafunga unaanza kazi. Yaani mwekezaji aanze kuja kutoa magugu na kung'oa miti na kutengeneza barabara? Kwa hiyo, niseme kwamba lazima tuongeze kasi katika maeneo haya. Tusipoongeza kasi kwa kweli mambo yataendelea kuwa siyo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu, mchango wa vyombo vyetu vya fedha katika kusisimua biashara nchini bado ni mdogo sana na ndiyo maana wawekezaji wengi wakubwa wanapofika mahali wakataka kuwekeza nchini, lazima waende kwenye vyombo vya fedha vya nje ili viweze kuwasaidia katika uwekezaji wao. Vinginevyo ikifika mahali wakaamua kutumia benki zetu, riba zetu siyo rafiki. Bado tuna benki haziheshimu tafiti, tuna benki haziheshimu *idea*, benki zinaheshimu *collateral* (mali ambayo inaonekana). Yaani huwezi kwenda na andiko na *idea* ukapewa

fedha. Wanakuuliza una nyumba? Una nini? Mambo ya kizamani kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mawazo kama ya Mheshimiwa Prof. Muhongo yale yanazidi nyumba, yanazidi ardhi. Unawekeza kwenye wazo, ilimradi umeita wataalamu wako wamekaa wameona wazo hili litaitoa nchi, litaleta ajira kwa watu, unatoa fedha. Benki zetu bado unafika mahali unakwenda na mradi mkubwa wanakuuliza ehe, sasa dhamana! Yaani wazo hili halitoshi kuwa dhamana? Lazima tubadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie kwa kuomba Serikali iliangalie sana sana eneo la Kigoma. Siyo kwa sababu ni mkoa ninaotoka mimi au kuna jimbo ninalotoka mimi. Iliangalie eneo la Kigoma kama eneo ambalo linaweza likatumika kama *hub* ya kibiashara baina yetu na nchi za *Congo*, Burundi na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia, na Mheshimiwa Dkt. Ishengoma jiandae. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na uongozi mzima wa Wizara kwa yote yale ambayo wametekeleza katika mwaka huu. Ninaamini kwamba wataendelea kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana kwa kusema kwamba anakutana na wafanyabiashara binafsi na kujaribu kutatua kero zao. Mimi ningeomba kwamba akutane na wazalishaji binafsi wazawa waliozaliwa hapa Tanzania, weupe au weusi. Azungumze nao ajue kero zao ili aweze kujenga mazingira wezeshi kwa uwekezaji katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimekutana na wachache. Juzi nilipokuwa Arusha nimekutana na wachache na wanasema,

kusema kweli Mtanzania mzawa kuanza biashara au uzalishaji wowote hapa inakuwa shida sana. Akiingia kwenye ofisi yoyote ya mamlaka au taasisi ya Serikali, wanamwangalia kama vile huyu mtu amekuja kuomba pesa. Kumbe amekuja kujaribu kupata leseni au kufanya malipo ili aweze kuendeleza biashara yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wanalalamika wanasema kwamba kwa mfano, Mheshimiwa Rais aliweka ukomo wa *TRA* kwa mfano kukagua au kutathmini hesabu za kampuni ili kuona kama vile walilipa kodi yao sawasawa lakini inakuwa ule ukomo waliouweka wa miaka mitatu, watu wanaingiza mbinu ya tathmini *(Investigative Audit)* ya *tax*. Kwa hiyo, unaweza ukakuta hata miaka 20 ule ukomo haufanyi kazi, halafu ule ukomo wenyewe haujawekwa kwenye Waraka ambao unakuwa unatekelezeka kwa watu wa *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tungeomba kwamba Waziri wa Viwanda na Biashara ambaye kazi yake na jukumu lake kubwa ni kuweka mazingira wezeshi, aone basi kwamba kila agizo lililotolewa na mamlaka au kila kilicho kwenye sheria kinatekelezeka kwa maslahi ya wawekezaji ili watu waweze kuwekeza kwa amani na wakijua kwamba hawatafuatiliwa ovyo ovyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, kuna tatizo hilo hilo linaweza likaendeleza mambo ya *TRA* kukagua akaunti za watu kwenye benki. Wanatuma *Agency Notices* kwamba huyu mtu hajalipa kodi kwa hiyo kama atapata malipo yoyote kwenye akaunti yake hayo malipo yaende moja kwa moja *TRA*. Haya mambo ni yale ambayo yalikuwa yameisha na mnaamini katika agizo la Mheshimiwa Rais kwamba wasibugudhi wafanyabiashara na wazalishaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ni hilo kwamba, siyo kutoa *Agency Notices* ambazo zinawapa watu shida sana katika kufuatilia na pia kutokuwa na amani katika uzalishaji wao. Ninaamini kwenye hilo Mheshimiwa Waziri atazungumza na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ili waweze kutatua. Kuna tatizo ulisema kwamba kuna kero 300 zimetolewa, wanatangaza hapa

Bungeni, lakini hata mimi ukiniambia hizo kero zilizoondolewa ni shida sana kuziona zimekuwa *published* kwenye gazeti ili wale ambao wanafaidika na kero zile waweze kutumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba kero zilizotolewa na amesema nyingine zimetolewa pia kwa wafanyabiashara wa Kariakoo, basi hizo nazo wajaribu kuziweka bayana ili watu waweze kuzitumia kero hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nichangie zaidi kwenye suala zima la mkakati wa viwanda. Mimi sasa hivi nasema kwamba mkakati huu tunaofuata wa viwanda vikubwa kwenda kuomba viwanda vikubwa wanakuja kuweka *assembly plans* hapa hatutatusaidia sana. Mkakati utakaotusaidia ni kuhakikisha kwamba tunaenda kwa viwanda vidogo vidogo hata kwenye majumba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi pale Mikocheni ukienda kwenye nyumba nyingi walizopangisha wageni fulani fulani hapa, wageni wa Taifa fulani fulani, wamekuja kuweka viwanda vidogo vidogo huko ndani wanatengeneza yebo yebo, wanatengeneza kila kitu. Halafu wanapeleka sokoni hawalipi kodi kwa sababu hivyo viwanda havijasajiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naona kwamba wanaharibu biashara za wengine kwa sababu wameweza kuweka viwanda vidogo vidogo. Vimashine vidogo vidogo wanatengeneza chipsi za ndizi, kila kitu wanatengeneza. Halafu tunasema tunakimbizana na viwanda vikubwa wakati tuna kilimo chetu. Kila kaya au kila kata inaweza ikachakata mazao yake kwa kuwa na viwanda vidogo tu na bei rahisi ambazo tunaweza tukaagiza kutoka nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala zima la kusema kwamba *SIDO* kama *TXP* wanatengeneza mashine, uongo huo. Ni kiwanda kipi kinatengeneza mashine (injini) hapa Tanzania? Mashine ni injini, siyo kudanganyadanganya hapa. Unapoteza hela nyingi kuvumbua kitu ambacho tayari kipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda utanunua mashine kwa bei nafuu, zile mashine utazi-*deploy* kwa kila mtu kwa bei nafuu kabisa. Kwa hiyo, hiyo hela ambayo tutatoa ruzuku kwa mashirika haya tunaweza tukawapa kata, kama ni ndizi wakafanya, kama ni viazi au nini, wakachakata. Ina maana wanaongeza thamani halafu pia wanaweka uwezo wa kuhifadhi yale mazao. Kwa hiyo, tukienda hivi tutakwenda haraka. Hatuwezi kufanya tu, yaani *leapfrogging* maana yake ni ku-*imitate*. Una *leapfrogging* kwa ku-*imitate* na kuorodhesha ile *imitation* uliyofanya ili uweze kupata tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi naomba *SIDO* wajiangalie na wajitathmini, liwe ni shirika la kubuni, la kuwezesha kuchukua *technology* nje kui-*customize* ili iweze ku-*fit scale* ya *production* kwenye maeneo yetu na tuanze mara moja kusambaza na kuuza, tunauza *cheap*. Unawapa kwa mkopo wataongeza thamani watapata fedha nzuri zaidi watalipa mkopo ule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii *TIB* nilikuwa ninasema igeuzwe kuwa ni benki ya *starter* ili watu waweze kupata mikopo kwa urahisi. Kwa hiyo, mimi naona hiyo itakuwa ni njia mojawapo ya kuongeza kasi ya kujenga uchumi wa viwanda katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka tulikuwa tunapewa idadi ya viwanda ambavyo vimeanzishwa ile idadi siku hizi hatupewi tena. Sijui ni kwamba imeisha, siku hizi viwanda havifunguliwi na siku zote tunasema kwamba kila wilaya iwe na *specialization*. Huo ni mkakati, huu mkakati umefia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba huo mkakati ufuatiliwe tena ili kwa mantiki hiyo kwamba kila mahali kwenye zao, tuwape watu nyenzo hizo za kuanza viwanda na kuchakata na kuongeza thamani ya hayo mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kwamba huko tunapoenda n`i kuzuri na ukiangalia vipaumbele vya mwaka unaokuja vilivyowekwa na Wizara, vipo vizuri vimekaa bayana

lakini naomba basi hiyo kasi ya kutekeleza kwa kushirikiana na kuhakikisha kwamba *local content* inakuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukiangalia hesabu zote tulizoambiwa hapa za *exports* za mazao na bidhaa za viwanda hatungeweza kuona uhaba wa dola hapa nchini, lakini ubaya hamwoni kwamba siyo sisi, wanatoa bidhaa kwenye *export processing zone* wanapeleka nje, pesa inaenda kwenye nchi, kwenye mataifa yale ambayo wale wawekezaji wapo, haiji Tanzania. Kwa hiyo, siyo hela yetu ile, hatutozi kodi, hatufanyi nini licha ya wafanyakazi wetu kufanyishwa kazi na kwenye mazingira magumu sana, lakini ukweli ni kwamba inapokuja ni *export* tunashangilia, tume-*export,* lakini hela hiyo ya kigeni iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukifanya sisi hii kuongeza thamani ya bidhaa zetu za kilimo, tukianzia kile tulichonacho halafu tukapeleka nje, nakwambia thamani ya *export* zetu itakuwa kubwa na zitakuwa *earned* na watu wetu hapa na ni lazima kweli kubali kwamba lazima tulinde na tujali masilahi ya wazawa. Wazawa, mimi sisemi wazawa ni weusi na weupe ambao wamekaa wanazaliwa hapa tuwatetee. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sophia, jiandae Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru nami kupata nafasi tena ya kuchangia Wizara hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi wewe ni msimamizi wa sera, lakini kwenye maamuzi au utekelezaji inakuwia vigumu sana. Nasema hivyo kwa sababu viwanda kuna wakati mwingine vinakwenda kwenye kilimo, leo hii ninapotaka kuzungumzia kiwanda cha chai kilichopo katika Wilaya ya Rungwe

kilichofungwa bila kufuata utaratibu na kutokulipa wafanyakazi mafao yao, nikikulaumu wewe Waziri wa Kilimo nae anakisimamia kiwanda hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sijafahamu tunafanyaje kama Taifa ili tunapokulaumu wewe mwenye kiwanda ujue namna gani utatusaidia. Mheshimiwa Waziri kuna shida hata ya viwanda ambavyo umevionesha katika hotuba yako kwamba kuna viwanda 70, viwanda 100, au 2,000 vimeanzishwa lakini usimamizi wake, wawekezaji wale jinsi ya kuwalipa wafanyakazi mafao yao, masaa yao ya kazi na haki zao, mwisho wa siku tukija kwako tunakwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba sasa Serikali isomane, Serikali iwe na nia moja, mwekezaji na wewe wa viwanda muwe mnafanya vitu kwa pamoja kuwasaidia Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii Mheshimiwa Waziri wewe unasimamia wafanyabiashara, lakini TAMISEMI ndiyo inaweka miundombinu ya wafanyabiashara, sasa wasipoweka sawasawa Mheshimiwa Waziri tunarudi pale pale kupiga kelele zisizotekelezeka. Tunaomba Serikali msomane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii wawekezaji hawa ambao sisi tunawahitaji, kwa sababu kama Taifa tupo *win win*, tunataka ajira ipatikane, tunataka watu wetu wapate kipato, tunataka watu wetu wapate fedha na vitu kama hivyo pamoja na kodi, lakini wawekezaji hawa vijana wetu wanapokwenda kufanya kazi kwenye hivyo viwanda ambavyo mmevitoa kwenye ripoti, kijana anaanza kazi saa moja na nusu asubuhi mpaka saa kumi na mbili analipwa chini ya shilingi 5,000/=. Mheshimiwa Waziri hiyo ni ajira au ni mateso? Vitu kama hivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri tunaamini viwanda vikubwa, uwekezaji mkubwa unaangukia kwa Mheshimiwa Kitila, yeye kama mtu wa uwekezaji. Zamani ilikuwa pamoja labda ilikuwa inawasaidia kufanya kwa pamoja lakini nimesema kwa sababu Serikali inasomana na ni Serikali moja, basi mtafute namna ambayo matatizo haya tunaweza tukayatatua kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado natoa angalizo la kuangalia wawekezaji na hasa kwenye mafao lakini hatuishii hapo Mheshimiwa, tunafikiri kwamba uwekezaji kama tulivyosema ni faida, basi wale wanaowekeza ni lazima wafuate masharti na kama kiwanda kinaonekana kinafungwa, basi watoe taarifa mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano kwenye masuala ya kilimo, leo hii umefunga Kiwanda cha Chai cha Katumba au umefunga kiwanda cha Chai cha Moo kilichopo pale Rungwe lakini umeacha watu wana chai zao mashambani, umeacha watu vijana ambao ulikuwa umewaajiri bila kuwapa mafao yao au hata kifuta jasho, Mheshimiwa Waziri kama kiongozi na Waziri wa Wizara hii tunaomba sana ulisimamie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja kwenye suala la *SIDO*, Mheshimiwa Kimei ametoka kueleza hapa, sisi Mbeya tunayo *SIDO* na tunao uwanja mkubwa sana wa *SIDO* ambao wafanyabiashara wamepewa kuuza pale. Ninaamini lengo la *SIDO* sote tunalifahamu, siyo vibanda vya biashara, *SIDO* ni viwanda vidogo vidogo. Leo hii ndugu zetu, wale wanakodisha maeneo, mtu akija na wazo lake la kibiashara tayari lile eneo limeshakodishwa na yule anayelikodisha anaenda kulipa kodi kwa *SIDO*. Hivi *SIDO* huwezi kwenda wewe mwenyewe ukachukue ile fedha badala ya mtu hapo katikati? Naomba ulifuatilie hilo Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru Mungu Waziri ameleta viongozi wake wa *SIDO* wa Mikoa wapo hapa, tunaomba sana *SIDO* ifanye kazi ya viwanda vidogo vidogo, ndiyo hasa jukumu la *SIDO*. *SIDO* pia ipo kwa ajili ya kusaidia wananchi na hasa hasa wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii *SIDO* imebahatika kuwa katika Wilaya na Mikoa lakini gharama kubwa sana kwenye vifungashio, kuna wamama wanaojifunza batiki, wananunua dawa kwao, wananunua vifungashio, vimekuwa vina gharama kubwa. Wamekuwa wakitoa semina, nakubali na zinasaidia lakini mwisho wa siku mama mdogo kabisa yule wa chini uwezo huo hana na lengo la Serikali ni kumsaidia mtu wa kawaida kabisa

kwamba ainuke atoke pale alipo na kusogea. Naamini kabisa tukiendelea kwa wazo la kwanza la *SIDO* tutakuwa tumefanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado linarudi Mheshimiwa Waziri kuhusu mavazi na vitendea kazi kwenye viwanda. Kuna buti, kuna vilinda kichwa kwa mfano kofia ngumu, sehemu nyingine watu hawafanyi, wanafanya kazi hatarishi kwenye hivyo viwanda na hivyo vitu hawapewi. Wenzetu wa *OSHA* wanasimama na wanaenda lakini kwa kuwa wanakuwa wametoa taarifa, basi kuna vifaa vimewekwa kwa ajili ya *show off* tu na siyo kwamba hawa watu wanavaa kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wanafanya kazi kwenye mazingira hatarishi sana na kuwafanya kuhatarisha maisha yao ya kila siku. Tunafahamu kuna viwanda ambavyo vinatumia kemikali, wasipokuwa na vitu vya kujikinga hatuwatendei haki Watanzania hawa. Mheshimiwa Waziri, mimi ninaamini kazi yako siyo mbaya, inaendelea vizuri lakini mwisho wa siku nasisitiza kufanya kazi kwa kusomana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu stakabadhi ghalani, kwa mara ya kwanza sisi watu wa Kyela imetusaidia kwenye zao la Cocoa. Safari hii kidogo wakulima wameridhika kutokana na utaratibu mliouleta, lakini bado uboreshaji unatakiwa. Siyo tu kwa Cocoa, tunayo mazao mengine ikiwezekana yaweze kutambulishwa huko. Tunaomba sana wakulima wapate haki yao kwa haraka na *speed* iongezeke pamoja na kuwasifia, lakini mwisho wa siku tunataka kazi hii iweze kufanyika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya Mheshimiwa Waziri nasisitiza wawekezaji lazima waangaliwe. Najua *BRELA* ipo chini yako, na jana nimezungumza habari ya *BRELA* wanafanya kazi vizuri, wamepunguza ile foleni ambayo ilikuwepo zamani kwa kutumia mtandao, lakini *staff* wao pia wanafanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bado najua wawekezaji wanaochukua Watanzania, kwa maana ya kuchukua majina yao ili wasajiliwe, basi mwendelee kuwafuatilia, ikiwezekana

mwongeze kijisheria hapo, kama Mtanzania ni mwekezaji, basi kila baada ya miaka mitatu, minne warudi Mezani na kuona je, mahusiano yao ya kwanza yanaendelea au yule mtu alichukuliwa kama bosheni ili leseni ipatikane!

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja kwa mara ya kwanza katika Wizara hii, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Dkt. Ishengoma, jiandae Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya. Mkoa wangu wa Morogoro ulikuwa ni Mkoa wa viwanda kwa miaka mingi ya nyuma lakini baadaye viwanda vimekufa, kuna viwanda baadhi ambavyo vinafanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujua mpango wa kuvifufua viwanda vya Mkoa wa Morogoro ambavyo mpaka sasa hivi havifanyi kazi, hivi viwanda vilikuwa vinaleta ajira kwa vijana pia na wanawake ambao vijana hawana ajira mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwa kusisitiza kuhusu Liganga na Mchuchuma. Liganga na Mchuchuma ni miradi ambayo ni ya muda mrefu. Ni miaka mingi ambayo miradi hii ya Liganga na Mchuchuma imeanza. Mheshimiwa Waziri, umeongea vizuri, hotuba yako ni nzuri sana kuhusu mipango ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana na ninasisitiza kuwa mipango aliyoitoa kwenye hotuba yake iweze kutekelezeka, mazungumzo anayoongea pamoja na mwekezaji yaweze kufikia mwisho ili kusudi watu wanaoishi Ludewa, na Watanzania wote waweze kufaidika na Liganga na Mchuchuma. Mkaa uendelee kuchimbwa hasa kuhusu chuma ambacho tunakihitaji sana hapa nchini kwenye miradi mingi ambayo tunaiendeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa hivi tunapoteza fedha nyingi, tunatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza chuma kutoka nje na huku tuna chuma chetu ambacho Liganga ingekuwa imemalizika tungeweza kutumia chuma chetu hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee kuhusu kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji. Tukiweka mazingira mazuri kwa wawekezaji, wataweza kujenga viwanda vingi vya kila aina. Kwa mfano, kwa kutumia malighafi yetu tunayotumia, kwa upande wa Kilimo tunazalisha sana pamba, tunazalisha mafuta, viwanda vya mbolea, tungeliweza kutumia malighafi yetu ya hapa nchini kwa kuweza kuwawekea sekta binafsi, mazingira mazuri kusudi waweze kuwekeza hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kupata viwanda vingi vikiwemo vya mbolea, Watanzania wengi waliopo hapa nchini ni wakulima wataweza kupata mbolea ya kutosha ambapo sasa hivi inasemekana bado tuna viwanda viwili tu, lakini Mheshimiwa Waziri, kwa upande wako kwenye viwanda tunaweza tukaongeza viwanda vingine vya mbolea kusudi tuweze kupata kilimo cha kisasa pamoja na mapinduzi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumebahatika, Tanzania tunafanya vitu vingi. Kamati imetembelea viwanda mbalimbali ikiwemo kiwanda cha *CAMARTEC, TEMDO* pamoja na Tafiti ya *TIRDO* pamoja na *KMTC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nakuomba kama hujafika, ufike na wewe. Wanafanya vitu vizuri sana, wanazalisha vitu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kama Waheshimiwa Wabunge ambao tunavyosema kuwa Serikali isomane, unaweza ukatumia vitu vyetu tunavyozalisha hapa hapa bila ya kuagiza nje. Kwa mfano, ukienda *CAMARTEC* wanatengeneza matrekta ambayo ni ya bei nafuu kuliko kuagiza matrekta ya nje. Watanzania nimeshasema kuwa wanategemea sana kilimo kwa asilimia 65.5, wanategemea sana kilimo ambapo wangeweza

kuelezwa na kununua hizi trekta zinazotengenezwa *CAMARTEC* na kuzitumia vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAMARTEC* wanatengeneza mashine za kutengeneza majani ya mifugo, wangeliweza hata wafugaji wakanufaika kwa upande huo, wanatengeneza pia mashine za kukamua asali ambazo asali nayo wafugaji wa nyuki wangeweza kufaidika huko huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye *KMTC*, *KMTC* imesimama kwa kweli kwa muda mrefu, kwa miaka zaidi ya 30 lakini sasa hivi nawapongeza sana Mheshimiwa Rais, na Mheshimiwa Waziri. *KMTC* sasa imefufuka, inazalisha, lakini bado haijafikia hatua kwa sababu hawana wataalam. Naomba sana waongezewe wataalamu na vifaa vingine bado vimechakaa. Naomba sana waongezewe vifaa ili kusudi waweze kuzalisha vipuli pamoja na mashine. Ni kiwanda pekee sana ambacho kinazalisha vipuli, kinaweza kutuendeleza hapa nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye *TIRDO,* vijana wale wanafurahisha sana, wanafanya utafiti ambao wanaweza kufanya wakazalisha hata nishati. Hata ukiwa hapa Dodoma unaweza ukawasha umeme wako nyumbani kwako Dar es Salaam, unaweza ukawasha umeme wako nyumbani kwako Kigoma. Kwa hiyo, ni vijana ambao ningeliomba waendelezwe kwa sababu ni wagunduzi, na ni watafiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia *TIRDO* iweze kupewa hela bajeti zaidi kwa sababu inafanya mambo mazuri ya kumwendeleza Mtanzania hasa kwa upande wa vijana lakini hawana wataalam wenye ujuzi. Napenda Mheshimiwa Waziri, awaangalie waweze kuendeleza wataalam ili waweze kuajiri wataalam wenye ujuzi *TIRDO* iweze kufanya kazi ambayo imejipangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TEMDO* wanafanya mambo makubwa mno mpaka wanatengeneza majokofu ya miili ya maiti, wanatengeneza viwanda vya sukari ambavyo unaweza ukachukua pale ukaenda ukasimika mahali ukaanza

kutengeneza sukari wewe mwenyewe. *TEMDO* wanafanya kazi nzuri na yenyewe naomba waongezewe fedha kusudi waweze kujiendeleza vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku ile nilimshauri Mheshimiwa Waziri wa Afya kuwa tembelea *TEMDO*, ukitembelea *TEMDO* utakuta huko labda *delivery beds,* wanavyo vitanda vile vya hospitalini hata vya kujifungulia akina mama. Kwa hiyo, naomba sana, kama tulivyosema, Serikali ikisomana tunaweza tukaishia hapa Tanzania kutumia na kununua vifaa vyetu tunavyotengeneza hapa nchini bila ya kutumia fedha nyingi kwenda kununua vifaa nje ya nchi kwa kutumia fedha za kigeni. Jambo la muhimu ni kuvitangaza hivi viwanda ambavyo vinafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo naomba niongelee kuhusu lumbesa. Wakulima wanaomba sana, vipimo vipo, kwa hiyo, naomba wapate elimu kusudi tuweze kuondokana na lumbesa. Tukiondokana na lumbesa tutaweza kumfaidisha mkulima kwa sababu anahangaika sana kwenye upande wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza niongelee masoko. Masoko mengine yamechakaa kwenye Halmashauri zetu, na kwenye Miji yetu. Naomba uwepo mwongozo kwa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na TAMISEMI waweze kutengeneza haya masoko. Nashukuru kwa Mkoa wangu wa Morogoro tunalo soko moja ambalo ni soko kubwa, ni soko la kisasa, ni soko zuri sana hata hapa Dodoma tuna soko la Ndugai ambalo ni zuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia soko lingine la Mawenzi Mkoani Morogoro, Manispaa ya Mjini naomba liangaliwe, kwa sababu unakuta wafanyabiashara wengi wanakwenda kwenye soko la Mawenzi. Kwa hiyo, ningeliomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu na wewe unatembelea sana pale Morogoro uweze kuliangalia soko la Mawenzi kusudi liweze kupewa kipaumbele. Kama ni wewe au unasaidiana pamoja na TAMISEMI kwa kushirikiana, soko la Mawenzi liweze kupewa kipaumbele kusudi

liweze kujengwa, liweze kuonekana kwa sababu wanalitumia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, mengi nimeyaongea, yanatosha kwa leo. Nawaomba sana wananchi wote waweze kutumia bidhaa zetu tunazozalisha hapa nchini, *TBS* inafanya kazi nzuri, kwa hiyo, tusipende bidhaa za nje, tupende bidhaa za hapa. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, naomba mwendelee vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya, jiandae Mheshimiwa Mheshimiwa *Eng.* Ulenge.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami natangulia kuunga mkono hoja lakini namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika nchi yetu ya Tanzania, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yote ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo maeneo mawili leo ningependa kuchangia. Eneo la kwanza ni kuhusu fursa za viwanda Manyoni; eneo la pili nitachangia muundo wa *TBS* na *TFDA* ambayo ilikuwepo hapo awali na nitapenda kuishauri Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri tumeongelea sana suala la fursa mbalimbali zilizopo Manyoni hususan chumvi. Vilevile tuna fursa ya korosho kule Manyoni. Nawaomba hawa Mawaziri watusaidie tupate viwanda kule Manyoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tulishafanya utafiti wa *deposit* za chumvi kule Manyoni katika Kata ya Majiri kwa vijiji vya Kinangali, Mpandagani na Mahaka. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, wale wawekezaji ambao wanakuja Tanzania wajue kule Manyoni vilevile tuna fursa ya chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Manyoni tunawekeza sana kwenye korosho. Tuna zaidi ya ekari 20,000 za korosho na tayari tulishaingia kwenye *phase* ya kuvuna korosho. Tunaiomba Serikali ivutie wawekezaji wa kuweka viwanda vya ku-*process* korosho ili basi tuweze kusafirisha korosho zilizobanguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo ningeweza kuchangia leo ni kuhusu *TBS*. Mwaka 2019 Serikali iliamua kuiongezea majukumu *TBS (Tanzania Bureau of Standards)* ikapewa jukumu la kusimamia vyakula na vipodozi *(food and cosmetics)* kwa kubadilisha sheria ya 2003 na kuja na sheria nyingine ya 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nia ya Serikali haikuwa mbaya, lakini nina wasiwasi kama tulijiridhisha vizuri kabla hatujafanya yale mabadiliko ya kuhamisha *food and cosmetics* kutoka *TFDA* kupeleka *TBS*. Kwa nini ninasema hivyo? Ukifanya *analysis* za kidunia duniani kote, kwa mfano ukaangalia *global practice* suala la *food, drug* na *cosmetics* lipo *administered* (linasimamiwa) na taasisi moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawatolea mifano; Zanzibar, wana *Zanzibar Food and Drug Administration Agency*, ukienda *UK* wana *UK FDA,* ukienda Australia wana *Australia FDA,* ukienda Marekani tena *a strong FDA,* ambayo nadhani wengi wetu sisi tunaiangalia wana *US FDA,* ukienda China ambao sisi ni soko letu kubwa wana *China FDA,* lakini ukienda Kenya majirani zetu wana *Kenya FDA. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa swali langu la msingi lilikuja, kwa nini tulitaka kujitenga na dunia tukaichomoa *food and cosmetics* tukaipeleka *TBS?* Inawezekana *motive* ilikuwa nzuri, lakini nadhani *motive* ya kwanza ambayo tunahitaji kuiangalia ni *public health and safety* (Suala la usalama wa chakula na afya ya watumiaji). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ndilo eneo ambalo kimsingi nadhani tulitaka kuliangalia. Kwa hiyo, ndiyo maana nimetangulia kusema inawezekana hatukufanya utafiti wa kina wakati tunataka kuhamisha masuala ya chakula na masuala ya

*cosmetics* kuyapeleka *TBS*. Kwa nini nasema hilo? Kwanza, tayari tumeenda kuificha kule ingawa *of course TBS* wanafanya vizuri sana kwenye maeneo mengi. Kimsingi suala la *food and cosmetics* ni kama tumelificha *TBS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, kwa nini tunajitenga na dunia? Kama *US* wana *framework* ya *FDA, China* wana *framework* ya *FDA,* Australia wana *framework* ya *FDA;* kwa nini tunataka kujitenga na dunia? Ni suala ambalo kimsingi tunahitaji kuliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine kama nilivyotangulia kusema suala la *food and cosmetics* naliona kama lipo *neglected*, kwa sababu ni suala ambalo kimsingi kitaifa linahitaji usalama zaidi. Kwa hiyo, ni eneo ambalo ambalo tunahitaji kuliangalia. Sasa ushauri wangu ni nini? Kama nilivyotangulia kusema inawezekana nia ya Serikali wakati inahamisha *food and cosmetic*s kupeleka *TBS,* haikuwa na lengo baya, lakini tunahitaji kujiridhisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashauri iundwe Kamati Maalum ikafanye mapitio ione, *is it fair globally speaking* kuiacha *food and cosmetics* ibaki *TBS* au tuirudishe irudie ile ya *TFDA? That is one of my points.*

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, alishatuambia jambo hili limefanyiwa kazi na limefika hatua za mwisho. Kwa hiyo, jambo la kuunda Kamati tutakuwa tunarudi nyuma. Ningependa kumpa hiyo taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Chaya.

**MHE. DKT. PIUS S. CHAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa hiyo taarifa. Nisisitize kama hilo jambo limefika mwisho, basi tunaomba sasa tupate mrejesho. Tuone ni jinsi gani sasa sisi kama nchi tunaenda kusimamia suala la *food and cosmetics*, hatutaki kujitenga na dunia. Nchi nyingine wanafuata *framework* ya *FDA,* sisi tunataka kuwa nani tuje na mfumo wetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *WHO* wanafuata *FDA,* sisi tunataka kuwa nani? Kwa hiyo, mimi ushauri wangu na hili siyo la Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa sababu kwanza yeye alilikuta ni suala la kitaifa. Tunahitaji kuhakikisha kwamba, tunafanana na wenzetu. *We are a globe*. Tunafanya kazi na watu wengi; *China our partners*, *US our partners* na *UK* ni *partner* wetu. Tunaenda kutengeneza *framework* ambazo siyo *compatible* na nchi nyingine, itatusumbua kibiashara. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu *TBS*. Tumetembelea *TBS* tumeona wanafanya kazi kubwa sana na wana wataalamu wa kutosha, lakini vilevile kuna upungufu wa baadhi ya wataalamu. *TBS* tunashauri waanzishe Ofisi za Kikanda, kwa sababu wanasimamia suala la *standards* ambalo ni kitu cha muhimu sana kwenye masuala ya biashara na viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeshauri tuimarishe *TBS* tuwape fedha wafungue Ofisi za Kikanda ili waweze kusimamia vizuri suala la biashara na suala la viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga tena mkono hoja. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa *Eng.* Ulenge.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Awali ya yote namshukuru Mungu Mwenye Enzi na Utukufu kwa kuniwezesha kusimama mahali hapa muda na wakati kama huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali inazochukua kuhakikisha Taifa letu linanufaika vema na biashara na mataifa ya nje pamoja na kuongeza tija na kupunguza mfumuko wa bei. Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake dada yangu mpendwa sana *role modal* wangu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, kwa kazi nzuri, nzuri kabisa anayoifanya kuhakikisha tunafanya biashara vyema na Taifa letu linaongeza nguvu ya uzalishaji na kuhamisha bidhaa zetu nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Mheshimiwa *Prof*. Muhongo na ninaomba kuunganisha nguvu kuanzia pale. Mheshimiwa *Prof*. Muhongo ametoa *kind of a little research,* amefanya tafiti na mchango wangu nami unakwenda kuelekea huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote tunakubaliana kwamba, tuna rasilimali za kutosha kuhakikisha Taifa letu linaweza kuuza nje zaidi pamoja na kuhakikisha tunakwenda kufanya biashara bila kuwa na mfumuko wa bei mkubwa. Ninachoamini, mafanikio ya Sekta ya Viwanda na Biashara yatategemea ni kiasi gani kama Taifa tunaibua na kuweka nguvu pamoja katika tafiti *(research and development)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ni namna gani tunaweza kufanya tafiti ambazo zitaboresha rasilimali zetu na kuhamisha maarifa ya kisayansi katika uzalishaji? Nimeangalia vipaumbele sita vya Bajeti hii ya 2024/2025. Sijaona kipengele ambacho kinazungumzia ni namna gani tunafanya tafiti ya rasilimali zetu ambazo zitaongeza nguvu katika uzalishaji. Hilo sijaliona katika kipaumbele cha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kiuhalisia tunafanya tafiti kwa kutumia fedha za wahisani *(DANIDA) na (IFDA)*. Tunapofanya tafiti, tunapowarudishia wahisani majibu ya tafiti yale, tunawaonesha mianya na *gap* la kuja kufanya biashara kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kama Taifa tusitenge fedha zetu wenyewe kwenye bajeti tukafanya tafiti zetu ambazo

sisi zikatuwezesha kuongeza thamani ya mazao yetu na kwenda kusafirisha nje ya nchi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wahisani wanapotupa fedha tutafanya tafiti kwa mujibu wa wanavyotaka wao. Tukiwapelekea tunawaonesha *opportunities* na fursa ambazo zipo kwetu na wao wanarudi kwetu kufanya biashara na sisi. Baada ya miaka kadhaa wanatuachia wao wameshanufaika, nchi inabaki bila chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kusisitiza katika eneo hili. Tuna rasilimali za kutosha, tuwekeze zaidi katika tafiti zetu. Kule kwetu Tanga ukiangalia tuna madini ya viwandani. Tuna *Mica* inayotuwezesha kutengeneza *screen* hizi za simu zetu. Tuna *Graphite* inatuwezesha kutengeneza betri za magari. Tuna *Quartz,* tuna *Feldspar*, tuna *Dolomite* na tuna madini lukuki kule Tanga. Mpaka leo sijawahi kusikia kama kuna mkakati mzuri umewekwa kuhakikisha tunanufaika kama Taifa au kama Mkoa kwa madini yale tuliyokuwepo nayo kule Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wachina wanachukua *Dolomite* kutoka kwetu, wanakwenda kutengeneza shanga, wanakuja kutuuzia *very expensive*. Naiomba sana Wizara hii ya Viwanda na Biashara, itusaidie sana katika kuhakikisha *gemstones* zilizopo Tanga zinafanyiwa tafiti za kutosha na madini ya viwandani yaliyopo Tanga, yanafanyiwa tafiti za kutosha ili tuone namna gani tunaweza kuongeza thamani na kuweza kusafirisha nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Kiwanda chetu cha *Tanga Fresh*, jamani maziwa ya *Tanga Fresh* yalikuwa matamu sana kuliko maziwa mengine yaliyokuwepo huko, lakini kiwanda kile kinayumbayumba mpaka sasa. Shida ni nini kwa *Tanga Fresh?* Kama *Tanga Fresh* itafanya vizuri, ina maana mwananchi mmoja mmoja anayezalisha maziwa ataweza kununua pale na tutaongeza mzunguko wa fedha katika Mkoa wetu wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shida ipo wapi ya *Tanga Fresh?* Kwa nini inayumbayumba? Natamani kusikia kutoka kwa dada

yangu mpendwa katika hitimisho lake. Ni namna gani wanatusaidia kuhakikisha *Tanga Fresh* inakwenda kusimama sawa sawa na tunaona faida ya kiwanda kile cha muda mrefu nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba kuzungumzia suala zima la zao la mkonge. Nimesikia vizuri umelizungumza katika bajeti yako, tunashukuru sana kwa hilo. Ili tuweze kutokusafirisha au wakulima wadogo wadogo kuuza ile *raw leaf* (lile jani lenyewe) wawezeshwe. Vilevile, kupata zile mashine za korona, hiyo ndio shida kubwa inayotukabili Tanga. Mashine za korona kule chini ni kidogo. Wanauza majani badala ya kuuza zile nyuzi ambazo zimeshachakatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Serikali katika hili waweke kipaumbele. Hata kutoka kwenye mkonge tunaweza kupata vitu mbalimbali ambavyo tunaweza kusafirisha nje ya nchi, lakini hata tukiusafirisha mkonge wenyewe tuna uwezo wa kupata fedha nyingi za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, naomba sana Serikali kwenye mradi uliopo pale Ubungo, *issue* siyo suala la watu wa Kariakoo kupata maeneo kwenye eneo lile la biashara la Afrika Mashariki. *Issue* ni namna gani tunaweza kuwa-*manage* Wachina wasifanye biashara za rejareja ambazo zinaweza kufanywa na Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawajua Wachina walivyo. Wachina ni watu ambao wanaweza kupenya. Wao ni wazalishaji, wao ni *supplier*s lakini wakati huo huo wanaweza kuingia mitaani wakauza vitu vile vile ambavyo Mtanzania amenunua kwao kwa bei ya rejareja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaipongeza Serikali, naiona dhamira yake ya kuhakikisha kwamba, Tanzania tuna *hubs* katika zile nchi ambazo hazina bahari *(Landlocked Countries)*. Ninaamini kupitia mradi ule pale tunaweza sana kuwasafirishia hata huko Congo alikosema kaka yangu Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, lakini *that is an issue*. *Chinese* wanajua kupenya kufanya biashara ambazo sisi Watanzania tunaweza kuzifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana mwangalie makubaliano mliyoingia na iwapo itatokea Mchina yeyote anakwenda kuingia mtaani kufanya biashara ambayo Mtanzania anaweza kuifanya, hatua kali zichukuliwe. Hata wale ambao wapo sasa hivi Tanzania wanauza mapazia na maua Kariakoo tuone namna gani ambavyo tunastopisha kwa sababu wapo na siku nyingi tunasema, na sijaona hatua ambazo zinachukuliwa dhidi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Watanzania na sisi tuna uwezo wa kufanya biashara na tutakua kiuchumi wakati tunatafuta namna ya uzalishaji. Hizi ni hatua muhimu ambazo zinapaswa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunao muda bado. Mheshimiwa Neema**.**

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa muda niweze kuchangia. Nitumie nafasi hii kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo anapambana kuweza kuhakikisha analeta fursa mbalimbali katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu na mimi nina yangu machache katika Wizara hii. Jambo kubwa kabla sijaenda kuchangia haya mengine ambayo nimedhamiria, kwanza natamani kuiona Wizara hii inautazama Mkoa wa Songwe kwa namna ya tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Songwe ni Mkoa wa kibiashara, ni Mkoa wa viwanda, ni Mkoa wa uzalishaji na ni Mkoa ambao unazalisha vyakula kwa wingi. Tunazalisha kahawa na madini mbalimbali. Kwa hiyo, natamani kama Wizara wauone kwamba Mkoa wa Songwe ni Mkoa wa kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee kwa maana ya Mji wa Tunduma kwamba Wizara naona haijafanya kitu kwa Mji

wa Tunduma. Nimekuwa naongea hapa mara nyingi kukumbusha namna ambavyo Wizara hii ya Viwanda na Biashara, iweze kuona Mji wa Tunduma kama ni Mji ambao wanaweza kutengeneza wafanyabiashara wakubwa wengi. Pia, wanaweza kutengeneza viwanda vingi kwa sababu ndiyo mji ambao upo kwenye lango la *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa namna ya tofauti na timu yake waende wakafanye *research* pale. Ni kwa namna gani Mji wa Tunduma unaweza ukawanufaisha kwa kuanzisha viwanda vikubwa? Pia, kwa kuweza kuanzisha biashara kubwa ambazo zinaweza zikahudumia Ukanda wa *SADC*. Kwa hiyo, ni namna ambayo wao kama Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Wizara ya Mipango, wanaweza wakajipanga kufanya kitu kwa ajili ya Mkoa wa Songwe na hususan kwa Mji wa Tunduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niungane na wenzangu ambao wameongea kwamba, kama nchi tumeona kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa dola. Tunapoongelea dola, ni kitu ambacho kama Taifa inaweza ikawa ni fursa kwa kuwa na *reserve* ya kutosha ya hela za kigeni kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mheshimiwa Mbunge ambaye sio mtaalamu sana wa masuala ya kiuchumi kwa maono yangu tu ya kawaida baada ya kusoma taarifa hii nimeona kwamba Wizara kama Wizara hawana malengo au mkakati maalum wa kulinda fedha za kigeni kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema nini? Hii ndiyo Wizara ambayo inaweza kutusaidia kutunza fedha zetu za ndani kwanza zisiondoke nje. Nilikuwa nasoma mahali hapa katika maandiko mbalimbali ambayo yameandikwa nikaona kwamba, kuna kiwango cha samaki ambacho kinaingizwa nchini. Niliwaza tu hiyo ni *sample* ya *product* ambayo nimeiona kwamba ni kitu ambacho kama Watanzania hatupaswi kuagiza. Minofu ya samaki imeingizwa yenye thamani ya dola bilioni 6.24 wanaagiza inaingizwa humu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo fedha tungetumia minofu iliyomo humu humu nchini. Tuna Maziwa ya kutosha tungeweza kuhifadhi hii fedha na tusiwe na uhaba huo wa fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa naenda kwa mazao ya kilimo ambayo yanaingizwa nchini kama vile ngano. Tunawezaje kuagiza ngano wakati hii ni fursa kwa wananchi wetu kuweza kulima na ku-*supply* kwa viwanda vyetu ambavyo vipo nchini ambavyo vinaagiza hizo ngano? Kwa hiyo, nataka kusema kwamba hii ndiyo Wizara pekee ambayo inaweza kutusaidia kama nchi kuhifadhi fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusoma taarifa yao, sijaona wao kwamba wana malengo gani ya ku-*balance* uwiano wa *impor*t na *export*. Nilikuwa najaribu kuangalia kwa biashara waliyofanya kwa hizi Jumuiya za Ulaya, sisi kama Taifa tuliweza ku-*import* vitu vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.05, lakini *export* ikaenda kwenye shilingi bilioni 3,835. Sasa nawaza, inakuwaje tunaweza tuka-*exceed;* kwamba sisi tu-*import* zaidi kuliko ku-*export?*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Wizara wanafanya mkakati gani wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na *expor*t nyingi? Kwa sababu tunatengeneza wafanyabiashara, tunatengeneza wajasiriamali wengi na tunatengeneza viwanda. Kama Wizara imejiwekea mkakati wa kutengeneza bidhaa ngapi ambazo ziingie kwenye masoko ya kimataifa? Kwa hiyo, hili nalo sijaliona huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Wizara watengeneze mpango kazi ambao utaonesha kwamba wana-*balance* vipi *import* na *export?* Pia wanatengeneza wafanyabiashara wangapi ambao wataweza kuingia soko la Kimataifa kwa ku-*export product* zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nirudi kwa Viwanda vya *SIDO.* Hii Taasisi ya *SIDO* ni Taasisi ambayo kama Watanzania tunaitegemea. Nilikuwa nasoma katika taarifa hapa, wananiambia eti nchi nzima *SIDO* wamekuza wajasiriamali

watano tu. Sasa nawaza Mkoa wa Mbeya, Songwe, Morogoro na mikoa yote Tanzania nzima, wakatuambia wamekuza wafanyabiashara watano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona ni kitu ambacho kama Taifa Wizara haina mkakati maalum wa kuhakikisha wanatengeneza wajasiriamali wengi zaidi ambao watahakikisha wanakua. Mimi nisiseme mengi, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa kwanza, tuchukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mradi huu wa Mchuchuma na Liganga, tumeuona zaidi ya miaka 40 lakini kipindi hiki sasa maamuzi sahihi yamefanywa. Maamuzi yamefanywa na Mama ameshatoa agizo na maelekezo kwenye Serikali yake huu mradi uanze kazi na uanze kutekelezwa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sasa kazi ipo kwenu Mawaziri mhakikishe huu mradi ufanye kazi na mtazame hizo *share* za zamani sana tujaribu za kwetu zipande juu kidogo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaanza na Mheshimiwa Ramadhan Ramadhan, Mheshimiwa Boniphace Getere, Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Kavejuru Felix.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni leo. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**21 MEI, 2024**

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu, tutaanza na Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Getere, Mheshimiwa Japhet Hasunga na Mheshimiwa Kavejuru ajiandae.

**MHE. RAMADHAN SULEIMAN RAMADHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ili nasi tupate kutoa mawazo yetu na michango kwenye Wizara au hoja iliyopo Mezani leo, hoja ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kabla sijaenda kwenye mchango wangu, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya, uzima na nguvu. Pia nawashukuru wananchi wa Chake Chake kwa namna wanavyoendelea kuniombea dua Mbunge wao ili niendelee kuwapambania na kuwawakilisha kwa yale waliyotuma kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue fursa hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa anavyoendelea kutupambania. Halali usiku na mchana, anaendelea kupambana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Tanzania inaendelea kuwa salama kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa napitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nilikuwa *very disappointed*. Moyo wangu ulivuja damu nilipoona anaomba shilingi bilioni 29 kwa ajili ya maendeleo. Wizara ya Viwanda na Biashara ni Wizara ambayo inabeba uchumi wa nchi hii. Viwanda nchi hii ndiyo ajira. Asilimia 75 ya Watanzania, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022, kwenye

*population* yetu ni vijana wenye umri wa miaka 35; na ndio hao ambao wao wapo kwenye soko la kutafuta ajira za nchi hii lakini Serikali haiwezi kuwaajiri wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwaajiri wapi zaidi ya kujenga viwanda vingi, maeneo ambayo ndiyo tutakayoweza kuwaajiri? Sasa nilivyoona shilingi bilioni 29, nikajiuliza, *are we serious* kweli? Shilingi bilioni 29 tunakwenda kufanya nini? Wizara hii ndiyo inayobeba sera, inabeba sera ya viwanda vya nchi hii. Unaipa shilingi bilioni 29 ikakarabati, ikafanye tafiti, ikaanzishe, ikaboreshe! Siyo sawa, siyo sawa hata kidogo. Hizi fedha hazitoshi, ni kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutarudi hapa mwakani, tutaimba *the same song,* nyimbo ile ile kila siku. Mheshimiwa Waziri anakwenda kufanya nini na shilingi bilioni 29? Shilingi bilioni 29 anakwenda kufanya nazo nini? Atakwenda kufanya yote hayo kwa shilingi bilioni 29? Hazitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba Serikali walitazame kwa jicho la huruma na kwa jicho la pili, wamwongezee Mheshimiwa Waziri fedha ili akafanye kazi ya kuviinua viwanda vyetu. Kila mtu aliyeinuka hapa amelia, kwamba viwanda vimekufa, kila mtu aliyeinuka hapa amelia kwamba ana *raw materials* lakini hana viwanda. Tunakwenda kuvianzishaje? Anakwenda kuhamasishaje watu waje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ombi langu la kwanza na la msingi ni kwamba tukamwongezee fedha Mheshimiwa Waziri; kama tupo *serious* na tunataka sekta ya viwanda na biashara, kwamba itutoe na itupeleke kwenye zile ndoto ambazo Watanzania tunaziota za kufikia Tanzania ya Viwanda. Hilo lilikuwa ombi langu la msingi na la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili. Wakati Mheshimiwa Prof. Muhongo anatoa mchango wake hapa asubuhi aliomba kwa Mkoa wa Mara akajengewe viwanda; kwa sababu ana pamba, akajengewe *textile industry.* Akasema yeye ndiye mvuvi mzuri, hivyo akajengwe viwanda vya ku-*process* mazao ya samaki. Akasema yeye hapa ni mkulima mzuri, kwa hiyo,

akajengewe pia viwanda vya ku-*process* mazao yanayotokana na kilimo na mifugo. Akalia kwa sababu ya viwanda vyake vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wakati natafakari mchango wake nikawa najiuliza, hivi huyu mwenye sera ambaye ndiye Wizara ya Viwanda na Biashara ambaye ndiye amekabidhiwa hii sera, anasimamia nini sasa hivi? Ana nini mkononi anachokisimamia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiangalia ki-*theory* tumemwambia yeye ndiye akasimamie viwanda. *Practically,* viwanda vyote vikubwa vya nchi hii ambavyo vipo kwenye mazao ya kilimo vipo Wizara ya Kilimo. Viwanda vya sukari, pamba, chai na vya *coffee* (kahawa); viwanda ambavyo vipo kwenye mazao ya mifugo (nyama, maziwa, ngozi) anavyo Mheshimiwa Ulega. Ndiye anayevifuatilia anavi-*control* anahakikisha ubora; yeye ndiye atakuja kusema maduhuli ya makusanyo. Sasa mwisho wa mwaka ukimwuliza Mheshimiwa Dkt. Ashatu au Mheshimiwa Waziri wa Viwanda anasimamia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mwekezaji mkubwa wa viwanda akija anaanza kwa Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji. Huku atakwenda ataomba apewe ardhi, ataomba asajiliwe *BRELA*, wao ndio watakaomsaidia na *one stops centre* yao. Sasa yeye ndiye tuliyempa sera, lakini tumemweka katikati sasa hivi, sijui hata nisemeje kwa lugha nyepesi. Kama vile tumempa sera aisimamie, lakini wenye *infrastructure* ni watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii ndiyo Wizara mama na ndiyo Wizara iliyopewa isimamie sera ya viwanda ya nchi hii na biashara pia. Hawa wafanyabiashara ambao Kamati iliwasema hapa asubuhi, sasa hivi Wamachinga wapo TAMISEMI. Kwa hiyo, unabaki tu *dilemma*. Atakuja hapa kila mwaka, atatueleza hatuoni kitu ambacho kipo *tangible* moja kwa moja kwake ambacho kitakuwa *legacy* yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya *legacy* yake Mheshimiwa Waziri na Serikali wakasimamie viwanda vidogo vidogo kupitia *SIDO*. Akasimamie *CHEMCO*, akasimamie *TIRDO*

kufanya *research*, akapambane na *KMTC*, akapambane na *CAMARTEC*. Huko ndiko kwenye *legacy* yake Mheshimiwa, akapambane huko. Tuje tuone jina lake linatajwa kesho kwamba yeye alikuwa *revolutionist* aliyepigana kwenye mapinduzi ya viwanda ya nchi hii ambayo kila mtu ataimba jina lake; lakini aombe aongezwe fedha, asione aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawezi kupambana kama hana hela za kutosha. Shilingi bilioni 29 hazimtoshi, hatafika popote, hatafanya chochote. Kila siku tutakapokuja itakuwa ni *the same story.* Amwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha ampatie fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 niliposimama hapa nilichangia kuhusu maendeleo ya viwanda vidogo vidogo vilivyopo katika nchi yetu na wajasiriamali wa Kitanzania wanaovianzisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya *industry* niliyoichangia ni *industry* ya *tailoring, industry* ambayo kwa sasa inakua *rapidly,* kwa kasi sana Tanzania; na inaajiri. Mshoni mmoja ana wastani wa watu 50 wamemzunguka. Nikasema mwaka 2023, na maneno hayo ninayarejea, bado hatujawasaidia wajasiriamali wadogo (Watanzania) wanaoanzisha viwanda Tanzania. Hatujawasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, akija mwekezaji akitaka kuanzisha kiwanda cha misumari au cha kutengeneza tenki anapata *incentives* za kodi akileta *raw materials.* Kwa mfano, akileta *raw materials* za *wire roads* kwa ajili ya kutengeneza msumari atapata *incentives* za kodi kwenye *raw materials,* tutakuja kumkamata baada ya msumari kuwa umekwishakuwa msumari au tenki limeshakuwa tenki na linauzwa. Tunawasaidiaje hawa *tailoring?* Akinunua kitambaa anakileta Tanzania kama bidhaa, siyo kama *raw material,* ni kama bidhaa amekwenda kukinunua India, China au Uturuki. Akinunua cherehani haileti kama mashine, analeta kama bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, atengeneze suti, akishatengeneza hiyo suti anakuwa ameshalipa cherehani na kitambaa. Kwa hiyo,

anaipandisha bei kiasi kwamba inashindwa ku-*compete* na bidhaa zinazotoka China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suti ya China unaweza kuinunua kwa 150,000 hadi 200,000 lakini *customer made suit* iliyotengenezwa hapa hapa, *designer* wa Kitanzania hawa wanaopambana watakuuzia kuanzia 350,000 hadi 400,000; na kwa sababu kutokana na kwamba hatuwalei, hakuna *incentives* za kuwasaidia wapambanaji wa Kitanzania wanaopambana kwenye kukuza viwanda vya nchi hii. Hiyo ni sekta moja ambayo inaweza kututoa tulipo. Sasa hivi kuna mtu anaweza akataka suti pea 200 hadi 300, akaagiza China au Uturuki. Kwa hiyo, ni kwa sababu ya bei na urahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilisema niwatambue Watanzania wazalendo wanaopambana kwenye sekta kama hizo. Mmoja ni *JM Collection*, ni kijana wa Kitanzania mpambanaji tu. Mwingine ni Suti Bega kijana wa Kitanzania ni *designer,* wanafanya vizuri tu. Mwingine ni *Mtani Design,* mwingine ni Kikoti, Dada yangu nje ya Bunge hapo *(Careen)* Carenito na kuna *Marafiki Suits.* Hao ni vijana wa Kitanzania wanaopambana kukuza viwanda vya Tanzania, lakini hatuchukulii kama *tailoring* inaweza ikawa sekta moja kati ya sekta ya viwanda kwa ajili ya kusaidia kukuza ajira, kupata fedha za kigeni na sisi kuuza bidhaa zetu. Tutaagiza mpaka lini? Tutavaa kutoka nje mpaka lini? Tupo mwaka wa 60 wa uhuru hatujaweza, tutaweza lini sisi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo uliokuwa mchango wangu kwa leo, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan. Nilimwita Mheshimiwa Mwita Getere, Mheshimiwa Japhet Hasunga ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara hii. Cha kwanza nampongeza Waziri wa Wizara, Naibu Waziri wake, Katibu Mkuu wake na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma baadhi ya hotuba za bajeti zilizotoka hapa ndani hii nayo inaweza kuwa hotuba mojawapo nzuri sana ambayo imeletwa na Wizara ya Viwanda na Biashara; na ukiisoma vizuri ni kwamba wamejiandaa sana kwenye hiyo hotuba, wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda mbali nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, wale wakubwa wa hapa Tanzania wanasema *big up.* Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 15.38 kwa ajili ya kuwalipa fidia watu wa Liganga na Mchuchuma. Heshima kubwa sana. Wale watu wamekuwa na kilio cha muda mrefu mno, wameteseka sana. Mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati hii. Nilikwenda siku moja tukakutana na akina mama wanalia, wanapiga magoti, wanasema mmetunyang'anya ardhi miaka nenda rudi, hatulimi na hatufanyi chochote. Mheshimiwa Rais ameamua kuwapa fidia ya shilingi bilioni 15. Heshima kubwa sana kwa watu wale waliotoa Liganga na Mchuchuma. Hii pia imetoa fursa kuona mradi wetu mkubwa wa Liganga na Mchuchuma sasa unaweza kwenda huko mbele tukapata nafuu ya kutekeleza mradi huu mkubwa sana. Hiyo heshima imekuwa kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kutoa hizo fedha *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamezungumzia suala la bajeti hapa. Unajua sijui kama mtu anaelewa maana ya viwanda ni nini? Hawa watu wa viwanda huyu Waziri wa Viwanda asipokuwa na fedha za kujenga *industrial park* kwenye maeneo mbalimbali na hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji wa matunda hali ni hatari mno. Unakwendaje kulima parachichi, ukilima, ukitaka kuuza huna mahali pa kuweka *at least* kupata muda wa siku tano ama nne ili usubiri bei iwe nzuri uuze. Huna uwezo, inaozea hapo. Tunapoteza thamani ya matunda ya maeneo yetu ya mazao kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima bajeti yao iongezeke ili wajenge *industrial park* ambayo itawawezesha wananchi wa kawaida kwenda kuweka mashine mle ndani. Watuuzie machungwa, maembe, na vitu vingine, hata mahindi na mchele. Kuna mtu anaweza kulima mahindi eka tano lakini hana mahali pa kutunzia. Akiwa ana maeneo ambayo anaweza kuweka samani inaweza ikampa nafasi ya kuuza. Kwa hiyo, nikiri kwamba

fedha za Wizara ni lazima ziongezwe ili wapate nafasi ya kujenga *industrial park* kwenye maeneo mbalimbali ili isaidie wakulima wetu. Nadhani jambo hili ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yenu nimeona kuwa wameunganisha ile *TFDA* kwenda *TBS*. Nimeona ubora walioutengeneza sasa hivi. Nawaomba wauongeze kasi kwa sababu sasa hivi wamefikia asilimia 66.4 ya ubora, wamepunguza gharama nyingi. Mimi na-*support* hili wazo, lakini waongeze kasi ya watumishi, waongeze thamani ya kusajili vyakula salama na vipodozi kwenye maeneo haya. Napongeza sana kwa hatua hii ambayo wamefikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni nchi inayokua sana, nchi yetu ni kubwa mno. Tunahamasisha watu wawe kwenye makazi mbalimbali na sasa tuna kitu kinaitwa *climatic change* (mabadiliko ya tabianchi). Hali ni mbaya sana kwenye nyumba za kawaida; wananchi wanataka kujenga nyumba za kudumu, bati gharama, *cement* gharama, nondo gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Waziri akija hapa hana mawazo ya kupunguza gharama za vifaa vya ujenzi kwa wananchi wetu, kwa mfano, hii *cement* wanasema kwamba viwanda vikubwa vipo saba na vinazalisha tani 9.107; na vina nakisi (akiba) ambayo inabaki hapa kama milioni moja hivi wanauza na nje. Leo bati linauzwa shilingi 46,000/=, au shilingi 50,000/= hadi shilingi 60,000/=. Haiwezekani jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tukubaliane kama ni kupunguza *VAT* au kama ni kuweka ruzuku, tuweke ili wananchi wetu waweze kujenga. Hata yule Dangote wakisema wanampa mazingira mazuri ya kumpunguzia *VAT,* anaweza kuuza *cement* kwa bei nafuu, lakini sasa bei ya vifaa inapanda na wanataka tujenge. Tunajengea nini? Tunajenga bati lipo juu? Siku hizi watu wanataka m-*south* ambayo bei yake ipo juu, mabati ya kawaida nayo bei ipo juu, nondo bei zipo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri aje na mkakati wa Serikali tushinikize tuone namna gani wananchi wetu wanaweza kupunguziwa vifaa vya ujenzi, *cement*, mabati ili bei

iwe nafuu na wananchi wetu waweze kukuza viwango vyao vya ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwenye Kamati, wanasema kuwa kuna vijana wetu wanaopata ufundi wanaosoma darasa la saba. Tukumbuke kuwa darasa la saba ni mtihani, ni masomo na Baraza la Mitihani linatambua kiwango cha darasa la saba kwenye nchi yetu; lakini wale vijana wetu wa darasa la saba wanapomaliza wanakwenda kujifunza udereva, wanakwenda kujifunza uanagenzi, wanajifunza na mafundi mchundo (mafundi asanifu) wanajifunza mambo yote. Muda wa kuajiriwa Serikalini wanasema wanahitaji cheti cha *Form Four*. Lazima walete sheria hapa ya kubadili mfumo huu wa ubaguzi ambao tunao. Hivi kinachoendesha gari ni cheti au ni weledi wa mtu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukubali wale ambao tumewapeleka kwenye mafunzo ya *VETA* na maeneo mengine, wa darasa la saba ambao hawakumaliza *Form Four* wakubalike kuajiriwa na Serikali. Hatuwezi kuwa na ubaguzi wa namna hiyo. Watu wanasoma ufundi mbalimbali, tunataka kwenda viwandani tunakuwa na fundi mchundo, lakini sasa mkienda huko wakitaka kuajiriwa Serikalini mnasema cheti cha *Form Four*. Lazima mlete sheria tubadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati, imezungumza vitu vizuri sana hapa vya kubadili suala la hizi sheria ili wananchi wetu waweze kupata nafuu ya kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni Wizara mama sana, tunaiomba Serikali kama kuna maelewano, kwa sababu hii ni Wizara mtambuka, ikubaliane na Wizara nyingine zinazohusika, wakae pamoja waangalie hili linafanyika na nani, hili linafanyika na nani ili wawe pamoja. Kuliko kuwa na Wizara ambayo unaipa bajeti ndogo na unakata ishughulike na mambo makubwa ambayo haina uwezo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo, nilitaka nichangie eneo hili ili niweze kuunga mkono bajeti, lakini mnafanya vizuri sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mheshimiwa Kavejuru Felix na Mheshimiwa Asia Halamga, mjiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo ndiyo imebeba maudhui na maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutegua kile kitendawili cha siku nyingi ambacho eneo la uchimbaji wa madini ya chuma kule Liganga na Mchuchuma, lilikuwa limesimama kwa muda mrefu na limekuwa ni kitendawili cha muda mrefu sana. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha hizo ili angalau sasa tuanze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuma ni muhimu na madini yote yanayopatikana pale yatachangia katika uchumi mkubwa wa nchi yetu. Pia, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri, Watendaji wote, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa taasisi zilizoko chini yake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Pia nawapongeza kwa hotuba nzuri. Hotuba haiendani na rasilimali, lakini ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema Wizara hii ni muhimu sana kwa sababu ukiangalia katika uhalisia, wenzetu wanasema neno 'uzalishaji', limegawanyika kwenye maeneo matatu; eneo la kwanza ni viwanda, eneo la pili ni biashara na eneo la tatu ni huduma za jamii. Sasa ukiangalia viwanda na biashara, vinaangukia kwenye Wizara hii na hili ndiyo eneo ambalo tunatarajia liweze kutatua matatizo ya msingi ya nchi yetu, ambapo matatizo ya msingi ya nchi yetu ni pamoja na umasikini mkubwa ambao uko kwa wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umasikini huu utatokana na viwanda tutakavyoweza kuvijenga hapa nchini. La pili, biashara mbalimbali watakazofanya, ndiyo wataweza kuchangia uchumi wa nchi yetu, lakini uchumi wetu unategemea sana katika hili

eneo. Kwa hiyo, ili tuondokane na umasikini na ili tutengeneze ajira za vijana wetu zote, ziko kwenye Wizara yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye viwanda tunasema, vipo viwanda vya kutafuta malighafi *(extractive industries)*, ambapo hapo kuna kilimo, mifugo, ufugaji, madini, misitu na kadhalika. Hivi vyote sisi tunaita ni viwanda *(extractive industries)*. Vipo viwanda vya kuongeza thamani *(Manufacturing Industries)* na vipo viwanda vya kuunda miundombinu *(constructive industries)*. Sasa utaona kwa hiyo, ina maana kilimo, uvuvi, misitu na madini, vyote Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ndio anabeba sera ya viwanda hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia katika uhalisia, nchi ambayo inategemea kilimo. Kilimo chetu hatuwezi kutegemea kiendelee kuzalisha mazao tunayauza kama malighafi. Lazima tuwe na viwanda vya kuongeza thamani ya hiyo malighafi. Tuwe na viwanda vya kuchakata kahawa na tujenge mpaka hadi kahawa ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mlowo, Mbozi pana kiwanda cha kukoboa kahawa, tunataka kisiishie kukoboa, tunataka kitengeneze kahawa ili Watanzania wanywe moja kwa moja kutoka hapa badala ya kuagiza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tunapouza mahindi ambayo tunalima sana katika maeneo mbalimbali, mahindi yale tuyasage tupate unga. Unga ule ndio twende tukauze *DRC* Congo na nje ya nchi, bidhaa ambazo zimeshakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote ambayo inauza mazao kama malighafi, hiyo maana yake imechagua kuwa nchi masikini duniani. Sisi Tanzania hatujachagua kuwa masikini, tunataka tuwe Tajiri; iwe ni nchi ya kimkakati ambayo italeta maendeleo ya nchi hii. Kwa hiyo, tunataka lazima tuwe na mkakati wa kutosha wa kuhakikisha kwamba tunaongeza thamani ya mazao yetu, kuongeza thamani ya madini yetu, kuongeza thamani ya misitu yetu na kadhalika ili nchi hii iweze kutengeneza ajira, tuweze kuondokana na umasikini na tuweze kujenga uchumi mkubwa wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri na timu yake unayo hiyo dhamana ni yeye mwenyewe hapo. Sasa hivi nimefurahi sana kusoma kwenye Hotuba yake amesema, "Tunavyo viwanda vya kutengeneza, kuunda magari," lakini hebu tuangalie hivyo viwanda vya kuunda magari alivyovisema, ni viwanda vichache. Ni hatua nzuri, tunampongeza lakini tunahitaji viwanda zaidi vya kuunda magari. Magari ni madogo kwa sababu ni eneo ambalo tunachukua fedha nyingi sana za kigeni kwenda kuzipeleka nje na kununua magari. Tunataka magari haya yaundwe hapa. Ikiwezekana tutengeneze hapa hapa na vipuli, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka zana za kilimo cha nchi hii ambapo Watanzania zaidi ya asilimia 65 ni wakulima, zana za kulima zitengenezwe hapa. Tunataka viwanda vya mbolea na madawa yatengenezwe hapa. Hapo ndipo tutakapoweza kujenga uchumi mzuri na wenye maendeleo mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kwenda bila viwanda. Viwanda ndiyo mhimili wa maendeleo ya nchi. Hebu tuangalie kidogo katika nchi zilizoendelea... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Janejerry.

## TAARIFA

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba, viwanda tunavyo. CAMARTEC inatengeneza matreka hapa Tanzania, lakini kikubwa ni hizi Wizara kuungana na kutumia viwanda vilivyo nchini; Wizara ya Kilimo na Wizara ya Uvuvi. Nenda kwenye maonesho pale vitu vyote viko pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima yake naipokea tu, lakini nataka nimwambie, viwanda vilivyopo ni vichache mno, havitoshelezi mahitaji ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumzia sisi, ni kwa uwanda mpana kuangalia mahitaji ya Taifa letu. Tunahitaji viwanda vingi, kwa mfano, suala la mafuta, nchi ya Tanzania tunaagiza mafuta ya kula nje ya nchi. Dola nyingi tu zinakwenda huko, hiyo kwa kweli haikubaliki. Tunatumia fedha, sasa hivi tunaagiza hadi sukari nje ya nchi, haikubaliki. Haya yote tuna uwezo wa kuzalisha hapa, matrekta na majembe, tunahitaji tuzalishe hapa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa nasema, kuna kitu kilitokea ambacho inabidi tuliombee Taifa hili. Nchi ya China mwaka 1949 walipopata uhuru, waliweka mkakati wa *industrialization* na wakafanikiwa kujenga viwanda mpaka leo China ni nchi ya pili duniani kwa viwanda. Nchi ya India waliweka mkakati wa namna ya kujenga viwanda, mpaka leo India wamefika hatua kubwa, nao walipata uhuru unaoendana hapo hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumepata uhuru mwaka 1961, tulichukua hatua za kuanza kujenga viwanda, tumejenga viwanda vingi karibu kila maeneo tulikuwa navyo, lakini hapo katikati shetani alipita, viwanda vyote vikakufa. Hatuwezi kukubali hili, tuangalie tulipokosea, turudishe viwanda vyote ambavyo vimepotea. Hili ndiyo litatuwezesha sisi tuweze kufika mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuimarisha biashara...

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa ya Mheshimiwa Condester.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumwongezea mchango Mheshimiwa Hasunga, alichokuwa anaongea yuko sahihi. Sisi hata Tanzania hatuna viwanda vya kutengeneza ila tuna viwanda vya kuungaunga. Mfano, *CAMARTEC*, injini za matrekta hawatengenezi wao,

zinatengenezwa nje. Kwa hiyo, Mheshimiwa Hasunga yuko sahihi kwenye mchango wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hasunga, unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Vyote hivyo ni viwanda, hata vya kuungaunga tunavihitaji. Maana yake ni lazima kwanza tuanzie kwenye viwanda vidogo vidogo ili tupige hatua tuje tufike kwenye viwanda vikubwa. Kwa hiyo, hata vidogo tunavihitaji, hakuna cha kidogo, kwa sababu hata Waingereza walianza kwenye *cottage industries;* walianzia nyumbani, wakajenga viwanda mpaka wakafika walipofika na sisi lazima tuanzie hapo hapo ndiyo tutakuja kufika huko kwenye viwanda vikubwa ambavyo tunavitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nazungumizia eneo la biashara. Nchi hii ni lazima tuigawe katika zone muhimu za biashara. Kwa sababu ni nchi ambayo iko *strategically located*. Tuangalie ni aina gani ya biashara zinaweza kututoa na ni maeneo gani yanaweza kututoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyosema kule kwenye Mchuchuma na Liganga kutatutoa, lazima tuweke fedha. Sasa Mheshimiwa Waziri, ukiangalia bajeti ya maendeleo ya shilingi bilioni 29 uliyopewa, una bajeti ya shilingi bilioni 110. Bajeti ya Maendeleo ya kufanyia kazi shilingi bilioni 29, hii inatuonyesha *we are not serious.* Hatuwezi kujenga viwanda kwa shilingi bilioni 29. Hiyo tutakuwa tunatania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Bunge tukae vizuri, tuliangalie kama kweli tuna nia ya kwenda. Kwa hiyo, kwenye biashara, maeneo kama Tunduma, Tunduma iko mpakani ni lango la SADC, zijengwe biashara, Watanzania wawezeshwe wawe na biashara kwenye maeneo yale mengi ya mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Mbozi, Vwawa wajenge ma-*go down* na maduka makubwa, Wazambia, Wazimbabwe na watu wengine waje kununua. Iwe ni *hub* ya kununua kama ambavyo tunataka kufanya Kariakoo na maeneo mengine.

Tukiangalia hivyo, tutaweza kufanya biashara na nchi yetu itaweza kupiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuna changamoto mbalimbali za wafanyabiashara. Hilo naamini Wizara ya Fedha watalishughulikia vizuri ili kuondokana na hiyo changamoto. Tunalo tatizo la masoko, Wizara yako imebeba dhamana ya kushughulikia masoko ya mazao yetu na bidhaa mbalimbali, hiyo mtashirikiana na Wizara nyingine mhakikishe kwamba kwa kweli masoko yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusema, tunahitaji mfuko wa kuchochea ujenzi wa viwanda, bila mfuko, hapa tutakuwa tunaimba tu na Bunge hili ili tutengeneze historia. Ni lazima tuunde mfuko wa kuchochea viwanda. Mfuko huo tukiwawezesha Watanzania wakajenga ile miundombinu inayojitosheleza, watu wanaotaka kwenda kununua teknolojia huko wawezeshwe, hawawezi kupata fedha kutoka kwenye benki zetu hizi. Ukienda kule kwenye benki, wanakwambia hili wazo zuri, una mtaji gani? Wewe umejiandaaje na una dhamana gani? Mtanzania yupi mwenye dhamana ya kuweza kununua kiwanda kutoka nje akaja akakiweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi teknolojia ya viwanda iko kule inatakiwa ikanunuliwe ije isimikwe, Mheshimiwa Waziri, kila mwaka tunatakiwa tutengeneze mkakati, Watanzania 500 wawezeshwe. Tukiwa na programu ya miaka 10, baada ya hapo tutakuwa tumepata walipa kodi wengi, tutaweza kujenga viwanda tukiwa na mfuko wa viwanda. Kwa hiyo, hili mimi naamini kwamba ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, tuwe na mfuko wa kuwasaidia wafanyabiashara. Wafanyabiashara wetu wanateseka sana, wengine wana uwezo wa kufanya biashara na wana uwezo wa kufurukuta, lakini hawana mitaji. Mitaji hiyo itaweza kupatikana tu kama Serikali itaweza kuwa na mfuko wa kuwasaidia wawekeze. Nchi zote duniani zimefanya hivyo na ndiyo zimeweza kufikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja tu, misingi ya maendeleo ya nchi yoyote duniani, tunahitaji mtaji wa asili yaani ardhi, maji, madini, misitu, wanyamapori na kadhalika, huo ni misingi ya kwanza na Tanzania tunao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa pili ni ujenzi wa miundombinu, yaani tunahitaji *physical capital* ili viwanda viweze kwenda mbele, tatu, tunahitaji rasilimali fedha ili tuweze kuijenga nchini na mwisho tunahitaji rasilimali watu na wahusiano *(Human capital* na *social capital),* hivi ndiyo vitatusaidia kuendesha nchi yetu na kuisukuma katika viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja na ninawatakia kila la heri, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, ahsante sana, nilimtaja Mheshimiwa Kavejuru Felix, Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Hussein Amar wajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii niweze kutoa mchango wangu kwenye Bajeti ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali, namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi kwa zawadi ya uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa hasa hasa nikianza na hiyo ambayo ametoa shilingi bilioni 15.4 kwa ajili ya kuwapa wananchi wanaopisha mradi ule wa Liganga na Mchuchuma, hongera sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu wako kwa Hotuba nzuri sana ambayo imeeleza mambo mengi sana, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara, maendeleo ni hatua, tunaiona hatua, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia kwenye maeneo matatu; moja, ni eneo la biashara za mpakani, ni Mbunge ninayetoka Mkoa wa Kigoma, Mkoa wa Kigoma unapakana na nchi karibu tatu; tuna Burundi, Congo *DRC* na kusini, siyo mbali sana, unaiona Zambia iko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara zetu zinategemea usafirishaji, miaka 10 ya nyuma iliyopita, biashara iliyokuwa ikifanyika katika Mkoa wa Kigoma na Wakongo ilikuwa ni kubwa ukilinganisha na sasa. Kwa nini imepungua? Ni kwa sababu chombo kilichokuwa kinatuunganisha na kilichokuwa kikisaidia usafirishaji wa bidhaa na wafanyabiashara ni meli, hamna kabisa mpaka sasa hivi ni miaka nane katika Ziwa Tanganyika hatuna meli inayo-*operate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuko karibu sana na biashara ili iweze kufanyika ni lazima kuwepo na maboresho ya miundombinu. Ujenzi wa barabara zetu nikianza na kilometa 51 ambayo inaanzia Malagarasi kwenda Uvinza, ambayo sasa inaenda kutuunganisha iweze kutusaidia na kuchochea biashara ya kwenda upande wa Congo kuja Kigoma na hatimaye twende Congo, bado haijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba ili tuweze kufanya biashara hiyo nzuri na Congo na tuweze kufaidika kama nchi, ni lazima miundombinu ya usafirishaji iboreshwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu mazao yetu, bado tunasafirisha nje ya nchi yakiwa ni malighafi. Nianze na zao la kahawa, wakulima kwa miaka mingi wakilalamika na hadi sasa wanalalamika, bei ya zao la kahawa bado ni ndogo. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Wizara yako ndiyo *credo* na taa ya kusaidia wakulima kutatua changamoto hii, tuna *TANTRADE* haijawajibika ipasavyo ili kuweza kutafuta masoko ya uhakika kwa zao hili la kahawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwa Serikali kwamba kwa kuwa miaka yote tumekuwa tukisafirisha malighafi, ninashauri sasa Wizara yako ihangaike usiku na mchana kutafuta masoko ya uhakika na kuzishawishi zile nchi ambazo wananunua zao hili la kahawa, ambazo ni Ujerumani, Japani, China, Marekani na Afrika Kusini; mwalete wajenge viwanda kwenye maeneo ambapo kahawa inazalishwa ili tusafirishe kahawa ambayo tayari imeshaongezewa thamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vijengwe kwenye mikoa ile ambayo inazalisha kahawa. Kwa mfano, ukijenga kiwanda cha kahawa Kigoma, utachukua malighafi ya Mkoa wote wa Kigoma na Katavi. Ukijenga kiwanda cha kuchakata kahawa Moshi, utachukua kahawa yote inayozalishwa Tanga, Manyara, Kilimanjaro na Mara. Ukijenga kiwanda cha kuchakata kahawa katika Mkoa wa Mbeya, utachukua kahawa yote inayozalishwa Mkoa wa Songwe, Rukwa na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, kwanza tutakuwa tumeongeza na tumetengeneza ajira nyingi ndani ya nchi na viwanda hivyo vitatumia umeme huu ambao sasa unaenda kuzalishwa kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, ni kuhusu *gap* au upungufu wa mafuta ya kula, Kigoma tuna zao la chikichi na tuna zao la alizeti ambalo linalimwa nchi nzima, kwa nini hatuoni uchungu? Bado tunaagiza mafuta ya kula nje ya nchi. Tunatumia zaidi ya shilingi bilioni 400 ya fedha za kigeni ambazo tungeweza kutumia kununua mahitaji mengine kama madawa. Bado tunaenda kununua kitu ambacho tunaweza tukazalisha ndani ya nchi. Bado Serikali inahitaji iweke mkakati wa ndani wa kusaidia kuhakikisha uzalishaji wa chikichi na alizeti unaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafuta haya ambayo yanazalishwa, yazalishwe ndani ya kutosheleza na hakuna haja ya kuendelea kununua kutoka nje ya nchi. Tujenge mazingira yaliyo mazuri kwa wawekezaji wa ndani na kwa *SIDO* ili iweze kuandaa mitambo midogo midogo ambayo inaweza ikachakata mazao haya. Tuwajengee uwezo Serikali ijenge uwezo kwa *TEMDO, CAMARTEC, VETA* ili hizi taasisi zote ziweze kusaidia katika

ujenzi wa viwanda vidogo vidogo ambavyo vinaweza kusaidia kuchakata mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nne ni mazingira ya uwekezaji. Bado mazingira ya uwekezaji katika nchi yetu siyo mazuri sana. Ukiongea na wawekezaji wa ndani na hata wa nje watakwambia *barrier* mojawapo ya uwekezaji katika viwanda, hususan ujenzi wake, ni kodi. Mtu ili awekeze kwenye viwanda kikwazo cha kwanza anachokutananacho ni utitiri wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta kuna mamlaka nyingi ambazo zote zinamwendea mwekezaji mmoja kumlipisha kodi pamoja na kumtoza tozo mbalimbali. Ninashauri iundwe mamlaka moja ambayo tayari tunayo *TRA*, iwe ni dirisha moja, mwekezaji akifika, basi malipo yote yafanyike pale, yatengenezwe mazingira ambayo ni mazuri. Tukifanya hivyo, itawezesha wawekezaji wa ndani na wa nje kuja kuwekeza kwenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwepo na biashara nzuri na uwekezaji mzuri wa viwanda ni lazima tuhakikishe miundombinu yetu imeboreshwa. Barabara zetu kutoka vijijini sehemu ambako bidhaa mbalimbali, hususan za kilimo, zinazalishwa ziboreshwe na reli zitengenezwe. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewezesha usafirishaji wa bidhaa na huduma kutoka kwenye maeneo ambapo zinazalishwa kwenda kwenye masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mpango wa kuboresha mazingira mazuri ya biashara Tanzania. Serikali ilikuja na mpango wa *blue print,* ninashauri mpango huo wa Serikali uendelee kusimamia ili kuweza kuweka mazingira bora ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, napendekeza yawepo Mabaraza ya Biashara ngazi ya Wilaya. Kwa sisi tuliopo kule mipakani, wafanyabiashara wadogo wadogo ambao wanafanya biashara na nchi tunazopakananazo kuna shida kubwa sana. Naomba Wenyeviti wa Mabaraza ya Biashara ambao mara nyingi ni Wakuu wa Wilaya wawezeshe kutengeneza mazingira mazuri ili zile biashara za mpakani ziende

vizuri bila kuwa na tozo zisizokuwa na idadi. Tukifanya hivyo, basi uchumi wetu utaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, ni Wizara hii, ili iweze kuleta mapinduzi ya viwanda inahitaji fedha nyingi. Hizi shilingi bilioni 110 ambazo tunaenda kuzipitisha hivi punde ni ndogo. Kwa hiyo, bado jitihada na uhitaji wa fedha nyingi unahitajika, ili tuweze kuleta mapinduzi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kavejuru Felix. Sasa namwita Mheshimiwa Justin Nyamoga, atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga. Mheshimiwa Asia Halamga ajiandae.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi hii. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa nafasi aliyoitoa ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara. Pia natoa shukrani zangu kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi anavyowajibika katika sekta zote, hasa kwa Jimbo langu la Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza Mheshimiwa Rais ameshatoa fedha shilingi milioni 700 kwa ajili ya kununua mitambo ya kusimika kwenye sehemu ya kiwanda cha chai pale Kidabaga. Tayari Bodi ya Chai wamepokea fedha hizo na wapo katika hatua za manunuzi ili kiwanda kile kiweze kufungwa. Hii ni historia wa sababu, kiwanda hiki kina zaidi ya miaka 30 kikiwa gofu, lakini leo kwa juhudi za Mheshimiwa Rais, tunaona mapinduzi makubwa na kiwanda hiki kinaenda kuanza kufanya kazi muda siyo mrefu ujao. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara hii kwa ushirikiano wanautoa katika mambo mbalimbali. Hapa nataja jambo moja, tumekuwa na mazungumzo na

majadiliano kuhusu ujenzi wa Chuo cha *CBE* katika eneo la Kata ya Lugalo, pale Mbigili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi huo kwa sasa tayari ile hati ipo tayari ni Wizara tu kwenda kuichukua. Sisi, kama Halmashauri tumelipia kabisa kwa hiyo, Wizara ni kutia saini tu na kuondoka na hati yao. Namwomba waje tuwakabidhi eneo, ili waanze kujenga chuo kwa sababu, ni muda mrefu tangu mazungumzo haya yameanza.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa, Mheshimiwa Jesca.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hicho Chuo cha *CBE* na *RCC* ya Iringa inakisubiri kwa hamu na tulibariki kwamba kikajengwe hapo. Tunaomba tafadhali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa hiyo, kwa sababu, najua Mheshimiwa Waziri ni msikivu, nina uhakika watakuja ili tuwakabidhi eneo. Sisi tupo tayari kuwakabidhi, hamlipi hata kitu kama Wizara, vyote vinafanywa na Kilolo. Kilolo tumejipanga na tupo tayari kupokea chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoka pale mpaka Iringa Mjini ni kilomita 30 tu kwa hiyo, tumetenga eneo zuri ambalo hata Waziri mwenyewe hapati usumbufu kufika pale. Baada ya kusema hilo narudia tena kuwashukuru kwa sababu, wameonesha ushirikiano mkubwa sana kwenye suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mambo machache ambayo bado nayadai kwenye Wizara hii; Mheshimiwa Waziri pamoja na Ofisi yake. Tumekuwa na mazungumzo kuhusu kiwanda kidogo

cha sukari, hapa mimi naomba nizungumze. Nimesoma kwenye taarifa yao na nimeona hapa wameandika kwamba, kuna kiwanda kidogo cha sukari kinatengenezwa na kikikamilika kitatoa ajira kwa zaidi ya watu 2000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo tupo tayari, kwanza *AMCOS* ya sukari ipo pale. Wale wameunda *AMCOS* na wameandaa mashamba. Mimi nipo tayari kwenda hapo Wizarani ili tupate mbegu na vitu vingine, kwa ajili ya kupanda miwa. Hilo wala siyo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri afanye jambo moja tu. Sisi kama halmashauri tutatafuta fedha, tutaandika hata nusu, shilingi milioni 800. Si ni shilingi bilioni 1.6 hapa, tutaandika tu hata kwa Mheshimiwa Rais, tuna zile 10% nyingi tu zimewekwa pale. Tutaomba watupatie shilingi milioni 800 kwa sababu, watakaotumika kwenye viwanda hivi watakuwa ni vijana, watakuwepo wanawake na hata wenye ulemavu watapewa nafasi. Tutaomba shilingi milioni 800.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Wizara ya Kilimo tutaendanao, tutaomba labda shilingi milioni 400 na wao watupatie 400 tujenge hicho kiwanda pale Kilolo. Ni kazi rahisi na hapo mimi nimetoa zaidi ya nusu. Mheshimiwa Waziri hivi kweli, atakataa ofa nzuri namna hii ambayo haijatolewa na Mheshimiwa Mbunge yeyote tangu tumeanza asubuhi hapa! Mheshimiwa Waziri nakuomba sana kiwanda hicho kijengwe, kiwekwe pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ninavyosema, nimeshajadiliana na Halmashauri yangu na tupo tayari kufanya hilo kwa sababu, Wananchi wa Kata ya Mahenge, Kijiji cha Magana na Kijiji cha Ilindi wana mashamba katika lile bonde lote. Kata ya Mahenge, pale Mgowelo mpaka Nyanzo yenyewe kuna mashamba, lakini hata pale Ruaha Mbuyuni kuna mashamba yameshapimwa na yanafaa, kwa ajili ya kiwanda cha sukari na unajua kuna upungufu wa sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nakupa hiyo *deal,* na kuwekea mezani Mheshimiwa Waziri, naomba tujadiliane

tuikamilishe ili hata mwakani tu tuanze kutoa sukari pale Kilolo. Naamini tutakuwa tumewatendea haki wananchi wa Kilolo kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, hilo lilikuwa jambo langu la pili ambalo naliomba ili kwa kweli tuweze kuona kwamba na sisi tumetendewa haki pale Kilolo kwa sababu, ni sehemu ambayo inaweza kustawisha miwa kwa ajili ya sukari na tayari tafiti zote zimethibitisha hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanayohusu Kilolo ni hayo na la mwisho ni hili la vipimo. Sisi tunauza mazao ya kilimo, mahindi, viazi, njegere, pamoja na mazao mengine, lakini sasa hivi kumekuja huu uuzaji wa kutumia mifuko. Kuna mbinu nyingi sana sasa hivi, kuna mifuko ambayo ni *elastic,* yaani inapanuka, ukijaza inapanuka, kwa hiyo, ukiweka mahindi badala ya kuwa madebe saba sasa hivi ni madebe nane, lakini bei bado inakuwa ni ya gunia kwa sababu, nchi yetu bado inatumia vipimo vya vifungashio badala ya mizani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kutumia vipimo vya vifungashio ni la muda mrefu na sisi tunaotoka kwenye maeneo ya kilimo, wengi tumelalamika muda mrefu, lakini bado tatizo hili lipo na limesababisha kero kubwa sana kwa wananchi. Hivi karibuni nimekuwa nikitumiwa picha za hiyo mifuko ambayo inapanuka, unaona kabisa gunia limekuwa nene kuliko ule unene wa kawaida, lakini wale wafanyabiashara ni mbinu ambayo wameibuni kuepuka lumbesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hivi siyo lumbesa tena ni ule mfuko tu wenyewe unakuwa *elastic,* unanenepa, badala ya lumbesa. Kwa hiyo, hutaona kwamba ni lumbesa, lakini kimsingi ukiliangalia lile gunia unajua kabisa hili siyo gunia la kawaida. Sasa wakipita kwenye mizani wanasema hii siyo lumbesa, lakini kimsingi bado tatizo hilo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi najiuliza, hii nchi tumeshindwa nini kuweka utaratibu wa kutumia vipimo katika kuuza bidhaa zetu? Kwa sababu, huo ndiyo ukombozi wa wakulima. Kama kilo ni shilingi 300, basi ni shilingi 300, au kama ni shilingi 500 basi ni shilingi 500, lakini kutumia ujazo haijawahi kuwa kawaida. Ninyi mnanunua vitunguu huko njiani, mnaona zile ndoo, unamimina,

inabidi uchungulie kule chini kwa sababu lazima pale kumewekwa angalau kisimenti kidogo ili vitunguu viwe vichache kwa sababu, tunatumia hivi vipimo ambavyo ni vipimo vya vifungashio badala ya kutumia vipimo vya mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni wakati wa kuleta mapinduzi katika nchi yetu, kwamba, utaratibu tunaokuwanao uwe ni ule wa kutumia vipimo vya uzito badala ya vipimo ambavyo vinamnyonya mkulima, vinamuumiza mkulima, vipimo ambavyo havimpi faida mkulima ambaye anakuwa ameteseka kwa muda mrefu katika kuhakikisha anapata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu ubunifu unaofanywa na muunganiko. Tumeona hapa kwamba, *TEMDO* wanatengeneza vifaatiba, vitanda kwa ajili ya *maternity* vinatengenezwa pale. Nadhani changamoto ni kwamba, wakishatengeneza kwanza mtaji ni mdogo, kwa hiyo, utengenezaji wao ni vitanda viwili, vitatu na tumeona sehemu vinakoenda, tunashukuru na tunapongeza ubunifu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri sasa ni wakati muafaka wa kutafuta namna bora ya ku-*mobilize* viwanda. Hapa, nimerudi kule, tuzungumze kwenye kuona je, hakuna Halamshauri yenye kipato kikubwa inayoweza kuwekeza kwenye viwanda kwa kutumia hizi 10% kwa mfano, lakini tuone pia, ni jinsi gani tunaweza tukawavutia wawekezaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvutia wawekezaji kutakuja hivi, hawezi kuchukua hii teknolojia ya *TEMDO* kama hana uhakika wa soko. Kwa hiyo, inabidi Wizara ya Afya iingie mkataba na huyu mwekezaji kwamba, vitu vitakavyotengenezwa atavinunua ili viweze kuzalishwa ndani na awe na uhakika wa lile soko.

Kwa hiyo, naomba hapo tusije tukaishia kwenye kutengeneza vitanda au bidhaa mbili tatu, tutafute namna ya kufanya *scale up* ambayo nina uhakika *TEMDO* hawezi kufanya. Ni lazima ile teknolojia ihamie kwenye viwanda ili vile viwanda viweze kuzalisha, tuweze kupata bidhaa nyingi za ndani ambazo sasa tukizitumia tutaona tunapata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina mengi, nina uhakika Wizara imesikia, maombi yangu siyo mengi. Chuo chetu cha *CBE* kijengwe, lakini pia, ofa yangu ya kiwanda cha sukari imesikika na Bunge zima na nimeona kabisa kwamba, Wizara imepokea. Nina hakika wakati wa majibu pengine nitajibiwa kabisa kwamba, hicho tayari kimeshapelekwa Kilolo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Justin Nyamoga. Nilimtaja Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa Asia Hamlaga na Mheshimiwa Benaya Kapinga wajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi nami kuchangia Wizara ya Viwanda na Biashara. Kwa kweli, naanza kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayofanya katika maendeleo ya nchi yetu na mojawapo ikiwa ni katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi kwa kweli, tunamwona Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Rais na viongozi wengine mbalimbali wakizunguka duniani huko kutafuta fursa za uwekezaji katika kukuza sekta ya Viwanda na Biashara. Nataka kukiri hapa mbele yako kwamba, Mheshimiwa Waziri wetu wa Viwanda na Biashara ni mtu rahimu, mama mzuri kabisa sina nongwa naye, sina shida naye. Amekuja mpaka Kilombero, porini kule kwetu, amefika Mang'ula, amesikiliza hoja yangu ambayo kwa kweli leo nataka kusema hapa, ndiyo miongoni mwa vitu vilivyonisukuma kuchangia kuhusu kufufuliwa kwa Kiwanda cha Mang'ula *Machine Tools*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Rais, na Serikali ya Awamu ya Sita amefufua baadhi ya viwanda kikiwemo *Kilimanjaro Machine Tools,* na sisi Kilombero tulikuwa tuna ajenda ya kufufua *Mang'ula Machine Tools*. Kiwanda hiki ni muhimu sana katika nchi yetu, wazee wetu wa zamani wanajua

umuhimu wa kiwanda hiki katika mchango wa nchi yetu, kwa Taifa, ajira na kadhalika na Mheshimiwa Waziri amefika pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nafikiri Mheshimiwa Waziri kwa urahimu wako huo, baadaye unipe ufafanuzi wa kina wa ni namna gani kiwanda hiki kinafufuliwa na kinafufuliwa lini? Kwa sababu, wataalamu wameshakuja wengi pale na Kamati ya Usalama ya Wilaya chini ya Wakili Msomi Dunstan Kyobya, Mkuu wetu wa Wilaya, tulitembelea pale tukaona baadhi ya vitu vinavyozidi kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba zilizopo pale zinaharibika mapaa, zimeendelea kuwa magofu. Kuna watu wanakaa mle, hata hatujui ni nani anakusanya kodi. Kuna vyuma vimeharibika, kuna mashine mle hata *oil* haziwekwi, zinazidi kuharibika, watu wanaondoka na miundombinu. Kuna ulinzi, lakini bado siyo wa kutosha, kuna mapori, nyoka wanafugwa pale, lakini Diwani alituambia kwamba,kuna ubakaji unaendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kweli, napenda kukiomba Chama changu cha Mapinduzi kinisamehe endapo nitashika shilingi ya Mheshimiwa Waziri. Nilikuwa napima kati ya kura za CCM na Mheshimiwa Rais katika Serikali za Mitaa pale Mwaya na Tarafa ya Mang'ula Kona na kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri, kipi ni kizito zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikagundua kura za CCM ni nzito zaidi, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kama hujanipa ufafanuzi nafikiria kushika shilingi yako. Nafanya kwa urahimu tu kwa sababu mwalimu wangu wa Kiswahili, Joram Nkumbi, anasema maendeleo na viwanda na biashara ni sako kwa bako, ni chanda na pete. Hivi vitu haviachani, kwa hiyo, nina nia hiyo Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani wananchi wangu wa Tarafa ya Mang'ula leo wanasikiliza. Waliniambia, wewe ulipoenda walikuzunguka pale ukaongea kwa nia nzuri. Sasa hebu Mheshimiwa Mbunge sema tukusikie umesema ili nongwa za Tarafa ya Mang'ula Kata ya Mwaya, Kata ya Kisawasawa,

Mangu'la A, Mang'ula B, wasikie ili waweze kuona kwamba, nimelifikisha jambo hilo vizuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo la kwanza. Mheshimiwa Waziri nisaidie mdogo wako nami ninusurike na Serikali za Mitaa na mwakani kwa jambo la kiwanda. Kilombero tumeshafanya mengi sana chini ya Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mengi kweli kweli, lakini hili limebaki nongwa kwa sababu vitu vinaharibika. Nafikiri pale kuna nyumba hata zaidi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikirudisha kile kiwanda Serikalini kutoka kwa mwekezaji. Kinamilikiwa na Serikali, lakini ni kwanini uwekezaji haufanyiki na hakifufuliwi kama wenzetu wa Kilimanjaro ambao *Kilimanjaro Mashine Tools* imeanza kuzalisha? Kwa hiyo, naomba kusisitiza sana kuhusu Mang'ula *machine tools*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri la pili ni *economics* ambayo mimi nimesoma diploma na degree kidogo, mwalimu wetu mmoja alikuwa anasoma Chuo cha *IFM* alikuwa anatuambia, katika maendeleo ya nchi *importation* na *exportation* ni vitu muhimu sana. Anasema uingizaji wa bidhaa ndani ya nchi na utoaji wa bidhaa nje ya nchi ni picha ya nchi ambazo zimeendelea, inatoa bidhaa zake nyingi nje kuuza kuliko inazoingiza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi zinazoendelea, ili tuendelee ni lazima tuwe na mkakati wa kina wa kupunguza *importation* na kuongeza *exportation* hata kwa kuwa na bidhaa chache kama 100. Zipo nchi hapa ukipeleka kitu chako kitapigwa kodi, ili ku-*discourage,* ili kukufifisha usipeleke hiyo bidhaa kwa kulinda soko la ndani. Sasa nimesoma na nimepitia bajeti yako, hatuwezi kushika yote, Mwalimu wangu wa uchumi Mheshimiwa Dkt. Mwigulu anajua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bidhaa chache tukiweka mkakati wa kuzizalisha wenyewe tutapunguza *importation* na kuna bidhaa ambazo tukiweka wawekezaji, tukiwahamasisha wawekezaji, tutaweza kupunguza kuchukua pesa zetu nyingi

kupeleka nje. Mimi nataka kutoa mfano leo kwenye hotuba yako kwenye mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema nchi yetu inahitaji tani 600,000 za mafuta ya kula. Mpaka leo tumeshindwa kuwa na mbegu za kutosha za kuzalisha mafuta ya kula, tuna upungufu wa tani 395,000 za mafuta ya kula. Mheshimiwa Waziri tangazieni dunia huko tunakonunua mafuta ya kula, mwekezaji yeyote akija Tanzania anaweza kuzalisha hizo tani 300,000. Tuna upungufu wa tani 395,000 anaweza kuzalisha tani 300,000 tumpe ardhi, tumpe vimisamaha vyote azalishe tani 300,000, tutapunguza fedha za kwenda kununua mafuta ya kula nje. Sasa leo umeandika kwenye hotuba yako, Mheshimiwa Waziri, viwanda vyote tulivyokuwanavyo, sijui mia saba na ngapi, havina mbegu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, watu wamewekeza kwenye viwanda, mbegu hakuna, na inaweza ikachukua zaidi ya miaka kumi. Tangazia dunia kwamba jamani anayeweza kuwekeza hata tani laki moja za mafuta ya kula hapa tunamtaka. Kesho utapata watu hapa watakuja wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni bodaboda. Tumeenda katika nchi moja *East Africa* hapa, wamekubaliana nchi nzima bodaboda ziko za aina moja. Kuna bodaboda (pikipiki) za mafuta na kuna pikipiki za kuchaji. Tulienda na baadhi ya Wabunge, nikauliza kwa nini nchi nzima hapa naona pikipiki fulani za Honda tu peke yake? Wakasema haya ni makubaliano ya nchi na nchi hiyo yenye kiwanda. Wana-*assemble* pale, pikipiki thamani yake ni kama milioni moja na laki mbili kwa sababu wamekubaliana, wamewekeza katika bodaboda ambazo zinaajiri vijana wetu wengi na sisi baada ya mafuta ya kula, twende kwenye pikipiki ambazo kila siku vijana wetu wananunua na sisi tunaombwa tununue pikipiki kwa vijana wetu kama ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubalianeni na watu waje wawekeze kiwanda hapa na kiwanda tunamaanisha, mashine ya kutengeneza injini ya pikipiki, mashine ya kutengeneza *mudguard* na mashine ya kutengeneza tairi kwa sababu raba tunayo, chuma tunacho, yaani *full* nondo yaani mashine ianze hapa,

mashine ina-*assemble* injini mpaka taa za kuwaka zile zinaweza zikatengenezwa hapa. Hiyo ndiyo itakuwa *full* kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika ile ile habari ya kusema *importation* na *exportation*, tazama mwaka 2022 na 2023 umesema nchi za Ulaya, *East Africa* na *Asia,* tuweke mkakati wa kudumu na *Asia*. Mheshimiwa Waziri, angalia umetuandikia mwaka 2023 tumeuza Asia vitu vyenye thamani ya shilingi trilioni 7.4 na 2022 tumeuza shilingi trilioni 10. Kununua; 2023 tumenunua shilingi trilioni 21 na mwaka 2022 shilingi trilioni 23. Hiyo ni *Asia* peke yake na ukiangalia mle ndani umesema India, China na *United Arab Emirates,* hawa Wachina wanachukua karibu hii 80%. Tukae nao tuzungumze nao, Mheshimiwa Waziri, China mbali, nimeenda China na Mheshimiwa Spika kanipeleka China. China mbali, mtu anatengeneza pikipiki anaisafirisha mpaka Tanzania na anauza kwa faida. Tukiweka mazingira mazuri, huyo anayetengeneza pikipiki kule na soko lote lililokuwepo hapa Tanzania na *East Africa* hawezi kuweka hata kiwanda kidogo hapa ili tukapunguza hii *deficit* ya China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti yetu shilingi trilioni 40, kama tunafanya biashara ya shilingi trilioni 21 na Asia peke yake na ambayo China wanachukua *80%* bara kubwa. Sasa lakini kule China tulivyozunguka vile viwanda vilikuwa vya namna gani? Akina bibi wamekaa wana-*assemble* miamvuli. Mheshimiwa Waziri Simbachawene, akina bibi wamekaa wanafungafunga miamvuli mpaka kule mwisho wanaiweka kwenye *nylon* wanai-*assemble* kwenye maboksi inakuja Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeenda kwenye viatu wanakusanyakusanya ngozi, huyu anagonga msumari Ngozi, kiatu kinaenda kule, mwisho kina-*assemble* kwenye maboksi kiatu kinatoka. Pia, mifuko hii ya kuweka, mtoto kule kaanza bibi yuko huku, mmoja kazi yake ni kusogeza tu, viwanda vya kawaida kabisa. Kwa hiyo, kuwaambia wenzetu Wachina, tuna urafiki nao mzuri, acheni hiyo biashara ya kusafirisha makontena kwenye maji huko, njooni hapa kuna eneo hapa *business park* mtapata msamaha fulani mwekeze hapa tuwe na bidhaa chache tunazoweza kuanza nazo kama bidhaa za msingi katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaingiza kijiti cha kuchokonolea meno sijui kwa Kingereza mnaitaje?

**MBUNGE FULANI:** *Tooth pick.*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *tooth pick*, nini? Mimi Mswahili; ya kuchokonolea masikio, yakuchokonolea pua, kitana, soksi, kiatu, kila kitu tunaingiza tu. Tuseme bidhaa hizi 1,000 Tanzania *importation* marufuku. Hatuwezi kuingia katika dunia ya *globalization* tunaachia tu, Mwalimu Nyerere alisema sisi tunaachia tu tunafungua madirisha wanaingia mbu, panya na kadhalika, lazima tuwe na vipaumbele, bidhaa chache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu wangu wa *economics* wa *diploma* na *degree* alinifundisha lazima tuseme bidhaa chache katika nchi ya Tanzania ukiziingiza utatandikwa kodi, hutaingiza. Nasi tuchukue bidhaa zetu kama hizo za chakula kule kwangu, Mheshimiwa unajua kunalimwa mpunga, lakini mpaka leo wananchi wanauza mpunga kama mpunga. Watu wanatoka India wanakuja kununua mpunga. Sasa wanaenda kuuchakata huko Dar es Salaam sijui wapi, mashine za kisasa wangeleta pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna shida ya mashine ya kukausha mpunga, bado tunataandika majamvi tunaanika mpunga kwa kutegemea jua. Wakulima wetu hawawezi kuingiza mashine za kukausha mpunga? Haya, hao wawekezaji wa hizo mashine waje waone soko watuuzie hizo mashine, wazitengenezee hapa hapa, wakulima wetu waweze kusindika mpunga ule unaonunuliwa India kwenye *packet supermarket* utoke hapa moja kwa moja. Hiyo ndiyo *exportation* unayosema. Sasa mimi nimesema kwa uchache kwa sababu kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu namwona pale, yeye ni mtaalamu wa uchumi atakuja kufafanua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Waziri kapewa bajeti 38% ya pesa zilizotengwa, sasa huyu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Waziri wa Fedha tutamuua bure hapa kwa sababu kila ukienda kwenye

Wizara kuna shida kwa sababu ya miradi mikubwa tunayofanya. Ni muhimu kupanga kutokana na tunachokusanya kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakari Asenga. Sasa namwita Mheshimiwa Zacharius Kamonga, Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu wajiandae.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wa bajeti yake kwa umahiri mkubwa. Nina imani umahiri huo utakwenda mpaka kwenye utekelezaji wa miradi ile ya Mchuchuma na Liganga. Hali kadhalika, niungane na Wabunge wengine kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuonesha dhamira yake ya dhati kwamba sasa miradi ile iweze kukwamuliwa, Mradi wa Mchuchuma na Liganga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokiomba tu ni kwamba yale majadiliano hatua yalipofikia, Wizara ingeangalia *multiply effects* waangalie manufaa ambayo nchi yetu inaweza kupata kutokana na kuanza kwa miradi hii. Kuna ajira nyingi pale za vijana, lakini tutaokoa fedha nyingi sana za kigeni kuagiza chuma nje ya nchi. Wanachoomba tu wananchi wa Ludewa ni viwanda, kipaumbele cha kujenga viwanda kiwekwe Ludewa. Kiwanda cha Chuma kijengwe pale Liganga kama ambavyo mpango ulikuwa toka awali na mambo mengine pia yaweze kufanyika eneo ambapo malighafi inapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuishukuru sana Serikali kwa kuwalipa fidia wananchi wale kiasi cha shilingi bilioni 15.4. Imekuwa ni upendo mkubwa kwa wananchi wale, imewapa moyo na faraja kubwa, wanaamini kwamba Serikali iko nao sambamba na wako tayari kuendelea kuiunga mkono Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wananchi wa Mundindi baada ya kulipwa zile fidia kiasi cha shilingi milioni 800 na pointi

walikaa mkutano wa Serikali ya Kijiji, wakakaa mkutano wananchi wote wa kijiji wakaazimia kwenye ile fedha ambayo walilipwa kwenye mashamba ya kijiji wakaenda kununua *bond* kwenye Benki ya CRDB, Kijani Bond. Fedha ile imeshaanza kuzaa, wamevuna awamu ya kwanza shilingi milioni 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, fedha hiyo, wameitumia katika kuwalipia bima wananchi wa kijiji hicho wasiopungua 3,000, kila mwananchi atalipiwa bima lakini chanzo ni fidia hii ya eneo la Liganga na Mchuchuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika wakiendelea kuvuna wanakusudia kukarabati shule za msingi kwenye kijiji hiki, lakini wananchi wengine mmoja mmoja nao wameweza kutokana na elimu ambayo tuliwapa fedha hizi wamezitumia kwa manufaa makubwa sana. Niliona nilisemee hili la Mundindi ambao wamenunua *bond CRDB* kwa sababu ni kitu ambacho ni cha kipekee. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Diwani wa Kata ile Mheshimiwa Wise Mgina na viongozi wote wa vijiji kwa maono, halikadhalika halmashauri na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Mtaka kwa kuweza kulisimamia jambo hili vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pale Liganga kulikuwa na miradi miwili, kulikuwa na mradi ulikuwa unaitwa Kasi Mpya na kulikuwa na ule *Main Liganga* ambao ni wa Mchina. Sasa ule mradi mdogo kuna mwekezaji mdogo ambaye ana viwanda huko Mkuranga Mkoa wa Pwani anatumia chuma chakavu. Chuma chakavu sasa hivi imekuwa ni adimu sana kupata, alikuwa anatarajia awekeze pale Viwanda Ludewa kwenye ile Liganga ndogo lakini bahati mbaya majadiliano nayo yamechukua muda mrefu sana. Imechukua siyo chini ya miaka miwili, mitatu kujadiliana naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kulikuwa na Azimio la Baraza la Mawaziri ambalo ikawa inahitajika tena hii *negotiation* na huyu mwekezaji irudi tena huko kwa maamuzi. Nisingependa kusema ni majadiliano gani, lakini namwomba sana Mheshimiwa Waziri, basi aharakishe hii ili mradi ule nao uweze kuanza. Kwa sababu ikianza tu ile Liganga ndogo tayari pale tutatoka jasho,

pato la Taifa litaongezeka, tutaokoa dola nyingi ambazo tunatumia kuagiza chuma nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali inakusudia kujenga reli kutoka Mtwara – *Mbamba bay*, tawi la Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo, chuma kitakachotoka pale kinaweza kikaokoa dola ambazo tunaagiza chuma nje ya nchi. Halikadhalika, tunavyozungumza *agenda* ya viwanda hapa nchini itakuwa na manufaa makubwa iwapo kutakuwa na malighafi, kutakuwa na chuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la Maganga Matitu kulikuwa na wananchi ambao walifanyiwa uthamini walikuwa bado hawajalipwa. Sasa wanavyoona wenzao wanapata bima za afya, wananunua matrekta, wananunua magari, wao bado, wameniomba mimi Mbunge wao nije niwasemee ili Mheshimiwa Waziri aweze kusimamia jambo hili ili nao wao walipwe kwa sababu fedha siyo nyingi kama ya mwanzo. Wana imani kwamba kama Mheshimiwa Rais aliweza kulipa shilingi bilioni 15 na hizi bilioni chache haziwezi kumpa shida. Kwa hiyo, naomba sana wale wananchi wa eneo la Maganga Matitu waweze kulipwa fidia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kuna lile eneo la makaa ya mawe kule Mchuchuma Kijiji cha Nkomang'ombe kuna wale wananchi wa eneo la Ketewaka ambao nao walifanyiwa uthamini fedha siyo nyingi kama za mwanzo, nao wana imani kama Mheshimiwa Rais aliweza kulipa shilingi bilioni 15 wana imani nao wanaweza kwenda kulipwa fidia hizi mapema sana ili nao waweze kufanyia shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu pia niweze kutoa pole kwa wale wananchi wa Kitongoji cha Mhumbi jirani sana na mradi huu wa Ketewaka. Waliona maji kutoka kwenye chanzo chao yanatoka machafu kama siku tatu, leo walikwenda eneo hilo kukagua kuona kwa nini maji yanakuwa machafu. Sasa walipofika huko wakaona ule mlima una ufa unaitwa Mlima Mhumbi, una ufa mkubwa halafu unatoa kelele (sauti). Sasa wale wananchi kwa sababu ni tukio ambalo hawajawahi kuliona hawajalizoea wakakimbia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeweza kuwasiliana na watu wa *GST* watatuma wataalamu ila tu wameshauri wananchi wasisogee eneo hilo wachukue tahadhari, kwa sababu wanasema tayari eneo kama la ekari moja pametokea maporomoko ya ardhi, lakini pia ule mlima unavyotoa kelele kunakuwa kama na matope. Sasa hatuna uhakika kama ni *volcanic activity* au *mass wasting* au nini, lakini wataalamu wameahidi kwenda. Eneo liko jirani sana na eneo hilo la wananchi ambalo wanadai fidia. Ni wananchi wa Kitongoji hiki cha Mhumbi ndio ambao wanadai fidia za eneo la Ketewaka, kwa hiyo, niombe hawa waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Wizara hii ilichukua *agenda* ya barabara wakati wa majadiliano na mwekezaji, ile barabara inayoanzia Mkiu - Liganga kwenda Madaba na barabara inayounganisha Liganga na Mchuchuma kilometa 70 na kile kipande cha kutoka Mawengi. Zipo barabara ambazo mwekezaji angetoa fedha ziweze kujengwa kwa kiwango cha zege. Kama hili litafanikiwa kwenye hayo majadiliano, nina imani litakuwa limerahisisha sana shughuli za uchukuzi na usafirishaji wa maeneo haya. Uwekezaji huwa unaenda sambamba na barabara bora za maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, machache, nishukuru sana kwa kupewa nafasi, nipongeze sana Wizara hii kwa kazi nzuri na naomba fidia zile kwa wananchi wachache waweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zacharius Kamonga. Nilimtaja Mheshimiwa Asia Halamga, Mheshimiwa Benaya Kapinga na Mheshimiwa Jesca Msambatavangu wajiandae.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizi zaidi ya shilingi bilioni 15 kwa ajili ya kulipa fidia kwa ule mradi wa Liganga na Mchuchuma. Tunamshukuru sana Rais, Mama amekuwa ni mwema, hapigi kelele, lakini kazi inayofanyika ni kubwa sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo za Mheshimiwa Rais, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. Ashatu Kijaji kwa kazi kubwa ambayo unaifanya katika Wizara hii. Niendelee kuwapongeza wananchi wako wa Kondoa Vijijini na hata pale walipokuita jina la Kamsese hawajakosea. Nani kweli, ni kamsese. Ila bila kusahau nitoe pongezi kwa Naibu wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye mchango wangu. Nimejaribu kuangalia Taarifa ya Wizara wakati Waziri anaisoma lakini pia nimejaribu kuangalia Taarifa ya Kamati. Nilitamani kuona jambo moja ambalo nakumbuka tarehe 13/4/2023 kwenye mchango wangu wa Wizara hii nilileta jambo mahususi jambo la Matrekta ya *Ursus*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kiti chako na naomba unifikishie salamu za wananchi kwa Mheshimiwa Spika wa Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, baada ya kutoa mchango ule wa kero ya Matrekta ya *Ursus,* Mheshimiwa Spika aliamua Kamati ya Bunge iweze kwenda Manyara na baadhi ya maeneo ili kukutana na wakulima na kuona changamoto hiyo. Hakika tunamshukuru sana Spika wetu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwatendea wananchi na wakulima wa Tanzania haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati, Mheshimiwa Spika alitoa maelekezo hapa kwamba Serikali ije na hitimisho la jambo hili. Kwa namna ya kipekee kabisa na kwa namna ambavyo ninamfahamu Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, mama na jirani yetu watu wa Manyara na Hanang ninaamini utakapokuwa unahitimisha bajeti yako utasema neno ili roho za Wakulima wa Tanzania ambao walipata hasara kupitia Matrekta ya *Ursus* na

kwa sababu wanamjua Rais wao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mama mlezi, ni mama asiyependa uonevu, ni mama ambaye anataka Watanzania waende mbele na hususan wakulima hawa ambao haki yao ilipotea kupitia Matrekta ambayo kwa kweli yamewatia hasara kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atasema neno ili wakulima wale wapone na walale usingizi ambao hawajalala kwa miaka kadhaa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati naendelea kufuatilia hili zipo tetesi kwamba kuna dalili njema ya tamko la Rais na kwa sababu Mheshimiwa Waziri yupo na tetesi hizo wakati nikifuatilia baadhi ya wakulima wameshaanza kupigiwa simu kutakiwa taarifa ya kile ambacho wamekipoteza. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, ahsante sana Serikali ya Awamu ya Sita, ahsante Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwasikiliza Wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili, nihitimishie hapo kwa sababu najua Mheshimiwa Waziri utakuja kuitoa kauli ambayo sasa wakulima wataisikiliza na watakuwa na kauli moja na kuachana na ubabaishaji wa simu tofauti tofauti na watapata maelekezo sahihi ya Rais wao mwema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwenye hilo naomba kuhitimisha hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niingie sehemu ya pili. Nchi yetu ina vijana wengi sana ambao wengi wao hawana ajira na Serikali yetu kimsingi kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Mama msikivu ameendelea kuhakikisha kila kunapokucha anaendelea kutoa fedha kwenye Wizara tofauti tofauti kwa ajili ya kutanua maendeleo ambayo yanaweza kusaidia vijana wengi kuja kuajirika. Kwenye hili naendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linaweza kutatua changamoto ya ajira kwa vijana wengi wasomi na ambao hawajasoma sana ni viwanda. Viwanda vikifufuliwa katika nchi yetu na niendelee kuipongeza Serikali kwa kuendelea kufufua viwanda, lakini bado tunatakiwa tuongeze *speed* kubwa ili

tuweze kufufua viwanda vingi ili kuweza kuzalisha na kutoa ajira kwa vijana wengi wa Kitanzania, wale wasomi na wale ambao hawajafanikiwa kusoma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku chache niliuliza swali na bahati nzuri lilijibiwa na Naibu Waziri wa Madini. Natolea mfano kwa eneo ambalo ninatoka. Mimi natokea Manyara Wilaya ya Hanang'. Wilaya ya Hanang' inayo chumvi ya kutosha ambayo inaweza kulisha ndani ya nchi pamoja na nje ya nchi na tukaingiza fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo kama Gendabi, Dawar, Balangdalalu Wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara ipo chumvi ya kutosha. Ukienda Babati Vijijini ipo chumvi ya kutosha. Kwa maeneo kama Gendabi kwa mwaka mmoja inazalishwa zaidi ya tani 85,000 na huo ni uchimbaji wa kawaida wa kienyeji kabisa wa kutumia mikono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Manyara, Singida na hapa Dodoma bado tunahitaji viwanda vingi ili kuweza kuwasaidia ajira vijana wa maeneo hayo na vijana wa Kitanzania. Mheshimiwa Waziri, naomba sana ile chumvi ya Hanang' isipotee hivi. Tunahitaji kiwanda, tunaomba tusaidiwe wawekezaji wakubwa, tunaomba mwasaidie wawekezaji wetu wa ndani wadogowadogo namna ya kutoka na kuweza kuzalisha chumvi ile kwa uhakika na ukubwa, kutoa ajira na kujipatia fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kilichopo Hanang' ni mali, kile kilichopo Manyara ni mali inayoweza kutanua ajira kwa watu wengi na hasa ukizingatia Manyara hatuna viwanda vya kutosha. Wananchi ni wengi, vijana ni wengi, akina mama ni wengi, tunaomba sana utuangalie katika suala la uwekezaji wa viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee kabisa niendelee kuiomba Serikali kuendelea kuwekeza kwenye kiwanda cha Minjingu ili kuhakikisha kwamba mbegu za wakulima wanazopanda zinakwenda kupata mbolea bora inayotokea hapa nchini na kutakuwa hakuna upungufu ili tuweze kulima kilimo chenye tija

kitakachokidhi mahitaji ya ndani pia kitakachokidhi mahitaji ya nje ili tuweze kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kiwanda cha Minjingu, kipo Kiwanda cha Mbolea cha *ITRACOM* hapa Dodoma, tuiombe Serikali iendelee kuangalia viwanda hivi kwa sababu vinatoa ajira kubwa kwa wananchi na vinao uwezo wa kutusaidia kupata mazao bora ambayo yatakidhi nchi na hadi nje kwa ajili ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo gesi asilia kule Mtwara. Hii ni tunu na bahati kubwa ambayo Mwenyezi Mungu ametubariki sisi Watanzania, lakini hakutubariki ili ikae tu ardhini, ametubariki ili tukiitumia katika matumizi sahihi na mapana yanaweza kuwa ni suluhisho la kugawa ajira kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile gesi asilia tunao uwezo wa kuitumia pia katika kutengeneza mbolea ya *urea*. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana kupitia Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kufanya uwekezaji katika mbolea na hasa kwa rasilimali hiyo kubwa ambayo inatoka Mtwara, Mwenyezi Mungu ametugawia kwa ajili ya nishati lakini tuna uwezo wa kuitumia kwa matumizi zaidi na ikaweza kuleta tija katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kumekuwa na mlolongo mkubwa wa kodi, Serikali imejitahidi sana kuendelea kupunguza kodi katika nchi yetu, bado niendelee kuiomba Wizara iendelee kufanya kazi kubwa ili kurahisisha mazingira mazuri ya wawekezaji wakubwa pia wawekezaji wetu wa ndani waweze kuwa ni sehemu ya kuvutiwa na upunguzwaji huo wa kodi ili waendelee kuwekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa juu una matarajio makubwa sana, mipango yako ni mizuri sana, unakutana na wafanyabiashara mara kadhaa tunakuona lakini bado una kazi ya kuwaambia watu wako wa chini waweze kujua changamoto zinazowakuta wafanyabiashara wadogo wadogo kwenye maeneo yao ili kuanza kutatua pia twende sambamba na huku juu katika ngazi ya Taifa ambapo unajua changamoto za wafanyabiashara wako wakubwa tofauti na kule wa ngazi ya

chini. Waendelee kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara wa ndani ambao siyo rahisi kukufuata hapa Dodoma kila mara lakini wapo wasimamizi wako kule chini, tunaomba wakae na wafanyabiashara katika mazingira ya kujua faida zao lakini pia kujua changamoto zao.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asia Halamga. Nilimwita Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu na Mheshimiwa Vedastus Manyinyi wajiandae.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Wataalam, kwa kweli wanafanya kazi nzuri katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa ili niweze kuchangia kwenye maeneo matatu na muda ukiniruhusu ni manne. Kwanza ni ombi, nilizungumza hapa mwaka 2023 kuhusu ombi la kiwanda. Nchi yetu hii imebarikiwa sana kuwa na malighafi nyingi za viwanda. Sifa mojawapo ya mtu kupeleka kiwanda sehemu ni pamoja na kupatikana kwa malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mbinga tunamshukuru Mungu, tunazo malighafi za kutosha. Tunazo malighafi kwenye kilimo kwa sababu tunazalisha vizuri sana mahindi, kahawa pia tunazalisha mazao mengine kama parachichi na karanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo bahati sana sasa hivi tunayo makaa ya mawe, zote hizi ni sifa za mtu kupeleka kiwanda katika eneo hilo. Niliomba mwaka 2023 kwamba tunaomba

kiwanda. Pale tuna viwanda vya kubangua kahawa, tuna viwanda viwili vina-*roast* kahawa kwa bahati mbaya hatupati ile kahawa ya mwisho kabisa *finest,* hatuipati. Ili tuipate ile Kahawa inachukuliwa inapelekwa Bukoba. Tunashukuru Bukoba ni sehemu ya nchi hii lakini ingependeza sana nasi pale Mbinga tungepata kiwanda cha aina hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kiwanda kikiwepo mahali husika wananchi wanapata ajira, lakini hata ile malighafi yenyewe tunaiongezea thamani, badala ya kuuza kwa namna tunavyouza sasa hivi, tungeuza kwa gharama zaidi na bei nzuri zaidi. Kwa hiyo, naiomba Wizara, najua Mheshimiwa Waziri halali anazunguka huko duniani. Pia, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, pale anapofanya ziara za namna hii ni lazima amchukue Waziri wa Viwanda na wanatembea kuzunguka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri huko unapokwenda, basi ututafutie kiwanda. Tutafutie kiwanda kwenye kahawa na kwenye mahindi kwa sababu najua tukiuza unga tutapata fedha zaidi kuliko tunapouza mahindi yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukitembea kule kwenye upande wanaochimba makaa ya mawe, wanasema waliwahi kuahidiwa kwamba watapelekewa kiwanda. Sasa kila nikipita huwa wananikumbusha hilo. Naomba nalo kwa sababu tuna makaa ya mawe mengi sana kiasi kwamba kuyapeleka tu huku hatutayamaliza, kwa hiyo, tupelekewe kiwanda pale ili wananchi hawa wanufaike na uwepo wa rasilimali za malighafi hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia leo ni mradi huu wa siku nyingi wa Liganga na Mchuchuma. Nilizungumza hapa mwaka 2023, lakini niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita kwa nia ya dhati kabisa kutenga hizi fedha shilingi bilioni 15.3 kwa ajili ya kulipa fidia. Hii ni nia thabiti kabisa ya kwamba Serikali hii ina lengo na mradi huu uweze kuendelea. Sasa umechukua muda kidogo toka walipe, mimi binafsi nilidhani kasi ile ingeendelea lakini inaonekana kuna maneno maneno yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara kwenye maneno haya tuyamalize. Mradi huu una historia ya siku nyingi mno.

Liganga, liganga lakini kwa kulipa hizi fedha tunadhihirisha kabisa Serikali yetu ya Awamu ya Sita iko tayari mradi huu uanze lakini sasa kwa kasi gani? Tunaomba sana mmalize huo mgogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maneno kwamba mwekezaji aliyekuwepo hayupo duniani, sina hakika, kama ni kweli basi tuyamalize haya maneno ili mradi huu uchukue kasi na Tanzania yetu inufaike na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata shida sasa hivi unaweza kuona tunaagiza chuma kutoka nje, kumbe Mungu ametujalia nchi hii tuna chuma hapa hapa. Kwa hiyo, mradi huu ukianza maana yake hatutaagiza chuma kutoka nje, tutachota pale, tunazalisha. Vivyo hivyo, itapelekea viwanda vyetu vizalishe malighafi katika nchi yetu isiwe juu. Sasa hivi tunapata shida bei ya bati iko juu, bei ya nondo iko juu, kumbe sasa kupitia malighafi tuliyokuwa nayo hapa, bidhaa hizi zitashuka bei. Nakuomba sana jambo hili tuende nalo kwa kasi kidogo ili liweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ningependa kuizungumzia na ambayo Mheshimiwa Waziri na Kamati wameizungumzia ni suala hili la stakabadhi za ghala. Tanzania ni wakulima ili twende vizuri ni lazima tufanye huu mkakati na mpango huu wa stakabadhi za ghala, kwa sababu ununuaji wa mazao holela mara nyingi hauwezi kumnufaisha mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna stakabadhi ya ghala ilivyo sasa hivi, kila mtu angependa kwenye eneo lake tuwe na hii stakabadhi ya ghala japo hatujafikia kule ambako stakabadhi ya ghala inataka, kwa sababu mnajua taratibu za stakabadhi za ghala, mtu akiwa nayo anaweza kwenda benki, kuchukua pesa au kufanya kitu chochote, lakini sasa hatujafikia huko. Ombi langu kwa Waziri ni kwamba ingefaa sana tufikie huko kwa sababu ile ni rasilimali, ile ni fedha lakini hata hapa tulipo tunakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi juzi tu nimesikia kwa kuunganisha na suala hili la *TMX* mmefika Songwe mmeuza ufuta na wananchi kule wana shangwe sana. Ningetamani sana hata kwenye zao la kahawa sasa hivi Mheshimiwa Waziri sasa hivi wako

wananchi wanalalamika, wameuza kahawa mwaka 2023 mwezi wa Saba mpaka leo hii baadhi ya *AMCOS* hazijalipa, lakini tukiwa na mifumo hii, nimeambiwa hapa *TMX* inalipa ndani ya masaa 24.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba wananchi hawa hawawezi kupata hizi kero, wananchi hawa wanapeleka mazao wanauza, wanapata fedha na hivyo kutakuwa na maendeleo ndani ya nchi. Kwa hiyo, nawapongeza sana na nawapongeza wataalamu, wanafanya vizuri, hongereni sana na endeleeni kuchapa kazi ili wananchi wetu wanufaike na mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine nilitaka kuongelea hili suala la bei, nimeligusagusa hapa; bei zetu za bidhaa hizi za viwandani ziko juu. Nampongeza Waziri kwa utaratibu aliouanzisha wa kutoa taarifa kila tarehe 15 ya mwezi, ni mzuri, lakini hoja ya kwa nini tunanunua bati la *gauge* 30 kwa shilingi 25,000? Kwa nini tunanunua nondo milimeta 10 kwa shilingi 25,000? Kwa nini tunanunua malighafi hizi za simenti kwa shilingi 18,000 au shilingi 20,000? Bado bei iko juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaanzisha baadhi ya viwanda hapa nchini, wananchi waliambiwa sasa tunaenda kupata bidhaa hizi kwa unafuu ikiwemo simenti. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri kuna jambo hapa linapaswa lifanyike, bidhaa hizi bado ziko juu, tutafute namna yoyote ikiwezekana hata tuweke ruzuku ili wananchi wetu hawa wapate hizi bidhaa kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba, sasa hivi nchi yetu hii malighafi ni nyingi. Kwa mfano, malighafi za bati nyingi zinapatikana hapa nchini, malighafi za simenti ikiwemo *clinker* inapatikana hapa hapa nchini. Sasa kwa nini simenti iuzwe kwa bei ya shilingi 20,000 kwa mfuko? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakuomba sana tutafute namna ili wananchi wetu hawa bidhaa hii waipate kwa bei ya chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inawezekana kabisa, maana yake suala la ujenzi sasa hivi baadhi ya maeneo wataendelea

kubaki na hawataweza kujenga kwa sababu malighafi hizi ziko juu sana, ili tuende kwa pamoja, basi tuzishushe bei malighafi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naona umewasha kipaza sauti, naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Kapinga. Nilimtaja Mheshimiwa Jesca Masambatavangu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga wajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi. Naipongeza Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya pia kwa lile jambo la Mchuchuma, tunawapongeza sana na tunawatakia kila la heri kuhakikisha kwamba linafika mwisho na tunaanza kuona matunda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa ku-*quote* hotuba ya Mheshimiwa Waziri ambayo anasema "Mheshimiwa Spika, sekta ya viwanda na biashara kwa kiasi kikubwa inategemea shughuli za sekta binafsi ambayo ndiyo inayowekeza mitaji yao viwandani na kwenye miamala ya kibiashara ili kuhakikisha upatikanaji wa bidhaa na huduma nchini unakuwepo wakati wote." Hivyo, Mheshimiwa Waziri anasema jukumu kubwa la Wizara yake yeye ni kusimamia masuala ya utafiti, ushauri, uratibu, kutoa mwelekeo kwenye tasnia hii ya viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haipingiki kwamba sekta binafsi ndiyo imebeba viwanda na biashara. Wakristo tunaambiwa katika Mhubiri 10:19 fedha ni majawabu ya mambo yote. Kwa maana hiyo ni kwamba, walioshika majawabu ya mambo mengi ya Taifa letu ni hawa wafanyabiashara ambao Mheshimiwa unawasimamia wewe na ambao umesema ni sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuainisha majukumu yako Mheshimiwa Waziri umesema mnaratibu masuala ya utafiti yanayohusiana na biashara, mnatoa ushauri na mnaonesha mwelekeo. Kwa maana hiyo, sekta hii binafsi inakutegemea sana

wewe Waziri wa Viwanda uwasaidie katika kuratibu mambo yao na sekta nyingine au Wizara nyingine ili wafanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Fedha alitusomea hapa mapato ambayo tumekusanya mwaka 2023 nayo yana-*reflect* hii taarifa yako, kwamba tulikuwa tumekusanya shilingi trilioni 38, ambapo shilingi trilioni 23.6 ilitoka kwenye mapato ya ndani ambayo Mamlaka yetu ya Mapato ilikusanya shilingi trilioni 23.6, hizo shilingi trilioni 13.4 ni fedha za mikopo, hiyo shilingi trilioni moja ni kutoka vyanzo vingine. Kwa hiyo, utaona kwamba fedha nyingi inayokusanywa hata kwenye mapato ya nchi hii inatoka kwenye sekta binafsi, kwa maana hiyo sekta hii inatakiwa iangaliwe kwa umakini mkubwa sana, wafanyabiashara na wawekezaji kwenye viwanda wanatakiwa kutunzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu manufaa ya biashara kwamba inafanya kuanzisha ajira kubwa sana katika nchi. Biashara inaleta makusanyo ya mapato, biashara inasaidia ujenzi wa miundombinu. Nikafikiria nikaona kumbe katika Mawaziri hawa wewe hapo ndiye Waziri mkubwa wao na wengine wote hawa wangekuwa ni Mawaziri wadogo wadogo kwako. Kwa sababu hakuna barabara bila biashara na fedha wala hakuna afya bila biashara na fedha. Hatuna miundombinu yoyote itakayofanyika kwenye nchi hii kama hatuna fedha. Pia, tumekusanya kodi kutoka kwa wafanyabiashara ambao ni sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri lazima ajifunge kibwebwe bila kuwa mpole ahakikishe mtu anayeivuruga Sekta ya Biashara anapambana naye. Kama anashindwa kupambana naye yeye kwa jinsi alivyo kwa sababu wote wana *rank* moja, basi aangalie hata namna ya kumchongea sehemu ili ashughulikiwe. Kwa sababu hapa kuna dhambi ambayo inawasumbua sana watoza ushuru tangu enzi za Yohana. Yohana alishughulika nayo akashindwa, amekuja Yesu akawaacha nayo mpaka sasa hivi kizazi hiki Manabii na Mitume wanashindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo dhambi ya watoza ushuru na hii imeandikwa katika Kitabu cha Luka 3:12-13 maneno ya Mungu yanasema hivi, "Watozaushuru nao au wakusanyakodi wakamwendea yule Nabii Yohana wakamwuliza hivi, "nasi tunataka kwenda mbinguni, tufanye nini? Nabii Yohana akawaambia, "msibambikize kodi watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhambi hii ya kubambikiza kodi watu ndiyo inayoharibu sekta binafsi. Mheshimiwa Waziri wewe ni kuratibu, ni ku-*coordinate,* ni kufanya mambo yawe *fair* kwenye sekta zote na kuongea na wenzio *professional* wengine ili kuona umuhimu wa biashara. Wao wanaona tu fedha zinatiririka Hazina hawajui wewe unazidi kuwa mfupi kwa kuhakikisha kwamba biashara huku zinakomaa zinazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri sasa asiwachekeechekee, awasemee kama anashindwa kupambana nao kwa sababu leo hii kuna watu bado wanafunga biashara. Iringa kwangu mimi wafanyabiashara wangu wananipigia simu wiki nzima, wanafungiwa biashara karne hii. Tunajifunza kwenye biashara kuwa meneja yeyote mwenye akili anatumia watu kufikia malengo yake na siyo nguvu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu hawa wakusanyaushuru na watoza ushuru waangalie kama wana mameneja ambao bado wanatumia nguvu, hawatumii akili wawatoe wawaweke wale wanaotumia akili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikwambie, Wahasibu sio Mameneja wazuri sana kwa sababu moja ya *theory* za uhasibu ni *conservatism,* kuwa *rigid* tu bila sababu. Yaani mtu anajimwambafai tu, yuko *rigid,* hataki kumsikiliza mtu, akipita amenuna tu, ndio *style*. Yaani *rigidity* au *conservatism* ni *one of the theories* ya wahasibu. Tafuteni mameneja. *(Makofi)*

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji anachangia vizuri sana nataka tu nimpe taarifa mchangiaji kwamba wahasibu hawa huwa wanachojua ni *debit and credit* wala siyo *conservative by nature*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jesca, unapokea hiyo taarifa?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Twaha, mwakilishi wa wananchi kutoka Kibiti ni Mhasibu lakini mimi pia nilisema siku ile ni Daktari wa *DBA*. Najua *theory* za wahasibu ni *conservatism* abishe kama siyo. *Conservatism* ni *one of their theories,* yaani ndiyo utaratibu wao na wewe sio mhasibu kama hauko *conservative*. Sasa ni kanuni na hawa sio mameneja, lakini mameneja ni watu ambao wanaweza wakaongea na mtu wakamtia moyo akamwelewa kwa maneno na akalipa kodi *willingly*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimekwambia Iringa leo watu wanafungiwa biashara, wanaandikiwa kodi za miaka iliyopita. Mtu amepewa *notice* ya kodi ya mwaka 2013. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisema jamani hizi kodi za miaka sita hizi hebu tuachane nazo. Ukishaona mtu siku zote anafuatilia viporo, huyo ameshafika mwisho hana uwezo wa ku-*deliver* kitu kipya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenye uwezo wa ku-*deliver* kitu kipya atatafuta mbinu mpya na vyanzo vipya vya mapato siyo kurudi kutafuta viporo walivyoviacha wenzie huko nyuma. Leo hii unaenda kufunga biashara, umeshindwa kuongea na haya mambo ilishasemwa yasifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo tena tuna jambo lingine hapo kwa wenzetu hawa wakusanya kodi. Nimesema kudai kodi za zamani, kubambikiza kodi na kutengeneza uadui na wafanyabiashara. Mheshimiwa Waziri lazima wakusanya kodi wajue kwamba hata mishahara yao na suti zao na viti wanavyokalia kule maofisini vinatoka kwa yule mfanyabiashara mdogo anayekuja kumkadiria kodi pale. Yaani wao sio mabosi

wao ni watumwa, wale wanaokwenda pale ndiyo wameshika majawabu ya maisha yao na mishahara yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho ndicho kinachotuangusha. Hawa *TRA* wangekuwa na uwezo wa kukusanya zaidi ya hizi shilingi trilioni 23.6. Halafu lazima wajue kwamba wafanyabiashara ni ma-*genius* na ma-*intelligent* ndiyo maana wako wachache. Ni watu wanaotumia akili kubwa sana huwezi kumshinda. Uchumi ukishaharibu mazalia yake ni kama uyoga kuurudishia ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunahangaika na dola kwamba hazipo. Hapa ni *practice* iliyofanywa wakati ule wa ku-*harass Bureau De Change* leo tumepoteza *style* mpaka turudi kwenye *line* itatupa shida. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri vitu kama hivi hutakiwi kuviruhusu semelea maana wengine watakusumbua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine naomba sasa, kuna mtu anauliza asemee wapi? Yeye anajua, mbona hajauliza! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri, muwe karibu na hawa wafanyabiashara wadogo kwa sababu kila unayemwona ni *tycoon;* leo alianza kama mbuyu ulioanza kama mchicha. Kwa hiyo, *harassment* ya wafanyabiashara wadogo kama machinga ndio hatuna *future* ya kuja kuwa na wafanyabiashara wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hii ni Sekta yake na anawasimamia Mama yangu. Naomba pamoja na kwamba wamepelekwa kule Maendeleo ya Jamii lakini wale ni wafanyabiashara. Ninyi Wizara zenu zinaingiliana; washikiliwe hawa wakuzwe watakua. Wakikua watatuletea kodi kubwa, wakishatuletea kodi kubwa hapa tuta-*solve* majawabu ya mambo mengi sana. Tunalalamikia umeme humu, tunadai barabara, tunadai madaraja, tunadai dawa na tunadai bima za afya. Wale ndiyo wameshika majawabu.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wa umma nchi hii siyo wengi, nao wanajitahidi sana,

wanalipa kodi sana na ni kati ya walipakodi wazuri; nao ni wa kuangaliwa. Wazabuni wa nchi ndio wafanyabiashara, ndio walioshika majawabu. Leo unam-*starve* mtu ana-*save* chakula kwenye shule, mama tu anasaga unga humlipi ile hela. Usipomlipa ile hela kwa miezi sita umemuua anaenda kununuaje mahindi aje aendelee kulisha na yeye aendelee na biashara? Kwa hiyo, wafanyabiashara wa ndani, wazabuni, walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna ombi lingine.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa, nimekuvumilia kidogo ili umalizie.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umeisha?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Haya, nakushukuru sana Mheshimiwa Jesca Msambatavangu. Nilimtaja Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Isack Francis Mtinga, ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hii bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Kusema kweli pale kwangu Musoma Mjini kama tunavyofahamu ni kwamba mji wowote ule au nchi yoyote ile mojawapo ya jukumu kubwa ni kuhakikisha kwamba watu wao wanapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa bahati mbaya sana ni kwamba pale Musoma watu wangu hawana ajira kabisa. Hii imetokana na nini? Viwanda vyote vilivyokuwa vinafanya kazi Musoma vimekufa. Tulikuwa na kiwanda cha nguo kimekufa, kiwanda cha ngozi kimekufa, kiwanda cha maziwa kimekufa, viwanda vya samaki vimekufa na hata sasa kimebaki kiwanda

kimoja ambacho kinafanya kazi ya kununua, kukusanya samaki na kupeleka Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa masikitiko yangu nimekuwa nikilisema hili mara kwa mara lakini *response* ya Wizara au ya Serikali ni ndogo sana. Wakati mwingine hawafiki hata kukaa tu na wale wenye viwanda na kujua matatizo yao na mambo gani yanasababisha viwanda vife. Kwa hiyo, kidogo kwetu imekuwa changamoto na kutokana na hali hiyo, maana yake ni kwamba watu wetu wengi mpaka leo hivi wanakosa ajira, siyo kwa sababu nyingine, ni kwa sababu viwanda vinaendelea kufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani kuna haja ya Serikali kuona ni namna gani itaendelea kusimamia na kuvisaidia vile viwanda vilivyopo na kuleta viwanda vingine ili watu wake waweze kupata ajira kwa sababu hilo ni mojawapo ya jukumu kubwa la Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hiyo ni changamoto ya kwanza ambayo nadhani Mheshimiwa Waziri unahitaji uone namna ya kutusaidia pale Musoma na maeneo mengine. Naomba kabisa kwamba basi utenge muda hasa baada ya Bunge hili la Bajeti uje pale tukae tuzungumze na tuone ni namna gani Serikali iko tayari kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, yako haya mashirika ya viwanda vidogo vidogo kama *SIDO* ambalo linaweza likasaidia sana katika kukuza ajira. Leo ukienda nchi kama pale China viko viwanda vidogo vidogo tu hivi na kazi yake kubwa hasa ni ile *packaging*. Sasa Shirika letu kama la *SIDO* lilikuwa linatoa mafunzo mengi mbalimbali ambayo yalikuwa yanasaida vijana wetu kupata ujuzi na vilevile yalikuwa yanawapa mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tumeliacha lile Shirika limekufa. Mfano pale Musoma zimebaki zile *godown* wanapangisha wanapata *rent,* basi biashara inaishia hapo. Kama tungeona namna ambavyo tungeweza kuwawezesha tafsiri yake ni kwamba nao wangepata nafasi ya kuwawezesha vijana na akina mama mbalimbali kupata mafunzo ya muda mfupi, lakini na kuona namna wanavyoweza kujiendesha ambayo ni pamoja na

kuwapa mikopo. Kwa hiyo, na hilo nalo bado ni changamoto kwamba *SIDO* nayo iko pale lakini inaelekea kufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inajitahidi sana kujenga masoko makubwa na masoko mazuri. Bahati nzuri hata mimi mwaka huu nashukuru kwamba nimekumbukwa kwa maana nimeweza kupata fedha kwa ajili ya kujenga ile stendi yetu kubwa iliyokuwa inatusumbua kwa muda mrefu iliyoko pale Bweri. Mbali na hilo, nimepata fedha kwa ajili ya kujenga soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa changamoto iliyopo unakuta soko zuri linajengwa, lakini wananchi wanafika mahali wanahama kutoka kwenye masoko mle wanahamia kule pembezoni. Wanahama mle kwa sababu wanachokumbana nacho tu ni kodi nyingi na mwisho wa yote wanaona kama ni afadhali akakaa kule pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, leo mfano kwa pale Mjini yapo masoko ambayo ni mazuri tu. Kuna Soko Kuu liko pale leo kuna baadhi ya wananchi wanahama kutoka humo. Unakuta kuna soko kama lile la Saa Nane ambalo ni Soko la Wakulima, yako masoko kama kule Nyamatare na baadhi ya masoko mengin, wanahama ni kwa sababu Serikali haijatengeneza mazingira mazuri yanayowawezesha wananchi kukaa mle na wakafanya biashara. Kuna Soko kama la Kamnyonge, limekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilichotaka kushauri hapo ambacho Serikali inaweza ikakifanya na leo ikiamua inaweza ikayaboresha yale masoko na yakaenda vizuri kwa sababu tayari baadhi ya masoko yamejengwa na ni mazuri na mengine yanaendelea kujengwa kama hilo Soko la Nyasho kama nilivyosema. Serikali inapaswa kwanza ijitahidi kuhakikisha kwamba kodi ndogo ndogo zenye kero zinapungua mle.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, mtu akishakaa mle sokoni basi tuweke utaratibu mzuri wa wao kupata mikopo ya gharama nafuu ili waendelee kufanya zile biashara zao. Sasa unakuta yuko mle, aliyeko nje ya soko yeye halipi ushuru, lakini

aliyeko mle bado anadaiwa alipe ushuru. Kwa hiyo, mtu anaona ni afadhali akakaa nje kuliko kukaa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana hata mimi nilifanya juhudi binafsi nikawapeleka katika baadhi ya benki zetu ili ziweze kukaa nao zione uwezekano wa kuwapa mikopo. Waliambulia tu kuwaambia, ili waweze kulipia ile kufungua *account,* baada ya hapo benki zikaishia, na wale wananchi wako pale sasa wanaendelea yaani wanaona kama fedha yao imechukuliwa bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunadhani hilo nalo kuna haja ya Serikali kuangalia na ikiwezekana kwa sababu watu wengi wanajifunza biashara, wale Maafisa Maendeleo wetu wa jamii na wale wote ambao ni wakufunzi wanaofundisha mambo ya biashara wakawepo pale kwa ajili ya kuwasaida watu wetu ili waendelee kufanya biashara zao vizuri. Pia, wapate mikopo na kutokana na hiyo mikopo, basi maisha yao ni imani yangu kwamba yatakuwa mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni suala la tozo. Unajua mpaka leo wapo watu wengi wanalalamika kwa sababu kwanza wanashindwa kutofautisha kodi na tozo. Sasa unakuta zote hizo watu wanaziweka pamoja na zinaonekana kwamba zote ni kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaambiwa kila mmoja anasema kwamba katika nchi ambazo zina mazingira magumu ya kufanyia biashara ni pamoja na Tanzania. Zina mazingira magumu kwa sababu ukiacha ile kodi unakuta mfano kuna watu wa *TBS* watafika pale watakusanya hela zao, watu wa *fire* watafika pale watakusanya hela zao, watu wa *NEMC* watapita pale watakusanya hela zao, *Weight and Measure* watapita pale watakusanya hela zao na bado *OSHA* hujawazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa zote hizo ukizikusanya kwa pamoja ukachanganya na ile kodi, matokeo yake sasa kwa yule Mtanzania wa kawaida anaona maisha ni magumu maana kila kukicha huyu amepita, asipopita asubuhi mwingine anapita mchana na mwingine anapita jioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hilo nadhani Mheshimiwa Waziri una haja ya kuona namna gani tuta-*harmonize* na ikiwezekana, basi hizi kodi zote zingekusanywa zikawekwa pamoja ili yule mfanyabiashara akishalipa mara moja, basi ajue kwamba kazi yake amemaliza na sasa anaweza kufanya biashara yake vizuri pasipokuwa na shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana shida moja kwa mfanyabiashara kwanza akiona tu mtu yeyote yule wa Taasisi ya Serikali, yaani anakuwa tayari amejenga hofu. Pia unakuta kwa sababu ya uelewa wetu ni mdogo, wengine hata hawafuatilii. Yaani mtu wa *OSHA* akija pale anajaribu kuangalia yule mtu wa *OSHA* hatoi hata elimu kwamba kwa nini anakuja kuomba ile kodi, anasema tu wewe unapaswa kulipa *OSHA,* basi tupe hii tozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hajui ni ya nini, anaona ni kama anadhulumiwa; hajakaa sawa mtu wa *fire* amepita. Sasa mtu anaangalia, hivi hapa kwangu *fire* atakuja kunisaidia nini? Sasa haya yote ni kati ya mambo ambayo katika nchi yetu hii yanasababisha Watanzania waone kama mazingira ya kufanyia biashara ni magumu na njia pekee sasa ni kuona namna ya ku-*harmonize* ili hizi kodi zote ziweze kuwa moja na kwa utaratibu huo sasa watu wetu wanaweza wakafanya biashara vizuri pasipokuwa na shida yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Serikali ina kila aina ya sababu ya kuyaangalia haya ili Mtanzania afanye biashara yake vizuri pasipo mashaka yoyote. Hii ndiyo itakayoendelea kuwapa moyo wa kuendelea kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Vedastus Manyinyi. Nilimtaja Mheshimiwa Isack Francis Mtinga.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii

ambayo ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa nchi, lakini vilevile ni kichocheo kikubwa cha ajira ambazo tunazihitaji sana kwa vijana wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Rais wangu kwa jinsi ambavyo amekuwa akitenda haki katika bajeti za Wizara mbalimbali. Wizara hii ilikuwa na bajeti ndogo sana lakini Mheshimiwa Rais ameonyesha nia njema ya kuongeza bajeti japokuwa bado haitoshi kulinganisha na umuhimu wa Wizara hii lakini kwa kiasi kikubwa tunaona mabadiliko kulinganisha na hali halisi ilivyokuwa huko nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na timu yake nzima kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakijitahidi kufanya kazi kwa weledi katika Wizara hii na sisi kama Wanakamati, kwa kweli tunaridhishwa na jinsi ambavyo kazi zimekuwa zikifanyika ndani ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia kwenye mambo mawili tu. Jambo moja linahusu zao la alizeti ambalo linalimwa kwa wingi katika jimbo langu la Iramba Mashariki, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama na Mkoa wa Singida kwa ujumla. Zao hili linapolimwa inabidi liende kiwandani kwa ajili ya kutoa mafuta ya kula, kitu ambacho kimekuwa ni changamoto kubwa kwa nchi yetu hasa kwa ajili ya kupoteza fedha nyingi za kigeni kwa sababu ya ku-*import* mafuta ya kula kwa kigezo kwamba mafuta yanayozalishwa ndani hayatoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesema kwamba viwanda vipo, lakini mbegu za alizeti hazitoshi. Mimi nataka tu niende kidogo tofauti na *statement* hii. Mwaka wa kilimo uliopita Mkoa wa Singida pekee ulizalisha alizeti tani 1,400,040 ambapo mbegu huwa zinatoa mafuta takribani 30%. Kwa hiyo, 30% ya tani hizi ni kama lita 330,000 za mafuta, kwa Mkoa wa Singida tu, tukiacha maeneo mengine ambayo wanalima kidogo kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaona kwamba hiki ni kiwango kikubwa sana cha mafuta. Kwa nini viwanda vinasema

havina mbegu? Hili jambo siyo la kweli. Kwa kiwango hiki na kwa tani hizi ulitegemea viwanda viendelee kusaga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea ni kwamba, mafuta ambayo siyo ya alizeti yanayotoka nje yanaingia nchini kiholela, yanaingia mafuta mengi kiasi kwamba mafuta yetu ya ndani ambayo yanatokana na mbegu hizi yanashindwa ku-*compete* kwenye bei. Kwa hiyo, kilichofanyika, wakulima wengi walikaa na mbegu zao ndani, kwa sababu anaona akipeleka kuuza kiwandani bei anayopewa hairudishi hata robo ya gharama alizotumia. Matokeo yake viwanda vinaona kwamba havina mbegu, ukidhani kwamba wakulima hawajalima, kumbe wakulima wamelima mbegu imeanguka. Matokeo yake ni kwamba mbegu haziendi kiwandani kwa sababu mtu akipeleka anaona ni hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu ambacho kinatakiwa kifanyike hapa ni kudhibiti uingiaji wa mafuta ya kula. Mafuta haya hayana mwenyewe. Mafuta ya kula yanaingia tu, yaani kama bidhaa. Mtu analeta tu anavyotaka, hakuna *regulation* yoyote, na Wizara haijapata takwimu sahihi za mafuta kiasi gani yamezalishwa nchini ili *gap* pekee ndilo liagizwe kutoka nje, kwamba kile kilichopungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu hakuna *data*, watu wamekaa na mbegu ndani, na kwa sababu mafuta ya kutoka nje yamejaa sokoni, matokeo yake kila mtu anaingiza mafuta anavyotaka. Sasa hii inasababisha watu wasiendelee kulima na matokeo yake tunaona kama viwanda vyetu havina mbegu kumbe watu wameziweka ndani kwa sababu hazina bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba sana Serikali na Wizara sasa mafuta ya kula yawe na mwenyewe ili *data* sahihi zipatikane kwamba ni kiasi gani cha mafuta kimezalishwa ndani ya nchi ili mafuta kiasi gani yaletwe kutoka nje? Pia hayo yanayoletwa kutoka nje yanaingia kwa kiwango kile tu ambacho kinatakiwa ambacho ni tofauti. Hapo utaona kwamba mafuta ya ndani yatakuwa na bei nzuri na wakulima watakuwa na uhakika kwamba wakipeleka mbegu zao kiwandani watapata bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwamba sasa mafuta haya yawe na sheria maalum na yawe na mtu kama ilivyo sukari, kwamba una uhakika kabisa. Kwa hiyo, wenye viwanda wanadanganya danganya tu kwamba hatuna mbegu ili wapate wengine na fursa ya kuendelea kuagiza mafuta kutoka nje ili wapate faida kubwa na wakulima wetu wanazidi kukaa na mbegu ndani. Nataka niishauri Serikali, ihakikishe kwamba mafuta ya kula yanakuwa na sheria yake na udhibiti ili tujue kiasi gani cha mafuta kinaingia na kiasi gani kinatakiwa wananchi walime na hapo tutaona viwanda vyetu vitapata mbegu za kutosha katika kukamua mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niende kwenye suala la *TFDA* na *TBS*. Asubuhi niliona hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanashauri kwamba *TFDA* irudi, kwa maana ya kwamba *TBS* isifanye kazi hizo. Jambo hili siyo la kufuata kabisa, kwa sababu faida tuliyoiona ya *TBS* kudhibiti badala ya *TFDA* ni kubwa zaidi ukilinganisha na kama tukitaka kuirudisha *TFDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tufahamu kwamba chakula ni biashara. Usalama wa mimea na mifugo, vyote hivi vinazalisha bidhaa ambazo mwisho wa siku zinakuwa biashara. Sasa biashara inadhibitiwa na *TBS*. Mtu hawezi kufanya biashara popote, nje na ndani ya nchi kama hana ile nembo ya *TBS* kuonesha ubora wa ile bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishasema ubora ndani yake kuna usalama wa chakula. Yaani ukishasema kitu hiki ni bora maana yake ndani yake kuna usalama. Sasa ukikitoa *TBS, TBS* inabeba hivi vitu vyote kwa pamoja. Kazi ambazo zilikuwa zinafanywa na *TFDA* ndizo hizo hizo zilikuwa zinafanywa na *TBS* tangu mwanzo. Matokeo yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfanyabiashara alikuwa anapata kazi mara mbili, kwamba *TFDA* ilikuwa inatoa kibali cha jengo, kwamba lazima iangalie kwamba jengo hili linafaa kutengeneza chakula na kadhalika. Hapo hapo wanachukua *sample* kwa ajili ya kuangalia ubora wa bidhaa, na hizo *sample* walikuwa

wanazipeleka *TBS* kwenda kuangalia ubora wa wake ili baadaye wampe huyu mtu kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baada ya hapo huyu mfanyabiashara inabidi aende tena *TBS*. Kwa hiyo, huku *TFDA* anatafuta vyeti viwili; cha jengo anachukua na *sample* kwa ajili ya ubora halafu anakwenda tena *TBS* na kule *TBS* hawawezi kumpa ile nembo ya ubora mpaka tena warudie kujua je, huyu mtu anazalishia wapi hii bidhaa? Kwa hiyo, wanarudi tena kwenye jengo hiyo huduma inajirudia mara ya pili. Tena wachukue *sample* kupima waone kwamba hiki kitu kina ubora gani ili tuweze kumpa hii nembo aweze kufanya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo gharama zote ujue zinaenda na tozo, haziendi bure. Maana yake ni kwamba kule kwenye *TFDA* anatoa tozo kwa kazi ile ile ambayo inaenda kufanywa tena na *TBS* kwa kutoa tozo. Tulichokuwa tunafanya ni urasimu ambao mwisho wa siku viwanda vingine vilikuwa vinaenda nchi za jirani kwenda kufunguliwa kwa sababu ya vitu ambavyo tunavifanya kwa *duplication.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ujue kwamba kazi za *TFDA* zinaweza kumezwa *TBS* kama zilivyofanyika, lakini kwa mujibu wa kisheria kazi za *TBS* haziwezi kwenda kufanywa na *TFDA*. Kwa hiyo, ilikuwa ni lazima mmoja amezwe ili kuondoa huu mlolongo wa tozo na usumbufu na upotevu wa mali ambao ulikuwa unafanyika. Kwa sababu kama mfanyabiashara inabidi *sample* apeleke *TFDA* zikapimwe, ni gharama; halafu akichukua *sample* nyingine apeleke *TBS* kwenda zikapimwe, ni gharama pia. Kwa hiyo, analipa tozo mara mbili na anapeleka vifaa mara mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Serikali inabidi ununue mitambo ya kupima kwenye maabara za *TFDA* halafu hiyo hiyo mitambo tena na hizo maabara ukanunue tena *TBS* ambako na huko tena mtu akafanye. Kwa hiyo, tunafanya kazi mara mbili, na haya ndiyo malalamiko. Hata mchangiaji aliyepita hapa alipokuwa analalamika masuala ya *OSHA* na mengine yanamuumiza mfanyabiashara, ndiyo haya ambayo yalikuwa yanafanyika kwa kuwepo *TFDA* na *TBS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, busara ya Serikali iliyofanyika na ikaleta sheria hapa Bungeni kuivunja *TFDA* na kuipeleka *TBS* lilikuwa ni suala la busara sana. Kizuri zaidi, wale wataalamu wote waliokuwa *TFDA* na mitambo yao, hakuna mtu aliyefukuzwa kazi, wala mitambo haikupunguzwa; walibebwa kama walivyo wakapelekwa *TBS* na wakaenda kuendelea na ile kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kizuri kwa mfanyabiashara na mwananchi wa kawaida, zile tozo ambazo zilikuwa *TFDA* hazijahama, kwa sababu zile tozo tayari zilikuwepo *TBS,* zilikuwa ni mara mbili. Kwa hiyo, ina maana kule wale wamehama na mitambo na tozo zao mbovu wakaziacha huko huko. Kwa hiyo, wameenda kuendelea na tozo zilizokuwepo *TBS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tayari ule mzigo wa mfanyabiashara na mwananchi umeshapunguzwa. Maana yake ni kwamba na mazingira bora sasa ya biashara yameshafanyika kwa sababu tumepunguza vitu ambavyo vilikuwa *duplication* na ambavyo vilikuwa vinaleta hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya wanayo mambo mengi sana ya kufanya, kama wanatamani sana *TFDA* yako mengi ya kufanya hayajafanyika na ambayo ni ya muhimu. Kwa hiyo, naomba hili suala libakie huko huko *TBS*...

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ummy.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naisubiri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mchangiaji ajikite katika hoja yake. Wizara ya Afya tuna mambo mengi kweli, wala hatung'ang'anii ku-*regulate* masuala ya chakula na vipodozi. Ni michango ya Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, ajikite katika michango ya Waheshimiwa Wabunge.

Serikali ni moja na tunafanya kazi kwa kushirikiana kama Serikali, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hiyo naipokea, lakini nilikuwa nawajibu wale ambao walisema kuhusu Wizara ya Afya, hakusimama Mheshimiwa Waziri ili aseme tuna mambo mengi ili wasiendelee kusema. Kwa hiyo, nimesema kwa mujibu wa wale ambao walitaka mambo haya yaende Wizara ya Afya wakati huku Wizara ya Viwanda na Biashara chini ya Kamati yetu pia hili jambo ni zuri na linawapendeza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, na nawapongeza *TBS* kwa kazi nzuri na mpaka wameweza kupata vyeti mpaka huko nje ya nchi kwa jinsi ambavyo wameendelea kufanya kazi hii nzuri na tumepunguza mlolongo wa tozo kwa wananchi wetu. Naomba hili liendelee na *TBS* najua ina watu makini sana, wengine ni *mate* wangu tulisoma wote. Kazi hii inakwenda vizuri na tutaendelea kuisimamia vizuri Wizara yetu kuhakikisha hili jambo linawafurahisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Isack Francis Mtinga.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri wenu kwa Serikali. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Naibu wake wako makini, hapa wanachukua yale ambayo wanahisi kuwa ni ya muhimu kwa Taifa letu.

Kwa hiyo, kwa vile hakuna tangazo lingine kwa siku ya leo, basi naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.09 Usiku Bunge, liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 22 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*